# Elimu ya Dini ya Kiislamu

## Madrasa na Shule za Msingi

# Kitabu cha Tano



Islamic Propagation Centre

# ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

Madrasa na Shule za Msingi

**Kitabu cha-V**

Islamic Propagation Centre

© Islamic Propagation Centre

Elimu ya Dini ya Kiislam
Madrasa na Shule za Msingi

Kitabu cha Tano

Waandishi: Islamic Propagation Centre

Chapisho la kwanza, August 02, 2003

Nakala:

Kimetayarishwa na Islamic Propagation Centre
P.O.Box 55105

Typesetting-Islamic Propagation Centre.

Kimechapwa na

# Neno la Awali

Shukurani zote anastahiki Allah(S.W) aliyetuwezesha kukamilisha na kutoa kitabu hiki kwa ajili ya watoto wa darasa la tano katika Madrasa na Shule za msingi. Tunawatakia Rehema na amani Mitume wote wa Allah(S.W) pamoja na watu wemawaliofuata mwenendo wao katika kulingania Uislamu kwa jamii zao.

Wanafunzi wote watakaopitia kitabu hiki wanashauriwa wajizatiti kuyaingiza matendoni yale yote wanayojifunza katika sura za kitabu hiki. Allah(S.W) anatukumbusha:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ لِمَ تَقُولُونَ مَا لَا تَفْعَلُونَ ﴿٢﴾ كَبُرَ مَقْتًا
عِندَ ٱللَّهِ أَن تَقُولُوا۟ مَا لَا تَفْعَلُونَ ﴿٣﴾

*Enyi mlioamini! Mbona mnasema msiyoyatenda? Ni chukizo kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu kusema msiyoyatenda(61:2-3)*

Tunamuomba Allah(S.W) atuwezeshe kutenda kama alivyotufunza Mtume wake na atujaalie sisi na watoto wetu kuwa Makhalifa wake hapa Ulimwenguni.

**Wabillah Tawfiiq**

**Mwalimu Mratibu**
**Islamic Propagation Centre**

# Yaliyomo


Neno la Awali.......................................................................................... (i)

Sura ya Kwanza.

Qur,an:..........................................................................................1

Kusoma na kuhifadhi....................................................................1

Kusoma na kutafsiri......................................................................1

Ujumbe wa Qur,an.........................................................................1

Suratul-Bayyinah...................................................................1

Suratul-Qadr..........................................................................3

Suratul-'Alaq...........................................................................4

Suratul-Tyn.............................................................................7

Suratul-Alam-nashrah...........................................................8

Suratudh-Dhuhaa..................................................................9

Suratul-Layl..........................................................................11

Suratush-Shams..................................................................13

Suratul-Balad.......................................................................15

Suratul-Fajr..........................................................................17

Suratul-Ghaashiyah............................................................21

Suratul-A 'alaa....................................................................23

Zoezi la kwanza...................................................................23

**Sura ya Pili**

Tawhiid..........................................................................................27

Kumuamini Allah(s.w)...................................................................27

Dalili kutokana na Historia ya mwanadamu...................27

Kuamini Malaika wa Allah(s.w).....................................................29

Malaika ni nani?..................................................................29

Je Malaika wanaishi wapi...................................................29

Kwanini hatuwaoni Malaika?.............................................30

Siku Mtu atakapowaona Malaika......................................31

Sifa za Malaika....................................................................32

Kazi za Malaika....................................................................35

Mtu anayeamini Malaika anatakiwa afanyeje?..............40

Kuamini vitabu vya Allah(s.w).........................................................40

Je, Biblia ni kitabu kitakatifu?...........................................42

Qur,an kitabu pekee cha Allah(s.w) kilicho kitakatifu...42

Tofauti ya Qur,an na vitabu vingine vya Allah(s.w)..........43

Maana ya kuamini Vitabu vya Allah(s.w)........................44

Zoezi la Pili..........................................................................45

**Sura ya Tatu**
Fiqh....47
Kusimamisha Swala....47
Maana ya swala....47
Umuhimu wa kusimamisha swala....47
Lengo la swala....49
Swala za Sunnah....49
Tahiyyatul-Masjid....50
Qabliyyah na Baadiyyah....50
Swala ya Witr....51
Swala ya Tahajjud....52
Swala za Idd Mbili....52
Faida za kusimamisha swala katika maisha....52
Zakkat na Sadaqa....53
Maana ya Zakkat....53
Maana ya Sadaqa....54
Umuhimu wa kutoa Zakkat na Sadaqat....54
Masharti ya utoaji wa Zakkat na Sadaqat....56
Lengo la Zakkat....57
Funga ya Ramadhani....57
Swala za usiku wa Mwezi wa Ramadhani....58
Lailatul-Qadr....58
Itiqaf katika mwezi wa Ramadhani....59
Zakkatul-Fitr....60
Iddil-Fitr....60
Funga za Sunnah....62
Siku zilizoharamishwa kufunga....63
**Sura ya Nne**
Akhlaq....65
Kujipamba na tabia njema....65
Vipengele vya tabia njema....65
kujielimisha kwa ajili ya Allah(s.w)....65
Kuwa na Ikhlas....66
Kujiepusha na riya....66
Kujiepusha na unafiki....67
Kuwa mkweli....68
Kujiepusha na uwongo....68
Kuwa muaminifu....69
Kuwa muadilifu....69
Kuchunga ahadi....70
Kuwa na kauli njema ....70

Kujiepusha na maongezi yasiyo na maana...................71
Kujiepusha na usengenyi...............................................72
Kujiepusha na dharau.....................................................73
Kujiepusha na matusi.....................................................74
Kujiepusha na mabishano.............................................75
Kujiepusha na kibri na kujiona.......................................76
Kujiepusha na kulaani ovyo............................................77
Kujiepusha na viapo.......................................................78
Kuwa na heshima............................................................78
Zoezi la Nne...................................................................81
**Sura ya Tano**
Tarekh..................................................................................82
Maana ya Historia kwa mujibu wa makafiri...............................82
Chimbuko la Mtazamo wa Makafiri juu ya Historia...................82
Udhaifu wa mtazamo wa makafiri. .............................................84
Charles Darwin hakuwa mwanasayansi.........................84
Chaguo la kimaumbile halizai viumbe vipya..................84
Mafuvu ya kale hayaoneshi kuwa mtu alikuwa sokwe..85
Ni muhali sokwe kubadilika kuwa mtu.......................... .86
Ghushi na uzushi wa makafiri........................................87
Makafiri hurubuni kwa michoro na masanamu..............88
Maana ya Historia kwa mujibu wa Uislamu...................89
Kwanini tujifunze historia?.............................................90
Historia ya Mitume...................................................................97
Nabii Adamu(a.s)...........................................................98
Mafunzo kwa muhtasari..................................................103
Nabii Idriss (a.s).............................................................104
Mafunzo kwa muhtasari..................................................104
Nabii Nuhu (a.s).............................................................105
Mafunzo kwa muhtasari..........................................108,114
Nabii Hud(a.s) ................................................................115
Kuadhibiwa watu wa Hud(a.s)........................................121
Kuokolewa nabii Hud(as) na watu wema.......................122
Nabii Saleh(a.s)..............................................................124
Njama za kumuua nabii Salehe(a.s)..............................128
Kuangamizwa watawala madhalimu..............................128
Nabii Ibrahim (a.s.).........................................................129
Mafunzo kwa muhtasari..................................................141
Nabii Lut (a.s.)................................................................142
Mafunzo kwa muhtasari..................................................144
Nabii Ismail (a.s.)............................................................145

Mafunzo kwa muhtasari....................................................148
Nabii Is'haq (a.s.) na Yaqub (a.s.)....................................149
Mafunzo kwa muhtasari....................................................151
Nabii Yusufu (a.s.).............................................................152
Mafunzo kwa muhtasari....................................................164
Nabii Musa(as)..................................................................166
Mafunzo kwa muhtasari....................................................178
Nabii Daud (a.s.)...............................................................180
Mafunzo kwa muhtasari....................................................184
Nabii Suleiman(a.s)..........................................................185
Mafunzo kwa muhtasari....................................................190
Nabii Zakaria (a.s).............................................................191
Mafunzo kwa muhtasari....................................................191
Nabii Yahya(a.s)...............................................................192
Mafunzo kwa muhtasari....................................................193
Nabii Isa(Yesu) (a.s).........................................................193
Je, nabii Isa(Yesu)ni mtoto wa Mungu?............198
Nabii Isa(Yesu) alitumwa kwa kina nani?...........198
Ujumbe wa nabii Isa(Yesu( (as)..........................199
Miujiza ni uwezo wa Isa(Yesu) mwenyewe?.......201
Njama za kutaka kumuuwa nabii Isa(Yesu)........203
Ahadi ya Allah(SW) kumuokoa nabii Isa(Yesu)..204
Aliyesulubiwa ni Simoni Mkirene, si Yesu...........205
Nabii Isa(Yesu) siku ya Kiama.............................206

## Sura ya Kwanza

# Qur'an

### KUSOMA NA KUHIFADHI

Mwanafunzi wa darasa la tano anatarajiwa aweze kusoma kwa ufasaha na kuhifadhi sura katika juzuu ya 28 kuanzia *Al-Mujadillah* hadi *At-Taghaabun.*

### KUSOMA NA TAFSIRI

Mwanafunzi wa darasa la tano anatarajiwa pia aweze kuhifadhi tafsiri ya Surat-Talaq mpaka Nuhu. Mwanafunzi atumie msahafu wa tafsiri ya Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy.

### Ujumbe wa Qur'an

Mwanafunzi wa darasa la tano anatarajiwa aweze kutoa kwa muhtasari mafunzo ya Suratul-Bayyina hadi Suratul-A'alaa.

Madinah **Suratul-Bayyinah(98)** Ina aya 8

| Tafsiri | aya |
|---|---|
| *Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehma, Mwenye Kurehemu.* | بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ |
| *1. Wale waliokufuru miongoni mwa watu wa kitabu na washirikiana (waliotoa ahadi kuwa) hawataacha (waliyonayo) mpaka iwajie hoja.* | لَمۡ يَكُنِ ٱلَّذِينَ كَفَرُواْ مِنۡ أَهۡلِ ٱلۡكِتَٰبِ وَٱلۡمُشۡرِكِينَ مُنفَكِّينَ حَتَّىٰ تَأۡتِيَهُمُ ٱلۡبَيِّنَةُ ١ |
| *2. (Naye) ni Mtume aliyetoka kwa Allah anayewasomea kurasa zilizotakaswa.* | رَسُولٞ مِّنَ ٱللَّهِ يَتۡلُواْ صُحُفٗا مُّطَهَّرَةٗ ٢ |
| *3. (Ambazo) ndani yake humo mna sharia madhubuti.* | فِيهَا كُتُبٞ قَيِّمَةٞ ٣ |

| | |
|---|---|
| 4. Wala hawakutengana (hawakufarikiana) wale waliopewa kitabu ila baada ya kuwajia hoja hiyo. | وَمَا تَفَرَّقَ ٱلَّذِينَ أُوتُوا۟ ٱلْكِتَـٰبَ<br>إِلَّا مِنۢ بَعْدِ مَا جَآءَتْهُمُ ٱلْبَيِّنَةُ ﴿٤﴾ |
| 5. Na wala hawakuamrishwa ila kumuabudu Allah kwa kumtakasia dini, wawache dini za upotofu na wasimamishe Sala na kutoa Zakat hiyo ndiyo dini iliyo sawa. | وَمَآ أُمِرُوٓا۟ إِلَّا لِيَعْبُدُوا۟ ٱللَّهَ<br>مُخْلِصِينَ لَهُ ٱلدِّينَ حُنَفَآءَ<br>وَيُقِيمُوا۟ ٱلصَّلَوٰةَ وَيُؤْتُوا۟ ٱلزَّكَوٰةَ<br>وَذَٰلِكَ دِينُ ٱلْقَيِّمَةِ ﴿٥﴾ |
| 6. Bila shaka wale waliokufuru miongoni mwa watu waliopewa kitabu na washirikina wataingia katika moto wa Jahannam, wakae humo milele, hao ni waovu wa viumbe. | إِنَّ ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ مِنْ أَهْلِ ٱلْكِتَـٰبِ<br>وَٱلْمُشْرِكِينَ فِى نَارِ جَهَنَّمَ خَـٰلِدِينَ<br>فِيهَآ ۚ أُو۟لَـٰٓئِكَ هُمْ شَرُّ ٱلْبَرِيَّةِ ﴿٦﴾ |
| 7. Hakika wale walioamini na kutenda mema basi hao ndio wema wa viumbe. | إِنَّ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ وَعَمِلُوا۟ ٱلصَّـٰلِحَـٰتِ<br>أُو۟لَـٰٓئِكَ هُمْ خَيْرُ ٱلْبَرِيَّةِ ﴿٧﴾ |
| 8. Malipo yao kwa Mola wao ni mabustani ya daima ambayo mito inapita mbele yake wakae humo milele; (hali ya kuwa) Allah amewaridhia nao wameridhika. (Malipo) hayo ni kwa yule anayemuogopa Mola wake. | جَزَآؤُهُمْ عِندَ رَبِّهِمْ جَنَّـٰتُ عَدْنٍ<br>تَجْرِى مِن تَحْتِهَا ٱلْأَنْهَـٰرُ خَـٰلِدِينَ<br>فِيهَآ أَبَدًا ۖ رَّضِىَ ٱللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا۟<br>عَنْهُ ۚ ذَٰلِكَ لِمَنْ خَشِىَ رَبَّهُۥ ﴿٨﴾ |

### Ujumbe wa Suratul-Bayyinah

Baada ya kuipitia surah hii kwa makini tunajifunza haya yafuatayo:

1. Katika zama zetu hizi muongozo pekee wa kumuongoza mwanaadamu ni Qur'an aliyokuja nayo Muhammad (s.a.w).

2. Wayahudi, Wakristo na Washirikina wengine wamehiari kuendelea kuwepo katika upotofu kwa jeuri tu. Kwani hawako tayari kuufuata uongofu ambao uko bayana katika Qur'an na Sunnah ya Mtume (s.a.w.).

3. Wana adhabu kali wale wanaofuata upotofu baada ya kuijua haki.

4. Wenye kuamini na kufanya amali njema watakuwa na amani hapa duniani na watakuwa na malipo mazuri ya kudumu milele huko Akhera.

Makka

## Suratul-Qadir (97)

Ina aya 5

| Tafsiri | aya |
|---|---|
| Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehma, Mwenye Kurehemu. | بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ |
| 1. Hakika Tumeiteremsha (Qur'an) katika Laylatul-Qadr (Usiku wenye heshima kubwa) (usiku wa mwezi wa Ramadhan). | إِنَّآ أَنزَلْنَٰهُ فِى لَيْلَةِ ٱلْقَدْرِ ﴿١﴾ |
| 2. Na jambo gani litakalokujulisha (hata ukajua) nini huo usiku wa LaylatulQadr? | وَمَآ أَدْرَىٰكَ مَا لَيْلَةُ ٱلْقَدْرِ ﴿٢﴾ |
| 3. Huo usiku wa hishma (huo) ni bora kuliko miezi Elfu. | لَيْلَةُ ٱلْقَدْرِ خَيْرٌ مِّنْ أَلْفِ شَهْرٍ ﴿٣﴾ |
| 4. Huteremka Malika na Roho (za viumbe watakatifu) katika usiku huo kwa idhini ya Mola wao kwa kila jambo. | تَنَزَّلُ ٱلْمَلَٰٓئِكَةُ وَٱلرُّوحُ فِيهَا بِإِذْنِ رَ<br>بِّهِم مِّن كُلِّ أَمْرٍ ﴿٤﴾ |
| 5. Ni amani (usiku) huo mpaka mapambazuko ya Alfajiri. | سَلَٰمٌ هِىَ حَتَّىٰ مَطْلَعِ ٱلْفَجْرِ ﴿٥﴾ |

**Ujumbe wa Suratul-Qadr**

Baada ya kuipitia sura hii kwa makini tunajifunza kuwa:

(1) Qur'an imeanza kushushwa usiku katika mwezi wa Ramadhani.

(2) Kwa heshima ya Qur'an, usiku huo umepandishwa daraja na Allah (s.w.) na kufanywa bora kuliko miezi 1,000 na umeitwa usiku wenye cheo yaani *Lailatul-Qadr.*

(3) Katika usiku huo kunakuwa na amani hadi alfajiri.

(4) Hatuna budi kuiheshimu Qur'an kama alivyoipa heshima Allah (s.w.). Tutakuwa tumeiheshimu Qur'an kwa kuisoma kwa mazingatio na kuifuata vilivyo katika maisha yetu yote.

(5) Amani itapatikana katika jamii pale Qur'an itakapoheshimiwa na kufanywa kuwa mwongozo pekee wa maisha yetu yote.

(6) Jamii yenye kuifanya Qur'an kuwa ndio mwongozo wake pekee wa maisha na kumtii Mtume Muhammad (s.a.w.) aliyeshushiwa Qur'an, huwa ni jamii bora kuliko jamii nyingine zote kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

كُنتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِٱلْمَعْرُوفِ
وَتَنْهَوْنَ عَنِ ٱلْمُنكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِٱللَّهِ

*"Nyinyi ndio umma bora kuliko umma zote zilizodhihirishiwa watu (ulimwenguni) mnaamrisha yaliyo mema na mnakataza yaliyo maovu, na mnamwamini Mwenyezi Mungu...". (3:110)*

Makka

## Suratul-'**Alaq (96)**

Ina aya 19

| **Tafsiri** | **aya** |
|---|---|
| Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehma, Mwenye Kurehemu. | بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ |
| 1. Soma kwa jina la Mola wako Aliyeumba. | ٱقْرَأْ بِٱسْمِ رَبِّكَ ٱلَّذِى خَلَقَ ﴿١﴾ |
| 2. Amemuumba Mwanadamu kwa pande la damu. | خَلَقَ ٱلْإِنسَٰنَ مِنْ عَلَقٍ ﴿٢﴾ |
| 3. Soma, na Mola wako ni Karimu sana. | ٱقْرَأْ وَرَبُّكَ ٱلْأَكْرَمُ ﴿٣﴾ |

| | |
|---|---|
| 4. Ambaye amemfundisha (Binadamu elimu zote hizi) kwa (msaada wa) kalamu. | ٱلَّذِى عَلَّمَ بِٱلْقَلَمِ ﴿٤﴾ |
| 5. Amemfundisha mwanadamu chungu ya mambo aliyokuwa hayajui. | عَلَّمَ ٱلْإِنسَـٰنَ مَا لَمْ يَعْلَمْ ﴿٥﴾ |
| 6. Sivyo hivi (Binadamu)! Kwa hakika binadamu hutakabari. | كَلَّآ إِنَّ ٱلْإِنسَـٰنَ لَيَطْغَىٰٓ ﴿٦﴾ |
| 7. Akijiona amepata utajiri! | أَن رَّءَاهُ ٱسْتَغْنَىٰٓ ﴿٧﴾ |
| 8. Bila shaka marejeo (ya watu) (wote) ni kwa Mola wako (tu). | إِنَّ إِلَىٰ رَبِّكَ ٱلرُّجْعَىٰٓ ﴿٨﴾ |
| 9. Je! Umemuona yule anayemkataza. | أَرَءَيْتَ ٱلَّذِى يَنْهَىٰ ﴿٩﴾ |
| 10. Mja (wa Mungu) akisali? | عَبْدًا إِذَا صَلَّىٰٓ ﴿١٠﴾ |
| 11. Je! umeona kama yeye yuko juu ya uongofu (kwa kufanya hivyo)? | أَرَءَيْتَ إِن كَانَ عَلَى ٱلْهُدَىٰٓ ﴿١١﴾ |
| 12. Au anaamrisha wema (kwa kufanya hivyo, au anafanya mabaya)? | أَوْ أَمَرَ بِٱلتَّقْوَىٰٓ ﴿١٢﴾ |
| 13. Je, unaonaje! Kama yeye anakadhibisha na kurudi nyuma? | أَرَءَيْتَ إِن كَذَّبَ وَتَوَلَّىٰٓ ﴿١٣﴾ |
| 14. Je! Hajui ya kuwa Allah (s.w.) anamuona? | أَلَمْ يَعْلَم بِأَنَّ ٱللَّهَ يَرَىٰ ﴿١٤﴾ |
| 15. Sivyo hivyo! Kama haachi, tutamkokota kwa nywele za utosi (wake tumtie motoni). | كَلَّا لَئِن لَّمْ يَنتَهِ لَنَسْفَعًۢا بِٱلنَّاصِيَةِ ﴿١٥﴾ |
| 16. Utosi muongo, wenye madhambi. | نَاصِيَةٍ كَـٰذِبَةٍ خَاطِئَةٍ ﴿١٦﴾ |

| | |
|---|---|
| 17. Basi nawaite wanachama wenzake (wamsaidie). | فَلْيَدْعُ نَادِيَهُۥ ﴿١٧﴾ |
| 18. Na sisi Tutawaita Malaika wa motoni (wamuadhibu). | سَنَدْعُ ٱلزَّبَانِيَةَ ﴿١٨﴾ |
| 19. Sivyo! Usimtii (mbaya huyo) bali sujudu na uwe karibu na Mola wako. | كَلَّا لَا تُطِعْهُ وَٱسْجُدْ وَٱقْتَرِب ﴿١٩﴾ |

**Ujumbe wa Suratul 'Alaq**

Kutokana na historia ya kushushwa Qur'an tunajifunza kuwa Mtume (s.a.w.) alianza kushushiwa aya tano za mwanzo za sura hii alipokuwa katika pango la Hira. Aya hizi zilishushwa katika usiku mmoja wa mwezi wa Ramadhani. Hizi aya tano za mwanzo zinatupa mafundisho yafuatayo:

(1) Amri ya kwanza ya Allah (s.w.) kwa Waislamu ni kutafuta elimu kwa ajili ya Allah (s.w.). Kusoma kwa ajili ya Allah (s.w.) ni kujielimisha ili tuweze kumuabudu Allah (s.w.) katika kila kipengele cha maisha yetu na ili tuweze kusimamisha na kuendesha dola ya Kiislamu.

(2) Neema kubwa aliyotunukiwa mwanaadamu na Mola wake kuliko neema zote ni elimu.

(3) Chanzo cha fani zote za elimu ni Allah (s.w.). Kila anachojua mwanaadamu amefundishwa na Allah (s.w.).

(4) Katika Uislamu hapana mgawanyiko wa elimu ya dini na elimu ya dunia. Fani zote za elimu ziko pale ili kumuwezesha mwanaadamu kumwabudu Mola wake katika kila kipengele cha maisha na kumuwezesha kusimamisha na kuendesha Dola ya Kiislamu.

Katika aya ya sita hadi ya 19 ya sura hii tunaendelea kupata mafunzo yafuatayo:

(5) Baadhi ya watu wanapopata utajiri na vyeo katika jamii hutakabari kwa kumuasi Mola wao na kuwazuia (kuwakwaza) waumini wasimwabudu Mola wao inavyostahiki. Kisha hujisifia kwa matendo yao hayo maovu.

(6) Watu hawa waovu wanapewa onyo kuwa kama hawataacha uovu wao huo Allah (s.w.) atawatia adabu hapa hapa duniani na katika maisha ya akhera watakuwa watu wa motoni.

(7) Waumini wa kweli wanaamriwa na Mola wao kuwa wasiwaogope wala wasiwatii hawa makafiri bali wamtii Mola wao na waendelee kumwabudu na kusimamisha Uislamu katika jamii.

Makka

# Suratul-tyn(95)

Ina aya 8

| Tafsiri | aya |
|---|---|
| Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehma, Mwenye Kurehemu. | بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ |
| 1. Naapa kwa Tini na Zaituni. | وَٱلتِّينِ وَٱلزَّيۡتُونِ ١ |
| 2. Na kwa Mlima Sinai. | وَطُورِ سِينِينَ ٢ |
| 3. Na kwa Mji huu (wa Makka) wenye amani. | وَهَٰذَا ٱلۡبَلَدِ ٱلۡأَمِينِ ٣ |
| 4. (Ya kwamba) Bila ya shaka Tumemuumba mwanadamu kwa umbo lililo bora kabisa. | لَقَدۡ خَلَقۡنَا ٱلۡإِنسَٰنَ فِيٓ أَحۡسَنِ تَقۡوِيمٖ ٤ |
| 5. Kisha tukamrudisha kuwa chini kuliko walio chini. | ثُمَّ رَدَدۡنَٰهُ أَسۡفَلَ سَٰفِلِينَ ٥ |
| 6. Ila wale wenye kuamini na kutenda mema, watakuwa na ujira usiokwisha, (unaendelea maisha). | إِلَّا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ فَلَهُمۡ أَجۡرٌ غَيۡرُ مَمۡنُونٖ ٦ |
| 7. Basi ni lipi likupalo kukadhibisha malipo baada (ya kuona hayo)? | فَمَا يُكَذِّبُكَ بَعۡدُ بِٱلدِّينِ ٧ |
| 8. Je! Allah si Hakimu muadilifu kuliko Mahakimu wote? | أَلَيۡسَ ٱللَّهُ بِأَحۡكَمِ ٱلۡحَٰكِمِينَ ٨ |

**Ujumbe wa Surat Tyn**

Baada ya kupitia sura hii kwa makini tunajifunza yafuatayo:

(1) Vitu vinne vilivyotajwa - mimea ya mitini na mizaituni, mlima wa Sinai na mji wa Makka - vinaashiria mazingira walimoishi baadhi ya Mitume wa Allah (s.w.). Mitume hawa ni Nabii Nuhu, Ibrahimu, Musa, Issa na Muhammad (Rehma na amani ziwe juu yao wote).

(2) Allah (s.w.) amemtukuza mwanaadamu kwa kumuumba katika

umbo bora na kumtunukia vipawa vya akili na ufahamu wa hali ya juu, kisha akampa mwongozo kupitia kwa Mitume wake na vitabu vyake.

(3) Wale wanaomwamini Allah (s.w.) na kuendesha maisha yao yote kwa kufuata mwongozo wake, watakuwa ni wabora wa viumbe na watakuwa na hadhi katika maisha ya dunia na akhera.

(4) Wale wenye kumkufuru Allah (s.w.) na kukataa mwongozo wake watakuwa ni waovu wa viumbe na watakuwa dhalili katika maisha ya dunia na katika akhera watakuwa na adhabu kali.

(5) Lazima iwepo siku ya mwisho ili waumini waliotenda vitendo vizuri kwa kufuata mwongozo wa Allah (s.w.) walipwe kwa uadilifu jaza ya vitendo vyao.

(6) Ni lazima pia iwepo siku ya mwisho ili waovu waliomkufuru Allah (s.w.) na kukataa mwongozo wake walipwe kwa uadilifu jaza ya vitendo vyao.

## Makka — Suratul-Alam-Nashrah(94) — Ina aya 8

| Tafsiri | aya |
|---|---|
| Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehma, Mwenye kurehemu. | بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ |
| 1. Je! Hatukukupanulia kifua chako. | أَلَمْ نَشْرَحْ لَكَ صَدْرَكَ ﴿١﴾ |
| 2. Na tukakuondolea mzigo wako. | وَوَضَعْنَا عَنكَ وِزْرَكَ ﴿٢﴾ |
| 3. Uliovunja mgongo wako? | ٱلَّذِيٓ أَنقَضَ ظَهْرَكَ ﴿٣﴾ |
| 4. Na tukatukuza utajo wako? | وَرَفَعْنَا لَكَ ذِكْرَكَ ﴿٤﴾ |
| 5. Basi kwa hakika baada ya dhiki (huja) faraja. | فَإِنَّ مَعَ ٱلْعُسْرِ يُسْرًا ﴿٥﴾ |
| 6. Hakika baada ya dhiki (huja) faraja. | إِنَّ مَعَ ٱلْعُسْرِ يُسْرًا ﴿٦﴾ |
| 7. Basi ukishamaliza (kulingania) shughulika (kwa Ibada nyingine). | فَإِذَا فَرَغْتَ فَٱنصَبْ ﴿٧﴾ |
| 8. Na jipendekeze kwa Mola wako. | وَإِلَىٰ رَبِّكَ فَٱرْغَب ﴿٨﴾ |

**Ujumbe wa Surat Alam Nashrah**

Kutokana na sura hii tunapata ujumbe ufuatao:

(1) Mtume (s.a.w.) alipanuliwa kifua kwa kuletewa Wahay na kupewa elimu na hekima ambavyo vilimwezesha kuona mambo katika uhalisi wake.

(2) Mzigo mzito uliomkabili Muhammad (s.a.w.) kabla ya kupewa Utume ni ile hamu na shauku ya maisha ya haki na usawa. Alikuwa akipata taabu sana moyoni mwake kuona wanyonge wakidhulumiwa haki zao na wale wenye nguvu katika jamii. Mzigo huu uliondoka pale alipopewa dira ya ukombozi yaani Utume na mwongozo wa Qur'an.

(3) Utatuzi wa matatizo yote yanayoikabili jamii ya wanaadamu hivi leo ni kufuata barabara mwongozo wa Qur'an na Sunnah ya Mtume (s.a.w.)

(4) Kazi ya kusimamisha Uislamu katika jamii ni jukumu zito, lakini Allah (s.w.) anawaahidi waumini kuwa wakijizatiti kufanya kazi hii, watapata mafanikio na maendeleo siku zinavyosonga mbele.

(5) Ili kufanikiwa kusimamisha Uislamu katika jamii, Waislamu wanahimizwa kujipendekeza na kujikurubisha kwa Allah (s.w.) kwa kufanya ibada za ziada, baada ya kutekeleza majukumu yao ya kijamii ya kila siku. Hapana muda wa kupoteza kwa Muislamu. Wakati wa mapumziko tunatakiwa tumdhukuru Allah (s.w.) kwa wingi.

Makka **Suratudh-Dhuhaa (93)** Ina aya 11

| Tafsiri | aya |
|---|---|
| Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehma, Mwenye kurehemu. | بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ |
| 1. Naapa kwa Mchana, | وَٱلضُّحَىٰ ﴿١﴾ |
| 2. Na kwa usiku unapotanda. | وَٱلَّيْلِ إِذَا سَجَىٰ ﴿٢﴾ |
| 3. Hakukuacha Mola wako wala Hakukukasirikia (ewe Nabii Muhammad). | مَا وَدَّعَكَ رَبُّكَ وَمَا قَلَىٰ ﴿٣﴾ |
| 4. Na bila shaka (kila) wakati ujao (utakuwa) ni bora kwako kuliko uliotangulia. | وَلَلْءَاخِرَةُ خَيْرٌ لَّكَ مِنَ ٱلْأُولَىٰ ﴿٤﴾ |
| 5. Na Mola wako atakupa mpaka uridhike. | وَلَسَوْفَ يُعْطِيكَ رَبُّكَ فَتَرْضَىٰٓ ﴿٥﴾ |

| | |
|---|---|
| 6. Je! Hakukuta yatima akakupa makazi (mazuri ya kukaa)? | أَلَمْ يَجِدْكَ يَتِيمًا فَـَٔاوَىٰ ٦ |
| 7. Na hakakukuta hujui kuongoza njia, akakuongoza? | وَوَجَدَكَ ضَآلًّا فَهَدَىٰ ٧ |
| 8. Na hakukuta fakiri, akakutajirisha? | وَوَجَدَكَ عَآئِلًا فَأَغْنَىٰ ٨ |
| 9. Basi usimuonee yatima. | فَأَمَّا ٱلْيَتِيمَ فَلَا تَقْهَرْ ٩ |
| 10. Wala usimkaripie aombaye. | وَأَمَّا ٱلسَّآئِلَ فَلَا تَنْهَرْ ١٠ |
| 11. Na neema ya Mola wako uisimulie. | وَأَمَّا بِنِعْمَةِ رَبِّكَ فَحَدِّثْ ١١ |

**Ujumbe wa Suratudh-Dhuhaa**

Katika sura hii tunajifunza kuwa:

(1) Allah (s.w.) ana haki ya kuapia chochote katika viumbe vyake na viapo hutumika ili kuweka msisitizo juu ya yale yanayoelezwa baada ya viapo.

(2) Hakuna kipindi chochote katika harakati za kusimamisha Uislamu ambacho Mtume (s.a.w.) hakupata msaada wa Mwenyezi Mungu. Hivyo Waislamu waliopo katika harakati za kusimamisha Uislamu, wasikate tamaa bali wawe na yakini kuwa Allah (s.w.) yupo pamoja nao.

(3) Waislamu wanahimizwa waangalie walikotoka na wawahurumie walioko chini yao kihali na kiumri pia.

(4) Allah (s.w.) pekee ndiye anayedhibiti hali zote na ana uwezo kubadili hali moja hadi nyingine wakati wowote apendao. Kwa mfano alimkuta Muhammad (s.a.w) yatima akampa malezi mazuri, akamkuta fakiri akamtajirisha na akamkuta hajui kuongoza akampa mwongozo. Hivyo tunatakiwa tumtegemee Allah (s.w.) na tutake msaada kwake pekee.

(5) Waislamu tuna wajibu wa kumshukuru Allah (s.w.) kwa kila neema tuipatayo na njia bora ya kushukuru neema ni kuitumia neema hiyo kwa mujibu wa maagizo ya Allah (s.w.)

(6)Kilele cha kushukuru neema za Allah(SW) ni kumwabudu inavyostahiki na kusimamisha Dini yake katika jamii kwa mali na nguvu zetu alizoturuzuku.

Makka

# Suratul-Layl (92)

Ina aya 21

| Tafsiri | aya |
|---|---|
| Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehma, Mwenye Kurehemu. | بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ |
| 1. Naapa kwa usiku ufunikapo (kila kitu). | وَٱلَّيۡلِ إِذَا يَغۡشَىٰ ١ |
| 2. Na kwa mchana uangazapo. | وَٱلنَّهَارِ إِذَا تَجَلَّىٰ ٢ |
| 3. Na kwa Aliyeumba kiume na kike. | وَمَا خَلَقَ ٱلذَّكَرَ وَٱلۡأُنثَىٰٓ ٣ |
| 4. Kuwa amali zenu ni mbali mbali (na jaza yenu itakuwa mbalimbali). | إِنَّ سَعۡيَكُمۡ لَشَتَّىٰ ٤ |
| 5. Yule anayetoa (zaka, sadaka, na vinginevyo) na kumcha Allah. | فَأَمَّا مَنۡ أَعۡطَىٰ وَٱتَّقَىٰ ٥ |
| 6. Na kusadiki jambo jema (na akalifuata). | وَصَدَّقَ بِٱلۡحُسۡنَىٰ ٦ |
| 7. Tutamsahilishia njia ya kuendea Peponi. | فَسَنُيَسِّرُهُۥ لِلۡيُسۡرَىٰ ٧ |
| 8. Na afanyae ubakhili, asiwe na haja ya viumbe wenzake. | وَأَمَّا مَنۢ بَخِلَ وَٱسۡتَغۡنَىٰ ٨ |
| 9. Na akakadhibisha mambo mema (asiyafanye). | وَكَذَّبَ بِٱلۡحُسۡنَىٰ ٩ |
| 10. Tutamsahilishia njia ya kwendea Motoni. | فَسَنُيَسِّرُهُۥ لِلۡعُسۡرَىٰ ١٠ |
| 11. Na mali yake hayatamfaa wakati anadidimia (Motoni humo). | وَمَا يُغۡنِي عَنۡهُ مَالُهُۥٓ إِذَا تَرَدَّىٰٓ ١١ |

| | |
|---|---|
| 12. Ni juu yetu (kuwabainishia viumbe) njia ya kheri na njia ya shari. | إِنَّ عَلَيْنَا لَلْهُدَىٰ ١٢ |
| 13. Na ni Yetu sisi Akhera na Dunia. | وَإِنَّ لَنَا لَلْآخِرَةَ وَالْأُولَىٰ ١٣ |
| 14. Basi anakuhadharisheni na moto uwakao (kwa nguvu). | فَأَنذَرْتُكُمْ نَارًا تَلَظَّىٰ ١٤ |
| 15. Hatauingia ila muovu. | لَا يَصْلَاهَا إِلَّا الْأَشْقَى ١٥ |
| 16. Anayekadhibisha na kuipa mgongo (hii dini ya haki). | الَّذِي كَذَّبَ وَتَوَلَّىٰ ١٦ |
| 17.Na amchaye (Allah) ataepushwa nao. | وَسَيُجَنَّبُهَا الْأَتْقَى ١٧ |
| 18. Ambaye hutoa mali yake kwa ajili ya kujitakasa. | الَّذِي يُؤْتِي مَالَهُ يَتَزَكَّىٰ ١٨ |
| 19. Na hali ya kuwa hakuna yeyote aliyemfanyia Ihsani ili awe amemlipa. | وَمَا لِأَحَدٍ عِندَهُ مِن نِّعْمَةٍ تُجْزَىٰ ١٩ |
| 20. Isipokuwa (anafanya haya) kwa kutaka radhi ya Mola mtukufu. | إِلَّا ابْتِغَاءَ وَجْهِ رَبِّهِ الْأَعْلَىٰ ٢٠ |
| 21. Basi atapata la kumridhisha. | وَلَسَوْفَ يَرْضَىٰ ٢١ |

**Ujumbe wa Suratul-Layl**

Baada ya kupitia Sura hii kwa makini tunapata ujumbe ufuatao:

(1) Kila mtu atalipwa kutokana na amali yake aliyoitanguliza.

(2) Wenye kumcha Allah (s.w.) kwa kutekeleza maamrisho yake yote kama vile kusimamisha Swala, kutoa Zakat, n.k. na kuwatendea wema viumbe, Allah (s.w.) atawarahisishia njia ya kwenda peponi.

(3) Wenye kumkadhibisha Allah (s.w.) kwa kuvunja amri zake kama vile kutosimamisha Swala, kutotoa Zakat n.k. na kutowajali na kuwadhulumu wanaadamu wenzao, Allah (s.w.) atawarahisishia njia ya kwenda Motoni.

(4) Hapana yeyote atakayeweza kujikomboa au kukombolewa na

yeyote kutokana na adhabu ya Allah (s.w.). Hivyo Muislamu hana budi kujiokoa na adhabu ya Allah (s.w.) kwa kujitahidi kufanya mema na kujitahidi kujiepusha na maovu. Tunakumbushwa katika Qur'an:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓا۟ أَنفِقُوا۟ مِمَّا رَزَقْنَٰكُم مِّن قَبْلِ أَن يَأْتِىَ
يَوْمٌ لَّا بَيْعٌ فِيهِ وَلَا خُلَّةٌ وَلَا شَفَٰعَةٌ ۗ وَٱلْكَٰفِرُونَ هُمُ ٱلظَّٰلِمُونَ

*"Enyi mlioamini! Toeni katika vile tulivyokupeni kabla haijafika siku ambayo hapatakuwa kujikomboa wala urafiki (wa kusaidiana) wala waombezi. Na waliokufuru ndio waliojidhulumu (kweli kweli). (2:254).*

(5) Allah (s.w.) ndiye pekee anayestahiki kumuwekea mwanaadamu mwongozo wa maisha kwa sababu ndiye Muumbaji pekee wa ulimwengu na vyote vilivyomo na ndiye Muumba na mmiliki pekee wa akhera.

Makka

## Suratush-Shams (91)

Ina aya 15

| Tafsiri | aya |
|---|---|
| Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehma, Mwenye Kurehemu. | بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ |
| 1. Naapa kwa jua na kwa muangaza wake. | وَٱلشَّمْسِ وَضُحَىٰهَا ﴿١﴾ |
| 2. Na kwa mwezi unapoliandama. | وَٱلْقَمَرِ إِذَا تَلَىٰهَا ﴿٢﴾ |
| 3. Na mchana unapolidhihirisha. | وَٱلنَّهَارِ إِذَا جَلَّىٰهَا ﴿٣﴾ |
| 4. Na kwa usiku unapolifunika. | وَٱلَّيْلِ إِذَا يَغْشَىٰهَا ﴿٤﴾ |
| 5. Na kwa mbingu na kwa Aliyezijenga. | وَٱلسَّمَآءِ وَمَا بَنَىٰهَا ﴿٥﴾ |
| 6. Na kwa ardhi na Aliyeitandaza. | وَٱلْأَرْضِ وَمَا طَحَىٰهَا ﴿٦﴾ |
| 7. Na kwa Nafsi na Aliyezitengeneza. | وَنَفْسٍ وَمَا سَوَّىٰهَا ﴿٧﴾ |
| 8. Kisha Akaifahamisha uovu wake na wema wake. | فَأَلْهَمَهَا فُجُورَهَا وَتَقْوَىٰهَا ﴿٨﴾ |

| | |
|---|---|
| 9. Bila shaka amefaulu aliyetakasa (nafsi yake). | قَدْ أَفْلَحَ مَن زَكَّىٰهَا ﴿٩﴾ |
| 10. Na bila shaka amejihasiri aliyeiviza (nafsi yake). | وَقَدْ خَابَ مَن دَسَّىٰهَا ﴿١٠﴾ |
| 11. Kina Thamudi walikadhibisha kwa sababu ya upotofu wao. | كَذَّبَتْ ثَمُودُ بِطَغْوَىٰهَآ ﴿١١﴾ |
| 12. Aliposimama muovu wao mkubwa (ili kumchi nja huyo ngamia wa miujiza). | إِذِ ٱنۢبَعَثَ أَشْقَىٰهَا ﴿١٢﴾ |
| 13. Hapo Mtume wa Allah aliwaambia, “(Huyu) ni ngamia wa Allah (s.w.) (muacheni) na kinywaji chake, (msimzuilie maji wala msimuue).” | فَقَالَ لَهُمْ رَسُولُ ٱللَّهِ نَاقَةَ ٱللَّهِ وَسُقْيَٰهَا ﴿١٣﴾ |
| 14. Lakini walimkadhibisha (huyo Mtume, Nabii Saleh) na wakamuua (huyo ngamia), kwa hiyo Mola wao, aliwaangamiza kwa sababu ya dhambi zao na Akawafuta kabisa. | فَكَذَّبُوهُ فَعَقَرُوهَا فَدَمْدَمَ عَلَيْهِمْ رَبُّهُم بِذَنۢبِهِمْ فَسَوَّىٰهَا ﴿١٤﴾ |
| 15. Wala haogopi matokeo yake. | وَلَا يَخَافُ عُقْبَٰهَا ﴿١٥﴾ |

**Ujumbe wa Suratush-Shams**

Baada ya kuisoma sura hii na tafsiri yake kwa makini tunapata ujumbe ufuatao:

(1) Allah (s.w.) ana haki ya kuapia chochote katika viumbe vyake. Lakini sisi viumbe hatuna hiari kuapia chochote ila tuape kwa jina la Allah tu kama inabidi.

(2) Viapo katika Qur'an vinasisitiza habari inayofuatia. Katika sura hii Allah (s.w.) ameapia jua na mwangaza wake, mwezi, mchana na usiku, mbingu na yule aliyezijenga ardhi na yule aliyeitandaza, nafsi na yule aliyeitengeneza na kuiongoza, kuwa vitu hivi na Yeye mwenyewe shahidi kuwa:

(a) Bila shaka amefaulu yule anayeitakasa nafsi yake kwa kufanya

mema kwa kufuata maamrisho yote ya Allah(s.w) na kuacha makatazo yake yote na kisha akaishi na watu kwa wema.

(b) Bila shaka amefeli yule aliyeihasirisha nafsi yake kwa kuamua kumuasi Mola wake kwa kuvunja amri zake.

(3) Wale wote wanaomkadhibisha Allah (s.w.) na Mitume wake watapata adhabu kali hapa hapa duniani na huko Akhera wanasubiriwa na adhabu kali zaidi.

(4) Allah (s.w.) anapohukumia jambo hajishauri wala hashauriani na yeyote bali hutekeleza hivyo hivyo. Yeye Allah (s.w.) hamchelei yeyote wala chochote. Yeye ni muweza juu ya kila kitu.

## Makka — Suratul-Balad (90) — Ina aya 20

| Tafsiri | aya |
|---|---|
| Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehma Mwenye kurehemu. | بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ |
| 1. Naapa kwa mji huu wa (Makka). | لَآ أُقۡسِمُ بِهَٰذَا ٱلۡبَلَدِ ١ |
| 2. Nawe utashuka (utateremka) katika Mji huu (ambao wamekutoa na utahalalishiwa). | وَأَنتَ حِلُّۢ بِهَٰذَا ٱلۡبَلَدِ ٢ |
| 3. (Na naapa) kwa kila kilichozaa na kile kilichozaliwa. | وَوَالِدٖ وَمَا وَلَدَ ٣ |
| 4.Kuwa Tumemuumba mwanadamu katika taabu. | لَقَدۡ خَلَقۡنَا ٱلۡإِنسَٰنَ فِى كَبَدٍ ٤ |
| 5. Je! Anadhani ya kuwa hakuna yeyote atakaye weza (kumtia mkononi)? | أَيَحۡسَبُ أَن لَّن يَقۡدِرَ عَلَيۡهِ أَحَدٞ ٥ |
| 6. Anasema, Nimeharibu mali nyingi (kwa ajili ya kupinga Uislmu). | يَقُولُ أَهۡلَكۡتُ مَالٗا لُّبَدًا ٦ |
| 7. Je! Anadhani yakuwa hakuna yeyote amuonaye? (Allah anamuona atamlipa). | أَيَحۡسَبُ أَن لَّمۡ يَرَهُۥٓ أَحَدٌ ٧ |
| 8. Je! Hakumpa macho mawili? | أَلَمۡ نَجۡعَل لَّهُۥ عَيۡنَيۡنِ ٨ |

| | |
|---|---|
| 9. Na ulimi na midomo miwili? | وَلِسَانًا وَشَفَتَيْنِ ﴿٩﴾ |
| 10. Na tukambainishia zote njia mbili (aliyemwema na mbaya)? | وَهَدَيْنَٰهُ ٱلنَّجْدَيْنِ ﴿١٠﴾ |
| 11. Je! Ameukata huo Mlima (njia nzito ya kumfikisha Peponi). | فَلَا ٱقْتَحَمَ ٱلْعَقَبَةَ ﴿١١﴾ |
| 12. Na nini kitakachokujulisha huo mlima (njia ya kukufikisha peponi). | وَمَآ أَدْرَىٰكَ مَا ٱلْعَقَبَةُ ﴿١٢﴾ |
| 13. (Kuukata mlima huo) ni kumpa mtumwa uungwana. | فَكُّ رَقَبَةٍ ﴿١٣﴾ |
| 14. Au kumlisha siku ya njaa. | أَوْ إِطْعَٰمٌ فِى يَوْمٍ ذِى مَسْغَبَةٍ ﴿١٤﴾ |
| 15.Yatima aliye jamaa (na asiyekuwa jamaa). | يَتِيمًا ذَا مَقْرَبَةٍ ﴿١٥﴾ |
| 16. Au masikini aliye hohe hahe. | أَوْ مِسْكِينًا ذَا مَتْرَبَةٍ ﴿١٦﴾ |
| 17. Kisha awe miongoni mwa walioamini, na wakausiana kusubiri na wakausiana kuhurumiana. | ثُمَّ كَانَ مِنَ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ وَتَوَا<br>صَوْا۟ بِٱلصَّبْرِ وَتَوَاصَوْا۟ بِٱلْمَرْحَمَةِ |
| 18. Hao ndio watu wa upande wa kheri. | أُو۟لَٰٓئِكَ أَصْحَٰبُ ٱلْمَيْمَنَةِ ﴿١٨﴾ |
| 19. Lakini waliokanusha Aya Zetu, hao ndio watu wa upande wa shari. | وَٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ بِـَٔايَٰتِنَا هُمْ أَصْحَٰبُ<br>ٱلْمَشْـَٔمَةِ ﴿١٩﴾ |
| 20. Moto uliofungiwa (kila upande) utakuwa juu yao. | عَلَيْهِمْ نَارٌ مُّؤْصَدَةٌۢ ﴿٢٠﴾ |

**Ujumbe wa Suratul-Balad**

Baada ya kuipitia sura hii kwa makini tunapata ujumbe ufuataο:

(1) Allah (s.w.) anatufahamisha kuwa mwanaadamu ameumbwa katika taabu. Yaani hatapata chochote katika mahitaji yake mpaka akitafute kwa taabu na mashaka. Hapati riziki mpaka aitafute, hapati elimu mpaka

aitafute na hapati chochote mpaka akihangaikie kwa bidii na uvumilivu mkubwa. Hii ndio hali halisi ya maumbile.

(2) Allah(s.w) amempa mwanaadamu akili na vipawa vya fahamu kisha akampa mwongozo kupitia kwa Mitume wake na vitabu vyake, unao bainisha njia ya kheri na njia ya shari.

(4) Mbele ya Allah (s.w.) ubora wa mtu haupimwi kwa kuwa na mali nyingi na kuwa na vitu vingi vya kifahari. Bali wabora mbele ya Allah (s.w.) ni wale waumini wanaotumia vile Allah (s.w.) alivyowaruzuku katika kuwahurumia wanaadamu wenzao kama vile kuwakomboa watumwa. Kisha wawe ni wenye subira na wawe wanawausia wengine kusubiri na kuhurumiana. Wabora hawa ndio watu wa kheri na watastahiki kutoka kwa Mola wao malipo mema hapa duniani na huko Akhera.

(5) Wenye kukanusha aya za Allah (s.w.) kwa kukataa kufuata mwongozo wake na wakawa ni wenye kutakakabari kwa mali walizonazo na vinginevyo walivyoruzukiwa na Allah(s.w) wakawa hawana haja na viumbe wenzao, watakuwa ni watu wa upande wa shari na watastahiki adhabu kali ya moto wa Jahannamu.

Makka

## Suratul-Fajir (89)

Ina aya 30

| Tafsiri | aya |
|---|---|
| Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehma, Mwenye Kurehemu. | بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ |
| 1. Naapa kwa Alfajir. | وَٱلۡفَجۡرِ ١ |
| 2. Na kwa masiku kumi. | وَلَيَالٍ عَشۡرٖ ٢ |
| 3. Na kwa “Shufwa na Witiri” | وَٱلشَّفۡعِ وَٱلۡوَتۡرِ ٣ |
| 4. Na kwa usiku unapopita. | وَٱلَّيۡلِ إِذَا يَسۡرِ ٤ |
| 5. (Naapa nasema) kuwa kuna katika haya (kuonekana) kiapo kwa mwenye akili (anaiogopa). | هَلۡ فِي ذَٰلِكَ قَسَمٞ لِّذِي حِجۡرٍ ٥ |
| 6. Je! Hukuona jinsi Mola wako alivyowafanya Adi (Iram). | أَلَمۡ تَرَ كَيۡفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِعَادٍ ٦ |

| | |
|---|---|
| 7. (Adi) Iram (waliokuwa) wana majumba marefu marefu. | إِرَمَ ذَاتِ ٱلْعِمَادِ ﴿٧﴾ |
| 8. Ambao hawakuumbwa mfano wao katika miji (mingine). | ٱلَّتِى لَمْ يُخْلَقْ مِثْلُهَا فِى ٱلْبِلَـٰدِ ﴿٨﴾ |
| 9. Na Thamudi waliochonga majabali (wakayafanya majumba) katika uwanja (wao). | وَثَمُودَ ٱلَّذِينَ جَابُوا۟ ٱلصَّخْرَ بِٱلْوَادِ ﴿٩﴾ |
| 10. Na Firauni mwenye majumba kama vigingi (Pyramids zilizoko Misri mpaka leo). | وَفِرْعَوْنَ ذِى ٱلْأَوْتَادِ ﴿١٠﴾ |
| 11. Ambao walifanya maovu katika miji. | ٱلَّذِينَ طَغَوْا۟ فِى ٱلْبِلَـٰدِ ﴿١١﴾ |
| 12. Kisha walizidisha humo mambo maovu | فَأَكْثَرُوا۟ فِيهَا ٱلْفَسَادَ ﴿١٢﴾ |
| 13. Kwa hivyo Mola wako aliwapiga mjeledi mmoja tu wa adhabu. | فَصَبَّ عَلَيْهِمْ رَبُّكَ سَوْطَ عَذَابٍ ﴿١٣﴾ |
| 14. Hakika Mola wako yuko katika malindizo! | إِنَّ رَبَّكَ لَبِٱلْمِرْصَادِ ﴿١٤﴾ |
| 15. Lakini mwanadamu, Mola wake anapomfanyia mtihani Akamtukuza na kumneemesha, basi husema, “Mola wangu amenitukuza”, (wala hajishughulishi kufanya mema ili kutengeneza Akhera yake). | فَأَمَّا ٱلْإِنسَـٰنُ إِذَا مَا ٱبْتَلَىٰهُ رَبُّهُۥ فَأَكْرَمَهُۥ وَنَعَّمَهُۥ فَيَقُولُ رَبِّىٓ أَكْرَمَنِ ﴿١٥﴾ |
| 16. Na Anapomfanyia mtihani Akampunguzia riziki yake, husema; “Mola wangu amenidhalilisha. | وَأَمَّآ إِذَا مَا ٱبْتَلَىٰهُ فَقَدَرَ عَلَيْهِ رِزْقَهُۥ فَيَقُولُ رَبِّىٓ أَهَـٰنَنِ ﴿١٦﴾ |
| 17. Sivyo hivyo (mnavyodhania) Bali nyinyi (matajiri) hamuwatazami mayatima kwa jicho la huruma. | كَلَّا ۖ بَل لَّا تُكْرِمُونَ ٱلْيَتِيمَ ﴿١٧﴾ |
| 18.Wala hamjihimizi (wala kuhimiza wengine) kulisha maskini. | وَلَا تَحَـٰٓضُّونَ عَلَىٰ طَعَامِ ٱلْمِسْكِينِ ﴿١٨﴾ |

| | |
|---|---|
| 19. Na mnakula urithi ulaji wa pupa. | وَتَأْكُلُونَ ٱلتُّرَاثَ أَكْلًا لَّمًّا ﴿١٩﴾ |
| 20. Na mnapenda mali pendo la kupita kiasi. | وَتُحِبُّونَ ٱلْمَالَ حُبًّا جَمًّا ﴿٢٠﴾ |
| 21. Sivyo hivyo (Kumbukeni) itakapovunjwa ardhi vipande vipande. | كَلَّآ إِذَا دُكَّتِ ٱلْأَرْضُ دَكًّا دَكًّا ﴿٢١﴾ |
| 22. Na kufika (amri ya) Mola wako na Malaika safusafu. | وَجَآءَ رَبُّكَ وَٱلْمَلَكُ صَفًّا صَفًّا ﴿٢٢﴾ |
| 23. Basi siku hiyo italetwa Jahanamu. Siku hiyo Mwanadamu atakumbuka, lakini kukumbuka huko kutamfaa nini? | وَجِاْىٓءَ يَوْمَئِذٍۭ بِجَهَنَّمَ ۚ يَوْمَئِذٍ يَتَذَكَّرُ ٱلْإِنسَٰنُ وَأَنَّىٰ لَهُ ٱلذِّكْرَىٰ ﴿٢٣﴾ |
| 24. Atasema, “Laiti ningelitanguliza (wema) kwa ajili ya Uhai wangu (huu wa leo). | يَقُولُ يَٰلَيْتَنِى قَدَّمْتُ لِحَيَاتِى ﴿٢٤﴾ |
| 25. Basi siku hiyo hata adhibu yeyote namna ya kuadhibu kwake (Allah). | فَيَوْمَئِذٍ لَّا يُعَذِّبُ عَذَابَهُۥٓ أَحَدٌ ﴿٢٥﴾ |
| 26. Na wala hatafunga yeyote jinsi ya kufunga kwake (Allah). | وَلَا يُوثِقُ وَثَاقَهُۥٓ أَحَدٌ ﴿٢٦﴾ |
| 27. Ewe nafsi yenye kutua! | يَٰٓأَيَّتُهَا ٱلنَّفْسُ ٱلْمُطْمَئِنَّةُ ﴿٢٧﴾ |
| 28. Rudi kwa Mola wako, hali yakuwa utaridhika (kwa utakayoyapata), na Allah aridhike na wewe. | ٱرْجِعِىٓ إِلَىٰ رَبِّكِ رَاضِيَةً مَّرْضِيَّةً ﴿٢٨﴾ |
| 29. Basi ingia katika kundi la waja wangu (wema). | فَٱدْخُلِى فِى عِبَٰدِى ﴿٢٩﴾ |
| 30. Uingie katika Pepo Yangu. | وَٱدْخُلِى جَنَّتِى ﴿٣٠﴾ |

**Ujumbe wa Suratul-Fajr**

Suratul-Fajr inatupa mafundisho yafuatayo:

(1) Pamoja na alama nyingi zinazothibitisha kuwepo Allah (s.w.), historia ya mwanaadamu ni dalili nyingine inayothibitisha ukweli huu. Mataifa ya Adi, Thamudi na ufalme wa Firauni yalikuwa na teknolojia ya hali ya juu katika ujenzi na mambo mengineyo. Wakuu wake walitakabari na kujifanya miungu badala ya Allah (s.w.). Lakini pamoja na uwezo wao huo, Allah (s.w.) alipoamua kuwatia mkononi, hawakufurukuta hata chembe. Wakawa ni wenye kufutika katika ardhi kama kwamba hawajakuwepo.

(2) Tutumie uwezo wa vipawa tulivyonavyo katika kumcha Allah (s.w.) kwa kufuata maamrisho yake na kuacha makatazo yake na katika kusimamisha dini yake. Tukifanya hivyo tutakuwa ni wenye shukrani na tutastahiki kupata radhi za Allah (s.w.).

(3) Mwanaadamu anaponeemeshwa na kutukuzwa na Mola wake, yuko katika mtihani, kwamba je, atamshukuru Mola wake kwa kutumia neema hiyo kwa ajili ya kumridhisha Allah (s.w.) kwa kuwapa masikini, yatima na kadhalika, au atatakabari kwa neema hiyo na kuitumia apendavyo na kuwa sababu ya kumzamisha katika maasi.

(4) Pia mwanaadamu anapopunguziwa rizki na Mola wake yuko mtihanini, kwamba, je atakata tamaa na Rehma za Allah (s.w.) na kuona kuwa kwakuwa Allah (s.w.) amempunguzia rizki hana haja ya kumuabudu inavyostahiki na akaishia kwenye kumuasi na kumshirikisha na miungu mingine. Hivyo inatakiwa muumini aridhike na kila hali inayomkuta. Akipata ashukuru aseme ***"Al-Hamdulillahi"*** na akikosa ashukuru vile vile aseme ***"Al-Hamdulillah Alaakulli haali"***

(5) Tujitahidi kutumia kila fursa tuliyonayo katika kumcha Allah (s.w.) katika maisha yetu yote ya hapa ulimwenguni ili tusije jutia fursa hizo, na tustahiki kuwa miongoni mwa wale watakaokaribishwa peponi na kuwa katika radhi za Allah (s.w.).

(6) Hatuna budi kuigopa adhabu ya Allah (s.w.) kwa kujitahidi kufanya mema na kujiepusha na maovu. Adhabu yake ni kali sana na hapana mfano wake. Pamoja na kujitahidi kujiepusha na adhabu ya Allah (s.w.),vile vile waja wa Allah(s.w) wanatakiwa waombe mara kwa mara kwa kusema:

رَبَّنَا ٱصْرِفْ عَنَّا عَذَابَ جَهَنَّمَ ۖ إِنَّ عَذَابَهَا كَانَ غَرَامًا ﴿٦٥﴾ إِنَّهَا
سَآءَتْ مُسْتَقَرًّا وَمُقَامًا ﴿٦٦﴾

*"...Mola wetu! Tuondolee adhabu ya Jahannamu, bila shaka adhabu yake ni yenye kuendelea. Hakika hiyo (Jahannamu) ni kituo kibaya na mahali (pabaya kabisa) pa kukaa". (25:65-66)*

Makka **Suratul-Ghaashiyah(88)** Ina aya 26

| Tafsiri | aya |
|---|---|
| Kwa Jina la Allah (s.w.) Mwingi wa Rehma Mwenye kurehemu. | بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَـٰنِ ٱلرَّحِيمِ |
| 1. Je! Imekuwasilia habari ya msiba utakaowafudikiza (viumbe). | هَلْ أَتَىٰكَ حَدِيثُ ٱلْغَـٰشِيَةِ ﴿١﴾ |
| 2. Nyuso siku hiyo ni zenye kudhalilika. | وُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ خَـٰشِعَةٌ ﴿٢﴾ |
| 3. Ni zenye kufanya kazi ngumu kabisa (huko motoni) zichoke (kuchoka kusikokuwa na mfano). | عَامِلَةٌ نَّاصِبَةٌ ﴿٣﴾ |
| 4.Waingie katika Moto uwakao kweli kweli. | تَصْلَىٰ نَارًا حَامِيَةً ﴿٤﴾ |
| 5. Watanyweshwa (humo) katika chemchem zichemkazo barabara. | تُسْقَىٰ مِنْ عَيْنٍ ءَانِيَةٍ ﴿٥﴾ |
| 6. Hawatakuwa na chakula isipokuwa cha miiba. | لَّيْسَ لَهُمْ طَعَامٌ إِلَّا مِن ضَرِيعٍ ﴿٦﴾ |
| 7. Hakinenepeshi wala hakiondoi njaa. | لَّا يُسْمِنُ وَلَا يُغْنِى مِن جُوعٍ ﴿٧﴾ |
| 8. Nyuso (nyingine) siku hiyo ni zenye kumemetuka. | وُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ نَّاعِمَةٌ ﴿٨﴾ |
| 9. Zitakuwa radhi kwa ajili ya amali zao. | لِّسَعْيِهَا رَاضِيَةٌ ﴿٩﴾ |
| 10. Zitakuwamo katika Pepo iliyotukufu. | فِى جَنَّةٍ عَالِيَةٍ ﴿١٠﴾ |
| 11. Hazitasikia humo yasiyo na maana. | لَّا تَسْمَعُ فِيهَا لَـٰغِيَةً ﴿١١﴾ |

| | |
|---|---|
| 12. Humo muna chemchem zinazotiririka (kwa vizuri). | فِيهَا عَيْنٌ جَارِيَةٌ ﴿١٢﴾ |
| 13. Humo mna viti vya fahari vilivyoinuka juu. | فِيهَا سُرُرٌ مَّرْفُوعَةٌ ﴿١٣﴾ |
| 14. Na glasi zilizowekwa (vizuri). | وَأَكْوَابٌ مَّوْضُوعَةٌ ﴿١٤﴾ |
| 15. Na matakia yaliyopangwa safusafu. | وَنَمَارِقُ مَصْفُوفَةٌ ﴿١٥﴾ |
| 16. Na mazulia yaliyotandikwa vizuri vizuri. | وَزَرَابِيُّ مَبْثُوثَةٌ ﴿١٦﴾ |
| 17. Je! hawatazami ngamia jinsi alivyoumbwa? | أَفَلَا يَنظُرُونَ إِلَى ٱلْإِبِلِ كَيْفَ خُلِقَتْ ﴿١٧﴾ |
| 18. Na mbingu jinsi zilivyoinuliwa? | وَإِلَى ٱلسَّمَآءِ كَيْفَ رُفِعَتْ ﴿١٨﴾ |
| 19. Na milima jinsi ilivyothibitishwa? | وَإِلَى ٱلْجِبَالِ كَيْفَ نُصِبَتْ ﴿١٩﴾ |
| 20. Na ardhi jinsi ilivyotandazwa | وَإِلَى ٱلْأَرْضِ كَيْفَ سُطِحَتْ ﴿٢٠﴾ |
| 21. Basi kumbusha, hakika wewe ni mkumbushaji (tu). | فَذَكِّرْ إِنَّمَآ أَنتَ مُذَكِّرٌ ﴿٢١﴾ |
| 22. Wewe si mwenye kuwateza nguvu. | لَّسْتَ عَلَيْهِم بِمُصَيْطِرٍ ﴿٢٢﴾ |
| 23. Lakini anayerudi nyuma na kukufuru. | إِلَّا مَن تَوَلَّىٰ وَكَفَرَ ﴿٢٣﴾ |
| 24. Allah (s.w.) atamuadhibu adhabu iliyo kubwa. | فَيُعَذِّبُهُ ٱللَّهُ ٱلْعَذَابَ ٱلْأَكْبَرَ ﴿٢٤﴾ |
| 25. Hakika marejeo yao ni Kwetu. | إِنَّ إِلَيْنَآ إِيَابَهُمْ ﴿٢٥﴾ |
| 26. Kisha, bila shaka, hisabu yao ni juu Yetu. | ثُمَّ إِنَّ عَلَيْنَا حِسَابَهُم ﴿٢٦﴾ |

**Ujumbe wa Suratul-Ghaashiyah**

Baada ya kuipitia kwa makini Suratul-Ghaashiyah tunajifunza yafuatayo:

(1) Motoni ni mahali pabaya kabisa pa kurejea mtu. Hivyo kila muumini wa kweli hana budi kujitahidi kujiepusha mbali na matendo yote yatakayompelekea kuingia motoni na aombe tena mara kwa mara aseme:

رَبَّنَآ ءَاتِنَا فِى ٱلدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِى ٱلْأَخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ ٱلنَّارِ

*"Mola wetu! Tupe mema duniani na (tupe) mema Akhera na utulinde na adhabu ya moto". (2:201)*

(2) Peponi ni mahali pazuri mno pa mtu kuwa ndio makazi yake ya milele. Hivyo kila muumini wa kweli hana budi kujitahidi kujiepusha na maovu na kujitahidi kutenda mema yatakayompelekea kupata radhi za Allah (s.w.) na kustahiki malipo ya Peponi.

(3) Kuna alama mbalimbali katika ardhi zinazothibitisha kuwepo kwa Allah (s.w.) miongoni mwa alama zilizotajwa ni ngamia, mbingu, milima na ardhi. Ukitafakari kitaalamu maumbile haya utaona kwa yakini kuwa Allah (s.w.) yupo na ni Muweza juu ya kila kitu.

(4) Wajibu wa Mitume na waumini ni kuwakumbusha watu juu ya kumcha Allah (s.w.). Faida ya kukumbushana ni kuwa wale walioghafilika, hutanabahi na kurejea katika ucha Mungu.

(5) Wale wanaoendelea kumuasi Allah (s.w.) hata baada ya kukumbushwa, watakuwa hawamkomoi yeyote,bali wanajidhulumu wenyewe nafsi zao na marejeo yao ni motoni kwenye adhabu kali.

## Makka — Suratul-A'alaa(87) — Ina aya 19

| Tafsiri | Aya |
|---|---|
| Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehma, Mwenye Kurehemu. | بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ |
| 1. Litukuze Jina la Mola wako aliye Mtukufu. | سَبِّحِ ٱسْمَ رَبِّكَ ٱلْأَعْلَى ﴿١﴾ |
| 2. Aliyeumba (kila kitu) akakitengeneza. | ٱلَّذِى خَلَقَ فَسَوَّىٰ ﴿٢﴾ |
| 3.Na akakikadiria (kila kimoja jambo lake) na Akakiongoza (kufanya jambo hilo). | وَٱلَّذِى قَدَّرَ فَهَدَىٰ ﴿٣﴾ |

| | |
|---|---|
| 4. Na Aliyeotesha ndisha (malisho). | وَٱلَّذِيٓ أَخۡرَجَ ٱلۡمَرۡعَىٰ ﴿٤﴾ |
| 5. Kisha Akaifanya mikavu yenye kupiga weusi. | فَجَعَلَهُۥ غُثَآءً أَحۡوَىٰ ﴿٥﴾ |
| 6. Tutakusomesha (tutakusomea) wala hutasahau. | سَنُقۡرِئُكَ فَلَا تَنسَىٰٓ ﴿٦﴾ |
| 7.Ila akipenda Mwenyezi Mungu. Yeye anajua yaliyo dhahiri na yaliyo fichika | إِلَّا مَا شَآءَ ٱللَّهُۚ إِنَّهُۥ يَعۡلَمُ ٱلۡجَهۡرَ وَمَا يَخۡفَىٰ ﴿٧﴾ |
| 8. Nasi tutakurahisishia, kutangaza dini iliyo nyepesi | وَنُيَسِّرُكَ لِلۡيُسۡرَىٰ ﴿٨﴾ |
| 9. Basi waidhisha ikiwa waadhi utafaa | فَذَكِّرۡ إِن نَّفَعَتِ ٱلذِّكۡرَىٰ ﴿٩﴾ |
| 10. Bila shaka atakumbuka mwenye kumuogopa (Allah (s.w.)). | سَيَذَّكَّرُ مَن يَخۡشَىٰ ﴿١٠﴾ |
| 11. Na mwingi wa mateso atajitenga mbali nayo hayo (mawaidha). | وَيَتَجَنَّبُهَا ٱلۡأَشۡقَى ﴿١١﴾ |
| 12. Ambaye atauingia Moto mkubwa. | ٱلَّذِي يَصۡلَى ٱلنَّارَ ٱلۡكُبۡرَىٰ ﴿١٢﴾ |
| 13. Kisha humo hatakufa wala hatakuwa hai. | ثُمَّ لَا يَمُوتُ فِيهَا وَلَا يَحۡيَىٰ ﴿١٣﴾ |
| 14. Hakika amekwishafaulu aliyejitakasa na mabaya. | قَدۡ أَفۡلَحَ مَن تَزَكَّىٰ ﴿١٤﴾ |
| 15. Akakumbuka Jina la Mola wake na akaswali. | وَذَكَرَ ٱسۡمَ رَبِّهِۦ فَصَلَّىٰ ﴿١٥﴾ |
| 16. Lakini nyinyi mnapenda zaidi maisha ya dunia. | بَلۡ تُؤۡثِرُونَ ٱلۡحَيَوٰةَ ٱلدُّنۡيَا ﴿١٦﴾ |
| 17. Hali ya kuwa akhera ni bora (zaidi kabisa) na yenye kudumu. | وَٱلۡأٓخِرَةُ خَيۡرٞ وَأَبۡقَىٰٓ ﴿١٧﴾ |
| 18. Hakika haya (mnayoambiwa humu katika Qur'an) yamo katika Vitabu vilivyotangulia. | إِنَّ هَٰذَا لَفِي ٱلصُّحُفِ ٱلۡأُولَىٰ ﴿١٨﴾ |
| 19. Vitabu vya Ibrahim na Musa . | صُحُفِ إِبۡرَٰهِيمَ وَمُوسَىٰ ﴿١٩﴾ |

.**Ujumbe wa Suratul-A'Alaa**

Suratul-A'Alaa inatupa mafunzo yafuatayo:

(1) Allah (s.w.) pekee ndiye anayestahiki kutukuzwa na kusifiwa. Yeye ndiye aliyeumba kila kitu kwa lengo na akakikadiria kila kitu jambo lake na ndiye anayekiongoza kila kitu kifikie lengo lake.

(2) Kila kilichoumbwa kitakufa. Hivyo kila muumini anatakiwa ajiandae kufa kwa kuzidisha kufanya mema na kujiepusha na maovu.

(3) Qur'an imehifadhiwa na Allah (s.w.) tangu ilivyoanza kushuka kwa Mtume (s.a.w.) mpaka hivi leo. Ahadi nyingine ya kuihifadhi Qur'an tunaipata katika aya ifuatayo:

إِنَّا نَحۡنُ نَزَّلۡنَا ٱلذِّكۡرَ وَإِنَّا لَهُۥ لَحَٰفِظُونَ ﴿٩﴾

*"Hakika Sisi ndio tulioteremsha mawaidha haya (hii Qur'an) na katika Sisi ndio tutakaoyashinda". (15:9).*

Hivyo Waislamu hawana budi kuisoma Qur'an na kuifuata vilivyo.

(4) Uislamu ni dini nyepesi kuifahamu na kuifuata. Uislamu ni dini ya maumbile inayosimamia maadili mema.

(5) Kuonya na kuwakumbusha watu juu ya kumcha Allah (s.w.) ni jambo la wajibu kwa kila Muislamu. Maonyo na makumbusho huwatanabahisha watu wanaomuogopa Allah (s.w.) wakarejea kwenye njia ya sawasawa baada ya kupotoka.

(6) Kila anayepuuza ukumbusho na akaendelea kufanya uovu atapata adhabu iumizayo.

(7) Maisha ya hapa duniani ni ya muda mfupi yenye starehe zinazopotosha na kuhadaa watu mpaka wanafikia kumsahau Muumba wao na marejeo yao ya akhera.

(8) Maisha ya Akhera ukiyalinganisha na maisha ya dunia ni bora zaidi kwa mara nyingi na ni ya kudumu milele. Kila mtu mwenye akili hatakubali kuipoteza akhera kwa thamani ndogo sana ya dunia.

(9) Dini ya Allah (s.w.) ni moja tu nayo ni Uislamu kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:


إِنَّ ٱلدِّينَ عِندَ ٱللَّهِ ٱلۡإِسۡلَٰمُۗ

*"Bila shaka dini (ya haki) mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu...". 3:19)*

وَمَن يَبْتَغِ غَيْرَ ٱلْإِسْلَـٰمِ دِينًا فَلَن يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِى
ٱلْـَٔاخِرَةِ مِنَ ٱلْخَـٰسِرِينَ ﴿٨٥﴾

*"Na anayetaka dini isiyokuwa ya Kiislamu basi haitakubaliwa kwake. Naye Akhera atakuwa katika wenye khasara (kubwa kabisa).(3:85).*

Mitume wote walikuwa Waislamu na wameletwa kuufundisha kinadharia na kimatendo.



**ZOEZI – 1**

1. Zoezi la kuhifadhi:

   (a)Kila siku wanafunzi wafanyishwe mazoezi ya kuwapima kiasi alichohifadhi katika sura zilizochaguliwa kwa darasa la tano na kudurusu sura walizotangulia kuhifadhi.

   (b)Kila siku pia wanafunzi wafanyishwe mazoezi ya kupima kiwango cheo cha kuhifadhi tafsiri ya sura zilizochaguliwa kwa darasa la tano katika muhutasari.

2.Wanafunzi wafanyishwe mazoezi ya kudonoa ujumbe kutokana na suratul-Bayyina hadi Suratul-A’alaa katika juzuu Amma.

## Sura ya Pili

# Tawhiid

**KUMUAMINI ALLAH (S.W.)**

Kuamini kuwepo kwa Allah(s.w) kunathibitishwa na dalili mbalimbali za maumbile yaliyomo mbinguni na ardhini.

Kuwepo kwa jua na kuchomozea Mashariki kila siku na kuchwea Magharibi, kutokea kwa usiku na mchana, kuogelea kwa jua, mwezi na nyota katika anga pasina kuanguka ni dalili za kuwepo kwa Allah (s.w.). Kuwepo kwa milima na mabonde, mito, bahari na maziwa, mimea na wanyama walioenea bara na baharini ni kielelezo kingine cha kudhihirisha kuwepo Allah (s.w.).

Mwanaadamu mwenyewe ni kielelezo tosha cha kuwepo Allah (s.w.) na sifa zake tukufu. Chanzo cha mwanaadamu, kukua kwake, umbile lake na sura yake, mgawanyiko wa watu katika makabila na mataifa mbalimbali, usingizi na kifo, ni dalili zilizo wazi zinazoonyesha kuwepo Allah(s.w).

Allah (s.w.) ndiye Muumba wa mbingu na ardhi na viumbe vyote vilivyomo ndani ya mbingu na ardhi. Allah (s.w.) ndiye pekee mwenye sifa za Uungu zilizokamilika. Katika kitabu hiki tutaangalia dalili nyingine inayothibitisha kuwepo Allah (s.w.) nayo ni Historia ya Mwanadamu.

**Dalili za kuwepo Allah (s.w.) kutokana na Historia ya Mwanaadamu**

Historia ya mwanaadamu imejawa na matukio yanayodhihirisha kuwepo kwa Allah (s.w.). Katika kitabu hiki tutarejea kisa cha *As-Habil-Fyl (*watu wa tembo) kinachotajwa katika Suratul-Fyl.

Katika mwaka wa 570 A.D. lilitokea tukio la ajabu huko Makka. Katika kipindi hicho Abdul Muttalib,babu yake Mtume Muhammad (s.a.w.), alikuwa ndiye kiongozi wa Makka ilipo Ka'aba. Wakati huo Yemeni ilikuwa chini

ya utawala wa Kikristo wa Uhabeshi na gavana wake aliitwa Abraha Ashram. Abraha aliona wivu kuwaona Waarabu wa Yemen wakienda Makka kuhiji kwenye Ka'aba. Kwa hiyo alijenga Kanisa kubwa na zuri akitarajia kuwa Waarabu watavutiwa kwenda kuhiji kwenye Kanisa hilo badala ya Ka'aba Makka. Waarabu walikataa kufanya hivyo. Waliendelea kwenda kuhiji kwenye Ka'aba.

Abraha alikasirika na kuandaa jeshi kubwa kwenda kuvunja Ka'aba ili Waarabu waende kuhiji Yemen. Katika jeshi lake palikuwa na tembo. Maquraish (watu wa Makka) chini ya uongozi wa Abdul-Muttalib hawakuwa na nguvu ya kupigana na jeshi la Abraha. Abdulmutalib aliwaamuru watu wake wahamie vilimani wampishe Abraha na jeshi lake watekeleze azma yao ya kuvunja Ka'aba. Abdul - Muttalib akamuambia Abraha kuwa wao hawana nguvu ya kupigana naye; wanamwachia **Allah (s.w.)** ailinde mwenyewe Ka'aba yake.

Abraha hakuweza kuvunja Ka'aba. Tembo walikataa kuisogelea na jeshi lake lilishambuliwa na ndege wadogo wadogo waliobeba vijiwe vya udongo wa kuokwa. Ndege hawa waliwashambulia askari wa jeshi la Abraha kwa vijiwe vile. Askari wengi walikufa pale pale na wengine walifia njiani.

Al-Ka'aba ilinusurika. **Allah (s.w.)** aliinusuru. Mwaka lilimotokea tukio hili la kihistoria ulijulikana kama mwaka wa tembo. Miezi michache baada ya tukio hili, Mtume (Muhammad (s.a.w.) alizaliwa. Hivyo mwaka aliozaliwa Mtume uliitwa "mwaka wa tembo". Tukio hili linaelezwa katika Suratul-Fyl kama ifuatavyo.

أَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِأَصْحَٰبِ ٱلْفِيلِ ﴿١﴾ أَلَمْ يَجْعَلْ
كَيْدَهُمْ فِى تَضْلِيلٍ ﴿٢﴾ وَأَرْسَلَ عَلَيْهِمْ طَيْرًا أَبَابِيلَ ﴿٣﴾
تَرْمِيهِم بِحِجَارَةٍ مِّن سِجِّيلٍ ﴿٤﴾ فَجَعَلَهُمْ كَعَصْفٍ مَّأْكُولٍۭ ﴿٥﴾

*"Je! Huoni jinsi Mola wako alivyowafanya watu wenye ndovu? Je! Hakujaalia vitimbi vyao kuharibika. Na akawapelekea ndege makundi kwa makundi wakawapiga kwa mawe ya udongo wa kuokwa. Akawafanya kama majani yaliyotafunwa". (105:1-5).*

Katika kisa hiki tunajifunza kuwa **Allah (s.w.)** yupo naye ndiye aliyeinusuru Ka'aba yake. Abraha alikuwa na uwezo wa kuivunja vunja Ka'aba mara moja. Abdul-Muttalib na watu wake walimwachia nafasi wazi. Lakini Allah(s.w) aliwachakaza kwa mashambulizi ya angani. Tukio hili ni ushahidi wa kihistoria kuwa Allah (s.w.) yupo na ana majeshi ya kila aina.

وَلِلَّهِ جُنُودُ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ ۚ وَكَانَ ٱللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا

*Na majeshi ya mbinguni na ya ardhini ni ya Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima(48:7)*

## KUAMINI MALAIKA WA ALLAH (S.W.)

### Malaika ni nani?

Malaika ni katika waja au viumbe wa Allah(SW) walioumbwa kutokana na nuru. Tunafahamishwa katika hadithi ifuatayo kuwa:

> *Aysha (r.a.) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w.) amesema: Malaika wameumbwa na nuru na majini wameumbwa kutokana na ndimi za moto na Adamu ameumbwa kwa udongo kama ilivyoelezwa kwenu (katika Qur'an).* (Muslim)

Na katika Qur,an tukufu, Allah(SW) anatubainishia kuwa, katika maumbile yao halisi, malaika ni viumbe wenye mbawa.

ٱلْحَمْدُ لِلَّهِ فَاطِرِ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ جَاعِلِ ٱلْمَلَٰٓئِكَةِ رُسُلًا أُو۟لِىٓ أَجْنِحَةٍ مَّثْنَىٰ وَثُلَٰثَ وَرُبَٰعَ ۚ يَزِيدُ فِى ٱلْخَلْقِ مَا يَشَآءُ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَىْءٍ قَدِيرٌ ﴿١﴾

*"Sifa zote njema ni za Allah, Muumba wa mbingu na ardhi. Aliyewafanya Malaika kuwa wajumbe wenye mbawa mbili-mbili, na tatu tatu, na nne nne. Huzidisha katika kuumba apendavyo. Bila shaka Allah ni Mwenye uweza juu ya kila kitu". (35:1)*

### Je, Malaika wanaishi wapi?

Katika Qur,an tunafahamishwa kuwa Malaika wanayo makazi maalumu lakini si hapa duniani. Allah(s.w) anawanukuu malaika wakisema:

وَمَا مِنَّآ إِلَّا لَهُۥ مَقَامٌ مَّعْلُومٌ ﴿١٦٤﴾ وَإِنَّا لَنَحْنُ ٱلصَّآفُّونَ ﴿١٦٥﴾ وَإِنَّا لَنَحْنُ ٱلْمُسَبِّحُونَ ﴿١٦٦﴾

*Hakuna yoyote miongoni mwetu ila anapo mahali pake mahususi. Na kwa yakini katika sisi wapo wajipangao safu. Na wako katika sisi wamtukuzao(Mwenyezi Mungu)(37:164-166)*

Kutokana na kazi zao, Malaika wengi tunaishi nao humu humu duniani na wako nasi muda wote.Kila mtu ana Malaika wawili wenye kuandika amali zake.

وَإِنَّ عَلَيْكُمْ لَحَـٰفِظِينَ ﴿١٠﴾ كِرَامًا كَـٰتِبِينَ ﴿١١﴾ يَعْلَمُونَ مَا تَفْعَلُونَ ﴿١٢﴾

*Hakika juu yenu kuna wenye kuwatunza, Malaika watukufu wenye kuandika. Wanayajua yote mnayoyatenda(82:10-12)*

Aidha, tunafahamishwa katika Qur,an kuwa kila mmoja wetu ana kundi la malaika mbele na nyuma yake.

لَهُۥ مُعَقِّبَـٰتٌ مِّنۢ بَيْنِ يَدَيْهِ وَمِنْ خَلْفِهِۦ يَحْفَظُونَهُۥ مِنْ أَمْرِ ٱللَّهِ ۗ

*Ana {kila mtu} kundi {la malaika} mbele yake na nyuma yake. Wanamlinda kwa amri ya Mwenyezi Mungu. .(13:11)*

**Kwanini hatuwaoni Malaika?**

Pengine mtu aweza akauliza kuwa kama tumezungukwa na Malaika mbele na nyuma, kulia na kushoto, kwanini basi hatuwaoni? Jibu ni kwamba, mwanadamu yupo kwenye mtihani. Mtihani wenyewe ni kufanya mema kwa kutaraji malipo ya Allah(s.w) na kuacha maovu kwa kuogopa adhabu zake.

تَبَـٰرَكَ ٱلَّذِى بِيَدِهِ ٱلْمُلْكُ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَىْءٍ قَدِيرٌ ﴿١﴾ ٱلَّذِى خَلَقَ ٱلْمَوْتَ وَٱلْحَيَوٰةَ لِيَبْلُوَكُمْ أَيُّكُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا ۚ وَهُوَ ٱلْعَزِيزُ ٱلْغَفُورُ ﴿٢﴾

*Ametukuka yule ambaye mkononi Mwake umo ufalme(wote); naye ni Mwenye uweza juu ya kila kitu. Ambaye ameumba mauti na uhai ili kukujaribuni; ni nani miongoni mwenu mwenye vitendo vizuri zaidi. Naye ni Mwenye nguvu na Mwenye msamaha(67:1-2)*

Malaika ndio wasimamizi wa mtihani huu, na wamefanywa wasionekane machoni petu ili kila mtu atumie uhuru wake wa ama kumuogopa Allah(s.w) kwa kutenda mema au kumkufuru Allah(s.w) kwa kumuasi. Lau Malaika wangelionekana, watu wengi wangelitenda mema kinafiki (ria) badala ya kufanya kwa ikhilaswi.

Mfano wake, ingekuwa kama vile watu wenye dhamira za kufanya uhalifu wanavyojidai watu wema pale wanapokuwepo askari waliovalia rasmi. Utendaji kazi wa malaika ni kama mashushushu au askari kanzu. Mtu muovu anapanga na kutenda maovu akidhani yupo peke yake, kumbe malaika wapo wanaandika. Na ndiyo maana muovu atakapoona kila jambo lake limerikodiwa, atashangaa siku ya Kiama kuwa alijulikanaje?

وَوُضِعَ ٱلْكِتَٰبُ فَتَرَى ٱلْمُجْرِمِينَ مُشْفِقِينَ مِمَّا فِيهِ وَيَقُولُونَ
يَٰوَيْلَتَنَا مَالِ هَٰذَا ٱلْكِتَٰبِ لَا يُغَادِرُ صَغِيرَةً وَلَا كَبِيرَةً إِلَّآ أَ
حْصَىٰهَا ۚ وَوَجَدُوا۟ مَا عَمِلُوا۟ حَاضِرًا ۗ وَلَا يَظْلِمُ رَبُّكَ أَحَدًا ﴿٤٩﴾

*Na madaftari yatawekwa (mbele yao). Utawaona wabaya wanayaogopa kwasababu ya yale yaliyomo; na watasema: "Ole wetu! Namna gani madaftari haya! Haliachi dogo wala kubwa ila yamelidhibiti. Na watakuta yote yale waliyoyafanya yamehudhuria hapo; na Mola wako hamdhulumu yeyote (18:49)*

**Siku mtu atakapowaona Malaika**

Kuna siku na muda maalumu ambapo kila mtu binafsi ataanza kuwaona malaika katika umbile lao halisi.

**(a) Siku ya kukata roho**

Hii ni siku na saa ambayo dakika chache baada ya hapo mtu hukata roho na kuiaga dunia. Kwa watu wema, watakuja Malaika wa kuwaliwaza:

تَتَنَزَّلُ عَلَيْهِمُ ٱلْمَلَٰٓئِكَةُ أَلَّا تَخَافُوا۟ وَلَا تَحْزَنُوا۟ وَأَبْشِرُوا۟
بِٱلْجَنَّةِ ٱلَّتِى كُنتُمْ تُوعَدُونَ ﴿٣٠﴾

*......Hao huwateremkia Malaika “Msigope wala msihuzunike, na furahini kwa pepo mliyokuwa mkiahidiwa.”{41:30-32}*

Watu wanaotenda maovu watapata mshituko mkubwa na kujawa na huzuni kubwa mno pale watakapowaona Malaika. Watasikitika sana kwa jinsi walivyokuwa wakijidanganya nafsi zao, wakatenda maovu kwa kudhania kuwa hakuna Malaika wanaorekodi matendo yao waliyokuwa wakiyafanya hadharani na mafichoni. Watafadhaika na kusema:

رَبِّ ٱرْجِعُونِ ﴿٩٩﴾ لَعَلِّىٓ أَعْمَلُ صَٰلِحًا فِيمَا تَرَكْتُ ۚ كَلَّآ ۚ
إِنَّهَا كَلِمَةٌ هُوَ قَآئِلُهَا ۖ

*....Mola wangu! Nirudishe(duniani). Ili nifanye mema sasa badala ya yale niliyoyaacha. Malaika watamwambia: "Hakika hili ni neno tu analosema yeye(mtu muovu)....(23:99-100)*

### (b) Siku ya Kiyama

Kuanzia pale mtu anapowaona malaika hakutakuwa tena na kizuizi cha kutowaona kama ilivyokuwa hapa duniani. Kuonekana Malaika siku ya kiama itakuwa ni ishara mbaya kwa watu waovu kuwa umeshafika wakati wa wao kuhukumiwa na Allah(s.w) na kuanza kutumikia adhabu za kudumu katika Moto wa Jahannam. Qur,an inatufahamisha kuwa:

يَوْمَ يَرَوْنَ ٱلْمَلَٰٓئِكَةَ لَا بُشْرَىٰ يَوْمَئِذٍ لِّلْمُجْرِمِينَ وَيَقُولُونَ
حِجْرًا مَّحْجُورًا ﴿٢٢﴾

*Siku watakayowaona Malaika haitakuwa furaha siku hiyo kwa wenye makosa; na watasema: "(Mungu) atuepushie mbali adhabu hii iliyotukabili(lakini haitawafaa kitu dua hiyo)(25:22)*

### (c) Motoni na Peponi

Malaika watahudhuria katika uwanja wa hukumu siku ya Kiyama. Kila mtu atawaona wamejipanga safu wakisubiri amri ya Mwenyezi Mungu.

يَوْمَ يَقُومُ ٱلرُّوحُ وَٱلْمَلَٰٓئِكَةُ صَفًّا ۖ لَّا يَتَكَلَّمُونَ إِلَّا مَنْ أَذِنَ
لَهُ ٱلرَّحْمَٰنُ وَقَالَ صَوَابًا ﴿٣٨﴾

*Siku ambayo zitasimama Roho na Malaika safu safu; hatasema siku hiyo ila yule ambaye(Allah) Mwingi wa rehema amempa idhini, na atasema yaliyo sawa(78:38)*

| | |
|---|---|
| 12. Humo muna chemchem zinazotiririka (kwa vizuri). | فِيهَا عَيْنٌ جَارِيَةٌ ١٢ |
| 13. Humo mna viti vya fahari vilivyoinuka juu. | فِيهَا سُرُرٌ مَّرْفُوعَةٌ ١٣ |
| 14. Na glasi zilizowekwa (vizuri). | وَأَكْوَابٌ مَّوْضُوعَةٌ ١٤ |
| 15. Na matakia yaliyopangwa safusafu. | وَنَمَارِقُ مَصْفُوفَةٌ ١٥ |
| 16. Na mazulia yaliyotandikwa vizuri vizuri. | وَزَرَابِيُّ مَبْثُوثَةٌ ١٦ |
| 17. Je! hawatazami ngamia jinsi alivyoumbwa? | أَفَلَا يَنظُرُونَ إِلَى ٱلْإِبِلِ كَيْفَ خُلِقَتْ ١٧ |
| 18. Na mbingu jinsi zilivyoinuliwa? | وَإِلَى ٱلسَّمَآءِ كَيْفَ رُفِعَتْ ١٨ |
| 19. Na milima jinsi ilivyothibitishwa? | وَإِلَى ٱلْجِبَالِ كَيْفَ نُصِبَتْ ١٩ |
| 20. Na ardhi jinsi ilivyotandazwa | وَإِلَى ٱلْأَرْضِ كَيْفَ سُطِحَتْ ٢٠ |
| 21. Basi kumbusha, hakika wewe ni mkumbushaji (tu). | فَذَكِّرْ إِنَّمَآ أَنتَ مُذَكِّرٌ ٢١ |
| 22. Wewe si mwenye kuwateza nguvu. | لَّسْتَ عَلَيْهِم بِمُصَيْطِرٍ ٢٢ |
| 23. Lakini anayerudi nyuma na kukufuru. | إِلَّا مَن تَوَلَّىٰ وَكَفَرَ ٢٣ |
| 24. Allah (s.w.) atamuadhibu adhabu iliyo kubwa. | فَيُعَذِّبُهُ ٱللَّهُ ٱلْعَذَابَ ٱلْأَكْبَرَ ٢٤ |
| 25. Hakika marejeo yao ni Kwetu. | إِنَّ إِلَيْنَآ إِيَابَهُمْ ٢٥ |
| 26. Kisha, bila shaka, hisabu yao ni juu Yetu. | ثُمَّ إِنَّ عَلَيْنَا حِسَابَهُم ٢٦ |

**Ujumbe wa Suratul-Ghaashiyah**

Baada ya kuipitia kwa makini Suratul-Ghaashiyah tunajifunza yafuatayo:

(1) Motoni ni mahali pabaya kabisa pa kurejea mtu. Hivyo kila muumini wa kweli hana budi kujitahidi kujiepusha mbali na matendo yote yatakayompelekea kuingia motoni na aombe tena mara kwa mara aseme:

رَبَّنَآ ءَاتِنَا فِى ٱلدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِى ٱلْءَاخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ ٱلنَّارِ

*"Mola wetu! Tupe mema duniani na (tupe) mema Akhera na utulinde na adhabu ya moto". (2:201)*

(2) Peponi ni mahali pazuri mno pa mtu kuwa ndio makazi yake ya milele. Hivyo kila muumini wa kweli hana budi kujitahidi kujiepusha na maovu na kujitahidi kutenda mema yatakayompelekea kupata radhi za Allah (s.w.) na kustahiki malipo ya Peponi.

(3) Kuna alama mbalimbali katika ardhi zinazothibitisha kuwepo kwa Allah (s.w.) miongoni mwa alama zilizotajwa ni ngamia, mbingu, milima na ardhi. Ukitafakari kitaalamu maumbile haya utaona kwa yakini kuwa Allah (s.w.) yupo na ni Muweza juu ya kila kitu.

(4) Wajibu wa Mitume na waumini ni kuwakumbusha watu juu ya kumcha Allah (s.w.). Faida ya kukumbushana ni kuwa wale walioghafilika, hutanabahi na kurejea katika ucha Mungu.

(5) Wale wanaoendelea kumuasi Allah (s.w.) hata baada ya kukumbushwa, watakuwa hawamkomoi yeyote,bali wanajidhulumu wenyewe nafsi zao na marejeo yao ni motoni kwenye adhabu kali.

Makka

## Suratul-A'alaa(87)

Ina aya 19

| Tafsiri | Aya |
|---|---|
| Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehma, Mwenye Kurehemu. | بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ |
| 1. Litukuze Jina la Mola wako aliye Mtukufu. | سَبِّحِ ٱسْمَ رَبِّكَ ٱلْأَعْلَى ﴿١﴾ |
| 2. Aliyeumba (kila kitu) akakitengeneza. | ٱلَّذِى خَلَقَ فَسَوَّىٰ ﴿٢﴾ |
| 3.Na akakikadiria (kila kimoja jambo lake) na Akakiongoza (kufanya jambo hilo). | وَٱلَّذِى قَدَّرَ فَهَدَىٰ ﴿٣﴾ |

| | |
|---|---|
| 4. Na Aliyeotesha ndisha (malisho). | وَٱلَّذِيٓ أَخۡرَجَ ٱلۡمَرۡعَىٰ ٤ |
| 5. Kisha Akaifanya mikavu yenye kupiga weusi. | فَجَعَلَهُۥ غُثَآءً أَحۡوَىٰ ٥ |
| 6. Tutakusomesha (tutakusomea) wala hutasahau. | سَنُقۡرِئُكَ فَلَا تَنسَىٰٓ ٦ |
| 7.Ila akipenda Mwenyezi Mungu. Yeye anajua yaliyo dhahiri na yaliyo fichika | إِلَّا مَا شَآءَ ٱللَّهُۚ إِنَّهُۥ يَعۡلَمُ ٱلۡجَهۡرَ وَمَا يَخۡفَىٰ ٧ |
| 8. Nasi tutakurahisishia, kutangaza dini iliyo nyepesi | وَنُيَسِّرُكَ لِلۡيُسۡرَىٰ ٨ |
| 9. Basi waidhisha ikiwa waadhi utafaa | فَذَكِّرۡ إِن نَّفَعَتِ ٱلذِّكۡرَىٰ ٩ |
| 10. Bila shaka atakumbuka mwenye kumuogopa (Allah (s.w.)). | سَيَذَّكَّرُ مَن يَخۡشَىٰ ١٠ |
| 11. Na mwingi wa mateso atajitenga mbali nayo hayo (mawaidha). | وَيَتَجَنَّبُهَا ٱلۡأَشۡقَى ١١ |
| 12. Ambaye atauingia Moto mkubwa. | ٱلَّذِي يَصۡلَى ٱلنَّارَ ٱلۡكُبۡرَىٰ ١٢ |
| 13. Kisha humo hatakufa wala hatakuwa hai. | ثُمَّ لَا يَمُوتُ فِيهَا وَلَا يَحۡيَىٰ ١٣ |
| 14. Hakika amekwishafaulu aliyejitakasa na mabaya. | قَدۡ أَفۡلَحَ مَن تَزَكَّىٰ ١٤ |
| 15. Akakumbuka Jina la Mola wake na akaswali. | وَذَكَرَ ٱسۡمَ رَبِّهِۦ فَصَلَّىٰ ١٥ |
| 16. Lakini nyinyi mnapenda zaidi maisha ya dunia. | بَلۡ تُؤۡثِرُونَ ٱلۡحَيَوٰةَ ٱلدُّنۡيَا ١٦ |
| 17. Hali ya kuwa akhera ni bora (zaidi kabisa) na yenye kudumu. | وَٱلۡأٓخِرَةُ خَيۡرٞ وَأَبۡقَىٰٓ ١٧ |
| 18. Hakika haya (mnayoambiwa humu katika Qur'an) yamo katika Vitabu vilivyotangulia. | إِنَّ هَٰذَا لَفِي ٱلصُّحُفِ ٱلۡأُولَىٰ ١٨ |
| 19. Vitabu vya Ibrahim na Musa . | صُحُفِ إِبۡرَٰهِيمَ وَمُوسَىٰ ١٩ |

.**Ujumbe wa Suratul-A'Alaa**

Suratul-A'Alaa inatupa mafunzo yafuatayo:

(1) Allah (s.w.) pekee ndiye anayestahiki kutukuzwa na kusifiwa. Yeye ndiye aliyeumba kila kitu kwa lengo na akakikadiria kila kitu jambo lake na ndiye anayekiongoza kila kitu kifikie lengo lake.

(2) Kila kilichoumbwa kitakufa. Hivyo kila muumini anatakiwa ajiandae kufa kwa kuzidisha kufanya mema na kujiepusha na maovu.

(3) Qur'an imehifadhiwa na Allah (s.w.) tangu ilivyoanza kushuka kwa Mtume (s.a.w.) mpaka hivi leo. Ahadi nyingine ya kuihifadhi Qur'an tunaipata katika aya ifuatayo:

إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا ٱلذِّكْرَ وَإِنَّا لَهُۥ لَحَـٰفِظُونَ ﴿٩﴾

*"Hakika Sisi ndio tulioteremsha mawaidha haya (hii Qur'an) na katika Sisi ndio tutakaoyashinda". (15:9).*

Hivyo Waislamu hawana budi kuisoma Qur'an na kuifuata vilivyo.

(4) Uislamu ni dini nyepesi kuifahamu na kuifuata. Uislamu ni dini ya maumbile inayosimamia maadili mema.

(5) Kuonya na kuwakumbusha watu juu ya kumcha Allah (s.w.) ni jambo la wajibu kwa kila Muislamu. Maonyo na makumbusho huwatanabahisha watu wanaomuogopa Allah (s.w.) wakarejea kwenye njia ya sawasawa baada ya kupotoka.

(6) Kila anayepuuza ukumbusho na akaendelea kufanya uovu atapata adhabu iumizayo.

(7) Maisha ya hapa duniani ni ya muda mfupi yenye starehe zinazopotosha na kuhadaa watu mpaka wanafikia kumsahau Muumba wao na marejeo yao ya akhera.

(8) Maisha ya Akhera ukiyalinganisha na maisha ya dunia ni bora zaidi kwa mara nyingi na ni ya kudumu milele. Kila mtu mwenye akili hatakubali kuipoteza akhera kwa thamani ndogo sana ya dunia.

(9) Dini ya Allah (s.w.) ni moja tu nayo ni Uislamu kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

إِنَّ ٱلدِّينَ عِندَ ٱللَّهِ ٱلْإِسْلَـٰمُ ۗ

*"Bila shaka dini (ya haki) mbele ya Mwenyezi Mungu ni Uislamu...". 3:19)*

وَمَن يَبْتَغِ غَيْرَ ٱلْإِسْلَٰمِ دِينًا فَلَن يُقْبَلَ مِنْهُ وَهُوَ فِى
ٱلْءَاخِرَةِ مِنَ ٱلْخَٰسِرِينَ ﴿٨٥﴾

*"Na anayetaka dini isiyokuwa ya Kiislamu basi haitakubaliwa kwake. Naye Akhera atakuwa katika wenye khasara (kubwa kabisa).(3:85).*

Mitume wote walikuwa Waislamu na wameletwa kuufundisha kinadharia na kimatendo.

**ZOEZI – 1**

1. Zoezi la kuhifadhi:

(a)Kila siku wanafunzi wafanyishwe mazoezi ya kuwapima kiasi alichohifadhi katika sura zilizochaguliwa kwa darasa la tano na kudurusu sura walizotangulia kuhifadhi.

(b)Kila siku pia wanafunzi wafanyishwe mazoezi ya kupima kiwango cheo cha kuhifadhi tafsiri ya sura zilizochaguliwa kwa darasa la tano katika muhutasari.

2.Wanafunzi wafanyishwe mazoezi ya kudonoa ujumbe kutokana na suratul-Bayyina hadi Suratul-A'alaa katika juzuu Amma.

### Sura ya Pili

# Tawhiid

**KUMUAMINI ALLAH (S.W.)**

Kuamini kuwepo kwa Allah(s.w) kunathibitishwa na dalili mbalimbali za maumbile yaliyomo mbinguni na ardhini.

Kuwepo kwa jua na kuchomozea Mashariki kila siku na kuchwea Magharibi, kutokea kwa usiku na mchana, kuogelea kwa jua, mwezi na nyota katika anga pasina kuanguka ni dalili za kuwepo kwa Allah (s.w.). Kuwepo kwa milima na mabonde, mito, bahari na maziwa, mimea na wanyama walioenea bara na baharini ni kielelezo kingine cha kudhihirisha kuwepo Allah (s.w.).

Mwanaadamu mwenyewe ni kielelezo tosha cha kuwepo Allah (s.w.) na sifa zake tukufu. Chanzo cha mwanaadamu, kukua kwake, umbile lake na sura yake, mgawanyiko wa watu katika makabila na mataifa mbalimbali, usingizi na kifo, ni dalili zilizo wazi zinazoonyesha kuwepo Allah(s.w).

Allah (s.w.) ndiye Muumba wa mbingu na ardhi na viumbe vyote vilivyomo ndani ya mbingu na ardhi. Allah (s.w.) ndiye pekee mwenye sifa za Uungu zilizokamilika. Katika kitabu hiki tutaangalia dalili nyingine inayothibitisha kuwepo Allah (s.w.) nayo ni Historia ya Mwanadamu.

**Dalili za kuwepo Allah (s.w.) kutokana na Historia ya Mwanaadamu**

Historia ya mwanaadamu imejawa na matukio yanayodhihirisha kuwepo kwa Allah (s.w.). Katika kitabu hiki tutarejea kisa cha *As-Habil-Fyl (*watu wa tembo) kinachotajwa katika Suratul-Fyl.

Katika mwaka wa 570 A.D. lilitokea tukio la ajabu huko Makka. Katika kipindi hicho Abdul Muttalib,babu yake Mtume Muhammad (s.a.w.), alikuwa ndiye kiongozi wa Makka ilipo Ka'aba. Wakati huo Yemeni ilikuwa chini

ya utawala wa Kikristo wa Uhabeshi na gavana wake aliitwa Abraha Ashram. Abraha aliona wivu kuwaona Waarabu wa Yemen wakienda Makka kuhiji kwenye Ka'aba. Kwa hiyo alijenga Kanisa kubwa na zuri akitarajia kuwa Waarabu watavutiwa kwenda kuhiji kwenye Kanisa hilo badala ya Ka'aba Makka. Waarabu walikataa kufanya hivyo. Waliendelea kwenda kuhiji kwenye Ka'aba.

Abraha alikasirika na kuandaa jeshi kubwa kwenda kuvunja Ka'aba ili Waarabu waende kuhiji Yemen. Katika jeshi lake palikuwa na tembo. Maquraish (watu wa Makka) chini ya uongozi wa Abdul-Muttalib hawakuwa na nguvu ya kupigana na jeshi la Abraha. Abdulmutalib aliwaamuru watu wake wahamie vilimani wampishe Abraha na jeshi lake watekeleze azma yao ya kuvunja Ka'aba. Abdul - Muttalib akamuambia Abraha kuwa wao hawana nguvu ya kupigana naye; wanamwachia **Allah (s.w.)** ailinde mwenyewe Ka'aba yake.

Abraha hakuweza kuvunja Ka'aba. Tembo walikataa kuisogelea na jeshi lake lilishambuliwa na ndege wadogo wadogo waliobeba vijiwe vya udongo wa kuokwa. Ndege hawa waliwashambulia askari wa jeshi la Abraha kwa vijiwe vile. Askari wengi walikufa pale pale na wengine walifia njiani.

Al-Ka'aba ilinusurika. **Allah (s.w.)** aliinusuru. Mwaka lilimotokea tukio hili la kihistoria ulijulikana kama mwaka wa tembo. Miezi michache baada ya tukio hili, Mtume (Muhammad (s.a.w.) alizaliwa. Hivyo mwaka aliozaliwa Mtume uliitwa "mwaka wa tembo". Tukio hili linaelezwa katika Suratul-Fyl kama ifuatavyo.

أَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِأَصْحَٰبِ ٱلْفِيلِ ﴿١﴾ أَلَمْ يَجْعَلْ
كَيْدَهُمْ فِى تَضْلِيلٍ ﴿٢﴾ وَأَرْسَلَ عَلَيْهِمْ طَيْرًا أَبَابِيلَ ﴿٣﴾
تَرْمِيهِم بِحِجَارَةٍ مِّن سِجِّيلٍ ﴿٤﴾ فَجَعَلَهُمْ كَعَصْفٍ مَّأْكُولٍ ﴿٥﴾

*"Je! Huoni jinsi Mola wako alivyowafanya watu wenye ndovu? Je! Hakujaalia vitimbi vyao kuharibika. Na akawapelekea ndege makundi kwa makundi wakawapiga kwa mawe ya udongo wa kuokwa. Akawafanya kama majani yaliyotafunwa". (105:1-5).*

Katika kisa hiki tunajifunza kuwa **Allah (s.w.)** yupo naye ndiye aliyeinusuru Ka'aba yake. Abraha alikuwa na uwezo wa kuivunja vunja Ka'aba mara moja. Abdul-Muttalib na watu wake walimwachia nafasi wazi. Lakini Allah(s.w) aliwachakaza kwa mashambulizi ya angani. Tukio hili ni ushahidi wa kihistoria kuwa Allah (s.w.) yupo na ana majeshi ya kila aina.

وَلِلَّهِ جُنُودُ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ ۚ وَكَانَ ٱللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا

*Na majeshi ya mbinguni na ya ardhini ni ya Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima(48:7)*

## KUAMINI MALAIKA WA ALLAH (S.W.)

**Malaika ni nani?**

Malaika ni katika waja au viumbe wa Allah(SW) walioumbwa kutokana na nuru. Tunafahamishwa katika hadithi ifuatayo kuwa:

> *Aysha (r.a.) amesimulia kuwa Mtume (s.a.w.) amesema: Malaika wameumbwa na nuru na majini wameumbwa kutokana na ndimi za moto na Adamu ameumbwa kwa udongo kama ilivyoelezwa kwenu (katika Qur'an).* (Muslim)

Na katika Qur,an tukufu, Allah(SW) anatubainishia kuwa, katika maumbile yao halisi, malaika ni viumbe wenye mbawa.

ٱلْحَمْدُ لِلَّهِ فَاطِرِ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ جَاعِلِ ٱلْمَلَٰٓئِكَةِ رُسُلًا
أُو۟لِىٓ أَجْنِحَةٍ مَّثْنَىٰ وَثُلَٰثَ وَرُبَٰعَ ۚ يَزِيدُ فِى ٱلْخَلْقِ مَا
يَشَآءُ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَىْءٍ قَدِيرٌ ﴿١﴾

*"Sifa zote njema ni za Allah, Muumba wa mbingu na ardhi. Aliyewafanya Malaika kuwa wajumbe wenye mbawa mbili-mbili, na tatu tatu, na nne nne. Huzidisha katika kuumba apendavyo. Bila shaka Allah ni Mwenye uweza juu ya kila kitu". (35:1)*

**Je, Malaika wanaishi wapi?**

Katika Qur,an tunafahamishwa kuwa Malaika wanayo makazi maalumu lakini si hapa duniani. Allah(s.w) anawanukuu malaika wakisema:

وَمَا مِنَّآ إِلَّا لَهُۥ مَقَامٌ مَّعْلُومٌ ﴿١٦٤﴾ وَإِنَّا لَنَحْنُ ٱلصَّآفُّونَ ﴿١٦٥﴾
وَإِنَّا لَنَحْنُ ٱلْمُسَبِّحُونَ ﴿١٦٦﴾

*Hakuna yoyote miongoni mwetu ila anapo mahali pake mahususi. Na kwa yakini katika sisi wapo wajipangao safu. Na wako katika sisi wamtukuzao(Mwenyezi Mungu)(37:164-166)*

Kutokana na kazi zao, Malaika wengi tunaishi nao humu humu duniani na wako nasi muda wote.Kila mtu ana Malaika wawili wenye kuandika amali zake.

وَإِنَّ عَلَيۡكُمۡ لَحَـٰفِظِينَ ١٠ كِرَامٗا كَـٰتِبِينَ ١١ يَعۡلَمُونَ مَا تَفۡعَلُونَ ١٢

*Hakika juu yenu kuna wenye kuwatunza, Malaika watukufu wenye kuandika. Wanayajua yote mnayoyatenda(82:10-12)*

Aidha, tunafahamishwa katika Qur,an kuwa kila mmoja wetu ana kundi la malaika mbele na nyuma yake.

لَهُۥ مُعَقِّبَـٰتٞ مِّنۢ بَيۡنِ يَدَيۡهِ وَمِنۡ خَلۡفِهِۦ يَحۡفَظُونَهُۥ مِنۡ أَمۡرِ ٱللَّهِۗ

*Ana {kila mtu} kundi {la malaika} mbele yake na nyuma yake. Wanamlinda kwa amri ya Mwenyezi Mungu. .(13:11)*

**Kwanini hatuwaoni Malaika?**

Pengine mtu aweza akauliza kuwa kama tumezungukwa na Malaika mbele na nyuma, kulia na kushoto, kwanini basi hatuwaoni? Jibu ni kwamba, mwanadamu yupo kwenye mtihani. Mtihani wenyewe ni kufanya mema kwa kutaraji malipo ya Allah(s.w) na kuacha maovu kwa kuogopa adhabu zake.

تَبَـٰرَكَ ٱلَّذِي بِيَدِهِ ٱلۡمُلۡكُ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيۡءٖ قَدِيرٌ ١ ٱلَّذِي خَلَقَ ٱلۡمَوۡتَ وَٱلۡحَيَوٰةَ لِيَبۡلُوَكُمۡ أَيُّكُمۡ أَحۡسَنُ عَمَلٗاۚ وَهُوَ ٱلۡعَزِيزُ ٱلۡغَفُورُ ٢

*Ametukuka yule ambaye mkononi Mwake umo ufalme(wote); naye ni Mwenye uweza juu ya kila kitu. Ambaye ameumba mauti na uhai ili kukujaribuni; ni nani miongoni mwenu mwenye vitendo vizuri zaidi. Naye ni Mwenye nguvu na Mwenye msamaha(67:1-2)*

Malaika ndio wasimamizi wa mtihani huu, na wamefanywa wasionekane machoni petu ili kila mtu atumie uhuru wake wa ama kumuogopa Allah(s.w) kwa kutenda mema au kumkufuru Allah(s.w) kwa kumuasi. Lau Malaika wangelionekana, watu wengi wangelitenda mema kinafiki (ria) badala ya kufanya kwa ikhilaswi.

Mfano wake, ingekuwa kama vile watu wenye dhamira za kufanya uhalifu wanavyojidai watu wema pale wanapokuwepo askari waliovalia rasmi. Utendaji kazi wa malaika ni kama mashushushu au askari kanzu. Mtu muovu anapanga na kutenda maovu akidhani yupo peke yake, kumbe malaika wapo wanaandika. Na ndiyo maana muovu atakapoona kila jambo lake limerikodiwa, atashangaa siku ya Kiama kuwa alijulikanaje?

وَوُضِعَ ٱلْكِتَـٰبُ فَتَرَى ٱلْمُجْرِمِينَ مُشْفِقِينَ مِمَّا فِيهِ وَيَقُولُونَ
يَـٰوَيْلَتَنَا مَالِ هَـٰذَا ٱلْكِتَـٰبِ لَا يُغَادِرُ صَغِيرَةً وَلَا كَبِيرَةً إِلَّآ أَ
حْصَىٰهَا ۚ وَوَجَدُوا۟ مَا عَمِلُوا۟ حَاضِرًا ۗ وَلَا يَظْلِمُ رَبُّكَ أَحَدًا ﴿٤٩﴾

*Na madaftari yatawekwa (mbele yao). Utawaona wabaya wanayaogopa kwasababu ya yale yaliyomo; na watasema: "Ole wetu! Namna gani madaftari haya! Haliachi dogo wala kubwa ila yamelidhibiti. Na watakuta yote yale waliyoyafanya yamehudhuria hapo; na Mola wako hamdhulumu yeyote (18:49)*

**Siku mtu atakapowaona Malaika**

Kuna siku na muda maalumu ambapo kila mtu binafsi ataanza kuwaona malaika katika umbile lao halisi.

**(a) Siku ya kukata roho**

Hii ni siku na saa ambayo dakika chache baada ya hapo mtu hukata roho na kuiaga dunia. Kwa watu wema, watakuja Malaika wa kuwaliwaza:

تَتَنَزَّلُ عَلَيْهِمُ ٱلْمَلَـٰٓئِكَةُ أَلَّا تَخَافُوا۟ وَلَا تَحْزَنُوا۟ وَأَبْشِرُوا۟
بِٱلْجَنَّةِ ٱلَّتِى كُنتُمْ تُوعَدُونَ ﴿٣٠﴾

*......Hao huwateremkia Malaika "Msigope wala msihuzunike, na furahini kwa pepo mliyokuwa mkiahidiwa."{41:30-32}*

Watu wanaotenda maovu watapata mshituko mkubwa na kujawa na huzuni kubwa mno pale watakapowaona Malaika. Watasikitika sana kwa jinsi walivyokuwa wakijidanganya nafsi zao, wakatenda maovu kwa kudhania kuwa hakuna Malaika wanaorekodi matendo yao waliyokuwa wakiyafanya hadharani na mafichoni. Watafadhaika na kusema:

رَبِّ ٱرْجِعُونِ ﴿٩٩﴾ لَعَلِّىٓ أَعْمَلُ صَٰلِحًا فِيمَا تَرَكْتُ ۚ كَلَّآ ۚ
إِنَّهَا كَلِمَةٌ هُوَ قَآئِلُهَا ۖ

*....Mola wangu! Nirudishe(duniani). Ili nifanye mema sasa badala ya yale niliyoyaacha. Malaika watamwambia: "Hakika hili ni neno tu analosema yeye(mtu muovu)....(23:99-100)*

### (b) Siku ya Kiyama

Kuanzia pale mtu anapowaona malaika hakutakuwa tena na kizuizi cha kutowaona kama ilivyokuwa hapa duniani. Kuonekana Malaika siku ya kiama itakuwa ni ishara mbaya kwa watu waovu kuwa umeshafika wakati wa wao kuhukumiwa na Allah(s.w) na kuanza kutumikia adhabu za kudumu katika Moto wa Jahannam. Qur,an inatufahamisha kuwa:

يَوْمَ يَرَوْنَ ٱلْمَلَٰٓئِكَةَ لَا بُشْرَىٰ يَوْمَئِذٍ لِّلْمُجْرِمِينَ وَيَقُولُونَ
حِجْرًا مَّحْجُورًا ﴿٢٢﴾

*Siku watakayowaona Malaika haitakuwa furaha siku hiyo kwa wenye makosa; na watasema: "(Mungu) atuepushie mbali adhabu hii iliyotukabili(lakini haitawafaa kitu dua hiyo)(25:22)*

### (c) Motoni na Peponi

Malaika watahudhuria katika uwanja wa hukumu siku ya Kiyama. Kila mtu atawaona wamejipanga safu wakisubiri amri ya Mwenyezi Mungu.

يَوْمَ يَقُومُ ٱلرُّوحُ وَٱلْمَلَٰٓئِكَةُ صَفًّا ۖ لَّا يَتَكَلَّمُونَ إِلَّا مَنْ أَذِنَ
لَهُ ٱلرَّحْمَٰنُ وَقَالَ صَوَابًا ﴿٣٨﴾

*Siku ambayo zitasimama Roho na Malaika safu safu; hatasema siku hiyo ila yule ambaye(Allah) Mwingi wa rehema amempa idhini, na atasema yaliyo sawa(78:38)*

Wakipewa amri na Allah(SW) malaika watawakamata waovu na kuwachungachunga kuelekea motoni kuadhibiwa.

وَسِيقَ ٱلَّذِينَ كَفَرُوٓا۟ إِلَىٰ جَهَنَّمَ زُمَرًا ۖ حَتَّىٰٓ إِذَا جَآءُوهَا
فُتِحَتْ أَبْوَٰبُهَا وَقَالَ لَهُمْ خَزَنَتُهَآ أَلَمْ يَأْتِكُمْ رُسُلٌ
مِّنكُمْ يَتْلُونَ عَلَيْكُمْ ءَايَـٰتِ رَبِّكُمْ وَيُنذِرُونَكُمْ لِقَآءَ
يَوْمِكُمْ هَـٰذَا ۚ

*Na waliokufuru watapelekwa katika jahannam makundi makundi mpaka watakapoifikia; itafunguliwa milango yake; walinzi wake(malaika) watawaambia: Je! hawakukujieni Mitume miongoni mwenu wakikusomeeni aya za Mola wenu na kukuonyeni juu ya makutano ya siku yenu hii(39: 71)*

Watu wema watasindikizwa na malaika mpaka kwenye pepo tukufu, na malaika wa huko watawakaribisha.

وَقَالَ لَهُمْ خَزَنَتُهَا سَلَـٰمٌ عَلَيْكُمْ طِبْتُمْ فَٱدْخُلُوهَا خَـٰلِدِينَ

*Na walinzi wake(malaika) watawaambia: Amani juu yenu, furahini, na ingieni humu mkae milele(39:73)*

### Sifa za malaika

*1.Ni viumbe watiifu wasiomuasi Allah(SW)*

Malaika ni viumbe watiifu kwa Allah(SW). Wakipewa amri ya kumuadhibu mtu muovu, hawagomi wala kumuonea huruma mtu huyo.

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ قُوٓا۟ أَنفُسَكُمْ وَأَهْلِيكُمْ نَارًا
وَقُودُهَا ٱلنَّاسُ وَٱلْحِجَارَةُ عَلَيْهَا مَلَـٰٓئِكَةٌ غِلَاظٌ شِدَادٌ
لَّا يَعْصُونَ ٱللَّهَ مَآ أَمَرَهُمْ وَيَفْعَلُونَ مَا يُؤْمَرُونَ ﴿٦﴾

*Enyi mlioamini! Ziokoeni nafsi zenu na nafsi za watu wenu na moto ambao kuni zake ni watu na mawe. Juu yake kuna Malaika wakali wenye nguvu. Hawamuasi Allah(SW) katika yale anayowaamuru, na wanatekeleza vile walivyoamrishwa.(66:6)*

*2. Wana elimu ya kutosha kutekeleza majukumu yao*

Malaika wana elimu inayowawezesha kutekeleza majukumu yao bila ya kubabaisha. Elimu waliyopewa Malaika ni sehemu ndogo sana katika ujuzi wa Allah(s.w). Na wenyewe walikiri mbele ya Allah(s.w)

قَالُوا۟ سُبْحَـٰنَكَ لَا عِلْمَ لَنَآ إِلَّا مَا عَلَّمْتَنَآ ۖ إِنَّكَ أَنتَ
ٱلْعَلِيمُ ٱلْحَكِيمُ ﴿٣٢﴾

*Wakasema: Utukufu ni wako! Hatuna elimu ila ile uliyotufundisha, bila shaka Wewe ndiye Mjuzi na Mwenye hekima(2:32)*

*3. Hawana jinsia*

Malaika hawana jinsia ya kike wala ya kiume. Qur,an inawakosoa watu wanaodhani kuwa Malaika ni wanawake. Inahoji:

وَجَعَلُوا۟ ٱلْمَلَـٰٓئِكَةَ ٱلَّذِينَ هُمْ عِبَـٰدُ ٱلرَّحْمَـٰنِ إِنَـٰثًا ۚ
أَشَهِدُوا۟ خَلْقَهُمْ ۚ سَتُكْتَبُ شَهَـٰدَتُهُمْ وَيُسْـَٔلُونَ ﴿١٩﴾

*Na wamewafanya Malaika ambao ni waja wa Mwingi wa Rehma kuwa ni wanawake. Je wameshuhudia kuumbwa kwao(43:19).*

*4. Ni viumbe wenye mbawa*

ٱلْحَمْدُ لِلَّهِ فَاطِرِ ٱلسَّمَـٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ جَاعِلِ ٱلْمَلَـٰٓئِكَةِ
رُسُلًا أُو۟لِىٓ أَجْنِحَةٍ مَّثْنَىٰ وَثُلَـٰثَ وَرُبَـٰعَ ۚ يَزِيدُ فِى
ٱلْخَلْقِ مَا يَشَآءُ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَىْءٍ قَدِيرٌ ﴿١﴾

*"Sifa zote njema ni za Allah, Muumba wa mbingu na ardhi. Aliyewafanya Malaika kuwa wajumbe wenye mbawa mbili-mbili, na tatu tatu, na nne nne. Huzidisha katika kuumba apendavyo. Bila shaka Allah ni Mwenye uweza juu ya kila kitu". (35:1)*

*5. Huweza kujimithilisha umbile la mwanaadamu*

Malaika huweza kujimithilisha kuwa kama wanadamu. Hufanya hivyo pale wanapotumwa na Allah(*s.w*)kuleta ujumbe kwa watu maalumu. Kwa mfano, Bibi Maryam mama yake nabii Isa(as), alijiwa na malaika katika umbo mithili ya mwanaume.

وَٱذۡكُرۡ فِي ٱلۡكِتَٰبِ مَرۡيَمَ إِذِ ٱنتَبَذَتۡ مِنۡ أَهۡلِهَا مَكَانٗا
شَرۡقِيّٗا ١٦ فَٱتَّخَذَتۡ مِن دُونِهِمۡ حِجَابٗا فَأَرۡسَلۡنَآ إِلَيۡهَا رُوحَنَا
إِلَيۡهَا رُوحَنَا فَتَمَثَّلَ لَهَا بَشَرٗا سَوِيّٗا ١٧

*Na mtaje katika kitabu, Maryam, alipojitenga na watu wake katika upande wa mashariki. Tukampelekea muhuisha sharia Yetu(Jibril) akajimithilisha kwake kwa sura ya binaadamu aliye kamilifu. (19:16-17)*

**Lengo la kuumbwa Malaika**

Lengo la kuumbwa malaika ni kumtumikia Allah(s.w).Katika kutekeleza lengo la kuumbwa kwao, malaika hawana hiyari katika kutekeleza amri za Allah(s.w), hufanya mambo yote vile anavyotaka Allah(s.w).

لَّا يَعۡصُونَ ٱللَّهَ مَآ أَمَرَهُمۡ وَيَفۡعَلُونَ مَا يُؤۡمَرُونَ ٦

*..Hawamuasi Allah{SW} katika yale anayowaamuru, na wanatekeleza vile walivyoamrishwa.(66:6)*

**Kazi za Malaika**

Malaika wamepewa kazi ya kumtumikia Allah(SW) kwa kumtukuza na kumtakasa, kama wanavyosema wenyewe:

وَمَا مِنَّآ إِلَّا لَهُۥ مَقَامٞ مَّعۡلُومٞ ١٦٤ وَإِنَّا لَنَحۡنُ ٱلصَّآفُّونَ ١٦٥
وَإِنَّا لَنَحۡنُ ٱلۡمُسَبِّحُونَ ١٦٦

*Hakuna yoyote miongoni mwetu ila anapo mahali pake mahususi. Na kwa yakini katika sisi wapo wajipangao safu. Na wako katika sisi wamtukuzao(Mwenyezi Mungu)(37:164-166)*

Malaika pia hushughulikia mambo ya wanadamu katika maisha ya duniani na Akhera. Miongoni mwa mambo hayo ni:

**(1) Kuleta ujumbe kwa wanaadamu kutoka kwa Allah (s.w)**

Kazi ya kwanza ya malaika ni kuleta ujumbe wa Allah(s.w) kwa wanaadamu. Ujumbe huo huweza kuwa ni mwongozo wa maisha(Wahy) au habari juu ya jambo fulani. Malaika hupeleka ujumbe wa Allah(s.w) kwa mitume au watu wa kawaida.

يُنَزِّلُ ٱلْمَلَٰٓئِكَةَ بِٱلرُّوحِ مِنْ أَمْرِهِۦ عَلَىٰ مَن يَشَآءُ مِنْ عِبَادِهِۦٓ
أَنْ أَنذِرُوٓا۟ أَنَّهُۥ لَآ إِلَٰهَ إِلَّآ أَنَا۠ فَٱتَّقُونِ ﴿٢﴾

*Huwateremsha Malaika na wahy kwa amri yake juu ya anaowataka katika waja wake kuwa "waonyeni kuwa hakuna wa kuabudiwa isipokuwa Mimi, basi niogopeni" (16:2)*

Jibril, ambaye ndiye mkuu wa Malaika, ndiye mjumbe mkuu aliyekuwa akiwaletea Mitume wote Wahyi. Yeye ni mwalimu mkuu ayeteuliwa na Allah(s.w) kuwafunza mitume namna ya kuwalingania watu Uislamu kwa maneno na matendo.

إِنَّهُۥ لَقَوْلُ رَسُولٍ كَرِيمٍ ﴿١٩﴾ ذِى قُوَّةٍ عِندَ ذِى ٱلْعَرْشِ

*Hakika hii Quran ni neno lililoletwa na mjumbe mtukufu, malaika mwenye nguvu na hadhi kubwa kwa Mwenyezi Mungu.(81:19-20)*

**(2) Kuandika amali za wanaadamu njema na mbaya.**

Kila mtu ana Malaika waandishi wawili, kulia na kushoto kwake. Unaposema au kutenda jema au baya hadharani au umejificha peke yako, malaika hawa wanakuona na kurekodi jambo hilo.

إِذْ يَتَلَقَّى ٱلْمُتَلَقِّيَانِ عَنِ ٱلْيَمِينِ وَعَنِ ٱلشِّمَالِ قَعِيدٌ ﴿١٧﴾ مَّا يَلْفِظُ
مِن قَوْلٍ إِلَّا لَدَيْهِ رَقِيبٌ عَتِيدٌ ﴿١٨﴾

*Wanapopokea wapokeaji wawili, anayekaa kuliani na anayekaa kushotoni. Hatoi (mtu)kauli yoyote isipokuwa karibu naye yupo(Malaika) tayari (kuandika.) (50-17-18).*

**(3) Kuwalinda wanaadamu.**

Kazi ya tatu ya malaika ni kumchunga na kumlinda kila mtu na vitu vya hatari vilivyo nje ya uwezo wake. Quran inatufahamisha:

لَهُۥ مُعَقِّبَٰتٌ مِّنۢ بَيْنِ يَدَيْهِ وَمِنْ خَلْفِهِۦ يَحْفَظُونَهُۥ مِنْ أَمْرِ
ٱللَّهِ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ لَا يُغَيِّرُ مَا بِقَوْمٍ حَتَّىٰ يُغَيِّرُوا۟ مَا بِأَنفُسِهِمْ ۗ وَإِذَآ
أَرَادَ ٱللَّهُ بِقَوْمٍ سُوٓءًا فَلَا مَرَدَّ لَهُۥ ۚ وَمَا لَهُم مِّن دُونِهِۦ مِن وَالٍ

*Ana (kila mtu) kundi (la malaika) mbele yake na nyuma yake. Wanamlinda kwa amri ya Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu habadili yaliyoko nafsini mwa watu mpaka wabadili wao yaliyomo katika nafsi zao. Na Mwenyezi Mungu anapowatakia watu adhabu, hakuna cha kuzuia wala hawana mlinzi yeyote badala ya Mwenyezi Mungu (13:11)*

Kwa ulinzi huu wa malaika utokao kwa Allah(s.w), mtu hata kama atachukiwa na dunia nzima na kwahiyo wakafanya njama za kutaka kumdhuru, hawataweza mpaka Allah(s.w) aondoe ulinzi wake.Vivyo hivyo, kama Allah(s.w)atauondoa ulinzi wake huu kwa mtu, hakuna wa kumkinga na shari hata kama atalindwa na mitambo madhubuti ya kisasa pamoja na wataalamu wa ulinzi wa ulimwengu mzima.

**(4) Kuwaombea waumini msamaha kwa Allah (s.w.)**

Malaika pia wana kazi ya kumwomba Allahx(s.w) awasamehe wale watu wanaotubia na kufuatisha vitendo vyema. Humwomba Allah(s.w) awasamehe, afute makosa yao, awarehemu kwa kuwalipa pepo na kuwaepusha na adhabu ya Moto.

ٱلَّذِينَ يَحۡمِلُونَ ٱلۡعَرۡشَ وَمَنۡ حَوۡلَهُۥ يُسَبِّحُونَ بِحَمۡدِ رَبِّهِمۡ
وَيُؤۡمِنُونَ بِهِۦ وَيَسۡتَغۡفِرُونَ لِلَّذِينَ ءَامَنُواْ رَبَّنَا وَسِعۡتَ كُلَّ
شَيۡءٖ رَّحۡمَةٗ وَعِلۡمٗا فَٱغۡفِرۡ لِلَّذِينَ تَابُواْ وَٱتَّبَعُواْ سَبِيلَكَ وَقِهِمۡ
عَذَابَ ٱلۡجَحِيمِ ٧

*"Wale wanaokichukua kiti cha enzi(cha Mwenyezi Mungu) na wale wanaokizunguka, wanamtukuza Mola wao na kumsifu na wanamuamini na wanawaombea msamaha waliaomini. Wanasema: "Mola wetu! Umekienea kila kitu kwa rehema na Elimu. Basi wasamehe waliotubu na kufuata njia yako na waepushe na adhabu ya Jahannam"(40:7)*

Na Mwenyezi Mungu anaahidi kuwa wale wanaotubu kwa kujuta juu ya maovu waliyofanya, wakamuamini Yeye ipasavyo, kwa kujizuia kuyaendea maovu na badala yake wakashikamana na mwenendo mwema; Atabadilisha maovu yao kuwa mema! Qur,an inathibitisha hili katika aya ifuatayo, inasema:

إِلَّا مَن تَابَ وَءَامَنَ وَعَمِلَ عَمَلًا صَٰلِحًا فَأُوْلَٰٓئِكَ يُبَدِّلُ ٱللَّهُ
سَيِّـَٔاتِهِمْ حَسَنَٰتٍ ۗ وَكَانَ ٱللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا ﴿٧٠﴾

*Ila yule atakayetubia na kuamini na kufanya vitendo vizuri; basi hao ndio Mwenyezi Mungu atawabadilishia maovu yao kuwa mema, na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe na Mwingi wa kurehemu.(25:70)*

**(5) Kuwasaidia waumini vitani katika kupambana na madhalimu**

Miongoni mwa kazi tukufu za malaika ni kuwasaidia waislamu kupambana na maadui wenye nguvu kubwa kijeshi katika vita. Qur,an inatueleza kuwa:

بَلَىٰٓ ۚ إِن تَصْبِرُوا۟ وَتَتَّقُوا۟ وَيَأْتُوكُم مِّن فَوْرِهِمْ هَٰذَا يُمْدِدْ
كُمْ رَبُّكُم بِخَمْسَةِ ءَالَٰفٍ مِّنَ ٱلْمَلَٰٓئِكَةِ مُسَوِّمِينَ ﴿١٢٥﴾

*Naam. Kama mtasubiri na kujilinda na makatazo yake(Allah) na maadui wakakufikieni kwa ghafla, hapo Mola wenu atakusaidieni kwa Malaika elfu tano washambuliao kwa nguvu(3:125)*

**(6) Kuwaangamiza watu waovu waliopindukia mipaka**

Malaika pia wana kazi ya kuwaangamiza watu waovu waliokubuhu na kupindukia mipaka. Watu wa nabii Lut(a.s) waliangamizwa na Malaika baada ya kubobea katika maovu na kukataa kwao kujirekebisha. Tunafahamishwa hili pale malaika walipomjibu nabii Ibrahiimu(as).

قَالُوٓا۟ إِنَّآ أُرْسِلْنَآ إِلَىٰ قَوْمٍ مُّجْرِمِينَ ﴿٥٨﴾
إِلَّآ ءَالَ لُوطٍ إِنَّا لَمُنَجُّوهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٥٩﴾

*Wakasema: "Hakika sisi tumetumwa kwa wale watu wakosa(tuwaangamize). Isipokuwa waliomfuata Lut. Bila shaka sisi tutawaokoa hao(15:58-59)*

**(7) Kutoa roho za watu.**

Kuna Malaika wengi wanaohusika na utoaji wa roho za wanadamu wakati muda wao wa kuishi duniani unapokamilika. Malaika mkuu wa kazi hii ni **Malakul-mauti**.

قُلْ يَتَوَفَّىٰكُم مَّلَكُ ٱلْمَوْتِ ٱلَّذِى وُكِّلَ بِكُمْ ثُمَّ إِلَىٰ
رَبِّكُمْ تُرْجَعُونَ ﴿١١﴾

*Sema: Atakufisheni Malaika wa mauti aliyewakilishwa kwenu, kisha mtarejeshwa kwa Mola wenu(32:11)*

**(8) Kuwaliwaza na kuwakaribisha watu wema peponi**

Kabla ya kutolewa roho, kila mtu aliyetenda mema na kutofanya maovu atashukiwa na Malaika wa kumliwaza. Watamwambia:

يَٰٓأَيَّتُهَا ٱلنَّفْسُ ٱلْمُطْمَئِنَّةُ ﴿٢٧﴾ ٱرْجِعِىٓ إِلَىٰ رَبِّكِ رَاضِيَةً
مَّرْضِيَّةً ﴿٢٨﴾

*Ewe nafsi yenye kutulia! Rudi kwa Mola wako hali ya kuwa utaridhika Naye amekuridhia.(89:27-28).*

Na siku ya Kiama watawapokea na kuwakaribisha kwenye pepo ya Allah(SW) yenye neema za kudumu. Watawaambia:

سَلَٰمٌ عَلَيْكُمْ طِبْتُمْ فَٱدْخُلُوهَا خَٰلِدِينَ

*Amani juu yenu, furahini, na ingieni humu mkae milele(39:73)*

**(9) Kuwaadhibu watu waovu motoni**

Watu wanaotenda maovu watakuwa katika adhabu kali kwenye Moto wa Jahannam. Mwenyezi Mungu amewaweka malaika maalumu kwa ajili ya kuwaadhibu watu waovu wasiotaka kutubia, kujirekebisha na kutenda mema. Allah(s.w) anamtangazia kila mtu mwenya tabia hizi kuwa:

سَأُصْلِيهِ سَقَرَ ﴿٢٦﴾ وَمَآ أَدْرَىٰكَ مَا سَقَرُ ﴿٢٧﴾ لَا تُبْقِى وَلَا
تَذَرُ ﴿٢٨﴾ لَوَّاحَةٌ لِّلْبَشَرِ ﴿٢٩﴾ عَلَيْهَا تِسْعَةَ عَشَرَ ﴿٣٠﴾

*Karibuni hivi nitamtia katika Moto. Na ni nini kitakachokujulisha Moto huo? Haubakizi wala hausazi, unababua ngozi mara moja. Juu yake wako malaika(walinzi) kumi na tisa.(74:26-30).*

Mkuu wa Malaika hawa wa adhabu katika Jahannam ni **Malik.** Kutokana na machungu ya adhabu watakayopata, watu waovu watalia na kutamani mauti, watamtaka Malik amwombe Allah(s.w) awafishe kuliko hiyo adhabu inayowakabili.

وَنَادَوْا۟ يَـٰمَـٰلِكُ لِيَقْضِ عَلَيْنَا رَبُّكَ ۖ قَالَ إِنَّكُم مَّـٰكِثُونَ ﴿٧٧﴾

*Nao watapiga kelele: watasema: "Ewe Malik! Na atufishe Mola wako!" (Maliki) atasema: "Kwa hakika mtakaa humu humu"(43:77)*

Na Mwenyezi Mungu anasifu kuwa adhabu watakayotoa Malaika hao kutokana na uwezo aliowapa haitakuwa na mfano wake katika adhabu hizi za duniani.

يَوْمَئِذٍ يَتَذَكَّرُ ٱلْإِنسَـٰنُ وَأَنَّىٰ لَهُ ٱلذِّكْرَىٰ ﴿٢٣﴾ يَقُولُ يَـٰلَيْتَنِى
قَدَّمْتُ لِحَيَاتِى ﴿٢٤﴾ فَيَوْمَئِذٍ لَّا يُعَذِّبُ عَذَابَهُۥٓ أَحَدٌ ﴿٢٥﴾
وَلَا يُوثِقُ وَثَاقَهُۥٓ أَحَدٌ ﴿٢٦﴾

*Siku hiyo mwanadamu atakumbuka, lakini kukumbuka huko kutamfaa nini. Atasema: "Laiti ningalitanguliza(wema) kwa ajili ya uhai wangu (huu wa leo). Basi adhabu ya(Allah) siku hiyo, haitolingana na adhabu aitoayo yeyote(katika wanadamu). Wala hatafunga yeyote jinsi ya kifungo chake (Allah)(89:23-26).*

**Je! Mtu anayeamini Malaika anapaswa afanyeje?**

Kwa kweli, mtu anayeamini kuwepo Malaika anapaswa:

(1) Ajiepushe asimshirikishe Allah (s.w.) na viumbe vyake hasa vile tusivyoviona kama vile Malaika na majini.

(2) Ajiepushe asifanye maovu ili kitabu chake kisichafuliwe na rikodi mbaya.

(3) Ajitahidi kufanya mema ili kitabu chake kijazwe mema mengi.

(4) Ajitahidi kufanya mema ili Malaika wamuombee rehema na msamaha kila wakati.

(5) Ajitahidi kufanya mema na kujiepusha na maovu ili wakati wa kufa kwake apokelewe na Malaika kwa huruma na upole.

(6) Apiganie dini ya Allah (s.w) kwa ujasiri akijua kuwa atapata msaada wa malaika.

## KUAMINI VITABU VYA ALLAH(SW)

Kuamini vitabu vya Allah ni nguzo ya tatu ya Imani ya Kiislamu. Vitabu vilivyotajwa katika Qur'an ni hivi vifuatavyo:

(1) Suhufi ya Nabii Ibrahiim(as)

(2) Suhufi ya Nabii Musa (as)

Allah(SW) amevitaja vitabu hivi katika aya zifuatazo:

إِنَّ هَٰذَا لَفِى ٱلصُّحُفِ ٱلْأُولَىٰ ﴿١٨﴾ صُحُفِ إِبْرَٰهِيمَ وَمُوسَىٰ ﴿١٩﴾

*Hakika haya (mnayoambiwa) yamo katika Vitabu(Suhufi) vilivyotangulia. Vitabu vya Ibrahiimu na Musa(87:18-19)*

(1) Taurati aliyoshushiwa Nabii Musa(as)
(2) Zaburi aliyoshushiwa Nabii Daud(as)
(3) Injili aliyoshushiwa Nabii Isa(as)
(4) Qur,an aliyoshushiwa Nabii Muhammad(s.a.w)

Tunaposoma Qur,an katika aya zifuatazo, tunakuta vitabu hivi vimetajwa katika surat mbalimbali.

نَزَّلَ عَلَيْكَ ٱلْكِتَٰبَ بِٱلْحَقِّ مُصَدِّقًا لِّمَا بَيْنَ يَدَيْهِ وَأَنزَلَ ٱلتَّوْرَىٰةَ وَٱلْإِنجِيلَ ﴿٣﴾ مِن قَبْلُ هُدًى لِّلنَّاسِ

*Amekuteremshia kitabu kwa haki, kinachosadikisha yaliyokuwa kabla yake. Na aliteremsha Taurati na Injili zamani ili ziwe mwongozo kwa watu.(3:3-4)*

وَلَقَدْ فَضَّلْنَا بَعْضَ ٱلنَّبِيِّـۧنَ عَلَىٰ بَعْضٍ ۖ وَءَاتَيْنَا دَاوُۥدَ زَبُورًا

*Na hakika tuliwafadhilisha baadhi ya Manabii kuliko wengine, na Daudi tulimpa Zaburi(17:55)*

Na Mtume Muhammad(s.a.w)aliambiwa:

إِنَّا نَحْنُ نَزَّلْنَا عَلَيْكَ ٱلْقُرْءَانَ تَنزِيلًا ﴿٢٣﴾

*Hakika sisi tunakuteremshia Qur,an kidogo kidogo(76:23)*

Hivi ndivyo vitabu vya Allah(s.w) vilivyotajwa ndani ya Qur,an. Ni vitabu vya Allah(s.w) kwa kuwa maneno yote yaliyoandikwa kwenye vitabu hivyo yalitoka moja kwa moja kwa Allah(s.w). Havikuwa hata na herufi moja iliyoandikwa na mtu kinyume na alivyotaka Allah(s.w).

**Je! Biblia ni Kitabu Kitakatifu?**

Biblia ni kitabu kinachojumuisha Agano la kale na Agano jipya. Miongoni mwa vitabu vya Agano la kale ni **'Kumbukumbu la Torati'**. Vitabu vilivyomo ndani ya Agano jipya ni pamoja na, **'Injili kama alivyoiandika'** Mathayo Mtakatifu, Marko Mtakatifu, Luka mtakatifu na Yohana Mtakatifu.

Kwahiyo, katika Biblia, hakuna Taurati yenyewe aliyopewa nabii Musa, ila yamo yale waliyoandika waandishi kwa namna wao walivyoweza kukumbuka maamrisho yaliyokuwemo ndani ya Torati. Na ndiyo maana Allah(s.w) anatutaka tuwaambie wanaodai kuwa wanayo **'Taurati',** wailete tuione! قُلْ فَأْتُوا۟ بِٱلتَّوْرَىٰةِ فَٱتْلُوهَآ إِن كُنتُمْ صَـٰدِقِينَ ﴿٩٣﴾

*Sema: "Ileteni hiyo Taurati muosome ikiwa mnasema kweli"(3:93)*

Vile vile, Agano jipya halina **Injili yenyewe** aliyopewa Nabii Isa(as) (Yesu) ila ina masimulizi ya watu waliodai kumuona (Yesu) nabii Isa(as) akitenda mambo au kuhubiri neno la Mungu. Masimulizi hayo kuhusu Nabii Isa(as)(Yesu) ndiyo waliyoyakusanya akina Mathayo, Marko, Luka na Yohana, kisha kila mmoja wao akaandika kwa namna yake. Na ndiyo maana Luka anasema:

> *"Kwa kuwa watu wengi wametia mikono kutunga kwa utaratibu habari za mambo yale yaliyotimizwa katika yetu, kama walivyotuhadithia wale waliokuwa mashahidi wenye kuyaona, na watumishi wa lile neno tokea mwanzo, nimeona vema nami, kwa kuwa nimejitafutia usahihi wa mambo hayo yote tangu mwanzo, kukuandikia kwa utaratibu, Theofilo mtukufu".*(Tazama Injili kama alivyoiandika Luka Mtakatifu 1:1-3)

Kwa hiyo, Biblia kama ilivyo, si maneno ya moja kwa moja kutoka kwa Mungu Muumba, bali ni simulizi za watu juu ya habari za Mitume. Ndiyo maana unakuta kuna Injili nne, wakati nabii Isa(a.s)(Yesu) alipewa Injili moja tu toka kwa Mwenyezi Mungu.

Katika Biblia, tunapaswa kuamini tu yale maneno machache yanayokubaliana na mafundisho ya Mitume wa Allah(S.W) na si kila neno.

**Qur'an ni kitabu pekee cha Allah kilicho Kitakatifu**

Kinyume cha Biblia, Qur,ani ni neno la moja kwa moja toka kwa Allah(SW). Qur,ani si masimulizi ya watu, ni mwongozo wa Allah(s.w) kwa wanadamu kupitia mtume Muhammad(s.a.w). Na wala Qur,ani si maneno ya Muhammad(s.a.w). Kwa kuwa si maneno yake, utakuta ndani ya Qur,an kuna aya zinamkosoa na kumrekebisha Mtume(s.a.w)na zingine zinamuamrisha kufanya jambo. Kwa mfano:

قُلْ هُوَ ٱللَّهُ أَحَدٌ ﴿١﴾ ٱللَّهُ ٱلصَّمَدُ ﴿٢﴾ لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ ﴿٣﴾
وَلَمْ يَكُن لَّهُۥ كُفُوًا أَحَدٌۢ ﴿٤﴾

*Sema: Yeye ni Mwenyezi Mungu mmoja. Mwenyezi Mungu tu ndiye anayestahiki kukusudiwa. Hakuzaa wala Hakuzaliwa. Wala hana anayefanana Naye hata mmoja(112:*1-4)

Kuhusu uhakika na utakatifu wa Qur,an Allah(SW) anatuhakikishia kuwa haikuingizwa batili yoyote ndani yake tangu wakati wa Mtume(SW) na itadumu hivyo mpaka kiyama. Allah(SW) anasema:

لَّا يَأْتِيهِ ٱلْبَـٰطِلُ مِنۢ بَيْنِ يَدَيْهِ وَلَا مِنْ خَلْفِهِۦ ۖ تَنزِيلٌ مِّنْ
حَكِيمٍ حَمِيدٍ ﴿٤٢﴾

*Haitaifikia batili mbele yake wala nyuma yake; kimeteremshwa na Mwenye hikima, Ahimidiwaye(41:42)*

Kutokana na ahadi hii, Qur'an imebakia vile vile kama ilivyoshushwa kwa Mtume Muhammad (s.a.w.) Hakuna awezaye kuibadilisha hata herufi moja. Hivyo hivi sasa kitabu kitakatifu ni kitabu kimoja tu. Nayo ni hii Qur'an. Qur'an ndio mwongozo sahihi uliopo kwa ajili ya walimwengu wote. Mtume (s.a.w.) ametuhakikishia kuwa tukiifuata Qur'an pamoja na sunna yake, hatutapotea njia daima.

**Tofauti ya Qur'an na vitabu vingine vya Allah (s.w.)**

Zifuatazo ni tofauti za msingi kati ya Qur'an na vitabu vingine vya Allah (s.w.) vilivyotangulia:

(1) Baada ya Mitume kuondoka vitabu vyote vya Allah (s.w.) viliingiizwa mikono ya watu na kuharibiwa. Isipokuwa Qur'an ambayo ipo katika asili yake ile ile.

(2) Lugha za vitabu vilivyoitangulia Qur'an zimeshatoweka. Hivi leo hata tukiokota ukurasa wa asili wa Taurati au Injili hatuwezi kuuelewa kwani lugha za asili za Taurati na Injili zimetoweka. Kinyume chake Qur'an mpaka leo ipo katika lugha yake ya asili, Kiarabu fasaha. Lugha ya Kiarabu ni miongoni mwa lugha kubwa za ulimwengu hivi sasa. Hata wataalamu wa Kiswahili wanatufahamisha kuwa zaidi ya asilimia 75 ya maneno ya

Kiswahili asili yake ni Kiarabu.

(3) Vitabu vyote vya Allah (s.w.) vilishushwa kwa mataifa maalum. Kwa mfano; Taurati, Zaburi na Injili vililengwa kwa Taifa la Israil - (Banil Israil). Kinyume chake Qur'an imelengwa kwa mataifa yote ulimwenguni.

(4) Qur'an ndio kitabu cha mwisho cha Allah (s.w.). Ndicho kilichokamilisha ujumbe wa Allah (s.w.) aliokusudia kuwafikishia walimwengu. Vitabu vingine havikukamilisha ujumbe ndio maana vilitokea vitabu vingine baada ya hivyo na Mitume wengine.

### Maana ya kuamini vitabu vya Allah (s.w.)

Muumini wa kweli wa vitabu vya Allah (s.w.) ni yule anayeendesha maisha yake yote kwa kufuata mwongozo wa vitabu hivyo. Hivi sasa kitabu cha Allah (s.w.) kilicho hai ni Qur'an pekee. Hivyo kwa wakati huu muumini wa kweli wa vitabu vya Allah (s.w.) ni yule anayeiamini Qur'an. Muumini wa kweli wa Qur'an ni yule:

(1) Anayeisoma na kuizingatia.

(2) Anayeifuata vilivyo katika kuyaendea maisha yake yote. Yaani hufanya kila jambo kwa kufuata mwongozo wa Qur'an.

## Zoezi la Pili

1.(a) Dalili tano katika ardhi zinazothibitisha kuwepo Allah (s.w) ni:
(i)______________(ii)_________________ (iii)_________________.
(iv)_________________(v)_________________.

(b) Dalili tatu katika anga (mbingu) zinazothibitisha kuwepo Allah (s.w) ni:
(i)______________(ii)_______________(iii)_______________

2.Mwanaadamu wa kwanza ameumbwa na Allah (s.w) kwa __________kisha akampulizia __________inayotokana na yeye mwenyewe.

3.Kutokana na kisa cha As-Habil-fyl tunajifunza kuwa kuangamizwa kwa jeshi la __________ na jeshi la ndege wadogowadogo ni dalili tosha kuwa __________.

4.(a) Malaika ni ______________ wa Allah (s.w) waliumbwa kutokana na ______________.

(b)Malaika wanasifika kwa sifa zifuatazo:
(i) _____ (ii)________(iii)________(iv)_________(v)___________

(c)Malaika hufanyakazi mbali mbali kama wanavyoamrishwa na Allah (s.w). Baadhi ya kazi za malaika ni hizi zifuatazo:
(i) ______(ii)______(iii)________(iv)_________(v)__________
(vi)_______________________ (vii)____________________

(d)Yafuatayo ni majina ya Malaika na kazi zao:

| Na. | Jina la Malaika | Kazi yake |
|---|---|---|
| 1. | ......................................... | ...................................... |
| 2 | ........................................... | ........................................ |
| 3 | ........................................... | ........................................ |
| 4 | ........................................... | ........................................ |
| 5 | ........................................... | ........................................ |

(e)Mtu anayeamini malaika kikweli kweli huwa na tabia ya kufanya yafuatayo:

(i)__________(ii)_________(iii)___________(iv)_________________

5.(a) Vitabu vya Allah vilivyotajwa katika Qur-an na mitume walioshushiwa ni:

| Na. | Jina la Kitabu | Mtume aliyeshushiwa |
|---|---|---|
| 1. | ............................ | ......................................... |
| 2. | ............................ | .......................................... |
| 3. | ............................. | ........................................... |
| 4. | ............................. | ........................................... |
| 5. | .............................. | ............................................ |
| 6. | .............................. | ............................................ |

(b)Biblia si kitabu cha Allah (s.w) kwa sababu:
___________________________.

(c)Muumini wa kweli wa vitabu vya Allah (s.w) huendesha maisha yake ya kila siku kwa ______________________________________________

Sura ya Tatu

# Fiqh

## KUSIMAMISHA SWALA

### Maana ya Swala

Kwa lugha ya Kiarabu neno *"Swala"* lina maana ya *"Dua"* au *"maombi".* Katika Fiq-h *Swala* ni maombi maalum kwa Allah (s.w.) yanayofanywa kwa kufuata utaratibu maalum ambao ndani yake kuna kusimama wima, kurukuu, kusujudu, kukaa, kuleta visomo na dhikiri mbalimbali na mwisho kutoa salaamu.

### Kuswali

Kuswali ni kutekeleza swala kivitendo. Mtu anaweza kuswali bila ya kuwa na udhu lakini akahesabika kuwa ameswali. Anaweza kuswali nje ya wakati wa swala bado akahesabika kuwa ameswali. Pia anaweza kuswali bila ya kuwa na khushui (unyenyekevu) na bado akahesabika kuwa ameswali.

### Kusimamisha Swala

Kusimamisha swala ni kuswali kwa kutekeleza kwa ukamilifu yafuatayo:

(1) Masharti yote ya swala.
(2) Nguzo zote za swala.
(3) Kuwa na khushui (unyenyekevu) wakati wa kuswali.

### Umuhimu wa kusimamisha swala

Kusimamisha swala kwa Muislamu si jambo la hiari bali ni jambo la lazima kwa sababu zifuatazo:

**(1) Kusimamisha swala ni amri ya Allah (s.w.) :**

Amri hii inadhihirika katika aya zifuatazo

فَأَقِيمُوا۟ ٱلصَّلَوٰةَ ۚ إِنَّ ٱلصَّلَوٰةَ كَانَتْ عَلَى ٱلْمُؤْمِنِينَ كِتَـٰبًا
مَّوْقُوتًا ﴿١٠٣﴾

*"... Basi simamisheni Swala, kwa hakika Swala kwa Waislamu ni faradh iliyowekwa nyakati makhsus". (4:103)*

وَأَقِيمُوا۟ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتُوا۟ ٱلزَّكَوٰةَ ۚ وَمَا تُقَدِّمُوا۟ لِأَنفُسِكُم تَجِدُوهُ
عِندَ ٱللَّهِ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿١١٠﴾

*Na simamisheni Swala na toeni Zakat; na Kheri mtakayoitanguliza kwa ajili ya nafsi zenu, mtazikuta kwa Mwenyezi Mungu . Hakika Mwenyezi Mungu anaona mnayoyafanya" (2:110)*

وَأْمُرْ أَهْلَكَ بِٱلصَّلَوٰةِ وَٱصْطَبِرْ عَلَيْهَا ۖ

*Na waambie watu wako waswali na uendelee mwenyewe kwa hayo..." (20:132).*

**(2) Kusimamisha swala ni nguzo ya pili ya Uislamu.**
Tunajifunza katika Hadith kuwa nguzo za Uislamu ni tano:
(i) Kutoa shahada mbili.
(ii) Kusimamisha Swala.
(iii) Kutoa Zaka.
(iv) Kufunga Ramadhani.
(v) Kuhiji Makka (Al-Ka'aba) kwa mwenye uwezo.

**(3) Kusimamisha swala ndio nguzo kubwa ya dini kama Mtume (s.a.w.) anavyotufahamisha:**

*"Swala ndio nguzo kubwa ya dini. Mwenye kusimamisha swala amesimamisha dini na mwenye kuiacha swala ameivunja dini".*

**(4) Kusimamisha swala ndio kitambulisho cha waumini wa kweli na wacha Mungu. Mtume (s.a.w.) amesema:**

*"Tofauti iliyopo kati yetu (Waislamu) na wengine (wasio kuwa Waislamu) ni swala".*

Qur'an inatufahamisha kuwa waumini wa kweli ni wale wanaosimamisha swala:

ٱلَّذِينَ يُقِيمُونَ ٱلصَّلَوٰةَ وَمِمَّا رَزَقْنَٰهُمْ يُنفِقُونَ ﴿٣﴾

*Ambao **wanasimamisha swala** na wanatoa katika yale Tuliyowapa. (8:3)*

**(5) Kusimamisha swala ni sababu ya kumpatia mtu mafanikio hapa duniani na huko akhera.**

Tunafahamishwa katika Qur'an:

يَوْمَ يُكْشَفُ عَن سَاقٍ وَيُدْعَوْنَ إِلَى ٱلسُّجُودِ فَلَا يَسْتَطِيعُونَ
﴿٤٢﴾ خَٰشِعَةً أَبْصَٰرُهُمْ تَرْهَقُهُمْ ذِلَّةٌ ۖ وَقَدْ كَانُوا۟ يُدْعَوْنَ إِلَى
ٱلسُّجُودِ وَهُمْ سَٰلِمُونَ ﴿٤٣﴾

*"Hiyo siku patakuwa na mateso makali na wataitwa kusujudu lakini hawataweza. Macho yatainama chini, unyonge umewafunika. Na hakika walikuwa wakiitwa kusujudu walipokuwa salama (hapa duniani na walikataa)".* (68:42-43).

Pia Mtume (s.a.w.) amesisitiza:

*"Usiache swala ya faradhi kusudi. Mwenye kuacha swala ya faradhi kaepukana na ahadi ya Allah ya kumuokoa na moto". (Ahmad, Ibn Majah).*

**Lengo la swala**

Lengo la swala linabainishwa katika aya ifuatayo:

ٱتْلُ مَآ أُوحِىَ إِلَيْكَ مِنَ ٱلْكِتَٰبِ وَأَقِمِ ٱلصَّلَوٰةَ ۖ إِنَّ ٱلصَّلَوٰةَ
تَنْهَىٰ عَنِ ٱلْفَحْشَآءِ وَٱلْمُنكَرِ ۗ وَلَذِكْرُ ٱللَّهِ أَكْبَرُ ۗ وَٱللَّهُ يَعْلَمُ
مَا تَصْنَعُونَ ﴿٤٥﴾

*"Soma uliyoletwa Wahay katika Kitabu na usimamishe swala. Bila shaka swala humzuilia (huyo mwenye kuswali) na mambo machafu na maovu, na kwa yakini kumbuko la Mwenyezi Mungu ( lililomo ndani ya swala ni jambo) kubwa kabisa (la kumzuilia mtu na mabaya). Na Mwenyezi Mungu anajua mnayoyatenda". (29:45).*

Katika aya hii tunajifunza kuwa **lengo la swala** ni kumtakasa mja aepukane na mambo machafu na maovu. Swala ikisimamishwa vilivyo ina uwezo wa kumtakasa Muislamu kwa sababu kuna kuomba na kumkumbuka Mwenyezi Mungu kwa wingi ndani ya swala.

**Swala za Sunnah**

Pamoja na swala tano za faradh Mtume (s.a.w.) alikuwa akileta swala

mbalimbali za ziada naye akatuamrisha tufanye hivyo. Swala hizi za ziada zinajulikana kama "Swala za Sunnah".

Ni muhimu sana kuswali swala hizi kwasababu ndio mwenendo wa Mtume(s.a.w). Na kufuata mwenendo wa Mtume(s.a.w) ndiyo kumtii Allah(s.w). Na Allah(s.w) anawapenda wale wanaofuata mwenendo wa Mtume(s.a.w). Kinyume chake, kuacha kufuata mwenendo wa Mtume(s.a.w)ni kumuasi Allah(s.w) na Allah(s.w) huwachukia wasiofuata mwenendo wa Mtume wake. Katika Qur,an Allah(s.w) anamwambia Mtume wake kuwa:

قُلْ إِن كُنتُمْ تُحِبُّونَ ٱللَّهَ فَٱتَّبِعُونِى يُحْبِبْكُمُ ٱللَّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ
ذُنُوبَكُمْ ۗ وَٱللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٣١﴾

*Sema: Ikiwa ninyi mnampenda Mwenyezi Mungu nifuateni mimi, Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakusameheni madhambi yenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe na Mwenye rehema(3:31)*

Kwahiyo, ni muhimu sana kila muislamu kujitahidi kwa kadri ya uwezo wake kufuata mwenendo wa Mtume(s.a.w) kwa kuswali swala za Sunnah zifuatazo:

***(1) Swala ya maamkizi ya Msikiti - Tahiyyatul-Masjid:***

Swala hii huswaliwa kwa rakaa mbili mara tu baada ya kuingia Msikitini kabla
ya kukaa chini.

***(2) Swala za kabla na baada ya swala za faradhi:***

Kuna Sunnah za kabla na baada ya swala tano za faradh kama ifuatavyo:

(i) Rakaa 2 kabla ya swala ya Alfajiri.
(ii) Rakaa 4 kabla ya swala ya Adhuhuri.
(iii) Rakaa 2 baada ya swala ya Adhuhuri.
(iv) Rakaa 2 kabla ya swala ya Magharibi.
(v) Rakaa 2 baada ya swala ya Magharibi
(v) Rakaa 2 baada ya swala ya Al-Ishai.

Hizi ni sunnah zilizokokotezwa sana. Kila Muislamu anatakiwa ajihimize kuzitekeleza.

**3. Swala ya Witri**

Swala ya Witri huswaliwa usiku baada ya swala ya Al-Ishai mpaka kabla ya Alfajiri. Hasa swala hii huswaliwa baada ya swala ya Tahajjud. Swala hii huswaliwa kwa rakaa tatu; rakaa mbili kisha rakaa moja. Swala ya Witri ni miongoni mwa swala zilizokokotezwa sana.

**Qunut katika Witri**

Katika rakaa ya mwisho ya witri, baada ya kuitidali na kusema "Samiallahu liman hamidah, ni Sunnah kuinua mikono na kuleta dua ifuatayo:

اَللّٰهُمَّ اهْدِنِي فِيمَنْ هَدَيْتَ

Ewe Mola Niongoze kama wale uliowaongoza

وَعَافِنِي فِيمَنْ عَافَيْتَ



Na uniokowe kama hao uliowaokoa.

وَتَوَلَّنِي فِيمَنْ تَوَلَّيْتَ

Na uninusuru kama hao uliowanusuru

وَبَارِكْ لِي فِيمَا أَعْطَيْتَ

Unitilie baraka katika haya uliyoni

وَقِنِي شَرَّ مَا قَضَيْتَ

Unikinge na shari ulizonikadiria

فَإِنَّكَ تَقْضِي وَلَا يُقْضَى عَلَيْكَ

Kwani wewe una hukumu wala uhukumi

إِنَّهُ لَا يَذِلُّ مَنْ وَالَيْتَ



Hakika hadhalililiki uliyemfanya rafi

تَبَارَكْتَ رَبَّنَا وَتَعَالَيْتَ

Umetasika Ewe Mola wetu na umetuku

**4. Swala ya Tahajjud**

Swala hii huswaliwa usiku na hasa katika theluthi ya mwisho ya usiku, yaani kuanzia saa 8.00 usiku mpaka kuingia kwa Alfajiri. Hii ni swala inayompatia mja hadhi kubwa mbele ya Allah(s.w). Allah(s.w) anatwambia

وَمِنَ ٱلَّيْلِ فَتَهَجَّدْ بِهِۦ نَافِلَةً لَّكَ عَسَىٰٓ أَن يَبْعَثَكَ رَبُّكَ

مَقَامًا مَّحْمُودًا ﴿٧٩﴾

*Na katika usiku jiondoshe usingizini kwa (kusoma Qur,an) ndani ya swala. Hii ni (ibada) zaidi. Huwenda Mola wako akakuinua cheo kinachosifika.(17:79)*

Swala hii ina rakaa 8 na kuswaliwa kwa rakaa mbili mbili. Katika swala hizi za usiku ni vizuri kurefusha kisomo cha Qur'an. Katika mwezi wa Ramadhani swala hii huitwa Taraweh na imekokotezwa kwa mwezi mzima wa Ramadhani.

**5. Swala za Idd mbili**

Swala za Idd mbili - Iddil - Hajj na Iddil Fitri ni miongoni mwa Sunnah zilizokokotezwa. Swala ya Iddil-Hajj huswaliwa asubuhi ya siku ya mwezi kumi Dhul-Hijja kama kilele cha kukamilisha ibada ya Hija. Swala ya Iddil-Fitri huswaliwa asubuhi ya mwezi mosi Shawwal ikiwa ni kielelezo cha furaha ya kumaliza mfungo wa Ramadhani.

**Faida ya kusimamisha swala katika maisha ya kila siku**

Kusimamisha swala humfaidisha Muislamu kiroho, kimwili na kijamii.

**Faida za kiroho**

(1) Swala humuwezesha Muislamu kumkumbuka Allah (s.w.) kila wakati.

(2) Swala humzoesha Muislamu kumtii Allah (s.w.).

(3) Swala humkumbusha Muislamu kila wakati juu ya sheria na maamrisho ya Allah (s.w.).

Kutokana na faida hizi swala humuwezesha Muislamu kujiepusha na mambo machafu na maovu.

**Faida za kimwili**

(i) Kusimamisha swala tano humfanya Muislamu awe msafi wa mwili na nguo muda wote. Kila wakati atajitahadhari na najisi na kila wakati atakuwa ananawa kwa kutia udhu.

(ii) Kuupa mwili mazoezi ya viungo. Kurukuu, kuitidali, kusuduju na kukaa tahiyyatu kwa kiasi fulani huzoesha viungo visikakamae hasa kwa wazee.

**Faida za kijamii**

Faida za swala hasa swala za jamaa katika jamii ni nyingi. Baadhi ya faida hizi ni:

(i) Umoja na udugu hupatikana kwa kule kukutana pamoja na kuswali pamoja.

(ii) Hudumisha usawa, upendo na mshikamano.

(iii) Kuwahi swali ya jamaa, hutuzoesha kuwa na tabia ya kuchunga wakati.

(iv) Swala ya jamaa hutufundisha kuchagua viongozi wajuzi na wacha Mungu.

(v) Swala ya jamaa hutuzoesha kuwatii viongozi.

(vi) Swala ya jamaa hutuzoesha kuwakosoa viongozi wetu na huwazoesha viongozi kuwa tayari kukosolewa. Kwani Imamu akikosea kwenye swala tunamkosoa kwa kumwambia "***Subhaanallah***" yaani Allah(s.w) peke yake ndiye aliyetakasika na upungufu wa aina yoyote.

(vii) Swala ya jamaa huwafunza viongozi kuwahurumia raia zao na wale wanaowaongoza.

## ZAKAT NA SADAQAT

**Maana ya Zakat**

*Zakat* ni neno la Kiarabu lenye maana ya *Utakaso*. Katika sharia ya Kiislamu Zakat ni sehemu ya mali ya tajiri ambayo ni haki ya fakiri, maskini, na wengine waliotajwa katika aya ifuatayo ndani ya Qur'an.


إِنَّمَا ٱلصَّدَقَٰتُ لِلْفُقَرَآءِ وَٱلْمَسَٰكِينِ وَٱلْعَٰمِلِينَ عَلَيْهَا
وَٱلْمُؤَلَّفَةِ قُلُوبُهُمْ وَفِى ٱلرِّقَابِ وَٱلْغَٰرِمِينَ وَفِى سَبِيلِ ٱللَّهِ
وَٱبْنِ ٱلسَّبِيلِ ۖ فَرِيضَةً مِّنَ ٱللَّهِ ۗ وَٱللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٦٠﴾

*Sadaqa (Zakkat) hupewa Mafakiri, masikini na wanaozitumikia na wanaotiwa nguvu nyoyo zao na katika kuwapa Uungwana watumwa na katika kuwasaidia wenye deni na katika mambo aliyoamrisha Mwenyezi Mungu na katika wasafiri(waliharibikiwa). Ni faradhi inayotoka kwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye hekima(9:60)*

Zakat hutolewa baada ya mwaka au baada ya mavuno ya mazao ya shambani.

**Maana ya Sadaqat**

Katika lugha ya Kiarabu neno "Sadaqat" linatokana na neno ***"Sidq"*** lenye maana ya ukweli. Katika sheria ya Kiislamu Sadaqat ni mali au huduma aitoayo Muislamu kumpa au kumfanyia mtu mwingine mwenye kuhitajia mali au huduma hiyo. Mathalan, kusaidia kusukuma mkokoteni au gari lisilobeba bidhaa za haramu ni sadaqat.



Mtume (s.a.w.) amebainisha wazi kuwa kila jambo jema Muislamu analolifanya ni sadaqa. Amebainisha, kwa mfano, kuwa kuondoa mwiba au ghasia yoyote njiani ni sadaqat, kumsaidia mtu kutwishwa kichwani mzigo wake ni sadaqat, mama kuwalisha na kuwahudumia watoto wake nyumbani ni sadaqat; n.k.




**Umuhimu wa kutoa Zakkat na Sadaqat**

Kutoa Zakat na Sadaqat si jambo la hiari kwa Muislamu bali ni jambo la lazima kutokana na sababu zifuatazo:

1. Kutoa Zakat ni nguzo ya tatu ya Uislamu.

2. Ukitoa Zakat na Sadaqat (vile alivyoturuzuku Allah(s.w) ikiwa ni pamoja na afya zetu, akili zenu, nguvu zetu, mali zetu, n.k.) ni amri ya Allah (s.w.) kama tunavyojifunza katika aya mbalimbali za Qur'an:

قُلْ لِعِبَادِيَ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ يُقِيمُوا۟ ٱلصَّلَوٰةَ وَيُنفِقُوا۟ مِمَّا رَزَقْنَـٰهُمْ سِرًّا وَعَلَانِيَةً مِّن قَبْلِ أَن يَأْتِىَ يَوْمٌ لَّا بَيْعٌ فِيهِ وَلَا خِلَـٰلٌ

*"Waambie waja wangu walioamini wasimamishe swala na watoe katika vile tulivyowaruzuku kwa siri na kwa dhahiri, kabla haijafika siku isiyokuwa na kujikomboa wala urafiki". (14:31).*

وَأَنفِقُوا۟ مِن مَّا رَزَقْنَـٰكُم مِّن قَبْلِ أَن يَأْتِىَ أَحَدَكُمُ ٱلْمَوْتُ فَيَقُولَ رَبِّ لَوْلَآ أَخَّرْتَنِىٓ إِلَىٰٓ أَجَلٍ قَرِيبٍ فَأَصَّدَّقَ وَأَكُن مِّنَ ٱلصَّـٰلِحِينَ ﴿١٠﴾

*"Na toeni katika yale tuliyokupeni, kabla mmoja wenu hayajamjia mauti, kisha akasema: Mola wangu! Huniakhirishi muda kidogo tu na kutoa sadaqa na nikawa miongoni mwa watendao mema". (63:10)*

3. Utoaji wa Zakat na Sadaqat ndio kitambulisho cha Uislamu wa mtu na ndio msingi wa udugu wa Uislamu. Tunafahamishwa katika Qur'an:

فَإِن تَابُوا۟ وَأَقَامُوا۟ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتَوُا۟ ٱلزَّكَوٰةَ فَإِخْوَٰنُكُمْ فِى ٱلدِّينِ ﴿١١﴾

*"Kama wakitubu na kusimamisha swala na wakatoa zakat, basi ni ndugu zenu katika dini...". (9:11)*

4. Utoaji wa zakat na sadaqat ndio kitambulisho cha muumini wa kweli na mcha Mungu. Qur'an inatufahamisha kuwa wacha Mungu ni wale:

ٱلَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِٱلْغَيْبِ وَيُقِيمُونَ ٱلصَّلَوٰةَ وَمِمَّا رَزَقْنَـٰهُمْ يُنفِقُونَ ﴿٣﴾

*"Ambao huyaamini yasiyoonekana na husimamisha Swala na hutoa katika yale tuliyowapa". (2:3).*

5. Utoaji wa zakat na sadaqat humpelekea mtu kufuzu hapa duniani na huko akhera:

قَدْ أَفْلَحَ ٱلْمُؤْمِنُونَ ﴿١﴾ ٱلَّذِينَ هُمْ فِى صَلَاتِهِمْ خَٰشِعُونَ ﴿٢﴾
وَٱلَّذِينَ هُمْ عَنِ ٱللَّغْوِ مُعْرِضُونَ ﴿٣﴾ وَٱلَّذِينَ هُمْ لِلزَّكَوٰةِ
فَٰعِلُونَ ﴿٤﴾

*"Hakika wamefuzu waumini. Ambao katika swala zao huwa ni wanyenyekevu, na ambao hujiepusha na mambo ya upuuzi, na ambao nguzo ya zakat wanaitekeleza. (23:1-4).*

6. Kutotoa zakat na sadaqat ni sababu tosha ya kumtumbukiza mtu motoni:

وَٱلَّذِينَ يَكْنِزُونَ ٱلذَّهَبَ وَٱلْفِضَّةَ وَلَا يُنفِقُونَهَا فِى سَبِيلِ
ٱللَّهِ فَبَشِّرْهُم بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿٣٤﴾ يَوْمَ يُحْمَىٰ عَلَيْهَا فِى نَارِ
جَهَنَّمَ فَتُكْوَىٰ بِهَا جِبَاهُهُمْ وَجُنُوبُهُمْ هَٰذَا مَا كَنَزْتُمْ
لِأَنفُسِكُمْ فَذُوقُوا۟ مَا كُنتُمْ تَكْنِزُونَ ﴿٣٥﴾

*"... Na wale wakusanyao dhahabu na fedha wala hawazitoi katika njia ya Allah (zakat na sadaqat) wape habari ya adhabu iumizayo. Siku mali yao yatakapotiwa moto katika moto wa Jahannam na kwa hayo vikachomwa vipaji vya nyuso zao na mbavu zao, na migongo yao (na huku wanaambiwa): Haya ndiyo (yale mali) mliyojilimbikizia nafsi zenu. Basi onjeni yale mliyokuwa mkikusanya". (9:34-35).*

Kutokana na sababu hizi hatuna budi kujitahidi kutoa zakat na sadaqat. Hata kama hatuna mali tuwasaidie wanaadamu wenzetu katika kuwapa huduma mbalimbali wanazohitajia. Muislamu daima anatakiwa awe mwepesi wa kutoa misaada kwa wengine bila ya kutarajia malipo yoyote kutoka kwao.

**Masharti ya utoaji wa zakat na sadaqat**

Ili zakat na sadaqat ya Muislamu ipokelewe na Allah (s.w.) na kupata malipo kutoka kwake ni lazima yazingatiwe masharti yafuatayo:

(1) Kutoa vilivyo halali.

(2) Kutoa vilivyo vizuri tunavyovipenda sisi wenyewe.

(3) Kutofuatilia kwa masimbulizi baada ya kutoa.
(4) Kutoa vilivyo ziada ya mahitaji muhimu na kutoa kwa kiasi (kwa kati na kati).
(5) Kuwapa wanaostahiki kama walivyo bainishwa katika Qur'an (9:60).
(6) Kujiepusha na ria

**Lengo la Zakat**

Lengo la utoaji Zakat linabainishwa katika aya ifuatayo:

خُذۡ مِنۡ أَمۡوَٰلِهِمۡ صَدَقَةٗ تُطَهِّرُهُمۡ وَتُزَكِّيهِم بِهَا وَصَلِّ عَلَيۡهِمۡۖ
إِنَّ صَلَوٰتَكَ سَكَنٞ لَّهُمۡۗ وَٱللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ١٠٣

*"Chukua Sadaqa katika mali zao uwatakase kwazo na uwaombee dua. Hakika kuwaombea kwako kutawapa utulivu. Na Mwenyezi Mungu ndiye Asikiaye Ajuaye". (9:103)*

Tunajifunza katika aya hii kuwa kutoa zakat na sadaqat kunaitakasa nafsi ya mtoaji kwa kumuepusha na uchumi haramu. Pia huitakasa nafsi ya mtoaji kwa kuipa hisia za kujali na kuwahurumia wanaadamu wenzake.

## FUNGA YA RAMADHANI

Funga ya Ramadhani si jambo la hiari kwa Muislamu bali ni lazima kwa sababu zifuatazo:

(1) Funga ya Ramadhani ni amri ya Allah (s.w.) kama ilivyobainishwa katika Qur'an:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ كُتِبَ عَلَيۡكُمُ ٱلصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى
ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِكُمۡ لَعَلَّكُمۡ تَتَّقُونَ ١٨٣

*"Enyi Mlioamini! Mmeamrishwa kufunga kama walivyoamrishwa wale waliokuwa kabla yenu ili mpate kumcha - Mwenyezi Mungu". (2:183).*

(2) Kufunga Ramadhani ni nguzo ya nne ya Uislamu. Mwenye kuacha kufunga makusudi atakuwa ameivunja nguzo hii na Uislamu wake pia utakuwa umevunjika. Mtume (s.a.w.) amesema:

*Uislamu umejengwa juu ya nguzo tano, kushuhudia kuwa hapana Mola ila Allah(s.w) na kushuhudia kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah(s.a.w); kusimamisha swala; kutoa zakkat kufunga Ramadhani na kuhij nyumba tukufu kwa mwenye uwezo(Bukhari na Muslim)*

(3) Funga ni ibada inayomuwezesha Muislamu kukata matamanio na tamaa za kimwili.

**Swala za usiku katika mwezi wa Ramadhani (Tarawehe)**

Kusimama usiku wa manane na kuswali ni sunna iliyokokotezwa sana katika miezi yote. Bali katika mwezi wa Ramadhani imekokotezwa zaidi. Swala ya usiku katika miezi mingine huitwa "Tahajjud" na katika mwezi wa Ramadhani hujulikana kwa jina la "Tarawehe". Mtume (s.a.w.) katika kuikokoteza swala ya usiku katika mwezi wa Ramadhani amesema:

> *"Yeyote yule atakayeswali usiku katika mwezi wa Ramadhani akiwa na imani ya yakini na mategemeo kupata malipo kwa Allah (s.w.) dhambi zake zote zilizopita zitasamehewa". (Bukhari).*

Swala ya usiku ina rakaa 8 ambazo huswaliwa mbili mbili. Baada ya rakaa nane kuna rakaa tatu za Witri.

**Lailatul - Qadr**

Lailatul-Qadr ni usiku wenye cheo na baraka unaotokea katika mwezi wa Ramadhani. Ni katika usiku huu Qur'an ilianza kushushwa kwa Mtume Muhammad (s.a.w.). Allah (s.w.) anatufahamisha juu ya utukufu wa usiku huu katika Suratul-Qadr:

إِنَّآ أَنزَلْنَٰهُ فِى لَيْلَةِ ٱلْقَدْرِ ﴿١﴾ وَمَآ أَدْرَىٰكَ مَا لَيْلَةُ ٱلْقَدْرِ ﴿٢﴾
لَيْلَةُ ٱلْقَدْرِ خَيْرٌ مِّنْ أَلْفِ شَهْرٍ ﴿٣﴾ تَنَزَّلُ ٱلْمَلَٰٓئِكَةُ وَٱلرُّوحُ
فِيهَا بِإِذْنِ رَبِّهِم مِّن كُلِّ أَمْرٍ ﴿٤﴾ سَلَٰمٌ هِىَ حَتَّىٰ مَطْلَعِ ٱلْفَجْرِ

> *"Hakika tumeiteremsha (Qur'an) katika Lailatul-Qadr (usiku wenye cheo). Ni jambo gani litakalokujulisheni ni nini huo usiku wenye cheo? Huo usiku wenye cheo ni bora kuliko miezi elfu. Huteremka Malaika na roho (za viumbe watakatifu) katika usiku huo kwa idhini ya Mola wao. Ni amani (katika usiku) huo mpaka mapambazuko ya Alfajiri". (97:1-5).*

**Tufanye nini katika usiku wenye cheo**

Usiku huu ni usiku mtukufu sana. Anatakiwa kila Muislamu ajitahidi akutwe na usiku huu akiwa anamtukuza na kumtasbihi Allah (s.w.), akiwa anasoma Qur'an na kuswali. Katika kuwasisitiza Waislamu wasimame kwa ibada katika usiku huu Mtume (s.a.w.) amesema:

*"... Na mwenye kusimama kwa swala katika usiku wa Qadr akiwa na imani na mategemeo ya kupata malipo kutoka kwa Allah, basi dhambi zake zote zilizotangulia zitasamehewa". (Bukhari)*

Pia Mtume (s.a.w.) ametusisitiza tuombe msamaha kwa Allah (s.w.) kwa makosa yetu mbalimbali tunayoyajua na tusiyoyajua. Mtume (s.a.w.) ametuhimiza katika usiku huo tuombe:

*"Ee Allah! Wewe ni Msamehevu Unayependa kusamehe, Basi (nakuomba) unisamehe".*

**Ni siku gani ya mwezi wa Ramadhani inayotazamiwa kupatikana Lailatul - Qadr?**

Usiku wa Lailatul-Qadr ni usiku uliofichwa na Allah (s.w.). Yaani haijulikani siku maalum ya mwezi wa Ramadhani ambamo usiku huu hutokea. Bali Mtume (s.a.w.) anatuhakikishia kuwa usiku huu hupatikana ndani ya kumi la mwisho la mwezi wa Ramadhani katika mausiku ya Witri - Usiku wa 21, 23,25, 27 na 29.

Pamoja na kutufahamisha juu ya mausiku haya ya Witri, Mtume (s.a.w.) hakutuelekeza tuyategemee mausiku hayo tu bali ametuhimiza kuitafuta Lailatul-Qadr katika masiku yote kumi ya kumi la mwisho la Ramadhani. Bibi Aysha (r.a.) mkewe Mtume (s.a.w.), ametufahamisha kuwa wakati usiku wa kumi la mwisho ulipoingia, Mtume (s.a.w.) alikuwa akikesha katika ibada na akiamsha familia yake kwa swala za usiku.

**Itiqaf katika mwezi wa Ramadhani**

Itiqaf ni ibada ya kukaa Msikitini na kufanya humo ibada mbalimbali kama vile kusoma Qur'an, kuswali, kumdhukuru na kumtasbihi Allah (s.w.), n.k. Ibada hii ya Itiqaf hufanywa wakati wowote kwa muda wowote - saa moja, siku moja, siku 10, n.k. Kukaa Itiqaf katika kumi la mwisho la mwezi wa Ramadhani ni sunnah iliyokokotezwa.

*"Aysha (r.a.) amesimulia kuwa Mtume wa Allah (s.w.) alikuwa akikaa Itiqaf katika siku kumi za mwisho wa Ramadhani mpaka alipotawafu. Kisha wakeze waliendelea kukaa baada yake". (Bukhari na Muslim).*

Itiqaf imekokotezwa sana katika kumi la mwisho la Ramadhani ili kumuwezesha Muislamu aweze kupata Lailatul-Qadr akiwa katika hali ya kumkumbuka Allah (s.w.).

**Zakatul-Fitri**

Zakatul-Fitri ni zakat inayomlazimu kila Muislamu mkubwa na mdogo hata akiwa mtoto mchanga. Watoto, wanawake na wazee wasioweza kujitegemea watatolewa zakatul-Fitri na wale wanaowategemea.

Zakatul-Fitr ni faradhi inayoambatana na faradh ya funga ya Ramadhani. Kila mwenye uwezo wa kupata ziada ya chakula cha usiku na mchana wa Idd, analazimika kutoa Zakatul-Fitri.

**Nani apewe Zakatul-Fitri**

Wanaostahiki kupewa Zakatul-Fitri wale wasiojiweza - mafakiri na maskini ambao hawana uwezo wa kujipatia mahitaji muhimu ya chakula katika usiku na mchana wa Idd. Lengo la Zakatul-Fitri ni kumuwezesha kila Muislamu au kila familia ya Kiislamu ifurahie Idd.

Ni dhuluma kubwa kutoa Zakatul-Fitri kuwapa Maimamu na Masheikh na wengine wenye uwezo na kuwanyima wale wasio na uwezo wa kusherehekea Idd.

**Kiwango cha Zakatul-Fitri**

Kiwango cha Zakatul-Fitri kwa kila mtu ni kutoa pishi (sai) moja ya aina ya chakula kinachotumiwa kwa wingi na watu wa sehemu hiyo. Kwa mfano watu waishio mijini na pwani hutumia kwa wingi mchele.

Kwa wastani pishi moja ya mchele ni sawa na kilo mbili na nusu. Pia unaruhusiwa kuthaminisha aina ya chakula kwa fedha taslim. Kwa mfano kwa wakazi wa Dar es Salaam Zakatul-Fitri yao hutolewa kwa thamani ya kilo mbili na nusu za mchele.

**Muda wa kutoa Zakatul-Fitri**

Zakatul-Fitri inatakiwa itolewe kabla ya swala ya Idd. Ikitolewa siku moja au mbili kabla ni bora zaidi ili kuwawezesha wale wenye kupewa waliwazike na kujiandaa mapema kwa sherehe ya Idd.


**Iddil-Fitri**

Iddil-Fitri ni sikukuu ya Kiislamu ya kusheherekea kumalizika kwa mfungo wa Ramadhani. Jambo kubwa la msingi linalofanyika katika kuadhimisha sikukuu ya Iddil-Fitri ni kuswali swala ya Iddil-Fitr ambayo ni miongoni mwa swala za sunnah zilizokokotezwa na kuswaliwa asubuhi-subuhi.

Swala ya Idd ina rakaa mbili na kila rakaa huanzwa kwa takbira nyingi. Rakaa ya kwanza, baada ya takriba ya kuhirimia, hufuatia takriba saba. Rakaa ya pili huanza kwa takbira tano. Baada ya kuswali rakaa mbili kwa jamaa, hufuatia khutuba.

**Namna ya kusherehekea Idd Kiislamu**

Ili tupate baraka za Idd, hatuna budi kusherehekea Idd kama alivyosherehekea Mtume (s.a.w.) na kama alivyotuagiza. Ni Sunnah siku ya Idd kukoga na kuvalia mavazi mazuri yenye kuchunga mipaka ya Uislamu. Ni sunnah kwa wanaume kupaka manukato. Ni sunna kuswali Idd uwanjani ili wakusanyike watu kutoka sehemu mbalimbali za mji. Vile vile katika kusherehekea Idd ni Sunnah kufanya yafuatayo:



(1) Kuandaa vyakula vizuri na vinywaji na mwenye uwezo achinje mnyama.
(2) Kuwakaribisha ndugu, jamaa, marafiki, jirani, maskini na yatima.
(3) Kuwatembelea ndugu, rafiki na jamaa na kuwapelekea zawadi.
(4) Kuwatembelea wagonjwa.
(5) Kuleta takbira mara kwa mara mpaka jua litue. Ufupi wa Takbira ni kusema:

ٱللَّهُ أَكْبَرُ ٱللَّهُ أَكْبَرُ ٱللَّهُ أَكْبَرُ

*Allah Mkubwa, Allah Mkubwa, Allah Mkubwa.*

لَآ إِلَـٰهَ إِلَّا ٱللَّهُ ٱللَّهُ أَكْبَرُ ٱللَّهُ أَكْبَرُ وَلِلَّهِ ٱلْحَمْدُ

*Hapana mola ila Allah (Mwenyezi Mungu) Allah Mkubwa, Allah Mkubwa na shukurani zote ni za Allah.*

ٱللَّهُ أَكْبَرُ كَبِيرًا وَٱلْحَمْدُ لِلَّهِ كَثِيرًا وَسُبْحَـٰنَ ٱللَّهِ بُكْرَةً وَأَصِيلًا

*Allah Mkubwa aliyetukuka, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa wingi, na namtakasa asubuhi na jioni.*

لَآ إِلَٰهَ إِلَّا ٱللَّهُ وَلَا نَعْبُدُ إِلَّآ إِيَّاهُ مُخْلِصِينَ لَهُ ٱلدِّينَ وَلَوْ
كَرِهَ ٱلْكَٰفِرُونَ

*Hapana mola ila Allah. Wala hatumuabudu yeyote ila Yeye peke yake, tunamtakasa Yeye na dini yake hata kama watachukia makafiri.*

لَآ إِلَٰهَ إِلَّا ٱللَّهُ وَحْدَهُ وَصَدَقَ وَعْدَهُ وَنَصَرَ عَبْدَهُ
وَأَعَزَّ جُنْدَهُ وَهَزَمَ ٱلْأَحْزَابَ وَحْدَهُ

*Hapana mola ila Allah peke yake. Ameisadikisha(ameitimiza) ahadi yake na akamnusuru mja(Mtume) wake, na akalitukuza jeshi lake, akalipa ushindi kundi lake.*

*Hapana mola ila Allah. Allah Mkubwa. Ewe; Allah, teremsha Rehma zako juu ya Muhammad, na Maswahaba wake Muhammad, na waliomnusuru Muhammad, na Wakeze Muhammad, na kizazi chake Muhammad, na uwape salama na amani kwa wingi.*

Ni vibaya mno kumuasi Allah(s.w) siku ya Idd. Mtume (s.a.w) amesema kuwa mwenye kumuasi Allah(s.w) siku ya Idd ni sawa na aliyemuasi Allah(s.w) katika uwanja wa hisabu(siku ya kiyama).

**Funga za Sunnah**

Funga za Sunnah ni funga za ziada anazofunga Muislamu kwa hiari yake baada ya mwezi wa Ramadhani. Mtume (s.a.w.) mbali ya mwezi wa Ramadhani, alikuwa akifunga mara kwa mara katika siku au tarehe maalum. Pia ametukokoteza tumuigize katika kutekeleza funga hizo. Funga za Sunnah zilizokokotezwa ni hizi zifuatazo:

(1) Kufunga siku sita katika mwezi wa Shawwal.
(2) Kufunga siku tatu kila mwezi. Ni vizuri kufunga siku hizi katika siku za mbala- mwezi kali, mwezi 13, 14 na 15.
(3)Kufunga siku za Jumatatu na Alhamisi.
(4) Kufunga siku ya Arafa - mwezi 9 Dhul-Hijjah.
(5) Kufunga siku ya mwezi 10 Muharram (siku ya Ashura).
(6) Kufunga kwa wingi katika mwezi wa Shaaban.

Funga za sunnah pamoja na kumkurubisha Muislamu kwenye ucha Mungu, huikamilisha funga ya Ramadhani pale ilipokuwa na mapungufu.

**Siku zilizoharamishwa kufunga Sunnah**

Kuna siku ambazo Waislamu wameharamishwa kufunga sunnah. Siku hizi ni:

(1) Sikukuu mbili za Idd.
(2) Siku za Tashrik - mwezi 11, 12 na 13 Dhul-Hijjah.
(3) Siku ya shaka. Siku ya shaka ni mwezi 29 au 30 Shaaban.
(4) Siku ya Ijumaa iwapo funga hiyo sio ya kuendelea.

## Zoezi la Tatu

1.(a) Swala itasimama pale Muislamu atakapotekeleza yafuatayo:

(i)_______(ii)________(iii)____________

(b)Muislamu analazimika kusimamisha swala kwa sababu kuu zifuatazo:

(i)_______________(ii)________________(iii)_______________

(c)Kwa mujibu wa Qur-an lengo la swala ni__________________.

2.(a) Swala zilizofaradhishwa kwa waislamu ni hizi zifuatazo:

(i)________(ii)_______(iii)_______(iv)______(v)________________.

(b)Orodhesha swala kumi (10) za sunnah.

(c)Waislamu wakisimamisha swala vilivyo hupata faida zifuatazo:

(i)______.(ii)______.(iii)_______.(iv)_______.(v)________.

(vi)______(vii)______(viii)_______(ix)_________(x) _____.

3. (a) Zakat ni neon la Kiarabu lenye maana ya _______ hivyo Zakat ______ mali ya mtoaji.

(b)Katika sheria ya Kiislamu sadaqa ni ___________________.

(c)Masharti ya utoaji wa Zakat na sadaqat ni:

(i)________(ii)________(iii)________(iv)________

4. (a) Nukuu aya ya Qur-an inayotuamrisha kufunga.

(b)Waislamu wameamrishwa kufunga ili ________.

(c)Lailatul-Qadr ni ____________________________________.

(d)Katika suiku wa Lailatul-Qadr, Mtume (s.a.w) ametuhimiza tuombe msamaha kwa Allah (s.w) kwa kusema: "__________________________.

(e)Itiqaf ni __________________________________________________.

(f)Baada ya mwezi wa Shawwal kuandamana na kabla ya ksuwali swala ya Iddil-fitr, kila Muislamu analazimika kutoa au kutolewa ________________.

(g)Katika kusheerehekea Idd Muislamu anatakiwa afanye yafuatayo:

(i)_______(ii)_______.(iii)______.(iv)_______(v)_______.

(h)Pamoja na Ramadhani, Musialmu anayemfuata Mtume (s.a.w) vilivyo hufunga sunnah zifuatazo:

(i)___________(ii)___________

(i)Siku zilizoharamishwa kufunga sunnah ni hizi zifuatazo:

(i)_______(ii)_______(iii)_______(iv)_______

## Sura ya Nne

# Akhlaq

**Kujipamba na tabia njema**

Tabia njema ndio kielelezo cha Uislamu wa mtu. Mtume (s.a.w.) katika kuonyesha umuhimu wa kujipamba na tabia njema anatufahamisha katika Hadith zifuatazo:

*(1) Abdullah bin Amr(r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Aliyebora kuliko wote miongoni mwenu ni yule aliyewazidi kwa tabia njema". (Bukhari na Muslim).*

*(2) Harithat bin Wahab(r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Ambaye tabia yake ni mbaya na katili hataingia peponi" (Abu Daud).*

*(3) Abu-Darda(r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah(s.w) amesema: "Kitu kizito kuliko vyote kitakachowekwa katika mizani ya muumini siku ya Hisabu ni tabia njema na Allah(s.w) anamchukia mtu asiye na haya mzungumzaji wa mazungumzo yasiyo na maana." (Tirmidh).*

Kiigizo chetu cha tabia njema ni Mtume Muhammad (s.a.w.) ambaye Allah (s.w.) anamsifu katika Qur'an:

وَإِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقٍ عَظِيمٍ ﴿٤﴾

*Na bila shaka una tabia njema kabisa". (68:4)*

**Vipengele vya tabia njema**

Baadhi ya vipengele vya tabia njema ambavyo Waislamu hawana budi kujipamba kwavyo ni:

**Kujielimisha kwa ajili ya Allah(s.w)**

Elimu ndio zana kuu ya kumuwezesha mwanaadamu kusimamisha utawala wa Allah (s.w.) hapa ulimwenguni. Ndio maana elimu imefanywa kuwa faradhi ya kwanza kwa Waislamu. Amri ya kwanza aliyopewa Mtume (s.a.w) ni:

ٱقْرَأْ بِٱسْمِ رَبِّكَ ٱلَّذِى خَلَقَ ﴿١﴾

*"Soma kwa jina la Mola wako aliyeumba". (96:1)*

Kila Muislamu anaamrishwa kutafuta elimu za fani zote aziwezazo ili aweze kumuabudu Mola wake ipasavyo na ili aweze kushiriki katika kusimamisha na kuendesha Dola ya Kiislamu.

**Kuwa na Ikhlas**

Ikhlas ni kufanya kila jambo jema kwa ajili ya Allah (s.w.) tu. Kuwafanyia watu Ihsan kwa kutoa huduma au mali bila ya kutarajia chochote kutoka kwao. Wale wanaotoa misada kwa wanaohitajia kwa Ikhlas wamesifiwa na Allah (s.w.) katika Qur'an:

وَيُطْعِمُونَ ٱلطَّعَامَ عَلَىٰ حُبِّهِۦ مِسْكِينًا وَيَتِيمًا وَأَسِيرًا
﴿٨﴾ إِنَّمَا نُطْعِمُكُمْ لِوَجْهِ ٱللَّهِ لَا نُرِيدُ مِنكُمْ جَزَآءً وَلَا
شُكُورًا ﴿٩﴾

*"Na huwalisha chakula maskini na yatima na wafungwa, na hali ya kuwa wenyewe wanakipenda. (Husema wenyewe katika nyoyo zao wana;powapa chakula hicho). Tunakulisheni kwa ajili ya kutaka radhi ya Allah tu, hatutaki kwenu malipo wala shukrani. (76:8-10).*

**Kujiepusha na Riya**

Riya ni kinyume cha Ikhlas. Kufanya riya ni kufanya jambo jema ili watu wakuone, wakusifu au wakulipe kwa njia moja au nyingine. Mtu anayefanya riya hafanyi wema kwa kutarajia malipo kutoka kwa Allah (s.w.) bali hufanya kwa kutarajia malipo ya hapa duniani tu, iwe ni mali au sifa au shukrani.

Mwenye kufanya riya hata akijiita Muislamu hana malipo yoyote mbele ya Allah(s.w), isipokuwa adhabu kali kama Qur'an inavyokamia:

فَوَيْلٌ لِّلْمُصَلِّينَ ﴿٤﴾ ٱلَّذِينَ هُمْ عَن صَلَاتِهِمْ سَاهُونَ ﴿٥﴾
ٱلَّذِينَ هُمْ يُرَآءُونَ ﴿٦﴾

*"Basi adhabu kali itawathibitikia wanoswali. Ambao wanapuuza swala zao, ambao hufanya riya". (107:4-6)*

Katika Hadith Mtume (s.a.w.) amesema:

*"Katika siku ya hukumu vitendo vyote vilivyofanywa hapa duniani vitahudhurishwa mbele ya Allah (s.w.). Vitendo vilivyofanywa kwa ajili ya Allah (s.w.) vitatengwa. Na vitendo vingine vilivyofanywa kwa riya vitatupwa motoni". (Baihaqi).*

**Kujiepusha na unafiki**

Mnafiki ni yule anayekubali Uislamu mdomoni (kwa kauli tu) lakini moyoni mwake na katika matendo yake anakanusha. Wanafiki wanabainishwa vyema katika aya ifuatayo:

وَمِنَ ٱلنَّاسِ مَن يَقُولُ ءَامَنَّا بِٱللَّهِ وَبِٱلْيَوْمِ ٱلْءَاخِرِ وَمَا هُم بِمُؤْمِنِينَ ﴿٨﴾ يُخَٰدِعُونَ ٱللَّهَ وَٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَمَا يَخْدَعُونَ إِلَّآ أَنفُسَهُمْ وَمَا يَشْعُرُونَ ﴿٩﴾

*"Na katika watu wako wasemao 'Tumemuamini Allah na siku ya Mwisho na hali ya kuwa wao si wenye kuamini. Wanataka kumdanganya Allah na wale walioamini, lakini hawadanganyi ila nafsi zao, na hawatambui". (2:8-9).*

Wanafiki ni maadui wakubwa wa Uislamu na ni wabaya zaidi kuliko Makafiri kwa sababu wao hutoa siri za ndani za Waislamu na kuwapelekea maadui wa Uislamu miongoni mwa makafiri, Wayahudi na Wakristo ili wapate kuuhilikisha Uislamu kirahisi. Hivyo watastahiki adhabu kali kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

إِنَّ ٱلْمُنَٰفِقِينَ فِى ٱلدَّرْكِ ٱلْأَسْفَلِ مِنَ ٱلنَّارِ وَلَن تَجِدَ لَهُمْ نَصِيرًا

*"Bila shaka wanafiki watakuwa katika tabaka ya chini kabisa katika moto. Hutamkuta kwa ajili yao msaidizi:. (4:145).*

Pamoja na sifa kadhaa zinazoainisha unafiki zilizoorodheshwa katika aya mbalimbali za Qur'an, Mtume (s.a.w.) anatufahamisha sifa nne za wanafiki katika Hadith ifuatayo:

*"Mtume (s.a.w) amesema: Mambo manne akiwanayo mtu humfanya awe mnafiki wa wazi hata kama anaswali, anafunga na anadai kuwa ni muumini. Anayesema uwongo kila anapoongea, anayevunja ahadi kila anapoahidi, anayehini amana kila anapoaminiwa na anayechupa mipaka kila unapotokea ugomvi". (Bukhari).*

Muislamu wa kweli hana budi kujiepusha na unafiki kwa kujiepusha na tabia za kinafiki.

**Kuwa mkweli**

Ukweli ni uhakika wa jambo. Muislamu wa kweli hana budi kuwa mkweli na kuwa tayari kusimamisha ukweli. Allah (s.w.) anatuamrisha tuwe wakweli katika kuendesha shughuli zetu zote.

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ ٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ وَكُونُوا۟ مَعَ ٱلصَّٰدِقِينَ ﴿١١٩﴾

*"Enyi mlioamini! Mcheni Allah na kuweni pamoja na wakweli". (9:119).*

"Msema kweli ni mpenzi wa Mungu". Msemo huu wa Kiswahili unathibitishwa na aya zifuatazo:

قَالَ ٱللَّهُ هَٰذَا يَوْمُ يَنفَعُ ٱلصَّٰدِقِينَ صِدْقُهُمْ ۚ لَهُمْ جَنَّٰتٌ
تَجْرِى مِن تَحْتِهَا ٱلْأَنْهَٰرُ خَٰلِدِينَ فِيهَآ أَبَدًا ۚ رَّضِىَ ٱللَّهُ
عَنْهُمْ وَرَضُوا۟ عَنْهُ ۚ ذَٰلِكَ ٱلْفَوْزُ ٱلْعَظِيمُ ﴿١١٩﴾

*"Allah (s.w.) atasema: Hii ndiyo siku ambayo wakweli utawafaa ukweli wao. Wao watapata bustani zipitazo mbele yake mito. Humo Watakaa milele. Allah amewawia radhi nao wana radhi naye. Huku ndiko kufaulu kukubwa". (5:119)*

**Kujiepusha na uwongo**

Uwongo ni kinyume cha ukweli. Uwongo ni "giza" na ukweli ni "nuru". Uwongo ni upotofu na ukweli ni uongofu. Ambapo ukweli ni uhakika wa asili wenye kudumu, uwongo ni uzushi ambao hutoweka mara tu ukweli unaposimama kama tunavyokumbushwa katika Qur'an:

وَقُلْ جَآءَ ٱلْحَقُّ وَزَهَقَ ٱلْبَٰطِلُ ۚ إِنَّ ٱلْبَٰطِلَ كَانَ زَهُوقًا ﴿٨١﴾

*"Na sema: Ukweli umefika na uwongo umetoweka. Hakika uwongo ndio wenye kutoweka". (17:81).*

Uwongo ni wenye kumuangamiza mtu hapa duniani na akhera. Uongo ni miongoni mwa maovu makubwa mbele ya Allah (s.w.) kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*"Abu Bakr(r.a) amesilimua kuwa Mtume wa Allah amesema: Nikufahamisheni juu ya madhambi makubwa katika madhambi makubwa? Sikia! Ni kumshirikisha Allah (s.w.), kutotii wazazi na kusema uwongo". (Bukhari - Muslim).*

Katika Hadith nyingine tunafahamishwa:

*"Abu Bakr (r.a) anasilimua kuwa Mtume wa Allah aliuliza: "Je, nikufahamisheni madhambi makubwa?" Aliuliza swali hilo mara tatu. Tukamjibu: Kwanini usitufahamishe, Ee Mtume wa Allah?" Akaeleza, kutotii wazazi na kuua mtu pasina hatia". Alikuwa ameinama. Kisha aliinuka na kuendelea, "Na kusema uwongo na kutoa ushahidi wa uwongo". Aliendelea kurudia hili mpaka tukaanza kujishauri kuwa ingekuwa vyema kama tusingelimuuliza". (Bukhari).*

Mtume (s.a.w) anatukataza kusema uongo hata kwenye mazungumzo ya utani. Pia Mtume (s.a.w) ametukataza hata kuwadanganya watoto wakati wa kuwabembeleza. Mtume (s.a.w) amesisitiza kuwa kama utambembeleza mtoto kwa ahadi ya kumletea pipi ni lazima umletee.

**Kuwa muaminifu**

Uaminifu ni uchungaji wa amana. Amana ni kitu chochote halali alichokabidhiwa mtu ili akihifadhi na kukirudisha kwa mwenyewe atakapokihitaji au ili akitumie kulingana na masharti ya halali aliyopewa au akifikishe mahali palipokusudiwa. Mali aliyokabidhiwa mtu na mtu mwingine au umma ni amana, uongozi au cheo alichopewa mtu na jamii ni amana, hadhi ya ukhalifa aliyotunukiwa mwanaadamu na Mola wake ni amana.

Muumini wa kweli ni yule anayejitahidi kuchunga amana kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

قَدْ أَفْلَحَ ٱلْمُؤْمِنُونَ ﴿١﴾ وَٱلَّذِينَ هُمْ لِأَمَٰنَٰتِهِمْ وَعَهْدِهِمْ رَٰعُونَ

*"Hakika wamefuzu waumini ... ambao amana zao na ahadi zao wanaziangalia". (23:1,8).*

Asiyechunga amana si muumini bali mnafiki. Miongoni mwa sifa za wanafiki alizoziainisha Mtume (s.a.w) ni yule anayekhini kila anapoaminiwa.

**Kuwa muadilifu**

Uadilifu ni usimamizi wa ukweli na kutoa haki kwa kila anayestahiki kulingana na ukweli. Allah (s.w.) ametuamrisha kuwa waadilifu kama ifuatavyo:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ كُونُوا۟ قَوَّٰمِينَ بِٱلْقِسْطِ شُهَدَآءَ لِلَّهِ وَ
لَوْ عَلَىٰٓ أَنفُسِكُمْ أَوِ ٱلْوَٰلِدَيْنِ وَٱلْأَقْرَبِينَ ۚ إِن يَكُنْ غَنِيًّا أَوْ
فَقِيرًا

*"Enyi mlioamini! Kuweni wenye kusimamia uadilifu, mtoao ushahidi kwa ajili ya Allah ijapokuwa ni juu ya nafsi zenu au wazazi au jamaa, akiwa tajiri au maskini". (4:135).*

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ كُونُوا۟ قَوَّٰمِينَ لِلَّهِ شُهَدَآءَ بِٱلْقِسْطِ ۖ وَلَا
يَجْرِمَنَّكُمْ شَنَـَٔانُ قَوْمٍ عَلَىٰٓ أَلَّا تَعْدِلُوا۟ ۚ ٱعْدِلُوا۟ هُوَ أَقْرَبُ
لِلتَّقْوَىٰ ۖ وَٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ خَبِيرٌۢ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿٨﴾

*"Enyi mlioamini! Kuweni wasimamizi kwa ajili ya Allah, muwe mkitoa ushahidi kwa uadilifu. Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutofanya uadilifu". (5:8)*

**Kuchunga ahadi**

Muislamu anapoahidi kutekeleza jambo fulani ambalo ni halali (au ni jema) analazimika kutekeleza ahadi hiyo kama Allah (s.w.) anavyotuamrisha:

وَأَوْفُوا۟ بِٱلْعَهْدِ ۖ إِنَّ ٱلْعَهْدَ كَانَ مَسْـُٔولًا ﴿٣٤﴾

*"Na timizeni ahadi. Kwa hakika ahadi itaulizwa". (17:34)*

Ahadi kubwa anayoitoa Muislamu ni shahada. Katika kushuhudia tunaahidi kuwa tutamuabudu Allah (s.w) pekee kwa kufuata maamrisho yake yote na kuacha makatazo yake yote na kuwa tutakifanya kitabu chake kiwe ndio mwongozo wetu pekee wa maisha kwa kuzingatia sunnah ya Mtume wetu (s.a.w). Tutakapoishi kinyume na shahada tutakuwa tumevunja ahadi ya shahada na tutakuwa wanafiki.

**Kuwa na kauli njema**

Muislamu anatakiwa kila mara azungumze maneno ya maana na ya kheri. Ulimi utumike kusema ukweli, kuamrisha mema, kukataza maovu, kuwashauri wengine juu ya mambo ya kheri, kupatanisha waliogombana, kumsabihi Allah (s.w.), kutoa elimu yenye kunufaisha watu na katika mazungumzo mengine ya kheri. Allah (s.w.) anatuamrisha kusema maneno mazuri katika aya ifuatayo:

وَقُل لِّعِبَادِى يَقُولُوا۟ ٱلَّتِى هِىَ أَحْسَنُ ۚ إِنَّ ٱلشَّيْطَـٰنَ يَنزَغُ
بَيْنَهُمْ ۚ ٱلشَّيْطَـٰنَ كَانَ لِلْإِنسَـٰنِ عَدُوًّا مُّبِينًا ﴿٥٣﴾

*"Na waambie waja wangu waseme daima maneno yaliyo mazuri. Maana shetani huchochea ugomvi baina yao. Hakika shetani kwa wanaadamu ni adui aliye dhahiri". (17:53).*

Hivyo Muislamu hana budi kuzungumza na watu kwa maneno mazuri yenye heshima. Maneno mazuri ya heshima hujenga na kuzidisha upendo baina ya watu. Kauli njema ni yenye kumuongoza mja kwenda peponi na kauli mbaya humuongoza mja kwenda motoni kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

"*Abu Hurairah(r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah(s.w) kasema: Mja atatamka neno lenye kumfurahisha Allah(s.w) bila ya kuona uzito wake, bado Allah humlipa malipo makubwa kutokana na neno hilo. Na mja atatamka neno lenye kumuudhi Allah(s.w) bila ya kuona uzito wake, na bado linakuwa ndio mwanzo wa kumuingiza motoni. (Bukhari)*

**Kujiepusha na maongezi yasiyo na maana**

Maongezi au mazungumzo yasiyo na maana ni yale yasiyoleta manufaa au kheri yoyote ila hasara tu. Mazungumzo haya yapo katika kupiga soga, kupiga porojo, kupiga hadithi za paukwa na pakawa, kutaniana, kubishana na mengine ya namna hiyo. Mara zote mazungumzo ya aina hii huwapelekea watu kusengenya, kusema uongo, kufitinisha, kugombana na kupoteza muda mrefu. Aidha mazungumzo ya aina hii huwasahaulisha watu kumkumbuka Allah (s.w.).

Muumini hana budi kujiepusha na tabia hii ya kujiingiza kwenye mazungumzo ya upuuzi. Miongoni mwa sifa za waumini ni pamoja na kujiepusha na mambo ya upuuzi kama tunavyojifunza katika Qur'an:

قَدْ أَفْلَحَ ٱلْمُؤْمِنُونَ ﴿١﴾ ٱلَّذِينَ هُمْ فِى صَلَاتِهِمْ خَـٰشِعُونَ ﴿٢﴾
وَٱلَّذِينَ هُمْ عَنِ ٱللَّغْوِ مُعْرِضُونَ ﴿٣﴾

"*Hakika wamefuzu waumini ambao katika swala zao ni wanyenyekevu. Na ambao hujiepusha na mambo ya upuuzi". (23:1-3).*

Muislamu anashauriwa daima abaki kimya kama hana la maana la kuzungumza. Mtume (s.a.w.) ametuusia:

"*Kuwa kimya. Hii ni njia ya kumfukuza shetani na kuimarisha dini yako" (Ahmad).*

*"Anayekuwa kimya (anaye nyamaza wakati hana la maana la kuzungumza) atakuwa salama". (Ahmad, Tirmidh).*

*"Ni katika ubora wa imani ya mtu kwa kuacha kujihusisha na mambo ya upuuzi". (Tirmidh)*

**Kujiepusha na usengenyi**

Kusengenya ni kumzungumza vibaya mtu asiyekuwapo hata kama hayo mazungumzo juu yake ni ya kweli. Maana ya kusengenya imefahamishwa vyema katika Hadith ifuatayo:

*Abu Hurairah (r.a.) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Wote mnajua kusengenya ni nini?" Walijibu, "Allah na Mtume wake ndio wajuzi zaidi". Alisema Mtume: "Maongezi juu ya ndugu yako ambayo hayapendi". Aliulizwa Mtume, "Je, kama kile kinachozungumzwa ni kweli juu ya ndugu yangu?" Akasema (Mtume): "Kama hilo unalomsengenya kwalo analo, bado utakuwa umemsengenya na kama hilo unalomsema kwalo hanalo, utakuwa umemzulia". (Muslim).*

Kama Muislamu anataka kuongea mambo mabaya ya mtu angoje mwenyewe awepo na iwe kwa nia ya kumrekebisha na wala sio kumuaibisha na kumfedhehesha. Mtume (s.a.w) ilipokuwa hanabudi aongee juu ya tabia mbaya ya mtu, alikuwa hamtaji muhusika moja kwa moja bali alikuwa akisema: "Wakoje watu hawa wanaofanya kadhaa kadhaa".

Kusengenya hakuishii tu kwenye ulimi, bali mtu aweza kusengenya kwa ishara ya macho, ulimi, midomo, mikono, miondoko na maandishi. Hata mwenye kusikiliza habari za kusengenya naye anahesabiwa kuwa amesengenya kama tunavyojifunza katika Hadith:

"*Ibn Umar(r.a) amesilimua kuwa Mtume wa Allah amesema: "Msikilizaji (wa maneno ya usengenyi) naye ni mmoja wa wasenganyaji". (Tabrani).*

Kusengenya ni miongoni mwa madhambi makubwa kwa mujibu wa Qur'an na Sunnah. Katika Qur'an Allah (s.w.) anatutahadharisha juu ya tabia ya usengenyi kama ifuatavyo:

وَيْلٌ لِّكُلِّ هُمَزَةٍ لُّمَزَةٍ ﴿١﴾

*"Adhabu kali itamthubutikia kila mlamba kisogo, msengenyi". (104:1)*

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ ٱجْتَنِبُوا۟ كَثِيرًا مِّنَ ٱلظَّنِّ إِنَّ بَعْضَ
ٱلظَّنِّ إِثْمٌ ۖ وَلَا تَجَسَّسُوا۟ وَلَا يَغْتَب بَّعْضُكُم بَعْضًا ۚ أَيُحِبُّ
أَحَدُكُمْ أَن يَأْكُلَ لَحْمَ أَخِيهِ مَيْتًا فَكَرِهْتُمُوهُ ۚ وَٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ ۚ إِنَّ
ٱللَّهَ تَوَّابٌ رَّحِيمٌ ﴿١٢﴾

*"Enyi mlioamini! Jiepusheni sana na dhana, kwani dhana ni dhambi. Wala msipeleleze (msipekue habari za watu). Wala baadhi yenu wasiwasengenye wengine. Je, mmoja wenu anapenda kula nyama ya nduguye aliye kufa? La! Hapendi. Na mcheni Allah. Bila shaka Allah ni mwenye kupokea toba na Mwingi wa kurehemu". (49:12).*

Katika Uislamu kusengenya kunaruhusiwa katika:

(a) Kushitakia dhuluma uliyofanyiwa na mtu kama inavyobainishwa katika Qur'an:

لَّا يُحِبُّ ٱللَّهُ ٱلْجَهْرَ بِٱلسُّوٓءِ مِنَ ٱلْقَوْلِ إِلَّا مَن ظُلِمَ ۚ وَكَانَ ٱللَّهُ
سَمِيعًا عَلِيمًا ﴿١٤٨﴾

*"Allah hapendi (watu) kutoa maneno ya kutangaza ubaya kwa watu wengine ila kwa yule mwenye kudhulumiwa, na Allah ndiye asikiaye ajuaye".(4:148)*

(b) Kueleza ubaya wa mtu kwa anayemuhusu ili amrekebishe.

(c) Kuwatahadharisha wengine na tabia mbaya ya mtu ili wasiathirike.

**Kujiepusha na dharau**

Kudharau wengine ni tabia mbaya na ni kitendo kiovu mbele ya Allah (s.w.). Katazo la kuwadharau watu liko bayana katika Qur'an:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ لَا يَسْخَرْ قَوْمٌ مِّن قَوْمٍ عَسَىٰٓ أَن يَكُونُوا۟
خَيْرًا مِّنْهُمْ وَلَا نِسَآءٌ مِّن نِّسَآءٍ عَسَىٰٓ أَن يَكُنَّ خَيْرًا مِّنْهُنَّ ۖ

﴿١١﴾

*"Enyi mlioamini! Wanaume wasiwadharau wanaume wenzao, huwenda wakawa bora kuliko wao; wala wanawake wasiwadharau wanawake wenzao, huwenda wakawa bora kuliko wao ..." (49:11)*

يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ إِنَّا خَلَقۡنَٰكُم مِّن ذَكَرٖ وَأُنثَىٰ وَجَعَلۡنَٰكُمۡ شُعُو
بٗا وَقَبَآئِلَ لِتَعَارَفُوٓاْۚ إِنَّ أَكۡرَمَكُمۡ عِندَ ٱللَّهِ أَتۡقَىٰكُمۡۚ إِنَّ ٱللَّهَ عَلِيمٌ
خَبِيرٞ ﴿١٣﴾

*"Enyi watu! Kwa hakika tumekuumbeni (nyote) kwa (yule) mwanamume (mmoja; Adamu) na (yule yule) mwanamke (mmoja; Hawwa). Na tumekufanyeni mataifa na makabila (mbalimbali) ili mjuane (tu basi; siyo mkejeliane). Hakika ahishimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule amchaye Mungu zaidi katika nyinyi. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye habari (za mambo yote). (49:13).*

Aya hii kwa ujumla inatuwekea msingi wa usawa. Inatukumbusha kuwa watu wote asili yao ni moja; ni watoto wa Adamu ambaye ameumbwa kutokana na udongo.

وَلَقَدۡ خَلَقۡنَا ٱلۡإِنسَٰنَ مِن صَلۡصَٰلٖ مِّنۡ حَمَإٖ مَّسۡنُونٖ ﴿٢٦﴾

*Na tulimuumba mtu kwa udongo mkavu unaotoa sauti, wenye kutokanana matope meusi yaliyovunda". (15:26).*

Tofauti za rangi, kabila, taifa, n.k. ziko pale kwa ajili ya anuani tu na kamwe zisiwe msingi wa kubaguana na kudharauliana. Pia tofauti za vipawa zilizopo kati ya watu kama vile elimu, utajiri, ufalme n.k. Isiwe sababu ya kubaguana. Vipawa hivyo ametunukiwa mwanaadamu kama mtihani kwake. Ima atamshukuru Mola wake kwa kutumia vipawa hivyo kwa ajili yake kama inavyostahiki awe mwenye kufaulu au atatakabari kwa kutumia vipawa hivyo apendavyo kinyume na maagizo ya Mola wake awe ni mwenye kufeli.

**Kujiepusha na matusi**

Mtu anayetukana ana lengo la kumdhalilisha mwingine. Waislamu tumekatazwa kutukanana na hata kuitana majina tusiyoyapenda kwa kejeli:

وَلَا تَنَابَزُواْ بِٱلۡأَلۡقَٰبِۖ بِئۡسَ ٱلِٱسۡمُ ٱلۡفُسُوقُ بَعۡدَ ٱلۡإِيمَٰنِۚ وَمَن
لَّمۡ يَتُبۡ فَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلظَّٰلِمُونَ ﴿١١﴾

*"... Wala msitukanane kwa kabila wala msiitane majina mabaya (ya kejeli). Jina baya kabisa kuitwa mtu ni "Fasiqi" baada ya kuwa yeye ni Muislamu. Na wasiotubu basi hao ndio madhalimu". (49:11).*

Fasiq ni yule aliyebobea katika uasi. Yaani mtu anayejizatiti kumuasi Allah (s.w.) kwa namna mbalimbali kama vile mwizi, mlevi, mzinzi na kadhalika. Ni vibaya mno mbele ya Allah (s.w.) kumpachika Muislamu sifa mbaya na huku hanayo. Kwa mfano ni katika madhambi makubwa kumsingizia au kumwita Muislamu mwizi na huku si mwizi au kumwita mnafiki au kafiri na huku ni Muislamu kamili. Tabia hii imekemewa vikali katika Qur'an:

إِنَّ ٱلَّذِينَ يُحِبُّونَ أَن تَشِيعَ ٱلْفَـٰحِشَةُ فِى ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ لَهُمْ
عَذَابٌ أَلِيمٌ فِى ٱلدُّنْيَا وَٱلْءَاخِرَةِ ۚ وَٱللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنتُمْ لَا تَعْلَمُونَ

*"Kwa yakini wale wanaopenda kuwabambikiza uovu wale walioamini watapata adhabu iumizayo katika dunia na katika akhera, na Allah ndiye ajuaye, na nyinyi hamjui". (24:19).*

Kutokana na makemeo haya, muumini wa kweli hana budi kujiepusha na tabia ya kuwaita watu kwa majina mabaya kwani kufanya hivyo mtu hujilaani mwenyewe kiasi kwamba hayo majina mabaya yatamgeukia, kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Abu Dh-dhari(r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Hapana mtu atakayemsingizia mwingine uasi kwa Allah au akamwita "kafiri", ila hayo yatamgeukia yeye mwenyewe iwapo huyo aliyemsingizia hayuko hivyo". (Bukhari)*

**Kujiepusha na mabishano**

Mabishano husababisha ugomvi, maudhi au kudharauliana. Mabishano yaweza kutibua uhusiano mzuri kati ya watu. Hivyo Uislamu unatukataza kubishana. Tunafundishwa katika Qur'an kuwa tukizungumza na watu ambao hawataki kuelewa bali wanafurahia ubishi tu, basi tusiendelee kuzungumza nao. Bali tuagane nao kwa usalama:

وَعِبَادُ ٱلرَّحْمَـٰنِ ٱلَّذِينَ يَمْشُونَ عَلَى ٱلْأَرْضِ هَوْنًا وَإِذَا
خَاطَبَهُمُ ٱلْجَـٰهِلُونَ قَالُوا۟ سَلَـٰمًا ﴿٦٣﴾

*"Na waja (wema) wa Rahman ni wale wanaotembea katika ardhi kwa unyenyekevu na wajinga wakisema nao, huwajibu "salama". (25:63).*

**Kujiepusha na kibri na kujiona**

Kibri, majivuno na majigambo ni katika tabia mbaya iliyokemewa vikali katika Qur'an kama ifuatavyo:

وَلَا تَمْشِ فِى ٱلْأَرْضِ مَرَحًا ۖ إِنَّكَ لَن تَخْرِقَ ٱلْأَرْضَ وَلَن تَبْلُغَ
ٱلْجِبَالَ طُولًا ﴿٣٧﴾ كُلُّ ذَٰلِكَ كَانَ سَيِّئُهُۥ عِندَ رَبِّكَ مَكْرُوهًا

"*Wala usitembee (usiende) katika ardhi kwa maringo. Hakika wewe huwezi kuipasua ardhi wala huwezi kufikia urefu wa mlima. Haya yote ubaya wake ni wenye kuchukiza mbele ya Mola wako". (17:37-38)*

Mtu mwenye kiburi hujiona kuwa ni bora, wa juu na wa maana zaidi kuliko wengine. Kibri na kujiona husababishwa na neema mja alizomtunukia na Mola wake kama vile utajiri, madaraka, umaarufu, elimu, nguvu nyingi, uzuri wa sura n.k. Mwenye kibri na kujiona anasahau kuwa kama alivyozipata neema hizi bila ya kupeleka barua yoyote ya maombi kwa Allah (s.w.) ndivyo anavyoweza kukatikiwa na neema hizi na asiweze kufanya chochote.

Katika Qur'an tunapigiwa mfano wa Karuni aliyetakabari kutokana na hiyo neema ya mali aliyokuwa nayo. Lakini Allah alipomuondolea neema hiyo hakuweza kufanya lolote. (Rejea Qur'an 28:76-83)

Kibri na majivuno humfanya mtu kuwa muovu mwenye tabia mbaya ya Dharau, ukatili, uonevu, udhalimu na kutoshaurika. Waislamu tunaaswa tujiepushe mbali na tabia hii mbaya ambayo malipo yake ni moto wa Jahannam kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

قِيلَ ٱدْخُلُوٓا۟ أَبْوَٰبَ جَهَنَّمَ خَٰلِدِينَ فِيهَا ۖ فَبِئْسَ مَثْوَى
ٱلْمُتَكَبِّرِينَ ﴿٧٢﴾

*Itasemwa: "Ingieni milango ya Jahannam mkae humo". Basi ni ubaya ulioje makazi ya wanaotakabari!* (39:72)

Pia Hadith zifuatazo zinatubainishia kina cha uovu wa kibri:

*Abu Hurairah (r.a.) amesimulia kuwa, Mtume wa Allah amesema: "Yule ambaye moyoni mwake mna chembe (punje) ya kibri hataingia peponi". Sahaba mmoja akauliza: "Je, kama mtu anapenda nguo nzuri na viatu?" Mtume (s.a.w) akasema: "Allah (s.w.) ni mzuri na anapenda vizuri. Kibri ni kukataa ukweli na kupuuza watu". (Muslim)*

*Abu Hurairah (r.a.) amesema kuwa Mtume wa Allah amesema: "Siku ya Kiyama, Allah (s.w.) hatamwangalia yule anayevaa vazi lake kwa kibri". (Bukhari na Muslim).*

Msingi mkuu wa kibri ni ukafiri - kumkadhibisha Allah (s.w.) na ujumbe wake:

سَأَصْرِفُ عَنْ ءَايَٰتِىَ ٱلَّذِينَ يَتَكَبَّرُونَ فِى ٱلْأَرْضِ بِغَيْرِ ٱلْحَقِّ
وَإِن يَرَوْا۟ كُلَّ ءَايَةٍ لَّا يُؤْمِنُوا۟ بِهَا وَإِن يَرَوْا۟ سَبِيلَ ٱلرُّشْدِ لَا
يَتَّخِذُوهُ سَبِيلًا وَإِن يَرَوْا۟ سَبِيلَ ٱلْغَىِّ يَتَّخِذُوهُ سَبِيلًا ذَٰ
لِكَ بِأَنَّهُمْ كَذَّبُوا۟ بِـَٔايَٰتِنَا وَكَانُوا۟ عَنْهَا غَٰفِلِينَ ﴿١٤٦﴾

*"Nitawaepusha na (kuzingatia) aya zangu wale wanaotakabari katika nchi pasipo haki; na ambao kila hoja wanayoiona hawaiamini; na kama wakiiona njia ya uwongofu hawaishiki kuwa ndiyo njia; lakini wakiona njia ya upotofu (upotevu) wanaishika kuwa ndiyo njia. Hayo ni kwa sababu ya kuzikadhibisha aya zetu na kuzipuuza". (7:146).*

وَٱلَّذِينَ كَذَّبُوا۟ بِـَٔايَٰتِنَا وَٱسْتَكْبَرُوا۟ عَنْهَآ أُو۟لَٰٓئِكَ أَصْحَٰبُ ٱلنَّارِ ۖ
هُمْ فِيهَا خَٰلِدُونَ ﴿٣٦﴾

*"Na wale watakaokadhibisha aya zetu na kuzifanyia kiburi hao watakuwa watu wa motoni, watakaa humo daima". (7:36)*

**Kujiepusha na kulaani ovyo**

Kulaani ovyo kumekatazwa katika Uislamu. Mtu anapolaani wengine amejisahau kuwa naye ni mkosaji. Mtume (s.a.w.) ametukataza kulaani ovyo katika Hadith ifuatayo:

*Ibn Umar (r.a.) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Si sawa kwa muumini kuwa mkubwa wa kulaani". Na katika upokezi mwingine, Mtume amesema: "Si stahiki ya muumini kuwa mkubwa wa kulaani". (Tirmidh).*

Muislamu anatakiwa ajiepushe na tabia ya kulaani na badala yake awe mwingi wa kuwasamehe wenye kukosea na kuwatakia msamaha kwa Allah (s.w.) ili naye asamehewe dhambi zake.

**Kujiepusha na viapo**

Waislamu tumekatazwa kuapa ovyo. Kiapo kinakubalika tu pale inapobidi kutolewa mbele ya kadhi kama ushahidi.

Mara nyingi mtu anayeapa apa ovyo ni muongo. Anaapa ili ahalalishe uongo wake. Kuapa apa ovyo ni tabia ya kinafiki kama tunavyofahamishwa katika Qur'an kuwa

ٱتَّخَذُوٓاْ أَيۡمَـٰنَهُمۡ جُنَّةً فَصَدُّواْ عَن سَبِيلِ ٱللَّهِۚ إِنَّهُمۡ سَآءَ مَا
يَعۡمَلُونَ ٢

*Wamevifanya viapo vyao kuwa ngao za kujikingia, wakajikinga kupitishwa njia ya Mwenyezi Mungu. Kwa hakika ni mabaya kabisa waliyokuwa wakiyaafanya(63:2)*

**Kuwa na heshima**

Katika Uislamu kila mtu anayo haki ya kuheshimiwa. Heshima ni haki ya mwanaadamu aliyozaliwa nayo. Miongoni mwa mambo ya msingi aliyousia Mtume (s.a.w.) katika khutuba yake ya kuaga aliyoitoa katika uwanja wa Arafa 9 Dhul-Hijjah 10 A.H ni kulinda heshima ya kila mtu. Aliusia:

*"Enyi watu hakika damu yenu (yaani uhai wenu), mali zenu na heshima yenu ni vitu vitakatifu. Kamwe visiharibiwe hadi mtakaposimamishwa mbele ya Mola wenu, kwani utukufu wa vitu hivyo ni kama ulivyo utukufu wa siku hii, na mwezi huu na mji huu. Kwa hakika mtakutana na Mola wenu atakuulizeni juu ya vitendo vyenu. Je, nimefikisha ujumbe? Ee! Allah shuhudia".*

Kutokana na usia huu,a kila muumini analazimika kuwaheshimu wanaadamu wenzake wakubwa na wadogo. Aseme nao kwa vizuri, asiwadharau, asiwadhalilishe, asiwafedheheshe na asiwavunjie heshima

kwa namna yoyote ile. Awatii wazazi, wenye mamlaka juu yake na walio wakubwa kwake katika mambo yanayowafikiana na Qur'an na Sunnah, awahurumie na kuwasikiliza walio chini yake au wadogo kwake. Kwani Mtume (s.a.w.) amesema:

> *"Si katika sisi yule ambaye hamheshimu mkubwa wetu na kumhurumia mdogo wetu".*

Kuwaheshimu watu kama ilivyosisitizwa katika Qur'an ni pamoja na:

(i) Kuzungumza na watu kwa kauli nzuri, kwa upole na huruma. Qur'an inatuamrisha:

وَقُولُوا۟ لِلنَّاسِ حُسْنًا

*"... Na semeni na watu kwa wema...". (2:83).*

(ii) Kuwatii wazazi, kuwahurumia na kusema nao vizuri:

وَقُل لَّهُمَا قَوْلًا كَرِيمًا

*".. Na sema nao (wazazi) kwa msemo wa heshima (kabisa)" (17:23)*

(iii) Kuanza kutoa salaam kwa waumini:

وَإِذَا جَآءَكَ ٱلَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِـَٔايَـٰتِنَا فَقُلْ سَلَـٰمٌ عَلَيْكُمْ ۖ

*"Na wanapofika wale wanaoamini aya zetu waambie, "Assalaam alaykum" (yaani amani iwe juu yenu)..." (6:54).*

(iv) Kurudisha salaam kwa ucheshi baada ya kusalimiwa:

وَإِذَا حُيِّيتُم بِتَحِيَّةٍ فَحَيُّوا۟ بِأَحْسَنَ مِنْهَآ أَوْ رُدُّوهَآ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ
كَانَ عَلَىٰ كُلِّ شَىْءٍ حَسِيبًا ﴿٨٦﴾

*"Na mnapoamkiwa kwa maamkio yoyote yale; basi itikieni kwa* yaliyo *bora kuliko hayo, au rejesheni hayo hayo. (4:86).*

(v) Kuwaheshimu watu wa dini nyingine kwa kutowabughudhi, kutowadharau au kutowadhalilisha kwa namna yoyote ile:

وَلَا تَسُبُّوا۟ ٱلَّذِينَ يَدْعُونَ مِن دُونِ ٱللَّهِ فَيَسُبُّوا۟ ٱللَّهَ عَدْوًۢا
بِغَيْرِ عِلْمٍ ۗ

*"Wala msiwatukane ambao wanaabudu kinyume cha Allah, wasije wakamtukana Allah kwa jeuri zao bila kujua...". (6:108)*

ٱدْعُ إِلَىٰ سَبِيلِ رَبِّكَ بِٱلْحِكْمَةِ وَٱلْمَوْعِظَةِ ٱلْحَسَنَةِ ۖ وَجَٰدِلْهُم
بِٱلَّتِى هِىَ أَحْسَنُ ۚ ﴿١٢٥﴾

*"Waite (watu )katika njia ya Mola wako kwa hekima na mawaidha mema, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora". (16:125).*

(vi) Kuwakaribisha wageni na kuwapisha kwenye viti au nafasi ya kukaa:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓا۟ إِذَا قِيلَ لَكُمْ تَفَسَّحُوا۟ فِى ٱلْمَجَٰلِسِ
فَٱفْسَحُوا۟ يَفْسَحِ ٱللَّهُ لَكُمْ ۖ وَإِذَا قِيلَ ٱنشُزُوا۟ فَٱنشُزُوا۟ يَرْفَعِ
ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ مِنكُمْ وَٱلَّذِينَ أُوتُوا۟ ٱلْعِلْمَ دَرَجَٰتٍ ۚ وَٱللَّهُ
بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرٌ ﴿١١﴾

*"Enyi mlioamini mnapoambiwa (katika mikutano). Wafanyieni wasaa wenzenu katika (nafasi za) kukaa, wafanyieni nafasi. Na Mwenyezi Mungu atakufanyieni nafasi (duniani na akhera). Na hata ikisemwa, "simameni", basi (simameni) ondokeni. Mwenyezi Mungu atawainua wale walioamini miongoni mwenu, na waliopewa elimu watapata daraja zaidi. Na Mwenyezi Mungu anazo habari za mnayoyatenda yote". (58:11).*

Ili mtu aheshimiwe hana budi kujiheshimu na kuwaheshimu wengine. Mtu asiyejiheshimu hujidharaulisha yeye mwenyewe kwa wanaadamu wenzake. Mheshimiwa zaidi mbele ya Allah (s.w.) ni yule amchaye Allah zaidi:

إِنَّ أَكْرَمَكُمْ عِندَ ٱللَّهِ أَتْقَىٰكُمْ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٌ ﴿١٣﴾

*"... Hakika aheshimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Allah ni yule amchaye Allah zaidi katika nyinyi. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye habari (za mambo yote)". (49:13)*

## ZOEZI – 4

1. (a) Orodhesha vipengele kumi (10) vya tabia njema unavyotakiwa ujipambe navyo.

   (b) Toa maelezo mafupi juu ya kila kipengele ulichochagua 1(a),

2. (a) Orodhesha vipengele vitano (5) vya tabia mbayaunavyotakiwa ujiepushe navyo:


   (b) Toa maelezo mafupi juu ya kila kipengele cha tabia mbaya ulichokiorodhesha

## Sura ya Tano

## Tarekh

### Maana ya Historia kwa mujibu wa makafiri

Makafiri wanasema, historia ni kumbukumbu ya matendo ya mwanadamu katika mapambano yake dhidi ya maumbile asilia(nature) yaliyomwezesha kupata mahitaji yake muhimu ambayo ni chakula, nguo na makazi.




Makafiri wanadai kuwa mtu wa kwanza alitokana na sokwe. Wanasema kuwa sokwe huyo alibadilika mwili akawa sokwe-mtu, kisha akawa mtu kamili.


### Chimbuko la Mtazamo wa Makafiri juu ya Historia

Chimbuko la dhana hii potofu ya makafiri juu ya Historia linatokana na uzushi wa Charles Robert Darwin juu ya asili ya mwanadamu.

Darwin anadai kuwa, mwanadamu ni mnyama aliyetokana na jamii ya masokwe.


**Hakuna ushahidi wowote wa kweli unaoweza kuthibitisha kuwa mwanadamu katokana na sokwe.Na ndiyo maana alipotakiwa kuthibitisha, Darwin alisema "Sio kwamba naweza kuthibitisha angalau jamii moja kwamba imebadilika kutoka hali moja hadi nyingine.."[1]**

[1]M. Vernet, ' L' Evolution du Monde Vivant. (1950)




Japo Darwin amekiri hawezi kuthibitisha, makafiri wanafanya jitihada kubwa sana kupotosha asili na historia halisi ya mwanadamu hapa duniani. Mfano wa upotoshaji huu ni ule uliomo katika kitabu cha Historia kwa Shule za Sekondari kilichoandikwa na Taasisi ya Elimu, kuwa:

> *" hapo mwanzo, mwanadamu alikuwa katika jamii ya manyani ijumuishayo kima, tumbili, na masokwe. Awali mwili wa sokwemtu ulionekana kufanana sana na kima. Ulikuwa mwili mkubwa wenye manyoya tele. Kadiri alivyopiga hatua katika kuboresha mbinu za upataji wa chakula, makazi na mavazi, ndivyo sokwemtu huyo alivyobadilika umbo na kuwa mtu wa sasa".*



**Makafiri hawana ushahidi wa kweli unaothibitisha kuwa mwanadamu katokana na sokwe. Michoro hii ya kubuni imepachikwa kwenye kitabu cha kwanza cha historia shule za sekondari ili kupotosha historia halisi ya mwanadanu**


**Udhaifu wa mtazamo wa makafiri juu ya historia ya mwanadamu.**

Mtazamo wa makafiri juu ya Historia ya mwanadamu hauna ushahidi wowote wa kisayansi kama wanavyojitahidi kutangaza makafiri ili kuwaghilibu watu wakubali dhana yao.

**Charles Darwin hakuwa mwanasayansi**


Kwanza, Charles Darwin aliyezusha fikra kuwa mwanadamu katokana na jamii ya masokwe hakuwa mwanasayansi. Kitabu cha historia ya wavumbuzi wa mambo mbalimbali ya kisayansi kinaeleza kuwa:

> *“Charles Darwin alizaliwa Shrewsbury, Uingereza, mtoto wa kiume wa Daktari. Alianza shule mnamo 1818 lakini hakupenda masomo na hakufaulu. Baadaye alikwenda kusomea taaluma ya tiba huko Edinburgh, Scotland, lakini hakufanya vizuri. Kwahiyo baba yake akampeleka chuo kikuu cha Cambridge kusomea mafunzo ya uchungaji wa Kanisa. Kwa mara nyingine tena akawa mwanafunzi  mchovu asiyemudu masomo,na akatumia muda mwingi katika anasa zake za kuwinda na kutalii mazingira"*[2]




**Chaguo la kimaumbile haliwezi kuibua viumbe vipya**

Pili, madai ya Darwin na wafuasi wake kuwa chaguo la kimaumbile liliweza kubadili jamii ya masokwe kuwa wanadamu si ya kweli. Ni madai ya uongo kwasababu kisayansi chaguo la kimaumbile halina uwezo wa kumuongezea kiumbe sifa mpya  kuweza kumbadili kuwa kiumbe wa jamii nyingine. Kwa mfano, ni muhali kwa chaguo la kimaumbile(natural selection) kumuongezea panya sifa mpya  kuweza kumbadili kuwa paka au swala akawa twiga.





2 Marshall Cavendish Limited -Growing up with Science-The illustrated Encyclopedia of Invention (1990) uk 2195.

Chaguo la kimaumbile huendeleza wale waliomadhubuti katika jamii ya viumbe waliopo. Kwa mfano tuseme umetokea ukame katika mbuga ya wanyama ambamo ndani yake wanaishi tumbili, nyani, na sokwe; ni wazi kuwa wale waliodhaifu katika tumbili, nyani na sokwe watashindwa kuhimili taabu ya ukame na wanaweza kufa. Ila wale waliomadhubuti wataweza kusalia na kuendeleza kizazi cha jamii yao. Lakini chaguo la kimaumbile haliwezi kuwabadili nyani wawe masokwe au masokwe kuwa watu. Kisayansi imethibitika kuwa hilo haliwezekani katu kwa kuwa ni kinyume cha sheria alizoziweka Allah(s.w)

فَأَقِمْ وَجْهَكَ لِلدِّينِ حَنِيفًا فِطْرَتَ ٱللَّهِ ٱلَّتِى فَطَرَ ٱلنَّاسَ عَلَيْهَا
لَا تَبْدِيلَ لِخَلْقِ ٱللَّهِ ذَٰلِكَ ٱلدِّينُ ٱلْقَيِّمُ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ
ٱلنَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٣٠﴾

*Basi uelekeze uso wako katika dini iliyo sawa sawa, ndilo umbile Mwenyezi Mungu alilowaumbia watu. Hakuna mabadiliko katika maumbile ya viumbe vya Mwenyezi Mungu. Hiyo ndiyo dini iliyo ya haki lakini watu wengi hawajui (30:30)*

**Mifupa na mafuvu ya kale haioneshi kuwa mtu katokana na sokwe.**

Tatu, tafiti zilizofanywa juu ya mifupa na mafuvu ya kale yaliyofukuliwa chini ya ardhi hazioneshi kuwa mwanadamu ametokana na jamii ya masokwe kupitia mabadiliko ya kimwili. Lau kama katika mifupa na mafuvu hayo yangelikuwemo yale ya nyani-mtu na sokwe-mtu;madai ya Darwin na wafuasi wake yangelikuwa angalau na ukweli fulani. Lakini mifupa na mafuvu yote yaliyofukuliwa hayaonyeshi hivyo.





Mathalan, fuvu la Neanderthal lilifukuliwa mwaka 1856 na kudaiwa kuwa ni la sokwe-mtu aliyekuja badilika kuwa mwanadamu. Baada ya utafiti ikagundulika kuwa fuvu la Neanderthal halikuwa la sokwe-mtu ila la mwanadamu, hivyo dai kuwa fuvu hilo ni uthibitisho dhana ya Darwin na wafuasi wake kuwa mwanadamu katokana na sokwe likatupiliwa mbali mwaka 1960. Aidha, mnamo mwaka 1959, lilipatikana fuvu liitwalo "Zinja"(zinjanthrophus), na kufanywa kuwa ushahidi wa kuthibitisha madai

ya makafiri juu ya historia ya mwanadamu. Hata hivyo, mwaka 1960 makafiri wakaumbuka baada ya kugundulika kuwa fuvu lile lilikuwa la masokwe halisi, halikuwa na uhusiano wowote na mwanadamu.

**Ni muhali masokwe kubadilika kuwa mtu anayetembea wima**

Nne haiwezekani sokwe kubadilika kuwa mtu anayetembea wima. Kwasababu maumbile ya mifupa na viungo vya sokwe humuwezesha kutembea kwa miguu na mikono bila shida. Mifupa ya mikono ya sokwe ni mirefu na uti wa mgongo umepinda kwa mbele ili kuwawezesha kutembea kwa mikono na miguu. Hii ni tofauti na mwanadamu ambaye mifupa na viungo vyake hufanya kutembea wima kwa miguu miwili kuwa jambo la kawaida kwake.





**Muundo wa mifupa ya mwili wa sokwe ni tofauti na mwanadamu, ni muhali sokwe kubadilika kuwa mtu anayetembea wima**

Tano, ushahidi mwingine unaokanusha kuwa sokwe hawawezi kubadilika na kuwa mwanadamu anayetembea wima kwa miguu miwili ni kutofautiana kwa ***semisekula*** kanali zilizoko katika sehemu za ndani ya sikio(cochlea). Muundo na kazi ya semisekula kanali humfanya kiumbe ama atembee kwa miguu minne au atembee wima kwa miguu miwili.Utafiti uliofanywa na mwanasayansi Fred Spoor umeonesha kuwa muundo wa semisekula kanali za sokwe ni maalum kwa kumpa 'balance' ya kutembea kwa miguu na mikono. Lakini mwanadamu ni tofauti kabisa na sokwe, muundo wa semisekula kanali za mwanadamu hufanya kazi ya kumpa 'balance' ya kutembea wima kwa miguu miwili.

**Ghushi na uzushi wa makafiri**

Sita, walipokosa ushahidi wa mifupa na mafuvu ya sokwe-mtu iliotarajiwa kuwa ingethibitisha mtazamo wao, makafiri wakaanza kughushi ushahidi bandia kutaka kuonesha kuwa uwongo wao juu ya historia ya mwanadamu kwamba katokana na jamii ya masokwe, ni jambo la kweli.




OtaBenga aliyetekwa na makafiri akiwa amefungwa kwenye zizi na kudhalilishwa kama mnyama


Mnamo mwaka 1904 makafiri walivamia Congo na kumteka mwafrika aliyeitwa Ota Benga, wakamfunga minyororo na kumtia kwenye tundu, kisha wakampeleka Marekani. Katika maonyesho ya kimataifa ya mtakatifu Luis na yale ya New York , Ota Benga akadhalilishwa kwa kuwekwa zizini pamoja na nyani, kima na sokwe. Kisha pasina kuona haya, William T. Hornaday akatoa hutuba akieleza kuwa Ota Benga ni mfano mzuri wa sokwe aliyebadilika na kuwa sokwe-mtu anayefanana na mwanadamu.

Mwaka1912, mfuasi wa Darwin aitwaye Charles Dawson alifukua fuvu la mtu na taya la sokwe huko Piltdown, Uingereza. Kisha akaviunganisha na kudai kuwa ni la sokwe-mtu aliyekuja kuwa mwanadamu. Lakini Baada ya miaka arobaini kupita, jopo la watafiti likang'amua mwaka 1953 kuwa palikuwa pamefanyika ghushi ya kuunganisha fuvu la mtu na taya la sokwe kwa lengo la kupotosha historia halisi ya mwanadamu.




**Makafiri hurubuni kwa michoro na masanamu ya uwongo**

Saba, hakuna ushahidi wowote wanaoweza kutoa makafiri kuuthibitishia ulimwengu kuwa sisi wanadamu tumetokana na masokwe. Wamebaki kutumia uwongo wa kuchora na kuchonga viumbe wa kufikirika ambao hawajawahi kabisa kuishi katika dunia. Michoro na masanamu yote ya nyani-mtu au sokwe-mtu imekuwa ikibuniwa na makafiri ili kuwazuga watu na kupotosha historia ya mwanadamu.



**Hii ni michoro ya kubuni tu! Hakuna ushahidi wowote wanaoweza kutoa makafiri kuuthibitishia ulimwengu kuwa sisi wanadamu tumetokana na masokwe**

Uzushi huu wa makafiri kubuni michoro ya uongo umewafanya wanasayansi kuandika vitabu mbalimbali ili kukosoa ghiliba za makafiri hawa. Miongoni mwa vitabu hivyo ni vile vilivyoandikwa na Tuane Gish, Lee Spetner na Jonathan Wells. Vitabu hivi vimeandikwa kwa lugha ya Kiingereza.




**Hivi ni baadhi tu ya vitabu vinavyopinga uzushi wa makafiri kuhusu historia ya mwanadamu**

**Maana ya Historia kwa mujibu wa Uislamu**

Kwa mujibu wa Uislamu, historia ni kumbukumbu za matendo ya watu na matokeo ya matendo hayo katika maisha ya dunia na akhera. Allah(s.w) aliumba ulimwengu na vilivyomo na baada ya muda mrefu kupita akamuumba mtu na kumleta duniani:

هَلْ أَتَىٰ عَلَى ٱلْإِنسَٰنِ حِينٌ مِّنَ ٱلدَّهْرِ لَمْ يَكُن شَيْـًٔا مَّذْكُورًا

*Hakika ulimpita binadamu wakati mrefu katika dahari, hakuwa kitu kinachotajwa(76:1)*

Kwa maneno mengine, historia ni rekodi ya amali zote za mwanadamu alizozifanya kwa kuacha au kufuata mwongozo wa Mwenyezi Mungu kwa mujibu wa lengo la uhai na hadhi yake hapa duniani pamoja na athari za matendo hayo katika maisha ya dunia na kesho Akhera. Maana hii inajitokeza pale Mwenyezi Mungu anaposema ndani ya Qur,an kuwa:

إِنَّا نَحْنُ نُحْىِ ٱلْمَوْتَىٰ وَنَكْتُبُ مَا قَدَّمُوا۟ وَءَاثَٰرَهُمْ ۚ
وَكُلَّ شَىْءٍ أَحْصَيْنَٰهُ فِىٓ إِمَامٍ مُّبِينٍ ﴿١٢﴾

*Kwa yakini Sisi tutawafufua wafu, na Tunayarekodi matendo waliyoyafanya pamoja na athari za matendo hayo. Na kila kitu tunakihifadhi katika daftari linalobainisha(36:12)*

Matendo ya wanadamu kijamii, kiuchumi na kisiasa huweza kuwa mema au maovu. Amali za waumini kisiasa, uchumi na mahusiano yao katika jamii zimejikita katika matendo mema yanayonufaisha walimwengu wote. Lakini makafiri wanaomkanusha Mwenyezi Mungu hutenda maovu katika kuchuma na hawatendi mema ipasavyo katika siasa na mahusiano yao na jamii.

Hii ni kutokana na kutokujua asili na lengo la maisha ya mwanadamu hapa duniani kwa kule kupuuza kwao mwongozo wa Mwenyezi Mungu aliyewaumba, na kufuata matashi ya nafsi zao. Hivyo matendo yao huiathiri vibaya jamii na hatima ya maongozi yao ni kuwatia watu katika maisha ya dhiki hapa duniani na adhabu ya moto huko akhera.

وَمَنْ أَعْرَضَ عَن ذِكْرِى فَإِنَّ لَهُۥ مَعِيشَةً ضَنكًا وَنَحْشُرُهُۥ يَوْ
مَ ٱلْقِيَٰمَةِ أَعْمَىٰ ﴿١٢٤﴾

*Na atakayejiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini ataishi maisha ya dhiki( hapa duniani), na siku ya Kiyama Tutamfufua hali ya kuwa kipofu(20:124)*

## Kwanini tujifunze Historia?

### Historia hutuonesha asili na hadhi yetu juu ya viumbe wengine hapa duniani

Tumeona kwamba hakuna ushahidi wowote wa historia au sayansi unaothibitisha madai ya makafiri kuwa mwanadamu katokana na jamii ya masokwe(apes). Historia inaonesha na kutufunza kuwa tangu awali mwanadamu aliumbwa akiwa mtu kamili aliyekuwa na fahamu na elimu kubwa juu ya mazingira ya maisha ya duniani. Mwenyezi Mungu amemtunukia mwanadamu ufahamu au uwezo mkubwa wa kujielimisha pamoja na elimu kubwa kulingana na hadhi yake ya kuwa Khalifa hapa duniani. Hadhi hii ya mwanadamu kuutawala ulimwengu na viumbe wote kwa kutumia mwongozo wa Allah(s.w) inadhihirishwa katika aya zifuatazo:

وَلَقَدْ كَرَّمْنَا بَنِيٓ ءَادَمَ وَحَمَلْنَٰهُمْ فِي ٱلْبَرِّ وَٱلْبَحْرِ وَ
رَزَقْنَٰهُم مِّنَ ٱلطَّيِّبَٰتِ وَفَضَّلْنَٰهُمْ عَلَىٰ كَثِيرٍ مِّمَّنْ خَلَقْنَا
تَفْضِيلًا ﴿٧٠﴾

*Na bila shaka tumemtukuza mwanadamu, na tumempa vya kupanda nchi kavu na baharini, na tumewaruzuku vitu vizuri vizuri na tumewatukuza kuliko wengi katika wale tuliowaumba kwa utukufu ulio mkubwa (17:70)*

### Hutukumbusha lengo la kuumbwa kwetu na namna ya kulifikia

Historia pia hutukumbusha lengo la kuumbwa kwetu na namna ya kulifikia lengo hilo. Tunafahamishwa katika Qur,an kuwa kabla hatujayaanza maisha ya duniani, Mwenyezi Mungu kwa uweza wake alituwezesha kumtambua na kisha tukachukua ahadi kuwa hatutamwabudu kiumbe yeyote wala kufuata mwongozo wa asiyekuwa Mwenyezi Mungu katika kuendesha maisha yetu yote ya hapa duniani. Tukio hilo limeelezwa katika aya ifuatayo:

وَإِذْ أَخَذَ رَبُّكَ مِنۢ بَنِيٓ ءَادَمَ مِن ظُهُورِهِمْ ذُرِّيَّتَهُمْ
وَأَشْهَدَهُمْ عَلَىٰٓ أَنفُسِهِمْ أَلَسْتُ بِرَبِّكُمْ قَالُوا۟ بَلَىٰ شَهِدْنَآ
أَن تَقُولُوا۟ يَوْمَ ٱلْقِيَٰمَةِ إِنَّا كُنَّا عَنْ هَٰذَا غَٰفِلِينَ ﴿١٧٢﴾

*Na Mola wako alipowaleta wanaadamu kutoka miongoni mwa kizazi chao, na akawashuhudisha juu ya nafsi zao; (akawaambia)*

*"Je mimi si Mola wenu?" wakasema: "Ndiyo tunashuhudia". Allah akasema: "Msije mkasema Siku ya kiyama kuwa sisi tulikuwa tumeghafilika na hayo(hatujui). Au mkasema, "Baba zetu ndio walioshirikisha zamani, nasi tulikuwa kizazi nyuma yao, basi utatuangamiza kwa sababu ya yale waliyoyafanya waovu?"(7:172-173)*

Na katika aya nyingine Mwenyezi Mungu anatukumbusha jinsi mwanadamu aliposisitizwa hili hapo awali kabisa wakati anaanza maisha katika dunia kuwa ni wale tu watakaofuata mwongozo wa Mwenyezi Mungu katika kuendesha maisha yao ya kila siku ndio watakaoishi kwa furaha na amani hapa duniani na kustahiki starehe za kudumu katika pepo zenye neema huko Akhera. Na akaonya wale watakaokataa kufuata mwongozo wake, kwamba watakuwa na maisha ya dhiki duniani, na akhera watadumu katika adhabu ya moto.

قُلْنَا ٱهْبِطُوا۟ مِنْهَا جَمِيعًا ۖ فَإِمَّا يَأْتِيَنَّكُم مِّنِّى هُدًى فَمَن تَبِعَ
هُدَاىَ فَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٣٨﴾
وَٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ وَكَذَّبُوا۟ بِـَٔايَـٰتِنَآ أُو۟لَـٰٓئِكَ أَصْحَـٰبُ ٱلنَّارِ ۖ
هُمْ فِيهَا خَـٰلِدُونَ ﴿٣٩﴾

*Tukasema shukeni humo nyote, na kama ukikufikieni uongozi utokao kwangu, basi watakaoufuata uongozi wangu huo haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika. Lakini wenye kukufuru na kuyakadhibisha maneno Yetu, hao ndio watakaokuwa watu wa Motoni, humo watakaa milele.(2:38-39)*

**Hutuonesha namna Mwenyezi Mungu alivyotuneemesha ili tuweze kumwabudu ipasavyo**

Kila umma au kaumu katika historia ya mwanadamu iliruzukiwa neema mbalimbali katika rasilimali, elimu na teknolojia zilizolenga kuwawezesha kufikia lengo la maisha kwa urahisi. Katika hili historia inatuonesha ukweli usiopingika kuwa Mwenyezi Mungu ametuneemesha zaidi sisi kuliko kaumu zilizotangulia. Maendeleo ya sayansi na teknolojia tuliyonayo sasa yameifanya dunia kuwa kama kijiji kwa kumuwezesha mwanadamu kufika au kuwasiliana na watu wa pande zote za dunia. Kwahiyo inakuwa rahisi katika zama hizi kuitikia wito wa Mwenyezi Mungu pale alipotuamrisha kuwa:

قُلۡ سِيرُواْ فِي ٱلۡأَرۡضِ فَٱنظُرُواْ كَيۡفَ بَدَأَ ٱلۡخَلۡقَۚ ثُمَّ ٱللَّهُ يُنشِئُ ٱلنَّشۡأَةَ ٱلۡأٓخِرَةَۚ إِنَّ ٱللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيۡءٖ قَدِيرٞ ٢٠

*Sema: Tembeeni katika ardhi ili muone namna Mwenyezi Mungu alivyoanzisha maumbile; Kisha atavirudisha kwa mara ya pili. Na Mwenyezi Mungu ni Mweza juu ya kila kitu. (29:20)*

Hivyo tusipojielimisha na kuuchunguza ulimwengu ili kumjua vema Mwenyezi Mungu na kumwabudu ipasavyo ni kukanusha neema kulikopea. Maana wenzetu wa nyuma hawakuwa nazo, na Mwenyezi Mungu hakufanya upendeleo ila kafanya hivyo kutokana na haja ya wakati tulionao. Ni kwa msingi huu Qur,an inatwambia kuwa tutaulizwa juu ya neema tulizopewa tulizitumia vipi.

ثُمَّ لَتُسۡـَٔلُنَّ يَوۡمَئِذٍ عَنِ ٱلنَّعِيمِ ٨

*"kisha kwa hakika siku hiyo mtaulizwa juu ya neema (mlizopewa mmezitumiaje)" (102:8)*

**Hutuonesha madhara ya kutofuata mwongozo wa Mwenyezi Mungu**

Historia pia hutuonesha madhara yanayoikumba jamii ya wanadamu zilizokataa kufuata mwongozo wa Mwenyezi Mungu na badala yake ikaishi kwa kufuata sheria na kanuni zilizobuniwa na wanadamu kwa kufuata matashi ya nafsi. Jamii hizo ziligubikwa na giza nene za dhulma, ukandamizaji, ukatilili, ubabe, ufuska, alimuradi kila mtu aliishi kwa wasiwasi pasina amani wala furaha ya kweli. Mfano wa jamii hizi ni ule wa Ad, kaumu Lut na watu wa nabii Shu'aib ambao historia yao tutaiona baadaye katika historia ya mitume wa Allah(s.w).

**Hutuonesha namna mitume na watu wema walivyosimama imara katika kupambana na dhulma na watawala madhalimu**

Historia pia hutuonesha namna mitume na watu wema walivyosimama imara katika kupambana na dhulma na watawala madhalimu. Kwa maneno mengine historia inatuonesha na kutufunza umuhimu wa kupigania haki na uadilifu viwepo katika jamii na kuondoa aina zote za dhulma na ukandamizaji wanazofanyiwa wanadamu.

Katika mitume, funzo hili tunalipata kwenye kisa cha nabii Hud(a.s), Musa(a.s) na Muhammad(s.a.w). Nabii Hud alipambana na watawala madhalimu wa wakati wake walioasisi sera ya ubabe na kufanya dhulma kuwa ndiyo mtindo wao wa maisha.

فَأَمَّا عَادٌ فَٱسْتَكْبَرُوا۟ فِى ٱلْأَرْضِ بِغَيْرِ ٱلْحَقِّ وَقَالُوا۟ مَنْ أَشَدُّ مِنَّا
قُوَّةً ۖ أَوَلَمْ يَرَوْا۟ أَنَّ ٱللَّهَ ٱلَّذِى خَلَقَهُمْ هُوَ أَشَدُّ مِنْهُمْ قُوَّةً ۖ

*Ama watu wa Adi walifanya kibri katika ardhi bila ya haki. Na wakasema: "Ni nani mwenye nguvu kuliko sisi?" Je hawakuona kwamba Mwenyezi Mungu aliyewaumba ndiye Mwenye nguvu zaidi kuliko wao.(41:15)*

Nabii Musa alipambana na Fir,aun ambaye alijipa uungu wa kutunga sheria za ukandamizaji na kuwafanya wanadamu waliopaswa kumwabudu Allah(s.w), kuwa watumwa wanaomwabudu yeye.

إِنَّ فِرْعَوْنَ عَلَا فِى ٱلْأَرْضِ وَجَعَلَ أَهْلَهَا شِيَعًا يَسْتَضْعِفُ
طَآئِفَةً مِّنْهُمْ يُذَبِّحُ أَبْنَآءَهُمْ وَيَسْتَحْىِۦ نِسَآءَهُمْ ۚ إِنَّهُۥ كَانَ مِنَ
ٱلْمُفْسِدِينَ ﴿٤﴾

*Hakika firaun alitakabali katika ardhi, na akawafanya watu wa huko makundi mbalimbali. Akalidhoofisha kundi moja miongoni mwao, akawachinja watoto wao wanaume na kuwawacha hai watoto wao wanawake. Hakika yeye alikuwa miongoni mwa waharibifu kabisa.(28:4)*



Kwahiyo, kama walivyofanya mitume na watu wema, ndivyo historia inavyotutaka sisi tufuate nyayo zao katika maisha yetu yote hapa duniani kwa kuhakikisha kuwa haki na uadilifu vinastawi katika jamii ya wanadamu kupitia mwongozo wa maisha aliouleta Mwenyezi Mungu.

وَمَا لَكُمْ لَا تُقَٰتِلُونَ فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ وَٱلْمُسْتَضْعَفِينَ مِنَ ٱلرِّجَالِ
وَٱلنِّسَآءِ وَٱلْوِلْدَٰنِ ٱلَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَآ أَخْرِجْنَا مِنْ هَٰذِهِ
ٱلْقَرْيَةِ ٱلظَّالِمِ أَهْلُهَا وَٱجْعَل لَّنَا مِن لَّدُنكَ وَلِيًّا وَٱجْعَل لَّنَا
مِن لَّدُنكَ نَصِيرًا ﴿٧٥﴾

*Na mna nini hampigani katika njia ya Mwenye Mungu na kuwakomboa watu madhaifu katika wanaume na wanawake na watoto, ambao wanasema kumwambia Mola wao: Mola wetu! Tutoe katika mji huu ambao watu wake ni madhalimu. Na utupe ulinzi kutoka kwako na utupe ushindi kutoka kwako.(4:75)*

**Hutupatia fursa ya kujifunza toka kwa kaumu zilizopita na kuchukua tahadhari kabla hayajatufika yaliyowasibu**

Historia hutupatia fursa ya kujifunza masahibu yaliyowakuta kaumu zilizopita bila sisi kuwa pamoja nao katika makosa waliyofanya. Tunasoma na kuona makosa yao, madhara waliyoyapata na maangamizi yaliyowakumba. Kaumu ya Lut iliangamizwa kwasababu ya kufanya kwao ubaradhuli wa kutamaniana na kuendeana wanaume kwa wanaume. Hakika watu hawa walifanya uchafu na uovu mkubwa kabisa wenye kuchukiza mbele ya Allah(s.w) na watu wema. Mwishowe wakaangamizwa!

فَنَجَّيْنَٰهُ وَأَهْلَهُۥٓ أَجْمَعِينَ ﴿١٧٠﴾ إِلَّا عَجُوزًا فِى ٱلْغَٰبِرِينَ ﴿١٧١﴾
ثُمَّ دَمَّرْنَا ٱلْءَاخَرِينَ ﴿١٧٢﴾ وَأَمْطَرْنَا عَلَيْهِم مَّطَرًا ۖ فَسَآءَ مَطَرُ
ٱلْمُنذَرِينَ ﴿١٧٣﴾ إِنَّ فِى ذَٰلِكَ لَءَايَةً ۖ وَمَا كَانَ أَكْثَرُهُم
مُّؤْمِنِينَ ﴿١٧٤﴾

*Basi tukamuokoa yeye(Lut) na watu wake wote. Isipokuwa kikongwe katika wakaao nyuma. Kisha tukawaangamiza mabaradhuli. Bila shaka katika haya kuna mazingatio, lakini wengi katika wao hawakuwa wenye kuamini(26:170-174)*

Kwa kuzingatia hayo tunachukua tahadhari ya kutoyaendea makosa yaliyopelekea maangamizi yao, na kufanya jitihada ili pasiwepo na mtu au kikundi cha watu katika jamii watakaoachiwa kufanya ovu lolote la kuihilikisha jamii nzima.

**Kujitathimini na kuongeza jitihada za kusimamisha haki na uadilifu kama walivyofanya Mitume na watu wema waliotangulia**

Historia pia hutupatia fursa ya kuona jitihada zilizofanywa na mitume na watu wema waliotangulia katika kusimamisha haki na uadilifu kwenye jamii zao. Kwa kuzilinganisha jitihada zao na zetu na mafanikio waliyoyapata, tunaweza kuona ni kwa kiwango gani tunazembea kwa kudharau au kubweteka kwa kuridhika na ile sehemu ndogo ya ibada tunazofanya kama vile kuswali, kufunga na kuhiji, hali ya kuwa Mtume(s.a.w) na waislamu waliokuwa pamoja naye waliyafanya yote hayo na kuweza kuiongoza jamii ya wanadamu kwa sheria za Mwenyezi Mungu zilizoleta maisha ya furaha na amani ya kweli kwa walimwengu. Ni kutokana na ukweli na jitihada kubwa walizofanya ndipo Allah(s.w) akawakamilishia ahadi yake anayoitaja katika aya ifuatazo:

وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ مِنكُمْ وَعَمِلُوا۟ ٱلصَّٰلِحَٰتِ
لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِى ٱلْأَرْضِ كَمَا ٱسْتَخْلَفَ ٱلَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ
وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ ٱلَّذِى ٱرْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّنۢ بَعْدِ
خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِى لَا يُشْرِكُونَ بِى شَيْـًٔا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ
ذَٰلِكَ فَأُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْفَٰسِقُونَ ﴿٥٥﴾

*Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, kuwa Atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya makhalifa wale waliokuwa kabla yao, na kwa hakika Atawasimamishia dini yao Aliyowapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya khofu yao(24:55)*

**Hutuonesha kuwepo kwa Mwenyezi Mungu na mamlaka yake juu ya mwanadamu**

Jambo lingine kubwa ni kwamba, historia hudhihirisha kuwepo Mwenyezi Mungu na mamlaka yake juu ya wanadamu. Jamii mbalimbali zilizokuwa na nguvu kubwa kuliko zingine zilifutwa na kusahaulika kabisa na nguvu kubwa iliyokuwa juu ya uwezo wao. Kwa mfano, tunakumbushwa

historia ya kaumu ya Ad, Thamud na Firaun ambao walikuwa na nguvu kubwa kijeshi na maendeleo makubwa ya teknolojia, lakini leo hii hawapo tena:

أَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِعَادٍ ﴿٦﴾ إِرَمَ ذَاتِ ٱلْعِمَادِ ﴿٧﴾ ٱلَّتِى لَمْ
يُخْلَقْ مِثْلُهَا فِى ٱلْبِلَٰدِ ﴿٨﴾ وَثَمُودَ ٱلَّذِينَ جَابُوا۟
ٱلصَّخْرَ بِٱلْوَادِ ﴿٩﴾ وَفِرْعَوْنَ ذِى ٱلْأَوْتَادِ ﴿١٠﴾ ٱلَّذِينَ طَغَوْا۟
فِى ٱلْبِلَٰدِ ﴿١١﴾ فَأَكْثَرُوا۟ فِيهَا ٱلْفَسَادَ ﴿١٢﴾ فَصَبَّ عَلَيْهِمْ
رَبُّكَ سَوْطَ عَذَابٍ ﴿١٣﴾

*Je, huoni Mola wako alivyowafanya Ad? Iram waliokuwa na majumba marefu marefu; ambao hawakuumbwa mfano wao katika miji. Na Thamud waliochonga majabali wakafanya nyumba katika uwanja wao; Na Firaun mwenye majumba kama vigingi, ambao walifanya maovu katika miji, kisha walizidisha humo maovu, kwahiyo Mola wako aliwapiga mjeledi mmoja tu wa adhabu (89:6-13)*

## HISTORIA YA MITUME

Idadi ya Mitume wote walioteuliwa na Allah (s.w.) kwa wanaadamu haikudhihirishwa kwetu. Katika Qur'an tumefahamishwa tu kwamba baadhi ya Mitume tumetajiwa majina na habari zao na wengine hatujatajiwa.

Mitume waliotajwa katika Qur'an ni 25. Mitume hawa ni:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. Adamu. | 2. Idris. | 3. Nuhu. | 4. Hud. |
| 5, Swaleh. | 6. Ibrahimu. | 7. Lut. | 8. Ismail. |
| 9. Is-haq. | 10. Yaaqub. | 11. Yusuf. | 12. Ayyub. |
| 13. Shuaib. | 14. Musa. | 15. Harun. | 16. Al-Yassa. |
| 17. Dhulkiflil | 18. Daud. | 19. Suleiman | 20.Ilyaas. |
| 21. Yunus. | 22. Zakariya | 23. Yahya. | 24. Issa |

25. Muhammad (Rehma na amani za Allah ziwe juu yao wote).

Historia ya Mitume na kaumu zao iliyobainishwa katika Qur'an inatuonesha kuwa kila alipokuja Mtume na ujumbe kutoka kwa Allah(s.w), watu waligawanyika katika makundi mawili. Wale walioupokea mwongozo wa Allah (s.w.) na kuufuata, na wale waliokataa kuufuata mwongozo huo. Hii ni kwa sababu mwanaadamu amepewa uhuru wa kuchagua.

إِنَّا هَدَيْنَٰهُ ٱلسَّبِيلَ إِمَّا شَاكِرًا وَإِمَّا كَفُورًا ﴿٣﴾

*Hakika sisi tumemuongoza njia mbili. Basi atakuwa mwenye kushukuru au mwenye kukufuru(76:3)*

Uhuru huu wa kuchagua ni mtihani kwa mwanaadamu. Atakayechagua njia ya haki atakuwa na malipo mazuri na ya milele mbele ya Allah (s.w.). Na atakayefuata njia ya upotofu makazi mabaya ya motoni yatakuwa ndio marejeo yake.

إِنَّآ أَعْتَدْنَا لِلْكَٰفِرِينَ سَلَٰسِلَا۟ وَأَغْلَٰلًا وَسَعِيرًا ﴿٤﴾

*Hakika sisi tumewaandalia makafiri minyororo na makongwa na Moto mkali(76:4)*

Hataletwa tena Mtume mwingine kwa sababu Allah(s.w.) amechukua ahadi ya kuuhifadhi mwongozo (Qur'an) aliouleta kwa Mtume huyu wa mwisho. Aidha, Sunnah za Mtume (s.a.w.) zimehifadhiwa kikamilifu. Sababu nyingine ni kuwa Mtume Muhammad (s.a.w.) alipelekwa kwa watu wote. Msingi wa hoja hizi ni kwamba lililo muhimu siyo kuwepo kwa Mtume kimwili bali ni kuwafikia watu ujumbe uliokusudiwa.

## NABII ADAMU(A.S)

### Kuumbwa kwa Adam

Nabii Adamu (a.s.) ameumbwa kutokana na vitu mwili. Ameumbwa kwa udongo na kupuliziwa roho inayotokana na Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu anatufahamisha hili katika aya zifuatazo.

إِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلَٰٓئِكَةِ إِنِّى خَٰلِقٌۢ بَشَرًا مِّن طِينٍ ﴿٧١﴾ فَإِذَا
سَوَّيْتُهُۥ وَنَفَخْتُ فِيهِ مِن رُّوحِى فَقَعُوا۟ لَهُۥ سَٰجِدِينَ ﴿٧٢﴾

*(Kumbuka) Mola wako alipowaambia Malaika: "Hakika mimi nitaumba mtu kwa udongo. Na nitakapomkamilisha na kumpulizia roho inayotokana na mimi basi mwangukieni kwa kumtii. (38:71-72)*

Kuhusu roho Allah (s.w.) ametueleza wazi kuwa elimu hiyo hatunayo bali iko kwake pekee.

وَيَسْـَٔلُونَكَ عَنِ ٱلرُّوحِ ۖ قُلِ ٱلرُّوحُ مِنْ أَمْرِ رَبِّى وَمَآ أُوتِيتُم
مِّنَ ٱلْعِلْمِ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٨٥﴾

*Na wanakuuliza habari ya Roho. Sema: "Roho ni jambo lililohusika na Mola wangu. Nanyi hamkupewa katika ilimu ila kidogo kabisa". (17:85)*

### Kusudio la kuumbwa mwanadamu

Lengo la kuubwa Adamu na wanadamu kwa ujumla ni kuwa khalifa wa Allah(s.w).Ilikuwa ni kupenda kwa Allah (s.w.) kumpeleka Adamu duniani kama Khalifa (naibu). Kusudio hili limebainishwa katika aya ifuatayo

وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلَٰٓئِكَةِ إِنِّى جَاعِلٌ فِى ٱلْأَرْضِ خَلِيفَةً ۖ
قَالُوٓا۟ أَتَجْعَلُ فِيهَا مَن يُفْسِدُ فِيهَا وَيَسْفِكُ ٱلدِّمَآءَ

*Na pindi Mola wako Alipowaambia malaika: Mimi ni Mwenye kuweka Khalifa katika ardhi. Wakasema: Utaweka humo ataakaye fanya uharibifu na kumwaga damu..(2:30)*

**Kupewa Elimu kwa nabii Adamu(a.s)**

Ili Adamu(a.s) aweze kuwa khalifa atakayetawala dunia na viumbe kwa kutumia sheria za Allah, ilibidi Allah(s.w) amfunze elimu ya vitu na mambo yote yahusuyo dunia na ulimwengu kwa ujumla.

وَعَلَّمَ ءَادَمَ ٱلْأَسْمَآءَ كُلَّهَا ثُمَّ عَرَضَهُمْ عَلَى ٱلْمَلَـٰٓئِكَةِ فَقَالَ أَنۢبِـُٔونِى بِأَسْمَآءِ هَـٰٓؤُلَآءِ إِن كُنتُمْ صَـٰدِقِينَ ﴿٣١﴾

*Na Mwenyezi Mungu akamfundisha Adamu majina ya vitu vyote, kisha akaviweka mbele ya Malaika, akasema, "Niambieni majina ya hivi ikiwa ninyi mnasema kweli. .(2:31)*

قَالُوا۟ سُبْحَـٰنَكَ لَا عِلْمَ لَنَآ إِلَّا مَا عَلَّمْتَنَآ ۖ إِنَّكَ أَنتَ ٱلْعَلِيمُ ٱلْحَكِيمُ ﴿٣٢﴾

*Wakasema. "Utukufu ni wako! Hatuna elimu isipokuwa ile uliyotufundisha, bila shaka wewe ndiye Mjuzi Mwenye Hekima.(2:32)*

قَالَ يَـٰٓـَٔادَمُ أَنۢبِئْهُم بِأَسْمَآئِهِمْ ۖ فَلَمَّآ أَنۢبَأَهُم بِأَسْمَآئِهِمْ قَالَ أَلَمْ أَقُل لَّكُمْ إِنِّىٓ أَعْلَمُ غَيْبَ ٱلسَّمَـٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ ﴿٣٣﴾

*Akasema(Mwenyezi Mungu): "Ewe Adamu! Waambie majina yake". Alipowaambia majina yake, akasema(Mwenyezi Mungu) "Sikukwambieni kwamba mimi najua siri za mbinguni na za ardhini?(2:33)*

Nabii Adamu ambaye ndiye mtu wa kwanza, hakuwahi kuwa mjinga wala hakuwa mbumbumbu kama wasemavyo makafiri kwamba mtu wa kwanza alikuwa *"Primitive"* kwa kuwa alitokana na sokwe. Adamu aliumbwa akiwa mtu kamili aliyekusudiwa kuwa Khalifa wa Allah(s.w), hivyo elimu ndiyo neema na nyenzo ya kwanza kabisa aliyotunukiwa na Allah(s.w) ili aweze kuwa kiongozi na mtawala wa Ulimwengu.

**Ibilisi alaaniwa kwa kibri na majivuno yake**

Ibilisi aliye laaniwa ni jini aliyekuwa pamoja na Malaika wakati Allah(s.w) alipotoa amri ya kusujudiwa Adamu kutokana na hadhi ya

ukhalifa na elimu aliyokuwa nayo. Malaika wote walisujudu ila Ibilisi. Qur,an inasema:

وَإِذْ قُلْنَا لِلْمَلَٰٓئِكَةِ ٱسْجُدُوا۟ لِءَادَمَ فَسَجَدُوٓا۟ إِلَّآ إِبْلِيسَ كَانَ مِنَ ٱلْجِنِّ فَفَسَقَ عَنْ أَمْرِ رَبِّهِۦٓ ۗ

*Na tulipowaambia Malaika "Msujudieni Adam", basi wakamsujudia isipokuwa Ibilisi, yeye alikuwa miongoni mwa majini, na akavunja amri ya Mola wake(18:50)*

Ibilisi alijiona kuwa yu bora kuliko Adamu. Kibri na majivuno yake ya kikabila yalimpelekea kuasi amri ya Allah(s.w) na kulaaniwa pale alipoulizwa na Allah(s.w) kuwa:

يَٰٓإِبْلِيسُ مَا لَكَ أَلَّا تَكُونَ مَعَ ٱلسَّٰجِدِينَ ﴿٣٢﴾

*Ewe Ibilisi! Imekuwaje hukuwa miongoni mwa waliotii?(15:32)*

قَالَ لَمْ أَكُن لِّأَسْجُدَ لِبَشَرٍ خَلَقْتَهُۥ مِن صَلْصَٰلٍ مِّنْ حَمَإٍ مَّسْنُونٍ

*Akasema: "siwezi kumtii mtu uliyemuumba kwa udongo(15:33)*

أَنَا۠ خَيْرٌ مِّنْهُ ۖ خَلَقْتَنِى مِن نَّارٍ وَخَلَقْتَهُۥ مِن طِينٍ ﴿٧٦﴾

*"Mimi ni bora kuliko yeye. Umeniumba kwa moto, naye umemuumba kwa udongo.(38:76)*

قَالَ فَٱخْرُجْ مِنْهَا فَإِنَّكَ رَجِيمٌ ﴿٧٧﴾ وَإِنَّ عَلَيْكَ لَعْنَتِىٓ إِلَىٰ يَوْمِ ٱلدِّينِ ﴿٧٨﴾

*(Mwenyezi Mungu) Akasema: "Basi toka humo kwani umetengwa na rehema. Na hakika laana yangu itakuwa juu yako mpaka siku ya malipo(38:77-78)*

Hivyo akavuliwa nafasi ya heshima aliyokuwa nayo ya kuwa pamoja na Malaika na akafukuzwa kwa fedheha na izara. Hivyo majivuno yatokanayo na kujidhania ni bora kwa sababu ya nasaba, kabila au rangi, kwa hakika ni tabia ya Kiibilisi (shetani).

**Kuumbwa kwa Hawa**

Baada ya kumuumba Adamu (a.s) Allah(s.w) akamuumbia mkewe ambaye ni mama wa wanadamu wote. Yeye na Adamu ambaye ni baba wa watu wote, waliumbwa kwa lengo moja la kuwa makhalifa wanaomwabudu Allah(s.w) peke yake kwa kufuata mwongozo wake tu. Lengo la kuumbwa Adam, Hawa pamoja na kizazi chao; yaani wanaadamu, linaelezwa katika aya ifuatayo:

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ ٱتَّقُوا۟ رَبَّكُمُ ٱلَّذِى خَلَقَكُم مِّن نَّفْسٍ وَٰحِدَةٍ
وَخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَبَثَّ مِنْهُمَا رِجَالًا كَثِيرًا وَنِسَآءً ۚ

*Enyi watu! Mcheni Mola wenu ambaye amekuumbeni kutokana na nafsi moja. Na akamuumba mkewe katika nafsi ile ile. Na akaeneza wanaume wengi na wanawake kutoka katika wawili hao.(4:1)*

**Maisha ya Adamu na Hawa katika pepo**

Historia ya mwanadamu haianzii duniani. Adamu na Hawa walianza maisha yao peponi. Baada ya kuwaumba, Mwenyezi Mungu akasema:

يَـٰٓـَٔادَمُ ٱسْكُنْ أَنتَ وَزَوْجُكَ ٱلْجَنَّةَ وَكُلَا مِنْهَا رَغَدًا حَيْثُ
شِئْتُمَا وَلَا تَقْرَبَا هَـٰذِهِ ٱلشَّجَرَةَ فَتَكُونَا مِنَ ٱلظَّـٰلِمِينَ ﴿٣٥﴾

*Ewe Adam! Kaa wewe na mke wako katika bustani, kuleni humo kwa ukunjufu mahali mutakapo(2:35)*

Pamoja na kuwawekwa peponi, Allah(s.w) aliwatahadharisha Adamu na Hawa juu ya Ibilisi aliyelaaniwa kutokana na kibri na majivuno ya ukabila wake,aliwaasa wamuhadhari na kumuepuka. Allah(s.w) anamtahadharisha akimwambia:

يَـٰٓـَٔادَمُ إِنَّ هَـٰذَا عَدُوٌّ لَّكَ وَلِزَوْجِكَ فَلَا يُخْرِجَنَّكُمَا مِنَ
ٱلْجَنَّةِ فَتَشْقَىٰٓ ﴿١١٧﴾ إِنَّ لَكَ أَلَّا تَجُوعَ فِيهَا وَلَا تَعْرَىٰ ﴿١١٨﴾
وَأَنَّكَ لَا تَظْمَؤُا۟ فِيهَا وَلَا تَضْحَىٰ ﴿١١٩﴾

*Ewe Adam! Hakika huyu(Ibilisi) ni adui yako na wa mke wako. Basi asikutoweni katika Pepo (hii) mtaingia mashakani. Hakika hutakuwa mwenye njaa humo wala hutakuwa uchi. Na kwa yakini hutapata kiu humo wala hutapata joto.(20:117-119)*

فَوَسْوَسَ إِلَيْهِ ٱلشَّيْطَٰنُ قَالَ يَٰٓـَٔادَمُ هَلْ أَدُلُّكَ عَلَىٰ شَجَرَةِ ٱلْخُلْدِ
وَمُلْكٍ لَّا يَبْلَىٰ ﴿١٢٠﴾

*Lakini Shetani alimtia wasi wasi, akamwambia: "Ewe Adamu, Je! Nikujulishe mti wa umilele na ufalme usiokoma(20:120)*

فَأَكَلَا مِنْهَا فَبَدَتْ لَهُمَا سَوْءَٰتُهُمَا وَطَفِقَا يَخْصِفَانِ عَلَيْهِمَا مِن
وَرَقِ ٱلْجَنَّةِ ۚ وَعَصَىٰٓ ءَادَمُ رَبَّهُۥ فَغَوَىٰ ﴿١٢١﴾

*Basi wote wawili wakaula, na uchi wao ukadhihirika na wakaanza kujibandika majani ya Peponi. Na Adamu akamkosea Mola wake, na akateleza njia (20:121)*

**Kusamehewa kwao na kuletwa duniani**

Allah(s.w) kwa sifa zake za urehemevu na usamehevu, alimfundisha Adamu na Mkewe Hawa namna ya kutubia na kuomba toba ili wamuombe awasamehe.

فَتَلَقَّىٰٓ ءَادَمُ مِن رَّبِّهِۦ كَلِمَٰتٍ فَتَابَ عَلَيْهِ ۚ إِنَّهُۥ هُوَ ٱلتَّوَّابُ
ٱلرَّحِيمُ ﴿٣٧﴾

*Kisha Adamu akapokea maneno (ya toba) kwa Mola wake, (akaomba), na Mola wake akapokea toba yake. Hakika yeye ni Mwingi wa kupokea toba na Mwingi wa kurehemu(2:37)*

Tunafahamishwa katika Qur,an kuwa maneno waliyofunzwa Adamu na Hawa juu ya namna ya kutubia ni haya yanayopatikana katika dua ifuatayo pale Adamu na Hawa waliposema:

قَالَا رَبَّنَا ظَلَمْنَآ أَنفُسَنَا وَإِن لَّمْ تَغْفِرْ لَنَا وَتَرْحَمْنَا
لَنَكُونَنَّ مِنَ ٱلْخَٰسِرِينَ ﴿٢٣﴾

*Wakase:"Mola wetu! Tumedhulumu nafsi zetu; na kama hutatusamehe na kuturehemu, bila shaka tutakuwa miongoni mwa wenye hasara(7:23)*

Baada ya kujuta kosa lao na kutubia kwa Allah(s.w) kwa kuomba msamaha, Allah(s.w) aliwasamehe na kumchagua Adamu na mkewe Hawa kuwa makhalifa wake.

ثُمَّ ٱجْتَبَٰهُ رَبُّهُۥ فَتَابَ عَلَيْهِ وَهَدَىٰ ﴿١٢٢﴾

*Basi Mola wake Akamchagua na Akamkubalia toba yake na Akamuongoa (20:122)*

Kisha akawaleta duniani kutekeleza kujumu alilowapa. Tunafahamishwa kuwa, Allah(s.w) aliwaahidi kuwaletea Mwongozo watakaoutumia katika kuwaongoza kwenye kila kipengele cha maisha yao ya kila siku. akawaambia;

ٱهْبِطُوا۟ مِنْهَا جَمِيعًا ۖ فَإِمَّا يَأْتِيَنَّكُم مِّنِّى هُدًى فَمَن تَبِعَ هُدَا
ىَ فَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٣٨﴾

*Shukeni humo pia nyote, na utakapowajilia uwongozi utokao Kwangu, basi wenye kufuata uwongozi Wangu hawatakuwa na khofu wala hawatahuzunika(2:38)*

**Mafunzo kwa muhtasari**

(i) Mwanadamu hakutokana na sokwe, ila aliumbwa na Allah(s.w)akiwa mtu kamili.

(ii) Allah(s.w)ndiye chanzo cha elimu zote alizonazo mwanadamu.

(iii) Tunatakiwa kutafuta na kujifunza fani zote za elimu zitakazotuwezesha kuwa makhalifa wa Allah(s.w)kama alivyokuwa Adam(a.s).

(iv) Fisadi na umwagaji wa damu bila ya haki vitastawi na kuendelea kuwepo duniani endapo hatutafuata mwongozo wa Allah(s.w).

(v) Ni katika tabia njema mtu kukiri ujinga wake kuhusiana na jambo asilolijua kama walivyofanya malaika kuliko kujifanya kuwa anajua jambo hilo.

(vi) Kibri na majivuno yatokanayo na mtu kujidhania ni bora kwa sababu ya nasaba, kabila, rangi, utajiri au cheo, kwa hakika ni tabia mbaya ya kiibilisi.

(vii) Ibilisi ni adui mkubwa wa wanadamu. Hupamba matendo maovu na machafu ili kupoteza watu. Hufanya kazi hii na kushirikiana na wanadamu na majini waovu.

(viii) Tunapomkosea mtu au Mwenyezi Mungu yatupasa kuomba radhi au msamaha, na kisha kutubu kwa kutorudia tena kosa hilo kama walivyofanya Adamu na Hawa.

(ix) Hakuna dhambi ya asili anayorithi mwanadamu kutoka kwa Nabii Adamu(a.s). Kila mwanadamu huzaliwa akiwa huru pasina dhambi yoyote.

## HISTORIA YA NABII IDRISS (a.s)

Nabii Idris alimtangulia Nabii Nuhu lakini hakuna maelezo mengi yaliyotolewa katika Qur'an juu ya ujumbe wake. Tunachojua tu ni kwamba alikuwa Mtume na Siddiq (msadikishaji wa kweli), mwenye subira na aliinuliwa na kupewa cheo kikubwa na Allah. Katika Qur,an ametajwa kwenye surat Maryam (aya 56-57) na surat Anbiya (aya 58).

وَٱذْكُرْ فِى ٱلْكِتَـٰبِ إِدْرِيسَ ۚ إِنَّهُۥ كَانَ صِدِّيقًا نَّبِيًّا ﴿٥٦﴾ وَرَفَعْنَـٰهُ مَكَانًا عَلِيًّا ﴿٥٧﴾

*Na mtaje katika kitabu Idriss. Hakika yeye alikuwa mkweli sana na nabii. Na tulimuinua daraja ya juu kabisa(19:56-57)*

**Mafunzo kwa muhtasari**

Funzo kubwa linalopatikana katika kutajwa nabii Idriss ni mtu kuwa mkweli. Ukweli ni katika tabia njema kabisa ambayo muislamu anatakiwa kuwa nayo daima. Allah(s.w)anawapenda sana watu walio wakweli wa kauli na vitendo. Na siku ya kiyama Allah atawanusuru wakweli wasiingie katika Adhabu ya Moto na badala yake kuwaingiza katika pepo yake yenye neema zisizokatika.

قَالَ ٱللَّهُ هَـٰذَا يَوْمُ يَنفَعُ ٱلصَّـٰدِقِينَ صِدْقُهُمْ ۚ لَهُمْ جَنَّـٰتٌ تَجْرِى مِن تَحْتِهَا ٱلْأَنْهَـٰرُ خَـٰلِدِينَ فِيهَآ أَبَدًا ۚ رَّضِىَ ٱللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا۟ عَنْهُ ۚ ذَٰلِكَ ٱلْفَوْزُ ٱلْعَظِيمُ ﴿١١٩﴾

*Mwenyezi Mungu atasema: " Hii ndiyo siku ambayo wakweli utawafaa ukweli wao. Wao watapata Bustani zipitazo mito mbele yake. Humo watakaa milele. Na Mwenyezi Mungu amewawia radhi, nao wawe radhi naye. Huko ndiko kufuzu kukubwa.(5:119)*

Ni kutokana na uzuri na umuhimu wa sifa hii tunamkuta Allah(s.w)anamtaja nabii Idriss kwa sifa hii ya ukweli aliyokuwa nayo ili tumuige, na tupendwe na Allah(s.w) katika maisha ya duania na kesho Akhera.

## HISTORIA YA NABII NUHU (A.S)

Nabii Nuhu(a.s) aliwakuta watu wameshaacha kumuabudu Allah(s.w). Watu waliacha mafundisho ya nabii Adamu(a.s) ya kumuabudia Mungu mmoja na badala yake wakazama katika shirki ya kuabudia masanamu. Kupitia ushirikina viongozi waliwagawa watu katika matabaka na kuwanyonya.Allah(s.w)akamtuma kuwakomboa watu kutokana na dhulma iliyowazunguka kupitia ushirikina. Allah(s.w) anatufahamisha historia hii katika surat Nuhu kama ifuatavyo.

إِنَّآ أَرْسَلْنَا نُوحًا إِلَىٰ قَوْمِهِۦٓ أَنْ أَنذِرْ قَوْمَكَ مِن قَبْلِ أَن
يَأْتِيَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿١﴾

*Hakika sisi tulimtuma Nuhu kwa watu wake, ya kwamba waonye watu wako kabla ya kuwajia adhabu iumizayo.(71:1)*

قَالَ يَٰقَوْمِ إِنِّى لَكُمْ نَذِيرٌ مُّبِينٌ ﴿٢﴾ أَنِ ٱعْبُدُوا۟ ٱللَّهَ وَٱتَّقُوهُ
وَأَطِيعُونِ ﴿٣﴾

*Akasema: Enyi watu wangu! Kwa hakika mimi ni mwonyaji niliye dhahiri kwenu. Ya kuwa mwabuduni Allah na mcheni na mtiini.(71:2-3)*

يَغْفِرْ لَكُم مِّن ذُنُوبِكُمْ وَيُؤَخِّرْكُمْ إِلَىٰٓ أَجَلٍ مُّسَمًّى ۚ إِنَّ
أَجَلَ ٱللَّهِ إِذَا جَآءَ لَا يُؤَخَّرُ ۖ لَوْ كُنتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٤﴾

*Atakusemeheni madhambi yenu na atakuahirisheni ( bila ya balaa) mpaka muda uliowekwa. Hakika ijapo ajali itokayo kwa Allah haizuiliki. Laiti mngejua!(71:4)*

قَالَ رَبِّ إِنِّى دَعَوْتُ قَوْمِى لَيْلًا وَنَهَارًا ﴿٥﴾ فَلَمْ يَزِدْ
هُمْ دُعَآءِىٓ إِلَّا فِرَارًا ﴿٦﴾

*Akasema: Ee Mola wangu! Kwa hakika nimewalinganía watu wangu usiku na mchana. Lakini mwito wangu haukuwazidishia ila kukimbia;(71:5-6)*

وَإِنِّى كُلَّمَا دَعَوْتُهُمْ لِتَغْفِرَ لَهُمْ جَعَلُوٓا۟ أَصَٰبِعَهُمْ فِىٓ
ءَاذَانِهِمْ وَٱسْتَغْشَوْا۟ ثِيَابَهُمْ وَأَصَرُّوا۟ وَٱسْتَكْبَرُوا۟
ٱسْتِكْبَارًا ﴿٧﴾

*Na kila mara nilipowaita uwasamehe, waliziba masikio yao kwa vidole vyao, na walijifunika nguo zao (gubigugi), na walizidi kuendelea (na kukufuru) na wakafanya kiburi kingi(71:7)*

ثُمَّ إِنِّى دَعَوْتُهُمْ جِهَارًا ﴿٨﴾ ثُمَّ إِنِّىٓ أَعْلَنتُ لَهُمْ وَأَسْرَرْتُ
لَهُمْ إِسْرَارًا ﴿٩﴾

*Tena niliwaita kwa wazi. Kisha nikawatangazia kwa kelele; tena nikasema nao kwa siri(71:8-9)*

فَقُلْتُ ٱسْتَغْفِرُوا۟ رَبَّكُمْ إِنَّهُۥ كَانَ غَفَّارًا ﴿١٠﴾ يُرْسِلِ ٱلسَّمَآءَ
عَلَيْكُم مِّدْرَارًا ﴿١١﴾

*Nikawaambia: Ombeni msamaha kwa Mola wenu. Hakika Yeye ni Mwingi wa msamaha. Atakuleteeni mawingu yanyeshayo mvua nyingi.(71:10-11)*

وَيُمْدِدْكُم بِأَمْوَٰلٍ وَبَنِينَ وَيَجْعَل لَّكُمْ جَنَّٰتٍ وَيَجْعَل لَّكُمْ
أَنْهَٰرًا ﴿١٢﴾

*Na atakupeni mali na watoto, na atakupeni mabustani, na atakufanyieni mito.(71:12)*

مَّا لَكُمْ لَا تَرْجُونَ لِلَّهِ وَقَارًا ﴿١٣﴾ وَقَدْ خَلَقَكُمْ أَطْوَارًا ﴿١٤﴾

*Mumekuwaje hamuweki heshima ya Allah. Na hali yeye amekuumbeni namna baada ya namna? (71:13-14)*

أَلَمْ تَرَوْا۟ كَيْفَ خَلَقَ ٱللَّهُ سَبْعَ سَمَٰوَٰتٍ طِبَاقًا ﴿١٥﴾ وَجَعَلَ
ٱلْقَمَرَ فِيهِنَّ نُورًا وَجَعَلَ ٱلشَّمْسَ سِرَاجًا ﴿١٦﴾

*Je, hamuoni jinsi Allah alivyoziumba mbingu saba tabaka tabaka. Na akaufanya mwezi ndani yake uwe nuru na akalifanya jua kuwa taa?(71:15-16)*

وَٱللَّهُ أَنۢبَتَكُم مِّنَ ٱلۡأَرۡضِ نَبَاتٗا ﴿١٧﴾ ثُمَّ يُعِيدُكُمۡ فِيهَا
وَيُخۡرِجُكُمۡ إِخۡرَاجٗا ﴿١٨﴾

*Na Allah amekuotesheni katika ardhi (kama) mimea.Kisha atakurudisheni humo na atakutoeni tena(71:17-18)*

وَٱللَّهُ جَعَلَ لَكُمُ ٱلۡأَرۡضَ بِسَاطٗا ﴿١٩﴾ لِّتَسۡلُكُواْ مِنۡهَا سُبُلٗا
فِجَاجٗا ﴿٢٠﴾

*Na Allah amekufanyieni ardhi kuwa (kitu kizuri) mlichotandikiwa. Ili mtembee humo katika njia zilizopana.(71:19-20)*

قَالَ نُوحٞ رَّبِّ إِنَّهُمۡ عَصَوۡنِي وَٱتَّبَعُواْ مَن لَّمۡ يَزِدۡهُ مَالُهُۥ
وَوَلَدُهُۥٓ إِلَّا خَسَارٗا ﴿٢١﴾

*Nuhu akasema: Mola wangu! Hakika hao wameniasi na wamewafuata ambao mali yao na watoto wao hawakuwazidishia ila hasara(71:21)*

وَمَكَرُواْ مَكۡرٗا كُبَّارٗا ﴿٢٢﴾ وَقَالُواْ لَا تَذَرُنَّ ءَالِهَتَكُمۡ وَلَا
تَذَرُنَّ وَدّٗا وَلَا سُوَاعٗا وَلَا يَغُوثَ وَيَعُوقَ وَنَسۡرٗا ﴿٢٣﴾

*Na wakafanya hila kubwa kubwa. Na ambao waliwaambia (wafuasi wao): Msiache miungu yenu, wala msiwache Waddi wala Suwaa wala Yaghutha wala Yauka wala Nasra.(71:22-23)*

وَقَدۡ أَضَلُّواْ كَثِيرٗاۖ وَلَا تَزِدِ ٱلظَّٰلِمِينَ إِلَّا ضَلَٰلٗا ﴿٢٤﴾ مِّمَّا
خَطِيٓـَٰٔتِهِمۡ أُغۡرِقُواْ فَأُدۡخِلُواْ نَارٗا فَلَمۡ يَجِدُواْ مِّن دُونِ ٱللَّهِ
أَنصَارٗا ﴿٢٥﴾

*Nao wamekwishapoteza (watu) wengi; wala usiwazidishie madhalimu hawa ila kupotelea mbali! Basi kwa ajili ya makosa yao waligharikishwa wakaingizwa motoni, wala hawakupata wa kuwanusuru mbele ya Allah.(71:24-25)*

وَقَالَ نُوحٌ رَّبِّ لَا تَذَرْ عَلَى ٱلْأَرْضِ مِنَ ٱلْكَـٰفِرِينَ دَيَّارًا ﴿٢٦﴾
إِنَّكَ إِن تَذَرْهُمْ يُضِلُّوا۟ عِبَادَكَ وَلَا يَلِدُوٓا۟ إِلَّا فَاجِرًا كَفَّارًا ﴿٢٧﴾

*Na Nuhu (akazidi) kusema: Mola wangu! Usimuache juu ya ardhi mkazi wake yeyote katika makafiri. Hakika ukiwaacha watapoteza watu wako wala hawatazaa ila (watoto) waovu wenye kufuru (kama wao).(71:26-27)*

رَّبِّ ٱغْفِرْ لِى وَلِوَٰلِدَىَّ وَلِمَن دَخَلَ بَيْتِىَ مُؤْمِنًا وَلِلْمُؤْمِنِينَ
وَٱلْمُؤْمِنَـٰتِ وَلَا تَزِدِ ٱلظَّـٰلِمِينَ إِلَّا تَبَارًۢا ﴿٢٨﴾

*Mola wangu! nisamehe mimi na wazee wangu, na kila anayeingia nyumbani mwangu hali ya kuwa ni Muislamu, na Waislamu wanaume na Waislamu wanawake; wala usiwazidishie madhalimu ila maangamizo.(71:28)*

**Mafunzo kwa muhtasari**

Watu waliiacha njia sahihi ya Allah(s.w), Nuhu alifundisha Tawhiid na akawalingania watu wamwabudu Allah (s.w)peke yake. Akawaonya juu ya adhabu kali iwapo hawatakoma kumshirikisha Allah(s.w) na miungu wengine. Msimamo na mwelekeo wa Nabii Nuhu ulikuwa ni wenye mantiki inayotua akilini. Kwa kuwa binadamu anamtegemea Allah(s.w) kwa kila kitu na kwa kila hali katika maisha yake, tangu anapozaliwa hadi anapofariki dunia, basi hana budi kumsujudia Allah(s.w) peke yake pasina kumshirikisha na yeyote.


Kwa kumwabudu Allah na kutubia kwake, binadamu hunufaika kwa njia nyingi: Madhambi yake husamehewa na hivyo kunusurika na adhabu ya Allah hapa duniani na kesho huko Akhera. Ardhi kame hubarikiwa mvua na mazao. Rehma ya Allah na huja kwa njia ya kuneemeshwa mali na watoto. Hivyo nafuu na starehe anayoipata mtu katika dunia hii si matokeo ya juhudi zake tu za mitulinga bali kwa kiasi kikubwa nafuu hiyo huwa ni neema aipatayo kwa kufuata mwenendo wa uadilifu.

Nabii Nuhu alizitumia kikamilifu njia zote alizoziweza katika kuufikisha ujumbe wa Allah(s.w) kwa watu wake. Ingawa watu wake walionesha kiburi na waligoma kumsikiliza lakini yeye aliendelea na

kazi yake. Kwa kuonesha mfano bora kabisa wa subira na kujitolea nafsi yake ili kufikisha ujumbe wa Allah.

Nabii Nuhu aliwataka watu wake wahudhurishe fahamu zao katika kuumbwa kwa binadamu na katika dalili nyingine za Allah katika ulimwengu huu. Kadiri mtu anavyotafakari juu ya kuumbwa kwa ulimwengu huu ndivyo mtu anavyozidi kuyakinisha juu ya nguvu, uwezo na ufalme wa Allah(s.w)

Watu wa Nabii Nuhu walishughulika katika kuwaabudu miungu mbalimbali kama Waddi, Suwaa, Yaghutha, Yauka na Nasra. Miungu hao walikuwaje? Baadhi ya Hadith za Mtume (s.a.w.) zinatoa mwangaza juu ya suala hili. Mtume amesema: Waddi na wale waliotajwa pamoja naye walikuwa ni watu wacha Mungu katika jamii yao. Walipofariki watu wakaanza kuyazungukia na kuyaomba makaburi yao na shetani akakichochea kizazi kilichofuata kuunda sanamu za watu hao. Kwa kufanya hivi walidhani wangeweza kuwaiga vitendo vyao vyema kuwa na taswira za watu hao daima katika akili zao. Kizazi cha tatu kilishawishika kuamini kirahisi sana kuwa watu hao walikuwa ni miungu wanaostahiki kuabudiwa badala ya Allah(s.w)



Nabii Nuhu alikuja kuihuisha imani juu ya Mwenyezi Mungu mmoja pale shetani alipowapotosha watu hata wakaanza kuwaamini miungu wengi ambao kwa mawazo yao walidhani wangewakurubisha kwa Mwenyezi Mungu mmoja. Kwa hakika kila Mtume wa Allah(s.w) alifundisha neno hilo hilo juu ya Mwenyezi Mungu kama alivyofundisha Nuhu.

Dua za Nabii Nuhu za kuomba adhabu ya Allah juu ya watu wake zilikuja baada ya muda mrefu sana wa kuwanasihi na kuwahubiria watu hao.Aliwaombea msamaha waumini walioitikia wito wake.Mwanawe na mkewe walikuwa ni miongoni mwa waliopata adhabu ya Allah(s.w) kwa kule kukataa kwao ujumbe wa Allah(s.w).

Hivyo Muislamu na awaombee msamaha waumini na awaombee kwa ujumla wajaaliwe kupata mwangaza wa njia sahihi ya Allah(s.w)

**Allah(a.s) amuamuru Nuhu(a.s) kuchonga safina**

وَأُوحِيَ إِلَىٰ نُوحٍ أَنَّهُۥ لَن يُؤْمِنَ مِن قَوْمِكَ إِلَّا مَن قَدْ ءَامَنَ
فَلَا تَبْتَئِسْ بِمَا كَانُوا۟ يَفْعَلُونَ ﴿٣٦﴾

*Na akafunuliwa Nuhu kuwa: "Hataamini (sasa) yoyote katika watu wako isipokuwa wale waliokwishaamini; kwa hivyo usisikitike kwa yale waliyokuwa wakiyatenda". (11:36)*

وَٱصْنَعِ ٱلْفُلْكَ بِأَعْيُنِنَا وَوَحْيِنَا وَلَا تُخَٰطِبْنِى فِى ٱلَّذِينَ
ظَلَمُوٓا۟ ۚ إِنَّهُم مُّغْرَقُونَ ﴿٣٧﴾

*"Na unda jahazi mbele ya macho yetu na amri yetu. Wala usiniombe (kuwasamehe) wale waliodhulumu (nafsi zao), kwa yakini wao watazamishwa".(11:37)*

وَيَصْنَعُ ٱلْفُلْكَ وَكُلَّمَا مَرَّ عَلَيْهِ مَلَأٌ مِّن قَوْمِهِۦ سَخِرُوا۟ مِنْهُ ۚ
قَالَ إِن تَسْخَرُوا۟ مِنَّا فَإِنَّا نَسْخَرُ مِنكُمْ كَمَا تَسْخَرُونَ

*Na akawa anaunda jahazi, na kila wakipitia maraisi makafiri wa umma wake walikuwa wakimcheka na yeye husema: "Kama nyinyi mnatucheka, nasi tutakucheneni kama mnavyotucheka".(71:38)*

فَسَوْفَ تَعْلَمُونَ مَن يَأْتِيهِ عَذَابٌ يُخْزِيهِ وَيَحِلُّ عَلَيْهِ عَذَابٌ
مُّقِيمٌ ﴿٣٩﴾

*"Karibuni hivi mtajua ni nani itakayemjia adhabu ya kumhuzunisha [kumfedhehesha] na itakayemteremkia adhabu itakayokaa (naye maisha]".(11:39)*

**Gharka yawakumba watawala madhalimu na wafuasi wao**

حَتَّىٰٓ إِذَا جَآءَ أَمْرُنَا وَفَارَ ٱلتَّنُّورُ قُلْنَا ٱحْمِلْ فِيهَا مِن كُلٍّ زَوْ
جَيْنِ ٱثْنَيْنِ وَأَهْلَكَ إِلَّا مَن سَبَقَ عَلَيْهِ ٱلْقَوْلُ وَمَنْ ءَامَنَ ۚ وَمَآ
ءَامَنَ مَعَهُۥٓ إِلَّا قَلِيلٌ ﴿٤٠﴾

*Hata ilipokuja amri yetu, na ardhi ikaanza kufoka maji tulimwambia: "Pakia humo (jahazini) jozi moja katika kila (nyama, jike na dume) na (wapakie) watu wako wa nyumbani kwako isipokuwa wale ambao imewapitia hukumu. Na (wachukue wote)walioamini". Na hawakuamini pamoja naye ila wachache tu.(11:40)*

وَقَالَ ٱرْكَبُوا۟ فِيهَا بِسْمِ ٱللَّهِ مَجْر۪ىٰهَا وَمُرْسَىٰهَآ ۚ إِنَّ رَبِّى لَغَفُورٌ
رَّحِيمٌ ﴿٤١﴾

*Na akasema (Nuhu): "Pandeni humo, kwa jina la Allah kuwe kwenda kwake na kusimama kwake. Hakika Mola wangu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu".(11:41)*

**Mtoto wa Nuhu(a.s) akaidi amri ya babake**

وَهِىَ تَجْرِى بِهِمْ فِى مَوْجٍ كَٱلْجِبَالِ وَنَادَىٰ نُوحٌ ٱبْنَهُۥ وَكَانَ
فِى مَعْزِلٍ يَٰبُنَىَّ ٱرْكَب مَّعَنَا وَلَا تَكُن مَّعَ ٱلْكَٰفِرِينَ ﴿٤٢﴾

*Ikawa hiyo ( jahazi) inakwenda nao katika mawimbi kama milima. Na Nuhu akamwita mwanawe aliyekuwa mbali: Ewe mwanangu! Panda pamoja nasi wala usiwe pamoja na makafiri".(11:42)*

قَالَ سَـَٔاوِىٓ إِلَىٰ جَبَلٍ يَعْصِمُنِى مِنَ ٱلْمَآءِ ۚ قَالَ لَا عَاصِمَ ٱلْيَوْمَ
مِنْ أَمْرِ ٱللَّهِ إِلَّا مَن رَّحِمَ ۚ وَحَالَ بَيْنَهُمَا ٱلْمَوْجُ فَكَانَ مِنَ
ٱلْمُغْرَقِينَ ﴿٤٣﴾

*Akasema (huyo mtoto): "Nitaukimbilia mlima utakaonilinda na maji". Akasema (Nuhu): Hakuna leo wa kulindwa na amri ya Allah isipokuwa yule atakayemrehemu". Mara mawinbi yakaingia baina yao na akawa miongoni mwa waliogharikishwa.(11:43)*

**Kuangamia mtoto wa nabii Nuhu(as)**

وَنَادَىٰ نُوحٌ رَّبَّهُۥ فَقَالَ رَبِّ إِنَّ ٱبْنِى مِنْ أَهْلِى وَإِنَّ
وَعْدَكَ ٱلْحَقُّ وَأَنتَ أَحْكَمُ ٱلْحَـٰكِمِينَ ﴿٤٥﴾

*Na Nuhu alimuomba Mola wake (alipomuona mwanawe anaangamia) akasema: "Ewe Mola wangu! Mwanangu ni katika watu wa nyumbani kwangu (mbona anaangamia)? Na hakika ahadi yako ni haki; nawe ni Mwenye haki kuliko mahakimu (wote)".(11:45)*

قَالَ يَـٰنُوحُ إِنَّهُۥ لَيْسَ مِنْ أَهْلِكَ ۖ إِنَّهُۥ عَمَلٌ غَيْرُ صَـٰلِحٍ ۖ
فَلَا تَسْـَٔلْنِ مَا لَيْسَ لَكَ بِهِۦ عِلْمٌ ۖ إِنِّىٓ أَعِظُكَ أَن تَكُونَ
مِنَ ٱلْجَـٰهِلِينَ ﴿٤٦﴾

*Akasema (Allah) Ewe Nuhu! Huyu si miongoni mwa watu wako. Yeye ni (mwenye) mwendo usiokuwa mzuri. Basi usioniombe ambayo huyajui. Mimi nakusihi usiwe miongoni mwa wajinga".(11:46)*

قَالَ رَبِّ إِنِّىٓ أَعُوذُ بِكَ أَنْ أَسْـَٔلَكَ مَا لَيْسَ لِى بِهِۦ عِلْمٌ ۖ وَإِلَّا
تَغْفِرْ لِى وَتَرْحَمْنِىٓ أَكُن مِّنَ ٱلْخَـٰسِرِينَ ﴿٤٧﴾

*(Nuhu) akasema: Ewe Mola wangu! Mimi na jikinga kwako nisije kukuomba (tena) nisiyoyajua; na kama hutanisamehe na kunirehemu, nitakuwa miongoni mwa watakaopata khasara"(11:47)*

**Mwisho madhalimu**

وَقِيلَ يَٰٓأَرۡضُ ٱبۡلَعِي مَآءَكِ وَيَٰسَمَآءُ أَقۡلِعِي وَغِيضَ ٱلۡمَآءُ
وَقُضِيَ ٱلۡأَمۡرُ وَٱسۡتَوَتۡ عَلَى ٱلۡجُودِيِّۖ وَقِيلَ بُعۡدٗا لِّلۡقَوۡمِ
ٱلظَّٰلِمِينَ ﴿٤٤﴾

*Na ikasemwa: Ewe ardhi! Meza maji yako. Na Ewe Mbingu! Jizuie. Basi maji yakadididimia chini na amri ikapitishwa na (jahazi) likasimama juu ya (jabali linaloitwa) Judi. Na ikasema: "Wameangamiziliwa mbali watu madhalimu(11:44)*

**Mafunzo kwa muhtasari**

(i) Muumini daima anaiamini kauli ya Allah(s.w) na kuitekeleza hata kama viongozi makafiri na wafuasi wao watamcheka.

(ii) Tunajifunza pia kutokana na kuangamizwa kwa kundi kubwa la watu waovu kuwa kundi la watu wengi waovu halina thamani mbele ya Allah(s.w) isipokuwa tu kama litashikamana na haki. Kundi la watu wengi waovu waliodhamiria ufisadi ni kama rundo la takataka ambalo inabidi liondoshwe katika uso wa ardhi.Kundi la watu wema wanaofuata mwongozo wa Allah(s.w)japo liwe dogo lina haki ya kudumu.

(iii) Allah(s.w) peke yake ndiye Bwana wa kila kitu katika ulimwengu huu. Akitaka anaweza kumwokoa mtu katika hatari kwa kutumia kitu dhaifu kabisa bila kutumia kitu chochote.

(iv) Kutokana na kuangamia mtoto wa nabii Nuh licha ya kuombewa dua na babake, tunajifunza kuwa Allah anao utaratibu wake wa kutoa malipo mema na adhabu. Chini ya utaratibu huo aliouweka Allah kwa uadilifu ni amali zake mtu ndizo zinazohisabiwa. Haizingatiwi nasaba ya mtu, kabila rangi, taifa, mali wala cheo. Hatanufaika mwovu kwa wema wa wazee wake.

(v) Safina ya Nuhu ni alama ya uwezo wa Allah katika kuwanusuru watu wema.

وَلَقَدۡ أَرۡسَلۡنَا نُوحًا إِلَىٰ قَوۡمِهِۦ فَلَبِثَ فِيهِمۡ أَلۡفَ سَنَةٍ إِلَّا
خَمۡسِينَ عَامٗا فَأَخَذَهُمُ ٱلطُّوفَانُ وَهُمۡ ظَٰلِمُونَ ﴿١٤﴾

*Na hakika tulimtuma Nuhu kwa watu wake na akakaa nao miaka elfu kasoro hamsini, basi tufani iliwafika, na hali ya kuwa ni madhalimu(29:14)*

فَأَنجَيۡنَٰهُ وَأَصۡحَٰبَ ٱلسَّفِينَةِ وَجَعَلۡنَٰهَآ ءَايَةٗ
لِّلۡعَٰلَمِينَ ١٥

*Na tukamuokoa yeye na watu wake katika safina, na tukaifanya (safina) iwe alama kwa walimwengu(29:15)*

Safina ya Nabii Nuhu imeonekana katika kilele kimoja wapo cha milima ya Armenia. Mnamo mwaka 1922 tetemeko la ardhi liliifanya ikae pale ilipokutwa baada ya kufukuka kwenye theluji”. Kugunduliwa kwa safina hii ni ushahidi wa wazi kwa wale wanaofanya kibri cha kukataa ukweli.

(vi) Lingine tunalojifunza ni kwamba, majanga kama vile mafuriko, matetemeko ya ardhi, na milipuko ya Volkano ni katika mpango wa Allah(s.w) wa kutoa maonyo kwa watu watanabahi kuwa yupo Muumba anayemiliki uhai wao. Hivyo wasiache njia ya uadilifu katika maisha yao na kufuata matashi ya nafsi kwa kufanya dhulma na ufuska.

(vii) Allah(s.w) anamwambia Muhammad (s.a.w.) kuwa hakuzijua kabla habari za watu wa zama zilizopita, Hapa tunafundishwa kuwa habari za hakika na sahihi za Mitume waliopita kabla ya Muhammad(s.a.w) ni zile alizoeleza Allah(s.w) ndani ya Qur,an. Vitabu vingine vyote vina maelezo ambayo yamepunguzwa, kupotoshwa au kuchanganywa na ngano za watu.

## HISTORIA YA NABII HUD(a.s) NA WATU WA ‘AD

Ad walikuwa taifa kubwa lililoasisi ustaarabu mkongwe duniani.Lilitokea baada ya kugharikishwa watu wa nabii Nuhu(as). Waliishi kusini mwa Arabuni kutokea Oman hadi Hadharamaut na Yemen.

وَإِلَىٰ عَادٍ أَخَاهُمْ هُودًا ۗ قَالَ يَٰقَوْمِ ٱعْبُدُوا۟
ٱللَّهَ مَا لَكُم مِّنْ إِلَٰهٍ غَيْرُهُۥٓ ۚ أَفَلَا تَتَّقُونَ ﴿٦٥﴾

*Na kwa Adi (tulimpeleka) ndugu yao, Hud akasema: Enyi kaumu yangu! Muabuduni Allah; nyinyi hamna mungu ila yeye. Basi hamuogopi? (7:65)*

وَإِلَىٰ عَادٍ أَخَاهُمْ هُودًا ۚ قَالَ يَٰقَوْمِ ٱعْبُدُوا۟ ٱللَّهَ مَا لَكُم
مِّنْ إِلَٰهٍ غَيْرُهُۥٓ ۖ إِنْ أَنتُمْ إِلَّا مُفْتَرُونَ ﴿٥٠﴾

*Na kwa kina Adi tuliwapelekea ndugu yao, Hud. Akasema: “Enyi watu wangu! Mwabuduni Allah; nyinyi hamna mungu isipokuwa Yeye. Hamkuwa nyinyi ila ni watungao uwongo tu.(11:50)*

يَٰقَوْمِ لَآ أَسْـَٔلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا ۖ إِنْ أَجْرِىَ إِلَّا عَلَى ٱلَّذِى
فَطَرَنِىٓ ۚ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٥١﴾

*Enyi watu wangu! Sikuombeni ujira juu ya haya; Haukuwa ujira wangu ila kwa Yule aliyeniumba. Hamyatii akilini (haya ninayokwambieni)? (11:51)*

Nabii Hud aliwalingania watu wake wamwamini Allah(s.w) na kwamba wamwabudu na kumtii Yeye peke yake.Ni jambo la kawaida kumtaka mtumishi,mathalan amtumikie mwajiri wake peke yake madamu analipwa ujira mkubwa.Mtumishi atakuwa haini mkubwa iwapo atamtumikia mtu mwingine na ilhali analipwa ili mtumikie mwajiri wake tu. Halikadhalika, binadamu anao wajibu wa kumtii Allah(s.w) na kumwabudu Yeye peke yake, kwani Allah(s.w) ndiye aliyemruzuku neema zote alizonazo hapa duniani.

أَتَبْنُونَ بِكُلِّ رِيعٍ ءَايَةً تَعْبَثُونَ ﴿١٢٨﴾ وَتَتَّخِذُونَ مَصَانِعَ
لَعَلَّكُمْ تَخْلُدُونَ ﴿١٢٩﴾ وَإِذَا بَطَشْتُم بَطَشْتُمْ جَبَّارِينَ
﴿١٣٠﴾ فَاتَّقُوا اللَّهَ وَأَطِيعُونِ ﴿١٣١﴾ وَاتَّقُوا الَّذِي أَمَدَّكُم
بِمَا تَعْلَمُونَ ﴿١٣٢﴾ أَمَدَّكُم بِأَنْعَامٍ وَبَنِينَ ﴿١٣٣﴾ وَجَنَّاتٍ
وَعُيُونٍ ﴿١٣٤﴾ إِنِّي أَخَافُ عَلَيْكُمْ عَذَابَ يَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿١٣٥﴾

*Je, mnajijengea majumba kila palipoinuka, ni mchezo tu mnafanya? Na mnajijengea (majumba kama) ngome kama kwamba mnaona mtakaa milele. Na mnaposhambulia mnashambulia kwa jeuri. Basi mcheni Allah na nitiini. Mcheni yule ambaye amekupeni haya mnayoyajua, Amekupeni (chungu ya) wanyama na watoto wanaume. Na mabustani na chemchem, (mito). Hakika ninakuhofieni adhabu ya siku kubwa . (14:128-135)*

Yaelekea kuwa watu wa 'Adi walikuwa ni taifa la watu hodari wenye ustadi mkubwa wa kujenga karakana na majumba ya fahari. Lakini badala ya kumtukuza Allah kwa hizo neema zote walizojaaliwa, wakaelekeza mikono yao kwenye dhulma, wakawa ndio taifa la mwanzo lililoanzisha ukoloni wa kuvamia watu, kuwashambulia, wakipora mali na kutawala bila ya kutumia mwongozo wa Allah.

Nabii Hud (a.s.) aliwafahamisha ukweli huu. Akawanasihi tena na tena wamwamini Allah na wazitii sheria zake. Nabii Hud (a.s.) akawaambia:

وَيَا قَوْمِ اسْتَغْفِرُوا رَبَّكُمْ ثُمَّ تُوبُوا إِلَيْهِ يُرْسِلِ السَّمَاءَ عَلَيْكُم
مِّدْرَارًا وَيَزِدْكُمْ قُوَّةً إِلَىٰ قُوَّتِكُمْ وَلَا تَتَوَلَّوْا مُجْرِمِينَ ﴿٥٢﴾

*Na enyi watu wangu! Ombeni msamaha kwa Mola wenu, kisha mtubie kwake, atakuleteeni mawingu yateremshayo mvua tele na atakuzidishieni nguvu juu ya nguvu zenu. Wala msikengeuke kuwa waovu. (11:52)*

Nabii Hud (a.s.) aliwanasihi waombe maghfira kwa Allah na watubie kwake. Allah, kwa mujibu wa Sunnah zake alizojiwekea, huwatunuku wale

wanaorejea Kwake kwa makazi mema, mali na nguvu za kusonga mbele. Mtu mwadilifu hubarikiwa na hupata radhi za Allah(s.w) na malipo mema hapa duniani na huko Akhera.

**Kibri cha watawala madhalimu dhidi ya nabii Hud(as)**

Viongozi makafiri wakamwita Hud(a.s) juha na mrongo.Wakadai kuwa hakuna chochote cha maana katika mawaidha ya Hud(a.s) ila upumbavu mtupu. Aya zifuatazo zinabainisha maneno ya viongozi hawa;

قَالَ ٱلْمَلَأُ ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ مِن قَوْمِهِۦٓ إِنَّا لَنَرَىٰكَ فِى سَفَاهَةٍ وَإِنَّا
لَنَظُنُّكَ مِنَ ٱلْكَٰذِبِينَ ﴿٦٦﴾

*Wakasema wakuu waliokufuru katika kaumu yake; Sisi tunakuona umo katika upumbavu na tunakuona u miongoni mwa waongo. (7:66)*

Kuhusiana na shutuma hizi, Nabii Hud (a.s.) akajibu:

قَالَ يَٰقَوْمِ لَيْسَ بِى سَفَاهَةٌ وَلَٰكِنِّى رَسُولٌ مِّن رَّبِّ
ٱلْعَٰلَمِينَ ﴿٦٧﴾

*Akasema: Enyi kaumu yangu! Mimi sina upumbavu. Lakini mimi ni Mtume niliyetoka kwa Mola wa walimwengu.(7:67)*

أُبَلِّغُكُمْ رِسَٰلَٰتِ رَبِّى وَأَنَا۠ لَكُمْ نَاصِحٌ أَمِينٌ ﴿٦٨﴾ أَوَعَجِبْتُمْ
أَن جَآءَكُمْ ذِكْرٌ مِّن رَّبِّكُمْ عَلَىٰ رَجُلٍ مِّنكُمْ لِيُنذِرَكُمْ ۚ
وَٱذْكُرُوٓا۟ إِذْ جَعَلَكُمْ خُلَفَآءَ مِنۢ بَعْدِ قَوْمِ نُوحٍ وَزَادَكُمْ فِى
ٱلْخَلْقِ بَصْۜطَةً ۖ فَٱذْكُرُوٓا۟ ءَالَآءَ ٱللَّهِ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٦٩﴾

*Nakufikishieni ujumbe wa Mola wangu. Na mimi kwenu ni (mtu) nasihi muaminifu. Mnaona ajabu kukufikieni mauidha yanayotoka kwa Mola wenu kwa ulimi ( ulimi wa) mtu aliye mmoja katika nyinyi ili akuonyeni? (Mwabuduni Allah) na mkumbuke alivyokufanyeni makhalifa baada ya watu wa Nuhu. Na akakuzidishieni sana katika umbo. Basi zikumbukeni neema za Allah ili mpate kufaulu. (7:67-69)*

Kama muumini alivyo, jibu la Nabii Hud (a.s.) lilikuwa wazi na kweli. Lakini watu wake wakang'ang'ania njia za mababu zao.

قَالُوٓاْ أَجِئۡتَنَا لِنَعۡبُدَ ٱللَّهَ وَحۡدَهُۥ وَنَذَرَ مَا كَانَ يَعۡبُدُ ءَابَآؤُنَاۖ
فَأۡتِنَا بِمَا تَعِدُنَآ إِن كُنتَ مِنَ ٱلصَّٰدِقِينَ ٧٠

*Wakasema: Je! Umetujia ili tumuabudu Allah peke yake na tuyaache waliyokuwa wakiyaabudu mababu zetu?Basi tuletee unayotuahidi ukiwa ni miongoni mwa wasemao kweli. (7:70)*

Nabii Hud (a.s.) akawajibu:

قَالَ قَدۡ وَقَعَ عَلَيۡكُم مِّن رَّبِّكُمۡ رِجۡسٞ وَغَضَبٌۖ أَتُجَٰدِ
لُونَنِي فِيٓ أَسۡمَآءٖ سَمَّيۡتُمُوهَآ أَنتُمۡ وَءَابَآؤُكُم مَّا نَزَّلَ ٱللَّهُ
بِهَا مِن سُلۡطَٰنٖۚ فَٱنتَظِرُوٓاْ إِنِّي مَعَكُم مِّنَ ٱلۡمُنتَظِرِينَ ٧١

*Akasema: Bila shaka adhabu na ghadhabu zimekwisha kukuangukieni kutoka kwa Mola wenu. Mnanijadili kwa ajili ya majina (tu) mliyoyaita - nyinyi na baba zenu - ambayo Allah hakuyateremshia dalili? Basi ngojeni mimi pia ni pamoja nanyi katika wangojao. (7:71)*

Kufuata njia za mababu si jambo baya maadamu njia hizi zinafundisha utiifu kwa Allah(s.w). Ama watu wa 'Adi walitaka kufuata njia ambazo hawakufundishwa na Nabii Nuhu (a.s.). Watu wa 'Adi wakakataa kuyasikiliza mafundisho ya Hud (a.s.). Na katika ubishi huo wakazusha madai eti miungu yao imemfanya Nabii Hud (a.s.) apagawe.

قَالُواْ يَٰهُودُ مَا جِئۡتَنَا بِبَيِّنَةٖ وَمَا نَحۡنُ بِتَارِكِيٓ ءَالِهَتِنَا عَن
قَوۡلِكَ وَمَا نَحۡنُ لَكَ بِمُؤۡمِنِينَ ٥٣ إِن نَّقُولُ إِلَّا ٱعۡتَرَىٰكَ
بَعۡضُ ءَالِهَتِنَا بِسُوٓءٖۗ قَالَ إِنِّيٓ أُشۡهِدُ ٱللَّهَ وَٱشۡهَدُوٓاْ أَنِّي
بَرِيٓءٞ مِّمَّا تُشۡرِكُونَ ٥٤

*Wakasema: "Ewe Hud! Hujatuletea dalili zilizo wazi; wala hatuwezi kuiacha miungu yetu kwa usemi wako; wala sisi hatutakuwa wenye*

*kukuamini wewe. Hatusemi ila kwa kuwa baadhi ya miungu yetu imekwishakukutia taabani". Akasema: Mimi namshuhudia Allah, nanyi shuhudieni ya kwamba mimi niko mbali na hao mnaowashirikisha (na Allah(*s.w*)).(11:53-54)*

مِن دُونِهِۦ ۖ فَكِيدُونِى جَمِيعًا ثُمَّ لَا تُنظِرُونِ ﴿٥٥﴾
إِنِّى تَوَكَّلْتُ عَلَى ٱللَّهِ رَبِّى وَرَبِّكُم ۚ مَّا مِن دَآبَّةٍ إِلَّا هُوَ
ءَاخِذٌۢ بِنَاصِيَتِهَآ ۚ إِنَّ رَبِّى عَلَىٰ صِرَٰطٍ مُّسْتَقِيمٍ ﴿٥٦﴾

*Mkamuacha Yeye. Basi nyote nifanyieni hila kisha msinipe muhula wowote. Mimi nimemtegemea Allah, Mola wangu na Mola wenu. Hakuna kiumbe yoyote isipokuwa anamsarifu atakavyo. Bila shaka Mola wangu yuko juu ya njia iliyonyooka(11:55-56)*

فَإِن تَوَلَّوْا۟ فَقَدْ أَبْلَغْتُكُم مَّآ أُرْسِلْتُ بِهِۦٓ إِلَيْكُمْ ۚ
وَيَسْتَخْلِفُ رَبِّى قَوْمًا غَيْرَكُمْ وَلَا تَضُرُّونَهُۥ شَيْـًٔا ۚ إِنَّ
رَبِّى عَلَىٰ كُلِّ شَىْءٍ حَفِيظٌ ﴿٥٧﴾

*Na kama mtarudi nyuma, nimekwisha kukufikishieni niliyotumwa nayo kwenu; na Mola wangu atawafanya makhalifa watu wengine wasiokuwa nyinyi; wala nyinyi hamtaweza kumdhuru hata kidogo. Hakika Mola wangu ni Mwenye kuhifadhi kila kitu. (11:57)*

**Propaganda za Viongozi makafiri dhidi ya nabii Hud(as)**

Viongozi makafiri walimkana Hud (a.s.) kwa sababu alikuwa ni binadamu kama wao. Hiyo ni hila ya kukwepa kuukubali ukweli.

وَقَالَ ٱلْمَلَأُ مِن قَوْمِهِ ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ وَكَذَّبُوا۟ بِلِقَآءِ ٱلْءَاخِرَةِ
وَأَتْرَفْنَٰهُمْ فِى ٱلْحَيَوٰةِ ٱلدُّنْيَا مَا هَٰذَآ إِلَّا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ
يَأْكُلُ مِمَّا تَأْكُلُونَ مِنْهُ وَيَشْرَبُ مِمَّا تَشْرَبُونَ ﴿٣٣﴾

*Na wakubwa katika watu wake waliokufuru na kukadhibisha makutano ya akhera, na tuliwatajirisha katika maisha ya dunia, walisema: Hakuwa huyu ila ni mtu kama nyinyi, anakula katika vile mnavyokula na anakunywa katika vile mnavyokunywa.(23:33)*

وَلَئِنْ أَطَعْتُم بَشَرًا مِّثْلَكُمْ إِنَّكُمْ إِذًا لَّخَـٰسِرُونَ ﴿٣٤﴾ أَيَعِدُ
كُمْ أَنَّكُمْ إِذَا مِتُّمْ وَكُنتُمْ تُرَابًا وَعِظَـٰمًا أَنَّكُم
مُّخْرَجُونَ ﴿٣٥﴾

*Na kama mkimtii mtu kama nyinyi mtakuwa wenye kupata khasara. Je! Anakuahidini ya kwamba mtakapokufa na mkawa udongo na mifupa, kuwa mtatolewa (mtafufuliwa)?(23:34-35)*

هَيْهَاتَ هَيْهَاتَ لِمَا تُوعَدُونَ ﴿٣٦﴾ إِنْ هِىَ إِلَّا حَيَاتُنَا
ٱلدُّنْيَا نَمُوتُ وَنَحْيَا وَمَا نَحْنُ بِمَبْعُوثِينَ ﴿٣٧﴾ إِلَّا رَجُلٌ
ٱفْتَرَىٰ عَلَى ٱللَّهِ كَذِبًا وَمَا نَحْنُ لَهُۥ بِمُؤْمِنِينَ ﴿٣٨﴾

*Hayawi! Hayawi hayo mnayoahidiwa. Hakuna (maisha mengine) ila maisha yetu haya ya dunia, tunakufa na kuishi, basi wala sisi si wenye kufufuliwa. Hakuwa huyu ila ni mtu anayemzulia Allah uongo, wala sisi si wenye kuamini. (23:36-38)*

Kusema kweli, ni binadamu tu ndiye anayeweza kuwa mfano bora kwa binadamu wengine.

Kutokana na kushitadi kwa ukaidi wao, Nabii Hud (a.s.) alimwelekea Allah(s.w) na kuomba msaada wake:

قَالَ رَبِّ ٱنصُرْنِى بِمَا كَذَّبُونِ ﴿٣٩﴾

*(Hud) akasema: Mola wangu! Ninusuru kwa sababu wamenikabidhibisha. (23:39)*

**Kwa kibri chao watawala madhalimu waomba adhabu**

Kutokana na ujinga uliosababishwa na kibri cha watawala madhalimu wakamdhihaki Hud(as) kwa kumtaka awaletee adhabu.

قَالُوٓا۟ أَجِئْتَنَا لِتَأْفِكَنَا عَنْ ءَالِهَتِنَا فَأْتِنَا بِمَا تَعِدُنَآ إِن كُنتَ
مِنَ ٱلصَّـٰدِقِينَ ﴿٢٢﴾

*Wakasema: Oh! Umetujia ili ututenge mbali na miungu yetu? Basi tuletee unayotuahidi; ikiwa u miongoni mwa wasemao kweli.(46:22)*

قَالَ إِنَّمَا ٱلْعِلْمُ عِندَ ٱللَّهِ وَأُبَلِّغُكُم مَّآ أُرْسِلْتُ بِهِۦ
وَلَٰكِنِّىٓ أَرَىٰكُمْ قَوْمًا تَجْهَلُونَ ﴿٢٣﴾

*Akasema: Ilimu hasa iko kwa Allah, nami nitakufikishieni yale niliyotumwa kwayo, walakini ninakuoneni kuwa nyinyi ni watu mfanyao mambo ya ujinga. (46:23)*

**Kuadhibiwa watu wa Hud(a.s)**

Watu wa 'Ad waliyaona mawingu yakipeperushwa na upepo mkali, yakiwaelekea wao. Kwa sababu ya kudumu kwao katika kuyakana mafundisho ya Allah, hawakuweza kutambua adhabu iliyokuwa ikiwakabili. Waliingiwa na furaha walipoyaona mawingu hayo pambizoni mwa anga kwa kudhani kuwa yalikuwa yakileta mvua.

فَلَمَّا رَأَوْهُ عَارِضًا مُّسْتَقْبِلَ أَوْدِيَتِهِمْ قَالُوا۟ هَٰذَا عَارِضٌ مُّمْطِرُنَا
بَلْ هُوَ مَا ٱسْتَعْجَلْتُم بِهِۦ ۖ رِيحٌ فِيهَا عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٢٤﴾ تُدَمِّرُ
كُلَّ شَىْءٍۭ بِأَمْرِ رَبِّهَا فَأَصْبَحُوا۟ لَا يُرَىٰٓ إِلَّا مَسَٰكِنُهُمْ ۚ كَذَٰلِكَ
نَجْزِى ٱلْقَوْمَ ٱلْمُجْرِمِينَ ﴿٢٥﴾

*Basi walipoona wingu likiyaelekea mabonde yao, walisema: Wingu hili la kutunyeshea mvua. (Wakaambiwa): Bali hii ni ile (adhabu ya Allah) mliyokuwa mkitaka ije kwa upesi. Ni upepo ambao ndani yake iko adhabu iumizayo. Unaoangamiza kila kitu kwa amri ya Mola wake. Basi wakawa si wenye kuonekana tena ila nyumba zao tu (ndizo zilizosalia). Hivyo ndivyo tuwalipavyo watu waovu. (46:24-25).*

Upepo huo mkali uliochukua muda wa siku nane, uliwaangamiza makafiri wote:

وَفِى عَادٍ إِذْ أَرْسَلْنَا عَلَيْهِمُ ٱلرِّيحَ ٱلْعَقِيمَ ﴿٤١﴾ مَا تَذَرُ مِن شَىْءٍ
أَتَتْ عَلَيْهِ إِلَّا جَعَلَتْهُ كَٱلرَّمِيمِ ﴿٤٢﴾

*Na katika (habari za) ‘’Ad (ziko alama kadhalika). Tulipowalekea upepo wa papazi uangamizao. Haukucha chochote ulichojia ila ulikifanya kama kamba mbovu. (51:41-42)*

كَذَّبَتْ عَادٌ فَكَيْفَ كَانَ عَذَابِى وَنُذُرِ ﴿١٨﴾

*Walikadhibisha kina ‘Ad (nao); basi ilikuwaje adhabu Yangu na maonyo Yangu.*

إِنَّآ أَرْسَلْنَا رِيحًا صَرْصَرًا فِى يَوْمِ نَحْسٍ مُّسْتَمِرٍّ ﴿١٩﴾ تَنزِ
عُ ٱلنَّاسَ كَأَنَّهُمْ أَعْجَازُ نَخْلٍ مُّنقَعِرٍ ﴿٢٠﴾ فَكَيْفَ كَانَ عَذَابِى
وَنُذُرِ ﴿٢١﴾

*Hakika tuliwapelekea upepo mkali katika siku ya nuhsi iendeleayo (kwao mpaka leo).Ukiwang’oa kana kwamba ni magogo ya mitende iliyong’olewa. Basi ilikuwaje adhabu Yangu na maonyo Yangu. (54:18-21)*

Aliowapelekea mausiku saba na michana minane, moja kwa moja bila kusita; utaona watu wameanguka kama kwamba ni magogo ya mitende, matupu (ya wazi ndani).

فَهَلْ تَرَىٰ لَهُم مِّنۢ بَاقِيَةٍ ﴿٨﴾

*Basi je! unamuona mmoja wao aliyebaki? (69:6-8).*

**Kuokolewa nabii Hud(as) na watu wema**

Kulingana na Sunnah ya Allah(s.w), nabii Hud (a.s.) na waumini wengine walinusurika na adhabu hiyo:

فَأَنجَيْنَٰهُ وَٱلَّذِينَ مَعَهُۥ بِرَحْمَةٍ مِّنَّا وَقَطَعْنَا دَابِرَ ٱلَّذِينَ كَذَّبُوا۟
بِـَٔايَٰتِنَا ۖ وَمَا كَانُوا۟ مُؤْمِنِينَ ﴿٧٢﴾

*Basi tukamuokoa yeye (Hud) na waliokuwa pamoja naye kwa rehema zetu, na tukakata mizizi ya wale waliozikadhibisha Aya zetu, na (ambao) hawakuwa wenye kuamini. (7:72).*

Qur’an imeyasimulia maangamizi ya kutisha yaliyowafika watu wa ‘Ad ili yawe ukumbusho kwetu kwamba maangamizi yanawasubiri wale wote wanaoleta ufisadi, uovu, dhuluma na ukatili hapa duniani kwa sababu ya kuiacha kwao njia sahihi ya Allah(s.w).

أَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِعَادٍ ﴿٦﴾ إِرَمَ ذَاتِ ٱلْعِمَادِ ﴿٧﴾ ٱلَّتِى
لَمْ يُخْلَقْ مِثْلُهَا فِى ٱلْبِلَٰدِ ﴿٨﴾ وَثَمُودَ ٱلَّذِينَ جَابُوا۟ ٱلصَّخْرَ
بِٱلْوَادِ ﴿٩﴾ وَفِرْعَوْنَ ذِى ٱلْأَوْتَادِ ﴿١٠﴾ ٱلَّذِينَ طَغَوْا۟ فِى
ٱلْبِلَٰدِ ﴿١١﴾ فَأَكْثَرُوا۟ فِيهَا ٱلْفَسَادَ ﴿١٢﴾ فَصَبَّ عَلَيْهِمْ رَبُّكَ
سَوْطَ عَذَابٍ ﴿١٣﴾

*Je! Hukuona jinsi Mola wako Alivyowafanya 'Ad? Iram (walikokuwa) wana majumba marefu marefu. Ambao hawakuumbwa mfano wao katika miji (mingine) na Thamudi waliochonga majabali (wakayafanya majumba) katika uwanja (wao).Na Firauni mwenye majumba kama vigingi. Ambao walifanya maovu katika miji Kisha walizidisha humo mambo maovu? Kwa hivyo Mola wako Aliwapiga mjeledi mmoja tu wa adhabu. (89:6-13).*

## HISTORIA YA NABII SALEH (a.s) NA WATU WA THAMUD

Historia ya watu wa Thamud inafanana na ile ya watu wa ‘Ad. Kama babu zao wa ‘Ad, watu wa Thamudu pia waliyatupa mafundisho ya Mitume wa Allah waliotangulia na wakatumbukia katika ushirikina wa kuabudu masanamu. Nabii Saleh (a.s.) aliwafundisha Tawhid kama alivyofanya Nabii Hud (a.s). Kusini mwa Bara Arabu. Ujumbe aliokuja nao na upinzani alioupata umesimuliwa katika aya zifuatazo za Qur’an:

وَإِلَىٰ ثَمُودَ أَخَاهُمْ صَٰلِحًا ۚ قَالَ يَٰقَوْمِ ٱعْبُدُوا۟ ٱللَّهَ مَا لَكُم
مِّنْ إِلَٰهٍ غَيْرُهُۥ ۖ هُوَ أَنشَأَكُم مِّنَ ٱلْأَرْضِ وَٱسْتَعْمَرَكُمْ
فِيهَا فَٱسْتَغْفِرُوهُ ثُمَّ تُوبُوٓا۟ إِلَيْهِ ۚ إِنَّ رَبِّى قَرِيبٌ مُّجِيبٌ ﴿٦١﴾

*Na kwa Thamud tukampeleka ndugu yao, Saleh. Akasema:Enyi watu wangu! Muabuduni Allah; nyinyi hamna mungu ila Yeye. Yeye ndiye aliyekuumbeni katika ardhi, na akakulisheni humo. Basi muombeni msamaha, kisha mrejee Kwake. Hakika Mola wangu ni karibu; anapokea (maombi yao). (11:61).*

Makazi yao yalikuwa kaskazini mwa Bara Arabu sehemu iliyojulikana kama Al-Hijr Mada’in Salih. Waliongoza katika ubingwa wa kuchonga majabali. Kwa kuyachonga majabali hayo walijitengenezea majumba mazuri ya fahari.

وَٱذْكُرُوٓا۟ إِذْ جَعَلَكُمْ خُلَفَآءَ مِنۢ بَعْدِ عَادٍ وَبَوَّأَكُمْ فِى ٱلْأَرْضِ
تَتَّخِذُونَ مِن سُهُولِهَا قُصُورًا وَتَنْحِتُونَ ٱلْجِبَالَ بُيُوتًا ۖ فَٱذْكُرُوٓا۟
ءَالَآءَ ٱللَّهِ وَلَا تَعْثَوْا۟ فِى ٱلْأَرْضِ مُفْسِدِينَ ﴿٧٤﴾

*Na kumbukeni (Allah) alivyokufanyeni makhalifa baada ya ‘Ad na kukuwekeni vizuri katika ardhi; mnajenga majumba makubwa ya kifalme katika nyanda zake, na mnachonga majumba katika majabali (yake). Basi zikumbukeni neema za Allah, wala msifisidi katika ardhi kwa kufanya uharibifu. (7:74).*

وَلَقَدْ كَذَّبَ أَصْحَٰبُ ٱلْحِجْرِ ٱلْمُرْسَلِينَ ﴿٨٠﴾ وَءَاتَيْنَٰهُمْ
ءَايَٰتِنَا فَكَانُوا۟ عَنْهَا مُعْرِضِينَ ﴿٨١﴾ وَكَانُوا۟ يَنْحِتُونَ مِنَ
ٱلْجِبَالِ بُيُوتًا ءَامِنِينَ ﴿٨٢﴾

*Na bila shaka wakazi wa Hijri (pia) waliwakadhibisha Mitume. Na tuliwapa maonyo yetu; lakini walikuwa wakiyapuuza. Nao walikuwa wakichonga majumba katika majabali kwa amani. (15:80-82).*

**Ujumbe wa nabii Saleh(a.s) kwa watu wake**

Nabii Saleh (a.s) aliwalingania wamwamini Allah(s.w), watubie na waombe msamaha kwa dhambi zao na uasi wao. Aliwanasihi wamshukuru Allah(s.w) kwa neema zote alizowapa... wasaa, amani, bustani, mito, miti na majumba.

وَتَنْحِتُونَ مِنَ ٱلْجِبَالِ بُيُوتًا فَٰرِهِينَ ﴿١٤٩﴾ فَٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ
وَأَطِيعُونِ ﴿١٥٠﴾ وَلَا تُطِيعُوٓا۟ أَمْرَ ٱلْمُسْرِفِينَ ﴿١٥١﴾ ٱلَّذِينَ
يُفْسِدُونَ فِى ٱلْأَرْضِ وَلَا يُصْلِحُونَ ﴿١٥٢﴾

*Na Mnachonga milimani majumba mkistarehe tu basi. Mcheni Allah na nitiini. Wala msitii amri za wale maasi. Ambao wanafanya uharibifu tu katika ardhi wala hawaitengenezi. (26:149-152).*

Hapana shaka yoyote kuwa inampasa binadamu amshukuru Muumba wake, ambaye ndiye anayempatia yote anayohitaji. Lakini kiburi kinachosababishwa na uwingi wa mali na maisha ya anasa katika majumba ya fahari humsahaulisha wajibu wake huu.Nabii Saleh (a.s) aliwakumbusha baadhi ya neema za Allah(s.w) walizopewa ili kuwazindusha watekeleze wajibu wao kwa Muumba wao.Akawaonya wasifuate mwendo wa wale watu waovu katika jamii ambao ndio sababu ya ufidhuli na uasi.

**Propaganda za viongozi madhalimu dhidi ya nabii Saleh(a.s)**

Viongozi madhalimu wakazusha uvumi wakiwaambia watu kuwa Saleh(a.s) hakutumwa na Allah(s.w). Wakasema, Saleh(a.s) amerogwa.

قَالَ ٱلْمَلَأُ ٱلَّذِينَ ٱسْتَكْبَرُوا۟ مِن قَوْمِهِۦ لِلَّذِينَ ٱسْتُضْعِفُوا۟ لِمَنْ
ءَامَنَ مِنْهُمْ أَتَعْلَمُونَ أَنَّ صَٰلِحًا مُّرْسَلٌ مِّن رَّبِّهِۦ ۚ قَالُوٓا۟ إِنَّا بِمَآ
أُرْسِلَ بِهِۦ مُؤْمِنُونَ ﴿٧٥﴾ قَالَ ٱلَّذِينَ ٱسْتَكْبَرُوٓا۟ إِنَّا بِٱلَّذِىٓ ءَا
مَنتُم بِهِۦ كَٰفِرُونَ ﴿٧٦﴾

*Wakasema wakuu wa kaumu yake waliotakabari, kuwaambia wale walio dhaifu wenye kuamini miongoni mwao: Je! Mnaitakidi ya kwamba Salehe ametumwa na Mola wake? Wakasema: Hakika tunayaamini yale aliyotumwa (kuyafikisha).Wakasema wale waliotakabari: Sisi tunayakataa yale mnayoyaamini. (7:75-76).*

قَالُوا۟ يَٰصَٰلِحُ قَدْ كُنتَ فِينَا مَرْجُوًّا قَبْلَ هَٰذَآ ۖ أَتَنْهَىٰنَآ أَن نَّعْبُدَ
مَا يَعْبُدُ ءَابَآؤُنَا وَإِنَّنَا لَفِى شَكٍّ مِّمَّا تَدْعُونَآ إِلَيْهِ مُرِيبٍ ﴿٦٢﴾

*Wakasema: Ewe Saleh! Bila shaka ulikuwa unayetarajiwa (kheri) kwetu kabla ya haya. (Sasa umeharibika). Oh! Unatukataza kuabudu waliowaabudu baba zetu? Na hakika sisi tumo katika shaka inayotusugua (katika nyoyo zetu) kwa haya unayotuitia.(11:62)*

قَالَ يَٰقَوْمِ أَرَءَيْتُمْ إِن كُنتُ عَلَىٰ بَيِّنَةٍ مِّن رَّبِّى وَءَاتَىٰنِى مِنْهُ
رَحْمَةً فَمَن يَنصُرُنِى مِنَ ٱللَّهِ إِنْ عَصَيْتُهُۥ ۖ فَمَا تَزِيدُونَنِى غَيْرَ
تَخْسِيرٍ ﴿٦٣﴾

*Akasema: Enyi watu wangu! Mnaonaje, kama ninazo dalili zilizowazi zitokazo kwa Mola wangu, naye amenipa rehema kutoka Kwake, basi ni nani atakayeninusuru kwa Allah kama nikimuasi? Basi hamtanizidishia ila khasara. (11:63).*

قَالُوٓا۟ إِنَّمَآ أَنتَ مِنَ ٱلْمُسَحَّرِينَ ﴿١٥٣﴾ مَآ أَنتَ إِلَّا بَشَرٌ مِّثْلُنَا فَأْتِ
بِـَٔايَةٍ إِن كُنتَ مِنَ ٱلصَّٰدِقِينَ ﴿١٥٤﴾

*Wakasema: Hakika wewe ni miongoni mwa waliorogwa (wakakosa akili).Wewe si chochote ila ni mtu kama sisi; basi lete mwujiza ikiwa ni miongoni mwa wasemao kweli (26:153-154).*

Makafiri waliwakejeli wale waumini wachache waliovutwa na ukweli na mafundisho ya nabii Saleh (a.s.), na wakamkana Saleh(a.s) kwa sababu aliwakataza kufuata mwenendo usiokuwa sahihi wa babu zao. Nabii Saleh (a.s.) alikuwa na tabia njema na mwenendo ulio bora kabisa tangu wakati wa ujana wake. Jambo hilo liliwafanya watu wake wampende na kumheshimu na walikuwa na matumaini makubwa juu yake. Lakini la ajabu ni kwamba mtu huyo huyo waliyemwamini alipoteuliwa kuwa mtume wa Allah(s.w) ili awaongoze watu wake katika furaha ya milele watu wale wale wakaanza kumshutumu na kumpinga.

Aidha, wakamkana na kuonesha kutoridhika kwao kuwa mtu wa kawaida ametueliwa kufikisha ujumbe wa Allah(s.w) badala ya wao, wenye nguvu na mali.

**Kuuawa ngamia wa Muujiza**

Walidai tena na tena waoneshwe mwujiza kutoka kwa Allah. Kwa wahyi na idhini ya Allah(s.w) nabii Saleh(a.s) aliwaonesha mwujiza wa ngamia jike.Ulipangwa muda wa ngamia huyo kunywa maji kisimani na wakati huo watu wote walitakiwa wasiwanyweshe wanyama wao katika kisima hicho. Waliambiwa pia kuwa watakuwa salama maadamu hawatamdhuru ngamia huyo.

قَالَ هَـٰذِهِۦ نَاقَةٌ لَّهَا شِرْبٌ وَلَكُمْ شِرْبُ يَوْمٍ مَّعْلُومٍ ﴿١٥٥﴾

وَلَا تَمَسُّوهَا بِسُوٓءٍ فَيَأْخُذَكُمْ عَذَابُ يَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿١٥٦﴾

*Akasema: Huyu ngamia jike; awe na zamu yake ya kunywa, na nyinyi muwe na zamu yenu ya kuteka katika siku maalum. Wala msimguse kwa ubaya isije ikakushikeni adhabu ya siku kubwa.(26:155-156)*

فَعَقَرُوا۟ ٱلنَّاقَةَ وَعَتَوْا۟ عَنْ أَمْرِ رَبِّهِمْ وَقَالُوا۟ يَـٰصَـٰلِحُ ٱئْتِنَا

بِمَا تَعِدُنَآ إِن كُنتَ مِنَ ٱلْمُرْسَلِينَ ﴿٧٧﴾

*Na wakamtumbua (wakamwua) yule ngamia na wakaasi amri ya Mola wao na wakasema: Ee Saleh! Tuletee unayotuahidi ikiwa wewe ni miongoni mwa Mitume.(7:77)*

Kama fursa yao ya mwisho walipewa siku tatu za kutubia baada ya kitendo chao kiovu cha kumwua ngamia.

**Kamati ya madhalimu yapanga kumuua nabii Saleh(a.s)**

Lakini siyo tu kwamba walimwulia mbali ngamia huyo bali pia walikula njama ya kumwua nabii Saleh (a.s.).Tunafahamishwa juu ya njama zilizofanywa na kamati ya watu tisa mashuhuri katika jamii hiyo ili wamuue nabii Salehe (a.s.):

وَكَانَ فِي الْمَدِينَةِ تِسْعَةُ رَهْطٍ يُفْسِدُونَ فِي الْأَرْضِ وَلَا
يُصْلِحُونَ ﴿٤٨﴾ قَالُوا تَقَاسَمُوا بِاللَّهِ لَنُبَيِّتَنَّهُ وَأَهْلَهُ ثُمَّ
لَنَقُولَنَّ لِوَلِيِّهِ مَا شَهِدْنَا مَهْلِكَ أَهْلِهِ وَإِنَّا لَصَادِقُونَ ﴿٤٩﴾

*Na walikuwamo mjini watu tisa wakifanya ufisadi katika ardhi wala hawakusuluhisha (jambo ila kuharibu tu).Wakasema: Apianeni kwa Allah (ya kwamba) tutamshambulia usiku yeye (Saleh) na watu wake, kisha tutamwambia mrithi wake: Sisi hatukuona maangamio (yake wala) ya watu wake na bila shaka sisi ni wakweli kwao.(27:48-49)*

وَمَكَرُوا مَكْرًا وَمَكَرْنَا مَكْرًا وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٥٠﴾

*Basi wakapanga vitimbi (vyao); na sisi tukapanga mipango (yetu) na hali ya kuwa hawana habari.(27:50)*

**Kuangamizwa watawala madhalimu na wafuasi wao**

Mwisho wa siku ya tatu, makafiri waliangamizwa na tufani kali iliyoambatana na radi, dhoruba na umeme. Nabii Salehe (a.s.) na wafuasi wake wa kweli walinusurika.

فَأَخَذَتْهُمُ الرَّجْفَةُ فَأَصْبَحُوا فِي دَارِهِمْ جَاثِمِينَ ﴿٧٨﴾
فَتَوَلَّىٰ عَنْهُمْ وَقَالَ يَا قَوْمِ لَقَدْ أَبْلَغْتُكُمْ رِسَالَةَ رَبِّي وَنَصَحْتُ
لَكُمْ وَلَٰكِن لَّا تُحِبُّونَ النَّاصِحِينَ ﴿٧٩﴾

*Tetemeko la ardhi likazinyakua roho zao na wakawa wamekufa humo katika miji yao. Basi (Saleh) akawaacha, na huku anasema: Enyi watu wangu! Nilikufikishieni ujumbe wa Mola wangu na nikakunasihini, lakini hamuwapendi wenye nasaha(7:78-79)*

## HISTORIA YA NABII IBRAHIM (A.S.)

Matukio yanayohusiana na Mtume wa Allah(s.w), Ibrahim(a.s) yamesimuliwa katika sura ishirini na tano za Qur'an. Maisha yake ni kiigizo chema cha jinsi ya kuutii ujumbe wa Allah(s.w), na kujitahidi upeo wa jitihada katika kuwalingania watu ukweli.

Alizaliwa na kulelewa huko Iraq ambako babake aliyeitwa Azar alikuwa akichonga masanamu ya mbao na kuyauza kwa washirkina waliokuwa wakiabudu masanamu.

**Nabii Ibrahiim(a.s) amlingania Uislamu baba yake**

Ibrahiim(a.s) alitambua Upweke wa Allah(s.w) tangu alipokuwa bado yu ngali kijana. Aliufikisha ujumbe wa Allah(s.w) kwa namna nyepesi, iliyowazi na kwa kutumia hoja zenye nguvu.

وَٱذۡكُرۡ فِي ٱلۡكِتَٰبِ إِبۡرَٰهِيمَۚ إِنَّهُۥ كَانَ صِدِّيقٗا نَّبِيًّا ﴿٤١﴾
إِذۡ قَالَ لِأَبِيهِ يَٰٓأَبَتِ لِمَ تَعۡبُدُ مَا لَا يَسۡمَعُ وَلَا يُبۡصِرُ وَلَا يُغۡنِي
عَنكَ شَيۡـٔٗا ﴿٤٢﴾

*Na mtaje Ibrahim katika Kitabu (hiki). Bila shaka yeye alikuwa mkweli sana, Nabii. (Wakumbushe), alipomwambia baba yake: Ewe baba yangu! Kwanini unaabudu visivyosikia na visivyoona na visivyokufaa chochote?(19:41 -42)*

يَٰٓأَبَتِ إِنِّي قَدۡ جَآءَنِي مِنَ ٱلۡعِلۡمِ مَا لَمۡ يَأۡتِكَ فَٱتَّبِعۡنِيٓ أَهۡدِكَ
صِرَٰطٗا سَوِيّٗا ﴿٤٣﴾ يَٰٓأَبَتِ لَا تَعۡبُدِ ٱلشَّيۡطَٰنَۖ إِنَّ ٱلشَّيۡطَٰنَ
كَانَ لِلرَّحۡمَٰنِ عَصِيّٗا ﴿٤٤﴾ يَٰٓأَبَتِ إِنِّيٓ أَخَافُ أَن يَمَسَّكَ عَذَا
بٞ مِّنَ ٱلرَّحۡمَٰنِ فَتَكُونَ لِلشَّيۡطَٰنِ وَلِيّٗا ﴿٤٥﴾

*Ewe baba yangu! Kwa yakini imenijia ilimu isiyokujia. Basi nifuate nitakuongoza njia iliyo sawa.Ewe baba yangu! usimwabudu Shetani, hakika Shetani ni mwenye kumuasi (Allah) Mwingi wa rehema.Ewe baba yangu! Hakika naogopa kukupata adhabu inayotoka kwa Mwingi wa rehema, (ukifanya hivyo) utakuwa mwenziwe shetani.(19:43-45)*

قَالَ أَرَاغِبٌ أَنتَ عَنْ ءَالِهَتِى يَـٰٓإِبْرَٰهِيمُ ۖ لَئِن لَّمْ تَنتَهِ
لَأَرْجُمَنَّكَ ۖ وَٱهْجُرْنِى مَلِيًّا ﴿٤٦﴾

*Akasema (yule baba yake): Je! unaichukia miungu yangu, ewe Ibrahim? Kama huachi (haya unayosema) lazima nitakupiga mawe. Na niondokelee mbali, kwa muda mchache (huu).(19:46)*

قَالَ سَلَـٰمٌ عَلَيْكَ ۖ سَأَسْتَغْفِرُ لَكَ رَبِّىٓ ۖ إِنَّهُۥ كَانَ بِى حَفِيًّا ﴿٤٧﴾
وَأَعْتَزِلُكُمْ وَمَا تَدْعُونَ مِن دُونِ ٱللَّهِ وَأَدْعُوا۟ رَبِّى عَسَىٰٓ أَلَّآ
أَكُونَ بِدُعَآءِ رَبِّى شَقِيًّا ﴿٤٨﴾

*(Ibrahim) akasema: Amani iwe juu yako! Nitakuombea msamaha kwa Mola wangu, bila shaka Yeye ananihurumia sana.Na mimi nakuondokeeni na mnayoyaabudu kinyume cha Allah. Na nitamuomba Mola wangu: hakika sitakuwa mwenye kukhibu (kukosa ninalolitaka) kwa kumuomba Mola wangu.(19:47-48)*

**Katika aya hizi tunajifunza kuwa**

Ibrahim (a.s.) ametajwa kuwa ni mkweli kwa kiwango cha juu kabisa (Siddiq) na ni Mtume wa Allah(s.w).Alijitahidi sana kumsihi baba yake aepukane na shirk ya kuabudu masanamu.Alieleza kushangazwa kwake juu ya tabia ya washirikina ya kuviabudu vitu ambavyo havikuwa na uwezo wowote wa kuwanufaisha wala kuwadhuru kwa chochote.

Kutokana na wahyi alioupata Ibrahim (a.s.) aliweza kumwonesha baba yake njia iliyosahihi. Alijadiliana na baba yake ili kumzuia asimwabudu Shetani na asizifuate njia zake na alimuhadharisha pia juu ya adhabu ya Allah(s.w) endapo angeendelea kumtii Shetani.

Lakini ushauri huo wa Ibrahiim (a.s.) ulimchukiza baba yake, na akamkamia kumrujumu kama hakuacha kuishambulia miungu yao ya sanamu.

Nabii Ibrahim (a.s.) aliamua kuwahama washirikina hao akiwemo baba yake, ili akaisimamishe dini ya Kiislamu mahali pengine. Alimuahidi baba yake kuwa atamwombea dua njema kwa Allah ili amsamehe makosa

yake. Nabii Ibrahim (a.s.) alikuwa bado ana tamaa kuwa baba yake atakuwa Mwislamu. Lakini baadaye matumaini hayo yakamwondoka na akajitenga naye. Hili tunafahamishwa katika aya ifuatayo:

وَمَا كَانَ ٱسْتِغْفَارُ إِبْرَٰهِيمَ لِأَبِيهِ إِلَّا عَن مَّوْعِدَةٍ وَعَدَهَآ إِيَّاهُ
فَلَمَّا تَبَيَّنَ لَهُۥٓ أَنَّهُۥ عَدُوٌّ لِّلَّهِ تَبَرَّأَ مِنْهُ إِنَّ إِبْرَٰهِيمَ لَأَوَّٰهٌ حَلِيمٌ ﴿١١٤﴾

*Wala haikuwa Ibrahim kumtakia samahani baba yake ila kwa sababu ya ahadi aliyofanya naye. Lakini ilipombainikia kwamba yeye (huyo baba yake) ni adui wa (dini ya) Allah (kwa ukaidi tu si ujinga), alijiepusha naye. Kwa yakini Ibrahim alikuwa mwingi wa kurejea kwa Allah (na) mvumilivu. (9:114).*

**Nabii Ibrahiim ailingania jamii yake irejee katika Uislamu**

Baada ya kumlingania baba yeke, nabii Ibrahiim akaanza kuufikisha ujumbe wa Allah(s.w) kwa jamii yake na kuitaka irejee kwenye Uislamu. Akaanza kuhojiana na watu waliokuwa wakiabudia jua, mwezi, nyota, na masanamu.

فَلَمَّا جَنَّ عَلَيْهِ ٱلَّيْلُ رَءَا كَوْكَبًا قَالَ هَٰذَا رَبِّى فَلَمَّآ أَفَلَ قَالَ
لَآ أُحِبُّ ٱلْءَافِلِينَ ﴿٧٦﴾ فَلَمَّا رَءَا ٱلْقَمَرَ بَازِغًا قَالَ هَٰذَا رَبِّى فَلَمَّآ
أَفَلَ قَالَ لَئِن لَّمْ يَهْدِنِى رَبِّى لَأَكُونَنَّ مِنَ ٱلْقَوْمِ ٱلضَّآلِّينَ ﴿٧٧﴾
فَلَمَّا رَءَا ٱلشَّمْسَ بَازِغَةً قَالَ هَٰذَا رَبِّى هَٰذَآ أَكْبَرُ فَلَمَّآ أَفَلَتْ
قَالَ يَٰقَوْمِ إِنِّى بَرِىٓءٌ مِّمَّا تُشْرِكُونَ ﴿٧٨﴾ إِنِّى وَجَّهْتُ وَجْهِىَ
لِلَّذِى فَطَرَ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضَ حَنِيفًا وَمَآ أَنَا۠ مِنَ
ٱلْمُشْرِكِينَ ﴿٧٩﴾

*Na usiku ulipomwingilia Ibrahiimu aliona nyota; akasema, "nyota hii ni Mola wangu. Ilipopotea alisema: "Sipendi miungu wanaopotea. Na (usiku wa pili) alipouona mwezi unachomoza, alisema: "Huu ndio Mola wangu. Ulipotua alisema: " Asiponiongoza Mola wangu, bila shaka nitakuwa miongoni mwa watu wapotofu. Na (siku ya tatu) alipoliaona jua linachomoza alisema; "Hili ndilo*

*Mola wangu. Huyu Mola mkubwa kabisa. Lilipotua akasema: "Enyi watu wangu! Mimi simo katika hayo mnayomshirikisha (nayo Allah(*s.w*). Mimi nimeuelekeza uso wangu kwa yule aliyeziumba mbingu na ardhi, hali ya kuwa nimeacha dini za upotevu. Mimi si miongoni mwa washirikina(6:76-79)*

Katika aya hizi nabii Ibrahim (a.s.) alitoa hoja zilizodhihirisha udhaifu wa vitu hivyo vitatu kwani vilikuwa vikitokeza na baadaye kutoweka. Itawezekanaje kwa nyota, mwezi au jua kuwa miungu wakati vyenyewe vinadhibitiwa na nguvu kuu yenye mamlaka ya kuvifanya vitoweke pambizoni mwa anga baada ya muda mfupi?

Kwa njia hii nabii Ibrahim (a.s.) alizihudhurisha akili za watu wake zitanabahi juu ya kuwepo kwa Allah(s.w) na akawabainishia kuwa yeye hakumshirikisha Allah(s.w) na yeyote na kwamba alijitenga na washirikina. Neno la Kiarabu ‘Hanif’ limetumika hapa kuielezea imani hii. Neno hilo hilo limetumika katika Qur’an pale Ibrahim alipotajwa kuwa ni Hanif kinyume na madai ya Wayahudi au Wakristo waliyoyaleta baadaye kuwa yeye Ibrahim alikuwa ama Myahudi au Mkristo. Madai hayo hayana msingi kwa sababu nabii Ibrahim (a.s.) aliishi na kuondoka duniani kabla ya kuchipuka kwa dini hizo mbili za bandia.

يَٰٓأَهۡلَ ٱلۡكِتَٰبِ لِمَ تُحَآجُّونَ فِيٓ إِبۡرَٰهِيمَ وَمَآ أُنزِلَتِ ٱلتَّوۡرَىٰةُ
وَٱلۡإِنجِيلُ إِلَّا مِنۢ بَعۡدِهِۦٓۚ أَفَلَا تَعۡقِلُونَ ٦٥

*Enyi mliopewa Kitabu! Mbona mnabishana juu ya Ibrahiimu, na hali Taurati na Injili havikuteremshwa ila baada yake? Basi je, hamfahamu?(3:65)*

مَا كَانَ إِبۡرَٰهِيمُ يَهُودِيّٗا وَلَا نَصۡرَانِيّٗا وَلَٰكِن كَانَ حَنِيفٗا
مُّسۡلِمٗا وَمَا كَانَ مِنَ ٱلۡمُشۡرِكِينَ ٦٧

*Ibrahiimu hakuwa Myahudi wala Mkristo, lakini alikuwa mwongofu mtii; wala hakuwa katika washirikina(3:67)*

### Ujumbe wa Ibrahiim(as) kwa mfalme

Nabii Ibrahiim hakuishia kulingania Uislamu kwa baba yake na watu wake tu, bali alisonga mbele na kuufikisha ujumbe wa Allah kwa Namrud aliyekuwa mtawala wa jamii hiyo. Mfalme Namrud alikuwa akiwanyonya watu na kuwadhulumu kupitia kanuni na sheria za dini ya ushirikina. Nabii

Ibrahiim(a.s) alimkabili na mjadala mzito ukajiri kati yao. Allah(s.w) anatusimulia kuwa:

أَلَمْ تَرَ إِلَى ٱلَّذِى حَآجَّ إِبْرَٰهِـۧمَ فِى رَبِّهِۦٓ أَنْ ءَاتَىٰهُ ٱللَّهُ
ٱلْمُلْكَ إِذْ قَالَ إِبْرَٰهِـۧمُ رَبِّىَ ٱلَّذِى يُحْىِۦ وَيُمِيتُ قَالَ أَنَا۠
أُحْىِۦ وَأُمِيتُ ۖ قَالَ إِبْرَٰهِـۧمُ فَإِنَّ ٱللَّهَ يَأْتِى بِٱلشَّمْسِ مِنَ ٱلْمَشْرِقِ
فَأْتِ بِهَا مِنَ ٱلْمَغْرِبِ فَبُهِتَ ٱلَّذِى كَفَرَ ۗ وَٱللَّهُ لَا يَهْدِى ٱلْقَوْمَ
ٱلظَّـٰلِمِينَ ﴿٢٥٨﴾

*Hukumsikia yule aliyehojiana na Ibrahimu juu ya Mola wake kwa sababu Allah alimpa ufalme? Ibrahim aliposema: Mola wangu ni yule ambaye huhuisha na kufisha, yeye akasema: Mimi pia nahuisha na kufisha. Ibrahim akasema: Allah hulichomozesha jua mashariki, basi wewe lichomozeshe magharibi. Akafedheheka yule aliyekufuru; na Allah hawaongozi watu madhalimu.(2: 258)*

Mfalme alipodai kuwa yeye pia anahuisha na kufisha alikusudia ule uwezo wake wa kumhukumu mtu kifo au kumwachilia huru. Nabii Ibrahim (a.s) aliujua udhaifu wa hoja hii, lakini badala ya kuendelea kujadiliana naye juu ya madai yake haya akaamua kumpa pigo kwa kumtolea hoja hii:

*"Mwumba wangu hulichomozesha jua Mashariki. Wewe lichomozeshe Magharibi ikiwa wadai kuwa u Muumba."*

**Ibrahiim(a.s) avunja masanamu kuwatanabahisha washirikina**

Watu wake walikuwa wanauhama mji ule" kwenda kuadhimisha sherehe ya kidini hadharani. Wakamwalika Ibrahim (a.s.) aungane nao. Nabii Ibrahim (a.s.) aliukataa mwaliko huo. Nabii Ibrahim (a.s.) akatazama nyota kwa mtazamo mkubwa kana kwamba alikuwa akififikiri kwa makini sana halafu akasema:

إِنِّى سَقِيمٌ ﴿٨٩﴾

*"Hakika mimi ni mgonjwa." (Saffat: 32-89)*

Halafu akaingia hekaluni na akakuta vyakula vingi wamewekewa wale miungu wa sanamu.Mkasa huu unasimuliwa katika aya zifuatazo:

وَلَقَدْ ءَاتَيْنَآ إِبْرَٰهِيمَ رُشْدَهُۥ مِن قَبْلُ وَكُنَّا بِهِۦ عَٰلِمِينَ ﴿٥١﴾

إِذْ قَالَ لِأَبِيهِ وَقَوْمِهِۦ مَا هَٰذِهِ ٱلتَّمَاثِيلُ ٱلَّتِىٓ أَنتُمْ لَهَا عَٰكِفُونَ ﴿٥٢﴾

*Na hakika tulimpa Ibrahim uwongofu wake zamani na tulikuwa tukimjua (vizuri). Alipomwambia baba yake na watu wake: "Ni nini masanamu haya mnayakalia wakati wote (kuyaabudu)?(21:51-52)*

قَالُوا۟ وَجَدْنَآ ءَابَآءَنَا لَهَا عَٰبِدِينَ ﴿٥٣﴾

*Wakasema, "Tuliwakuta baba zetu wakiyaabudu"(21:53)*

قَالَ لَقَدْ كُنتُمْ أَنتُمْ وَءَابَآؤُكُمْ فِى ضَلَٰلٍ مُّبِينٍ ﴿٥٤﴾

*Akasema: "Bila shaka nyinyi na baba zenu mlikuwa katika upotofu ulio dhahiri." (21:54)*

قَالُوٓا۟ أَجِئْتَنَا بِٱلْحَقِّ أَمْ أَنتَ مِنَ ٱللَّٰعِبِينَ ﴿٥٥﴾

*Wakasema: "Je, umetujia kwa (maneno ya) haki au umo miongoni mwa wachezaji?(21:55)*

قَالَ بَل رَّبُّكُمْ رَبُّ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ ٱلَّذِى فَطَرَهُنَّ وَأَنَا۠ عَلَىٰ ذَٰلِكُم مِّنَ ٱلشَّٰهِدِينَ ﴿٥٦﴾

*Akasema: "(Siyo! Mimi si mchezaji) Bali Mola wenu ni yule Mola wa mbingu na ardhi ambaye ndiye aliyeziumba. Nami ni miongoni mwa wenye kuyashuhudia haya.(21:56)*

وَتَٱللَّهِ لَأَكِيدَنَّ أَصْنَٰمَكُم بَعْدَ أَن تُوَلُّوا۟ مُدْبِرِينَ ﴿٥٧﴾

*"Na Wallahi nitayafanyia mabaya masanamu yenu haya baada ya kunipa mgongo mkenda zenu."(21:57)*

فَجَعَلَهُمْ جُذَٰذًا إِلَّا كَبِيرًا لَّهُمْ لَعَلَّهُمْ إِلَيْهِ يَرْجِعُونَ ﴿٥٨﴾

*Basi akayavunja vipande vipande isipokuwa lile kubwa lao (aliliacha), ili wao walirudie.(21:58)*

Watu wake wakaja kugundua pigo lililowafika miungu wao.

قَالُوا۟ مَن فَعَلَ هَٰذَا بِـَٔالِهَتِنَآ إِنَّهُۥ لَمِنَ ٱلظَّٰلِمِينَ ﴿٥٩﴾ قَالُوا۟
فَتًى يَذْكُرُهُمْ يُقَالُ لَهُۥٓ إِبْرَٰهِيمُ ﴿٦٠﴾ قَالُوا۟ فَأْتُوا۟ بِهِۦ عَلَىٰٓ
أَعْيُنِ ٱلنَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَشْهَدُونَ ﴿٦١﴾

*Wakasema: "Nani aliyeifanya hivi miungu yetu? Hakika huyo yu miongoni mwa madhalimu." Wakasema: "Tulimsikia kijana mmoja akiwataja anayeitwa Ibrahim."Wakasema: "Basi mleteni mbele ya macho ya watu, wamshuhudie."(21:59-61)*

Makemeo ya Ibrahim dhidi ya miungu wao hayakuwa siri. Hivyo wakamkamata na kumshitaki hadharani.

قَالُوٓا۟ ءَأَنتَ فَعَلْتَ هَٰذَا بِـَٔالِهَتِنَا يَٰٓإِبْرَٰهِيمُ ﴿٦٢﴾

*Wakasema: Je! Wewe umeifanya hivi miungu yetu, ee Ibrahim?"(21:62)*

Nabii Ibrahim (a.s.) akapata fursa ya kuwarushia kombora ambalo lilikuwa ni kipigo chao cha mwisho.akawaambia,

قَالَ بَلْ فَعَلَهُۥ كَبِيرُهُمْ هَٰذَا فَسْـَٔلُوهُمْ إِن كَانُوا۟ يَنطِقُونَ ﴿٦٣﴾

*Akasema: "Siyo, Bali amefanya (hayo) huyu mkubwa wao, basi waulizeni kama wanaweza kunena!"(21:63)*

فَرَجَعُوٓا۟ إِلَىٰٓ أَنفُسِهِمْ فَقَالُوٓا۟ إِنَّكُمْ أَنتُمُ ٱلظَّٰلِمُونَ ﴿٦٤﴾ ثُمَّ
نُكِسُوا۟ عَلَىٰ رُءُوسِهِمْ لَقَدْ عَلِمْتَ مَا هَٰٓؤُلَآءِ يَنطِقُونَ ﴿٦٥﴾

*Basi wakajirudi nafsi zao na wakasema: "Hakika nyinyi mlikuwa madhalimu."Kisha wakainamisha vichwa vyao, (wakasema): "Hakika umekwishajua ya kwamba hawasemi, (kwa nini unatucheza shere?)"(21:64-65)*

Ilipofikia hatua hiyo Washirikina wakauona udhalilifu wa akili zao zilizowaongoza kumwacha Allah (s.w)na kwenda kuyaabudu masanamu dhaifu yasiyojiweza hata kujitetea yenyewe. Hapo nabii Ibrahiim akasema:

قَالَ أَفَتَعْبُدُونَ مِن دُونِ ٱللَّهِ مَا لَا يَنفَعُكُمْ شَيْـًٔا وَلَا يَضُرُّكُمْ
﴿٦٦﴾ أُفٍّ لَّكُمْ وَلِمَا تَعْبُدُونَ مِن دُونِ ٱللَّهِ ۖ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٦٧﴾

*Akasema: “Je! Mnaabudu badala ya Allah, (miungu) isiokufaeni chochote wala kukudhuruni?” Kefule yenu na ya hivyo mnavyoviabudu kinyume cha Allah. Je! hamfikiri?(21:66-67)*

**Allah(s.w) amnusuru Ibrahiim(a.s) na hila za makafiri**

Hatimaye waka muhukumu auliwe, Wakasema:

حَرِّقُوهُ وَٱنصُرُوٓاْ ءَالِهَتَكُمْ إِن كُنتُمْ فَٰعِلِينَ ﴿٦٨﴾

*Mteketezeni kwa moto na muinusuru miungu yenu, ikiwa nyinyi ni watendao jambo.(21:68)*

قُلْنَا يَٰنَارُ كُونِى بَرْدًا وَسَلَٰمًا عَلَىٰٓ إِبْرَٰهِيمَ ﴿٦٩﴾ وَأَرَادُواْ بِهِۦ
كَيْدًا فَجَعَلْنَٰهُمُ ٱلْأَخْسَرِينَ ﴿٧٠﴾ وَنَجَّيْنَٰهُ وَلُوطًا إِلَى ٱلْأَرْضِ
ٱلَّتِى بَٰرَكْنَا فِيهَا لِلْعَٰلَمِينَ ﴿٧١﴾

*”Tukasema: “Ewe mtoto! kuwa baridi na salamu kwa Ibrahim.”Na walimtakia ubaya, lakini tukawafanya wao ndio wenye kupata hasara.Na tulimuokoa yeye na Lut (tukawapeleka) katika ardhi tuliyoibarikia kwa ajili ya walimwengu.(21:68-71)*




**Nabii Ibrahiim(as) ahama**

Mtume hana budi kuwaacha watu wake anapoamriwa na Allah(s.w) kufanya hivyo.

وَقَالَ إِنِّى ذَاهِبٌ إِلَىٰ رَبِّى سَيَهْدِينِ ﴿٩٩﴾

*Na Ibrahiimu akasema: "Mimi nakwenda kwa Mola wangu. Ndiye atakayeniongoza.(37:99)*

Tunamkuta Ibrahim(a.s) akifanya safari nyingine kwenda Misri pamoja na mkewe Sarah. Huko Misri Ibrahim alimwoa Hajirah ambaye alikuwa ni mjakazi wa Sarah. Sarah alimpata mjakazi huyo huko huko Misri.

**Ibrahiim(as) amuomba Allah(s.w) amjaalie mtoto mwema**

Nabii Ibrahim (a.s.) aliomba kupata kizazi chema. Allah alimpa habari njema za kumpata mtoto mwenye tabia bora ya subira na upole (Halim).

رَبِّ هَبْ لِى مِنَ ٱلصَّٰلِحِينَ ﴿١٠٠﴾ فَبَشَّرْنَٰهُ بِغُلَٰمٍ حَلِيمٍ ﴿١٠١﴾

> *"Ewe Mola wangu! Nipe (mtoto awe) miongoni mwa watenda mema."Ndipo tukampa habari njema ya (kuwa atapata) mtoto mpole.(37:100-101)*

Hajirah alimzaa Ismail(a.s), mwana wa kwanza wa Ibrahim(a.s) Allah(s.w) alimuamuru Ibrahiim(a.s) ampeleke mkewe Hajirah na mwanawe Isma'il katika bonde kame la Makka. Bibilia imelitajwa bonde hilo kuwa ni jangwa la Parani.(Mwanzo 21:21 )

Ibrahiimu(a.s) aliwaacha familia yake Makka kwenye Nyumba Tukufu ya Allah (s.w) huku akiwaombea dua akisema:

رَّبَّنَآ إِنِّىٓ أَسْكَنتُ مِن ذُرِّيَّتِى بِوَادٍ غَيْرِ ذِى زَرْعٍ عِندَ بَيْتِكَ
ٱلْمُحَرَّمِ رَبَّنَا لِيُقِيمُوا۟ ٱلصَّلَوٰةَ فَٱجْعَلْ أَفْـِٔدَةً مِّنَ ٱلنَّاسِ تَهْوِىٓ
إِلَيْهِمْ وَٱرْزُقْهُم مِّنَ ٱلثَّمَرَٰتِ لَعَلَّهُمْ يَشْكُرُونَ ﴿٣٧﴾

> *"Mola wangu! Hakika mimi nimewaweka baadhi ya kizazi changu katika bonde lisilokuwa na mimea yoyote, katika nyumba yako takatifu. Mola wetu! Wajaalie wasimamishe swala. Na ujaalie nyoyo za watu zielekee kwao, na uwaruzuku matunda ili wapate kushukuru.(14:37)*

**Ibrahiim (as) atahiniwa kumchinja Ismail(as)**

Wakati mtoto huyo alipokuwa bado yu ngali kijana mdogo, Nabii Ibrahim(a.s) alioneshwa usingizini kuwa anamchinja mtoto huyo. Ismai'l, alipofahamishwa juu ya ndoto ya babake, akajitolea kuchinjwa pasina kusita na akalithibitisha hilo kwa kusema, "Utanikuta, Inshaallah miongoni mwa wanaosubiri." Qur'an inatufahamisha juu ya kule kuitikia kwao kwa moyo mkunjufu kutekeleza maamrisho ya Allah(s.w) kwa kutumia neno '***Aslama***' (yaani wote wawili walijisalimisha).

Mtihani huu unasimuliwa katika aya zifuatazo:

فَلَمَّا بَلَغَ مَعَهُ ٱلسَّعْىَ قَالَ يَٰبُنَىَّ إِنِّىٓ أَرَىٰ فِى ٱلْمَنَامِ أَنِّىٓ أَذْبَحُكَ
فَٱنظُرْ مَاذَا تَرَىٰ ۚ قَالَ يَٰٓأَبَتِ ٱفْعَلْ مَا تُؤْمَرُ ۖ سَتَجِدُنِىٓ إِن شَآءَ
ٱللَّهُ مِنَ ٱلصَّٰبِرِينَ ﴿١٠٢﴾

*Basi alipofikia (makamu ya) kwenda na kurudi pamoja naye, alimwambia: “Ee mwanangu! Hakika nimeona katika ndoto ya kwamba ninakuchinja. Basi fikiri, waonaje?” akasema: “Ee baba yangu! Fanya unayoamrishwa, utanikuta Inshaallah miongoni mwa wanaosubiri.”(37:102)*

فَلَمَّآ أَسْلَمَا وَتَلَّهُۥ لِلْجَبِينِ ﴿١٠٣﴾ وَنَٰدَيْنَٰهُ أَن يَٰٓإِبْرَٰهِيمُ ﴿١٠٤﴾
قَدْ صَدَّقْتَ ٱلرُّءْيَآ ۚ إِنَّا كَذَٰلِكَ نَجْزِى ٱلْمُحْسِنِينَ ﴿١٠٥﴾
إِنَّ هَٰذَا لَهُوَ ٱلْبَلَٰٓؤُا۟ ٱلْمُبِينُ ﴿١٠٦﴾

*Basi wote wawili walipojisalimisha (kwa Allah), na akamlaza kifudifudi (amchinje).Pale pale tulimwita: “Ewe Ibrahim.” Umekwishasadikisha ndoto. (Usimchinje mwanao)”. Kwa yakini hivi ndivyo tunavyowalipa watendao mema. Bila shaka (jambo) hili ni jaribio lililo dhahiri.(37:103-106)*

وَفَدَيْنَٰهُ بِذِبْحٍ عَظِيمٍ ﴿١٠٧﴾ وَتَرَكْنَا عَلَيْهِ فِى ٱلْءَاخِرِينَ ﴿١٠٨﴾
سَلَٰمٌ عَلَىٰٓ إِبْرَٰهِيمَ ﴿١٠٩﴾ كَذَٰلِكَ نَجْزِى ٱلْمُحْسِنِينَ ﴿١١٠﴾
إِنَّهُۥ مِنْ عِبَادِنَا ٱلْمُؤْمِنِينَ ﴿١١١﴾

*Basi tukamkomboa kwa mnyama wa kuchinjwa mtukufu.Na tukamuachia (sifa nzuri) kwa (watu wote) waliokuja baadaye. Amani kwa Ibrahim. Hivi ndivyo tunavyowalipa watendao mema. Bila shaka yeye alikuwa miongoni mwa waja wetu walioamini (kweli kweli).(37:107-111)*

**Allah(s.w) amzawadia Ibrahiim(a.s) mwana wa pili aitwaye Is-haqa**

وَبَشَّرْنَٰهُ بِإِسْحَٰقَ نَبِيًّا مِّنَ ٱلصَّٰلِحِينَ ﴿١١٢﴾

*Tena tukambashiria (kumzaa) Is-haqa. Nabii miongoni mwa watu wema (kabisa).(37:112)*

Ibrahim(a.s) ametajwa kuwa ni Muhsin (yaani mwenye kutimiza maamrisho ya Allah kwa upeo ulio bora). Kama jaza ya kiwango chake cha juu cha kujitolea na ucha-Mungu alipewa habari njema za kumpata mtoto mwingine Is'haq ambaye atakuwa Mtume pia. Kwa mujibu wa Qur,an, Is-haqa hakuwa mtoto wa kwanza, na hata katika Biblia, bado zimesalia alama zinazoonesha kuwa jina la Is-haq (Isaac) lilipachikwa palipostahiki jina la Ismail kinyume na ukweli wa mambo ulivyokuwa. Biblia yasema:

*Ikawa baada ya mambo hayo Mungu alimjaribu Ibrahimu, akamwambia, Ee Ibrahimu! Naye akasema, Mimi hapa. akasema, umchukue mwanao, mwana wako wa pekee, umpendaye, Isaka, ukaende zako mpaka nchi ya Moria, ukamtoe sadaka ya kuteketezwa huko juu ya mlima mmojawapo nitakaokuambia. (Mwanzo 22:1-2).*

Itayumkinikaje kwa Is-haqa kuitwa "mwana wako wa pekee" na ilhali alizaliwa miaka kumi na minne baada ya kuzaliwa kwa nduguye mkubwa, yaani Ismail? Msemo huu "mwana wako wa pekee" pia unaonesha wazi kuwa tukio la kuchinjwa lilitokea kabla ya kuzaliwa kwa Is'haq, wakati ambapo Ismail alikuwa ndiye mwana wa pekee katika familia.

**Ukarimu wa nabii Ibrahiim(a.s)**

Safari moja nabii Ibrahim (a.s.) aliendewa na wageni watatu walioonekana kuwa ni wa ajabu, wageni ambao baadaye aliwatambua kuwa ni malaika wa Allah(s.w), waliopelekwa kuwaangamiza watu wa miji ya Sodoma na Gomora ambao walidumu katika kiburi chao cha kumuasi Allah(s.w)

وَلَقَدْ جَآءَتْ رُسُلُنَآ إِبْرَٰهِيمَ بِٱلْبُشْرَىٰ قَالُوا۟ سَلَـٰمًا ۖ قَالَ سَلَـٰمٌ ۖ
فَمَا لَبِثَ أَن جَآءَ بِعِجْلٍ حَنِيذٍ ﴿٦٩﴾

*Na wajumbe wetu (Malaika kwa sura za kibinadamu) walimwendea Ibrahim kwa bishara (njema) wakasema: "Salam (alaykum)." Akasema (Ibrahim "Juu yenu pia iwe amani." Na hakukaa (Ibrahim ila mara alileta ndama (aliyechomwa vizuri).(11:69)*

فَلَمَّا رَءَآ أَيْدِيَهُمْ لَا تَصِلُ إِلَيْهِ نَكِرَهُمْ وَأَوْجَسَ مِنْهُمْ خِيفَةً ۚ
قَالُوا۟ لَا تَخَفْ إِنَّآ أُرْسِلْنَآ إِلَىٰ قَوْمِ لُوطٍ ﴿٧٠﴾

*Basi alipoona (Ibrahim) mikono ya (watu) wale haifikilii (chakula kile) aliwatilia shaka na akawaogopa. Wakasema: "Usiogope, hakika sisi tunapelekwa kwa watu wa Lut (tukawaangamize).(11:70)*

وَٱمْرَأَتُهُۥ قَآئِمَةٌ فَضَحِكَتْ فَبَشَّرْنَٰهَا بِإِسْحَٰقَ وَمِن وَرَآءِ
إِسْحَٰقَ يَعْقُوبَ ﴿٧١﴾

*Na mkewe (Ibrahim - Bibi Sarah) alikuwa kasimama wima; akacheka (aliposikia hivyo). Basi tukampa habari njema ya (kuwa watazaa mtoto wamwite) Is-haqa na baada ya Is-haqa (watapata mjukuu wamwite) Yaakub.(11:71)*

قَالَتْ يَٰوَيْلَتَىٰٓ ءَأَلِدُ وَأَنَا۠ عَجُوزٌ وَهَٰذَا بَعْلِى شَيْخًا ۖ إِنَّ
هَٰذَا لَشَىْءٌ عَجِيبٌ ﴿٧٢﴾

*(Mkewe Ibrahim) akasema: "Ee Mimi We! Nitazaa na hali mimi ni mkongwe, na huyu mume wangu ni mzee sana? Hakika hili ni jambo la ajabu."(11:72)*

قَالُوٓا۟ أَتَعْجَبِينَ مِنْ أَمْرِ ٱللَّهِ ۖ رَحْمَتُ ٱللَّهِ وَبَرَكَٰتُهُۥ
عَلَيْكُمْ أَهْلَ ٱلْبَيْتِ ۚ إِنَّهُۥ حَمِيدٌ مَّجِيدٌ ﴿٧٣﴾

*Wakasema (wale malaika): "Je! Unastaajabia amri ya Allah? Rehema ya Allah na Baraka zake ziko juu yenu, enyi watu wa nyumba hii! Hakika Yeye (Allah) ndiye anayestahiki kusifiwa na kutukuzwa."(11:73)*

فَلَمَّا ذَهَبَ عَنْ إِبْرَٰهِيمَ ٱلرَّوْعُ وَجَآءَتْهُ ٱلْبُشْرَىٰ يُجَٰدِلُنَا
فِى قَوْمِ لُوطٍ ﴿٧٤﴾

*Basi Khofu ilipomwondokea Ibrahim ikawa imemjia ile khabari njema, alianza kujadiliana nasi (kushindana na Malaika wetu) juu ya watu wa Lut (kuwaombea wasiangamizwe)(11:74)*

يَٰٓإِبْرَٰهِيمُ أَعْرِضْ عَنْ هَٰذَآ ۖ إِنَّهُۥ قَدْ جَآءَ أَمْرُ رَبِّكَ ۖ وَإِنَّهُمْ
إِنَّهُۥ قَدْ جَآءَ أَمْرُ رَبِّكَ ۖ وَإِنَّهُمْ ءَاتِيهِمْ عَذَابٌ غَيْرُ مَرْدُودٍ ﴿٧٦﴾

*(Tukamwambia) "Ewe Ibrahim! Wacha haya. Kwa hakika amri ya Mola wako imekwishakuja (ya kuangamizwa hao watu wa Lut) na hakika hao itawafika adhabu isiyorudishwa."(11:76)*

**Mafunzo kwa muhtasari**

(i) Tunatakiwa kuwakirimu wageni kama alivyofanya Nabii Ibrahiim(a.s) kwa wageni waliokuja kumpa habari njema za kumpata mtoto, na zile za kuangamizwa watu waovu wa Mji wa Sodoma.

(ii) Muumuni wa kweli hatakiwi kukata tamaa au kuwa na shaka juu ya uwezo wa Allah(s.w). Maana Allah(s.w) akitaka jambo huliamuru kwa neno "kuwa!", likawa.

## HISTORIA YA MTUME LUT (A.S.)

Mtume Lut (a.s.) alitokea katika kipindi cha maisha ya mtume Ibrahim (a.s.). Yeye alikuwa ni mpwawe mtume Ibrahim (a.s.) na alitumwa kuwa mtume na muonyaji kwa watu wa Sodom na Gomora. Miji ambayo baadaye iliangamizwa kabisa kutokana na maasi na uchafu uliokithiri waliokuwa wakifanya wakazi wake. Sehemu ilipokuwa miji hiyo leo yafahamika kama Transjordan.

Jamii aliyotumwa mtume Lut(a.s) ilikuwa imeyawacha mafundisho ya mitume waliotangulia. Wakawa, hawana mwongozo wa maisha ila matamanio ya nafsi zao. Katika hali hiyo jamii ikapoteza maadili mema na kuzama kwenye giza la upotofu na uasi. Usalama  na amani vikawa vitu adimu katika jamii, bali ufisadi na kudhulumiana ukawa ndio mtindo wa maisha.

Maovu mazito matatu yanatajwa katika Qur'an kuwa ni kielelezo cha maovu yaliyokuwa yakitendwa na watu wa Sodom.

وَلُوطًا إِذْ قَالَ لِقَوْمِهِۦٓ إِنَّكُمْ لَتَأْتُونَ ٱلْفَٰحِشَةَ مَا سَبَقَكُم بِهَا
مِنْ أَحَدٍ مِّنَ ٱلْعَٰلَمِينَ ﴿٢٨﴾

*Na (wakumbushe mtume) Lut alipowaambia watu wake. "Bila shaka nyinyi mnafanya uovu (ambao) hakuna yoyote aliyekutangulieni kwa (uovu) huo katika walimwengu.(29:28)*

أَئِنَّكُمْ لَتَأْتُونَ ٱلرِّجَالَ وَتَقْطَعُونَ ٱلسَّبِيلَ وَتَأْتُونَ فِى
نَادِيكُمُ ٱلْمُنكَرَ ۖ فَمَا كَانَ جَوَابَ قَوْمِهِۦٓ إِلَّآ أَن قَالُوا۟ ٱئْتِنَا بِعَذَا
بِ ٱللَّهِ إِن كُنتَ مِنَ ٱلصَّٰدِقِينَ ﴿٢٩﴾

*"Je, mnawaendea wanaume, na mnawakatia njia (watu kwa kuwaua na kuwanyang'anya njiani) na mnafanya maovu katika mikusanyiko yenu? Basi halikuwa jawabu la watu wake ila kusema: "Tuletee adhabu ya Mwenyezi Mungu ikiwa u miongoni mwa wasemao kweli"  (29:29)*

Watu wa zama za mtume Lut(a.s) walikuwa wameanguka sana kimaadili. Walifikia hali ya kuwa waovu zaidi ya wanyama licha ya kuwa walikuwa na maumbile yao ya kibinadamu. Katika aya hizi tunafahamishwa

kuwa:

(i) Walikuwa wakiwaendea wanaume wenzao kutosheleza matamanio yao.
(ii) Walikuwa wakifanya uharamia, uporaji wa mali za watu
(iii) Walifanya maovu katika hadhara (katika mikusanyiko).

Watu wa Sodom walikuwa binaadamu kama sisi tulivyo leo. Wanatokana na Adamu na Hawa kama walivyo watu wengine. Kwa ujumla hawakuwa na tofauti yoyote ya kimaumbile na watu wengine. Ilikuwaje basi watu hawa wakakiuka tabia za kibinaadamu na kuwa wenye kufanya vitendo viovu zaidi hata ya wanyama.Hapana sababu nyingine zaidi ya ile ya kuacha mwongozo wa Allah (s.w.).

**Sodom ya leo.**

Hivi leo kuna mashindano ya ***U-miss*** ambayo wasichana hutokeza jukwaani mbele ya watu wakiwa wamevaa viguo visivyositiri mwili. Na hali ni hiyo hiyo kwenye kumbi za madansi, madisko, na hata kwenye sherehe za kiserikali. Na wengine wameenda mbele zaidi hata kufikia kucheza sinema za matusi na ushenzi ule ule wa mabaladhuli wa mji wa Sodoma.

Ufuska na maovu haya husemwa kuwa ni utamaduni wa taifa, usanii, na kupigia debe kuwa ni burudani muhimu inayokuza na kuendeleza utamaduni wa taifa. Lakini Mwenyezi Mungu anaonya na kuasa kuwa:

وَلَا تَحْسَبَنَّ ٱللَّهَ غَٰفِلًا عَمَّا يَعْمَلُ ٱلظَّٰلِمُونَ ۚ إِنَّمَا يُؤَخِّرُ
هُمْ لِيَوْمٍ تَشْخَصُ فِيهِ ٱلْأَبْصَٰرُ ﴿٤٢﴾

*Wala usidhani Mwenyezi Mungu ameghafilika na haya wayatendao madhalimu. Hakika yeye anawaakhirisha tu mpaka siku ambayo macho yatakodoka(14:42)*

**Kuangamizwa kwa watu wa Sodom.**

Katika utaratibu wa Allah (s.w.) adhabu haiwajii watu mpaka wapelekewe muonyaji: Wakipuuza na kukadhibisha ndipo adhabu huwashukia.

Watu wa Sodom waliutupa mwongozo na kuzama kwenye maasi kama tulivyobainisha, Mtume Lut(a.s) alitumwa kwao kuwalingania kuwaonya lakini walimkadhibisha.Baada ya kupewa maonyo na wao kukadhibisha adhabu ya Allah (s.w) iliwashukia. Ardhi ikageuzwa chini juu na kumiminiwa mvua ya mawe.

Adhabu hii ilimkumba pia mke wa mtume Lut(a.s) kwani hakuamini na alikuwa pamoja na waovu. Kwa hiyo waliookolewa na maangamizi haya ni wale walioamini tu. Nasaba na udugu haukusaidia.

فَأَنجَيْنَٰهُ وَأَهْلَهُۥٓ إِلَّا ٱمْرَأَتَهُۥ كَانَتْ مِنَ ٱلْغَٰبِرِينَ ﴿٨٣﴾ وَأَمْطَرْ
نَا عَلَيْهِم مَّطَرًا ۖ فَٱنظُرْ كَيْفَ كَانَ عَٰقِبَةُ ٱلْمُجْرِمِينَ ﴿٨٤﴾

*Basi tukamuokoa yeye (Lut) na watu wake (walioamini) isipokuwa mke wake alikuwa miongoni mwa waliokuwa nyuma (wakaangamizwa)".Na tukawamiminia mvua kubwa ya adhabu. Basi tazama ulivyokuwa mwisho wa waovu (7:83-84).*

**Mafunzo kwa muhtasari:**

Baada ya kutufahamisha vipi waliangamizwa watu wa Lut(a.s), Qur'an inatuambia:

إِنَّ فِى ذَٰلِكَ لَءَايَةً لِّلْمُؤْمِنِينَ ﴿٧٧﴾

*"Hakika katika (masimulizi) haya yamo mazingatio (makubwa) kwa wanaoamini" (15:77).*

(i) Katika kuzingatia huku tunapaswa kufanya kila tuliwezalo ili kuhakikisha kuwa maovu yaliyopelekea kuangamizwa watu wa Sodoma hayasitawi katika jamii yetu.

(ii) Tusikae kimya kuyanyamazia maovu kwa kuwaacha watu waovu wafanye watakavyo, badala yake tupambane na waovu kama alivyofanya nabii Lut(as) na waumini waliokuwa pamoja naye.

(iii) Aidha tuwaidhike na kumuogopa Allah (s.w) kwani adhabu yake ni kali na hakuna awezaye kujinusuru nayo inapokuja. Kwa hiyo tufuate mwongzo wake na tuyaache yote aliyoyakataza.

(iv) Tukumbuke kuwa hatuwezi kupata radhi za Allah(s.w) na pepo yake siku ya kiyama kwa kuwa tu sisi ni Ummah bora wa mtume Muhammad(s.a.w) pasina kuamrisha mema na kukataza maovu. Kuangamizwa kwa mke wa Mtume Lut(a.s) ni kielelezo tosha cha kuonesha kuwa amali ya mtu ndio pekee itakayomsaidia.

(v) Kama ambavyo tumeona katika maelezo ya mitume waliotangulia Allah (s.w) hatupi jitihada za waja wake wema,. Hivyo khatima ya mapambano dhidi ya makafiri, waislamu huibuka washindi na makafiri hushindwa. La muhimu ni kuwa na imani thabiti, ucha-Mungu, kumuomba na kumtegemea Allah(a.s).

## HISTORIA YA NABII ISMAIL (A.S.)

Ismail ni mtoto wa kwanza wa Mtume Ibrahim (a.s.). Alizaliwa wakati uzee umekwishamfikia Ibrahim(a.s). Kama Qur'an inavyobainisha, katika umri huo wa uzeeni, mtume Ibrahim(a.s) alimuomba Mola wake ampe mtoto mwema atakaendeleza harakati za Kiislamu.

رَبِّ هَبْ لِى مِنَ ٱلصَّٰلِحِينَ ﴿١٠٠﴾ فَبَشَّرْنَٰهُ بِغُلَٰمٍ حَلِيمٍ ﴿١٠١﴾

*Ee Mola wangu! Nipe (mtoto awe) miongoni mwa watenda mema." Ndipo tukampa habari njema ya (kuwa atapata) mtoto mpole. (Basi akapata. Naye ndiye nabii (Ismail)."  (37:100-101).*

Mtume Ibrahim (a.s.) aliletewa mitihani migumu miwili juu ya mtoto huyu. Mosi ni kule kuamriwa kumwacha yeye pamoja na mamaye katika bonde kavu lisilo na watu wala maji. Hilo lilikuwa bonde la Makka. Maji ya zamzam (kisima) yaliyo katika Msikiti wa Makka, aliyabubujisha Allah (s.w) kwa ajili ya Ismail na mamaye. Kisima hicho kimedumu hadi leo. Aidha, vilima vya Safa na Marwa vimepata umaarufu na kuwa ni miongoni mwa vitu muhimu katika Uislamu, kutokana na kitendo cha mama yake Ismail - Hajar kukimbia baina ya vilima hivyo katika jitihada za kumtafutia mwanae Ismail maji.

Mtihani mwingine alioupata Mtume Ibrahim(a.s) juu ya Ismail(a.s) ni kule kuamrishwa amchinje. Huu haukuwa ni mtihani kwa baba tu, lakini pia mtoto Ismail(a.s). Hebu fikiri ungekuwa katika hali gani, kama ungekuwa mahali pa Ismail(a.s). Baba yako anakwambia ameamrishwa na Allah (s.w.) akuchinje! Hakika ni mtihani mgumu ila kwa wale wanaonyenyekea kikweli kweli kwa Muumba wao.

Qur'an yatufahamisha kuwa Ismail alikuwa mpole na mnyenyekevu kwa Mola wake. Kwa hiyo hakusita kutoa nafsi yake kwa ajili ya Muumba wake. bali alimhimiza baba yake. (Mtume Ibrahim) amchinje kama Allah (s.w) alivyomuamrisha.

فَلَمَّا بَلَغَ مَعَهُ ٱلسَّعْىَ قَالَ يَٰبُنَىَّ إِنِّىٓ أَرَىٰ فِى ٱلْمَنَامِ أَنِّىٓ أَذْبَحُكَ
فَٱنظُرْ مَاذَا تَرَىٰ ۚ قَالَ يَٰٓأَبَتِ ٱفْعَلْ مَا تُؤْمَرُ ۖ سَتَجِدُنِىٓ إِن شَآءَ
ٱللَّهُ مِنَ ٱلصَّٰبِرِينَ ﴿١٠٢﴾

*Basi alipofikia (makamu ya) kwenda na kurudi pamoja naye akamwambia: "Ee mwanangu! Hakika nimeona katika ndoto ya kwamba ninakuchinja. (Na ndoto ya mitume ni Wahayi). Basi fikiri, waonaje?" Akasema: "Ee baba yangu! Fanya unayoamrishwa, utanikuta Inshallah miongoni mwa wanaosubiri". (37:102).*

Utii na unyenyekevu huu wa nabii Ismail(a.s) ni kielelezo muhimu kwetu. Kwamba, amri ya Allah (s.w) ni lazima itiiwe kwa gharama yoyote ile ikiwa ni pamoja na roho zetu.

**Kuinua Kuta za Ka'bah.**

Kama tulivyoona katika maisha ya Mtume Ibrahim (a.s.), nabii Ismail (a.s.) alishirikiana na baba yake kuinua kuta za Ka'abah. Ka'abah ambayo ndiyo nyumba kongwe ya kufanyia Ibada na kituo kikuu cha harakati za Kiislamu duniani.

وَعَهِدْنَآ إِلَىٰٓ إِبْرَٰهِـۧمَ وَإِسْمَـٰعِيلَ أَن طَهِّرَا بَيْتِىَ لِلطَّآئِفِينَ
وَٱلْعَـٰكِفِينَ وَٱلرُّكَّعِ ٱلسُّجُودِ ﴿١٢٥﴾

*"Na tulimwusia Ibrahim na Ismail (tukawaambia): Itakaseni nyumba yangu kwa ajili ya wale wanaoyoizunguka kwa ajili ya kutufu na wanaokaa hapo na (kwa ajili ya) wanaorukuu na kusujudu hapo pia" (2:125).*

وَإِذْ يَرْفَعُ إِبْرَٰهِـۧمُ ٱلْقَوَاعِدَ مِنَ ٱلْبَيْتِ وَإِسْمَـٰعِيلُ رَبَّنَا
تَقَبَّلْ مِنَّآ ۖ إِنَّكَ أَنتَ ٱلسَّمِيعُ ٱلْعَلِيمُ ﴿١٢٧﴾

*"Na (kumbukeni khabari hii) Ibrahim alipoinua kuta za nyumba (hii ya Al-Ka'bah) na Ismail (pia) (wakaomba, wakasema): "Ee Mola wetu! Tutakabalie (amali yetu hii ya kujenga huu msikiti). Hakika wewe ndiwe Mwenye kusikia, na Mwenye kujua". (2:127).*

**Ismail(a.s) na Taifa la Waarabu**

Nabii Ismail(a.s) ndiye chimhuko la taifa la Waarabu. Baada ya kuachwa katika bonde la Makka lililokavu, Allah (s.w) alijaalia kupatikana maji na hatimaye watu kuhamia pale. Uhai wa mji ukaanza na kutokana na kizazi cha Ismail(a.s) wakapatikana Waarabu wa Hijaz (Saudi Arabia) ambao hufahamika kwa jina mashuhuri - Banu Quraysh (Makuraish).

Qur'an imemtaja ismail(a.s) kuwa alikuwa mtume mkweli wa ahadi aliyewausia watu wake swala na zakat.

وَٱذۡكُرۡ فِى ٱلۡكِتَـٰبِ إِسۡمَـٰعِيلَ ۚ إِنَّهُۥ كَانَ صَادِقَ ٱلۡوَعۡدِ وَكَانَ
رَسُولًا نَّبِيًّا ﴿٥٤﴾ وَكَانَ يَأۡمُرُ أَهۡلَهُۥ بِٱلصَّلَوٰةِ وَٱلزَّكَوٰةِ وَكَانَ
عِندَ رَبِّهِۦ مَرۡضِيًّا ﴿٥٥﴾

*"Na mtaje katika kitabu (hiki) Ismail. Bila shaka yeye alikuwa mkweli wa ahadi, na alikuwa mtume, nabii. Na alikuwa akiwaamrisha watu wake Sala na Zakat na alikuwa mridhiwa mbele ya Mola wake". (19:54-55).*

Qur'an hapa haimtaji Ismail kwa wema kwa vile alikuwa mtoto wa Mtume Ibrahim (a.s.), bali kwa vile alikuwa mtumishi wa Allah aliye mkweli, muamrisha mema na mkataza maovu. Nasaba hapa haikutajwa kabisa.

Baada ya Mtume Ibrahim(a.s) na mwanae Ismail kujenga upya Ka'bah na kutangaza Hija walimwomba Allah (s.w) alete Mtume atokanaye na kizazi chao ambaye ataendeleza harakati za Kiislamu kama walivyofanya wao. Aidha walikiombea kizazi chao kiwe ni cha watu wanyenyekevu:

رَبَّنَا وَٱجۡعَلۡنَا مُسۡلِمَيۡنِ لَكَ وَمِن ذُرِّيَّتِنَآ أُمَّةً مُّسۡلِمَةً لَّكَ
وَأَرِنَا مَنَاسِكَنَا وَتُبۡ عَلَيۡنَآ ۖ إِنَّكَ أَنتَ ٱلتَّوَّابُ ٱلرَّحِيمُ ﴿١٢٨﴾

*"Ee, Mola wetu! Utufanye tuwe wanyenyekevu kwako. Na miongoni mwa kizazi chetu (pia ufanye) umma mnyenyekevu kwako. na utuonyeshe njia ya Ibada yetu na utusamehe. Bila shaka Wewe ndiye Mwenye kusamehe na Mwenye kurehemu.(2:128)*

رَبَّنَا وَٱبۡعَثۡ فِيهِمۡ رَسُولًا مِّنۡهُمۡ يَتۡلُواْ عَلَيۡهِمۡ ءَايَـٰتِكَ وَيُعَلِّمُهُمُ
ٱلۡكِتَـٰبَ وَٱلۡحِكۡمَةَ وَيُزَكِّيهِمۡ ۚ إِنَّكَ أَنتَ ٱلۡعَزِيزُ ٱلۡحَكِيمُ ﴿١٢٩﴾

*"Ee, Mola wetu! Waletee mtume anayetokana na wao, awasomee Aya zako, na kuwafundisha kitabu (chako) na hikma (nyingine) na awafundishe kujitakasa (na kila mabaya). Hakika Wewe ndiye Mwenye nguvu Mwenye hikima" (2:128-129).*

Dua hii iliwafiki utaratibu wa Allah (s.w). Ilipofika zama za kuletwa Mtume wa mwisho, Allah (s.w.) akamleta kupitia kizazi cha Bani Quraysh

ambao wanatokana na Ismail(a.s). Ndiye Mtume wetu Muhammad (s.a.w.).

**Mafunzo kwa muhtasari**

(i) Muislamu anatakiwa kumuomba Allah(s.w) amjaalie mtoto mwema.

(ii) Mtoto mwema anayependwa na Allah(s.w) ni yule anayewatii wazazi wake wanapomtaka kutekeleza maamrisho ya Allah(s.w) na mtume wake.

(iii) Mtoto mwema hujitahidi kushiriki katika harakati mbalimbali za kujenga na kuimarisha vituo vya kiislamu kama alivyofanya nabii Ismail(as) katika kuujenga upya msikiti mtukufu wa Makka, akishirikiana na baba yake nabii Ibrahiimu(as).

(iv) Tunapaswa kusimamisha swala sisi wenyewe na kuwaamrisha wengine wasimamishe swala kama alivyofanya nabii Ismail(as)

(v) Kusema kweli na kutekeleza ahadi ni katika tabia njema anazozipenda Allah(s.w). Hivyo, hapana shaka kuwa Allah(s.w) huwapenda watu wanaosema kweli na wale wanaotekeleza ahadi zao kwa wengine. Na kinyume chake ni kuwa Allah(s.w) hawapendi watu waongo na wale wasiotekeleza ahadi. Allah(s.w) anawachukia watu wasiosema kweli!

(vi) Inatupasa kumuomba Allah(s.w) atupe yaliyo mema katika kila jambo tunalokusudia kufanya. Tumeona jinsi nabii Ismail(a.s) na Ibrahiimu(a.s) walivyomuomba Allah(s.w) awakubalie na kuzibariki jitihada zao za kuujenga upya msikiti mtukufu wa Makka. Hivyo ni wale watu wenye kibri tu ndio wasiomuomba Allah(s.w) wakijidanganya kuwa wao wanaweza kujitegemea wenyewe.

**HISTORIA YA NABII IS-HAQ (A.S.) NA YAQUB (A.S.)**

Ishaq ni mtoto wa pili wa nabii Ibrahiim(a.s), mama yake akiwa Sarah.Habari njema ya kumzaa Ishaq ilimjia nabii Ibrahim (a.s.) mara tu baada ya kufuzu mtihani wa kumchinja mwanae mkubwa Ismail. Alipolipongezwa kubashiriwa kuzaliwa kwa Ishaq (a.s.)

سَلَٰمٌ عَلَىٰٓ إِبۡرَٰهِيمَ ١٠٩ كَذَٰلِكَ نَجۡزِي ٱلۡمُحۡسِنِينَ ١١٠ إِنَّهُۥ
مِنۡ عِبَادِنَا ٱلۡمُؤۡمِنِينَ ١١١ وَبَشَّرۡنَٰهُ بِإِسۡحَٰقَ نَبِيّٗا مِّنَ
ٱلصَّٰلِحِينَ ١١٢

*Amani kwa Ibrahim. Hivi ndivyo tunavyowalipa watendao mema. Bila shaka yeye alikuwa miongoni mwa waja wetu walioamini (kweli kweli).Tena tukambashiria (kumzaa) Is-haq, Nabii miongoni mwa watu wema (kabisa). (37:109-112).*

Maelezo ya kuzaliwa Ishaq na hatimaye Yaquub (a.s.) zinapatikana katika kisa cha malaika waliompa nabii Ibrahiimu habari za kuangamizwa watu waovu wa mji wa Sodoma na zile za yeye kupata mtoto katika uzee wake.

وَٱمۡرَأَتُهُۥ قَآئِمَةٞ فَضَحِكَتۡ فَبَشَّرۡنَٰهَا بِإِسۡحَٰقَ وَمِن وَرَآءِ
إِسۡحَٰقَ يَعۡقُوبَ ٧١

*Na mkewe (Ibrahim - bibi Sarah) alikuwa kasimama wima, akacheka. Basi tukampa habari njema ya (kuwa watazaa mtoto wamwite) Is-haq na baada ya I'shaq (watapata mjukuu wamwite) Yaquub.(11:71)*

قَالَتۡ يَٰوَيۡلَتَىٰٓ ءَأَلِدُ وَأَنَا۠ عَجُوزٞ وَهَٰذَا بَعۡلِي شَيۡخًاۖ إِنَّ
هَٰذَا لَشَيۡءٌ عَجِيبٞ ٧٢

*(Mkewe Ibrahim) akasema: "Ee mimi we! Nitazaa na hali mimi ni mkongwe, na huyu mume wangu ni mzee sana? Hakika hili ni jambo la ajabu."(11:72)*

قَالُوٓاْ أَتَعۡجَبِينَ مِنۡ أَمۡرِ ٱللَّهِۖ رَحۡمَتُ ٱللَّهِ وَبَرَكَٰتُهُۥ
عَلَيۡكُمۡ أَهۡلَ ٱلۡبَيۡتِۚ إِنَّهُۥ حَمِيدٞ مَّجِيدٞ ٧٣

*Wakasema (wale Malaika): Je, unastaajabia amri ya Mwenyezi Mungu? Rehema ya Mwenyezi Mungu na Baraka zake ziko juu yenu, enyi watu wa nyumba hii! Hakika Yeye (Mwenyezi Mungu) ndiye anayestahiki kusifiwa na kutukuzwa." (11:73)*

**Shukurani za nabii Ibrahiimu(a.s) kwa Allah(s.w)**

Kwa neema hii ya kuruzukiwa watoto wawili - Ismail na Is-haqa(a.s), nabii Ibrahim (a.s.) alimshukuru Allah (s.w) kwa maneno yafuatayo:

ٱلْحَمْدُ لِلَّهِ ٱلَّذِى وَهَبَ لِى عَلَى ٱلْكِبَرِ إِسْمَـٰعِيلَ وَإِسْحَـٰقَ ۚ
إِنَّ رَبِّى لَسَمِيعُ ٱلدُّعَآءِ ﴿٣٩﴾

*"Namshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa juu ya uzee (wangu watoto wawili hawa):- Ismail na Is-haqa. Hakika Mola wangu ni mwenye kusikia maombi (ya waja wake)" (14:39).*

Is-haqa alipofikia utu uzima naye alipewa utume na akaruzukiwa mtoto - Yaqub(a.s) naye pia akapewa utume.

وَهَبْنَا لَهُۥٓ إِسْحَـٰقَ وَيَعْقُوبَ ۖ وَكُلًّا جَعَلْنَا نَبِيًّا ﴿٤٩﴾
وَوَهَبْنَا لَهُم مِّن رَّحْمَتِنَا وَجَعَلْنَا لَهُمْ لِسَانَ صِدْقٍ عَلِيًّا ﴿٥٠﴾

*Tulimpa Is-haqa na Yaakub, na kila mmoja tukamfanya nabii.Na tukawapa rehema zetu na tukawafanyia sifa za kweli tukufu. (19:49-50).*

وَجَعَلْنَـٰهُمْ أَئِمَّةً يَهْدُونَ بِأَمْرِنَا وَأَوْحَيْنَآ إِلَيْهِمْ فِعْلَ ٱلْخَيْرَٰ
تِ وَإِقَامَ ٱلصَّلَوٰةِ وَإِيتَآءَ ٱلزَّكَوٰةِ ۖ وَكَانُوا۟ لَنَا عَـٰبِدِينَ ﴿٧٣﴾

*Na tukawajaalia kuwa maimamu wanaoongoza kwa amri yetu, na tukawapelekea wahyi wa kuzifanya kheri na kusimamisha Sala na kutoa Zaka. Na walikuwa kwetu ni wenye kutunyenyekea. (21:73).*

Aya tulizozinukuu zaweka wazi kuwa Is-haqa na mwanawe Ya'aquub, walikuwa mitume na viongozi wa kusimamia utekelezaji wa sheria za Allah(s.w).

**Mafunzo kwa muhtasari**

(i) Katika historia hii tunajifunza umuhimu wa kutenda mema. Kutenda mema kunampatia mtendaji faida kubwa sana katika maisha ya dunia. Ni kutokana na wema alioutenda nabii Ibrahiimu (a.s)ndipo Allah(s.w) akamjaalia mtoto mwema, Ishaqa na mjukuu aitwaye Ya'aquub ambao wote walikuwa manabii. Na hii ni kanuni ya Allah(s.w) ya kumlipa kila anayetenda mema malipo mazuri hapa hapa duniani na siku ya kiama humuingiza peponi.

(ii) Kwa kutenda kwao mema, Allah(s.w) aliwafanya nabii Ibrahiimu, Ishaqa na Ya'aquub kuwa viongozi wa watu. Hapa tunajifuna kuwa ni lazima kujitahidi sana kutenda mema ili Allah(s.w) apendezwe nasi, na atuchague kuwa viongozi wanaoingoza jamii katika mema na kusimamia kila mtu atendewe haki na uadilifu.

(iii) Na kwa upande mwingine, Allah(s.w) anatufunza kuwachagua wale watendao wema kuwa viongozi wetu. Haifai na ni dhuluma kubwa kumchagua mtu muongo, mlevi, mwizi, mbabe au mzinifu kuwa kiongozi. Maana kiongozi muovu daima husimamia mambo maovu na machafu yashamiri katika jamii.

(iv) Ni katika tabia njema mtu kumshukuru Allah(s.w) aliyemneemesha kwa kumpatia ushindi, kufaulu au kupata jambo lolote lililo zuri na jema. Nabii Ibrahiimu alimshukuru Allah(s.w) aliyemruzuku watoto na mjukuu. Kumshukuru Allah(s.w) ni miongoni mwa tabia ya mitume na watu wema. Kumshukuru Allah(s.w) ni tabia ya watu wema watakaoingia peponi. Watu wa peponi watamshukuru Allah(s.w) wakisema:

ٱلْحَمْدُ لِلَّهِ ٱلَّذِى صَدَقَنَا وَعْدَهُۥ وَأَوْرَثَنَا ٱلْأَرْضَ نَتَبَوَّأُ مِنَ
ٱلْجَنَّةِ حَيْثُ نَشَآءُ ۖ فَنِعْمَ أَجْرُ ٱلْعَـٰمِلِينَ ﴿٧٤﴾

*Sifa zote njema ni za Allah, ambaye ametutimizia ahadi yake, na ameturithisha ardhi(ya peponi) tunakaa katika mabustani haya popote tupendapo. Basi ni malipo mazuri yaliyoje kwa watenda mema(39:74)*

## HISTORIA YA NABII YUSUFU (A.S.).

Mtume Yusufu(a.s) alikuwa mtoto wa Mtume Ya'aquub(a.s) na mjukuu wa Mtume Is-haqa (a.s.). Tunajua kuwa Is-haqa ni mtoto wa Ibrahim (a.s.), Kwa hiyo Yusufu(a.s) ni kijukuu (mjukuu wa mtoto) wa Mtume Ibrahim (a.s.).

Mtume Ya'aquub(a.s) alikuwa na watoto 12. Mtume Yusufu(a.s) alichangia mama na mmoja wa hao. Wengine 10 walikuwa na mama zao.

### Ndoto ya nabii Yusufu(a.s)

Maisha ya nabii Yusufu(a.s) yanaanza kusimuliwa ndani ya Qur'an pale alipomwambia babake kuwa:

إِذۡ قَالَ يُوسُفُ لِأَبِيهِ يَٰٓأَبَتِ إِنِّي رَأَيۡتُ أَحَدَ عَشَرَ كَوۡكَبٗا
وَٱلشَّمۡسَ وَٱلۡقَمَرَ رَأَيۡتُهُمۡ لِي سَٰجِدِينَ ﴿٤﴾

*Yusufu alipomwambia baba yake "Ewe babaangu! hakika nimeona katika ndoto nyota kumi na moja na jua na mwezi. Nimeviona hivi vikinisujudia(12:4)*

Mtume Ya'aquub, kwa ilimu aliyopewa na Mola wake alifahamu tafsiri ya ndoto ile kwamba inabashiri kuwa Yusufu atakuja kuwa mtu mwenye hadhi kubwa na Mtume. Akamtahadharisha kuwa:

قَالَ يَٰبُنَيَّ لَا تَقۡصُصۡ رُءۡيَاكَ عَلَىٰٓ إِخۡوَتِكَ فَيَكِيدُواْ لَكَ
كَيۡدًاۖ إِنَّ ٱلشَّيۡطَٰنَ لِلۡإِنسَٰنِ عَدُوّٞ مُّبِينٞ ﴿٥﴾

*Akasema (baba yake): "Ewe mwanangu! Usiwasimulie ndoto yako (hii) nduguzo wasije wakakufanyia vitimbi (kwa ajili ya husuda). Hakika Shetani kwa mwanadamu ni adui aliye dhahiri.(12:5)*

وَكَذَٰلِكَ يَجۡتَبِيكَ رَبُّكَ وَيُعَلِّمُكَ مِن تَأۡوِيلِ ٱلۡأَحَادِيثِ وَيُتِمُّ
نِعۡمَتَهُۥ عَلَيۡكَ وَعَلَىٰٓ ءَالِ يَعۡقُوبَ كَمَآ أَتَمَّهَا عَلَىٰٓ أَبَوَيۡكَ مِن
قَبۡلُ إِبۡرَٰهِيمَ وَإِسۡحَٰقَۚ إِنَّ رَبَّكَ عَلِيمٌ حَكِيمٞ ﴿٦﴾

*Namna hivi Mola wako atakuchagua na kukufundisha hakika ya mambo. Na atatimiza neema zake juu yako na juu ya kizazi cha Yaqub, kama alivyoitimiza zamani juu ya baba zako Ibrahim na Is-haqa. Bila shaka Mola wako ni Mjuzi na Mwenye hikima: (12:6).*

**Njama za kumuua nabii Yusufu(a.s)**

Kwa tabia zake njema Yusufu(a.s) alipendwa sana na baba yake. Ndugu zake Yusufu(a.s) wakajawa chuki na husuda wakijadiliana kuwa;

لَيُوسُفُ وَأَخُوهُ أَحَبُّ إِلَىٰٓ أَبِينَا مِنَّا وَنَحْنُ عُصْبَةٌ إِنَّ أَبَانَا لَفِى
ضَلَـٰلٍ مُّبِينٍ ﴿٨﴾

*“Hakika Yusufu na nduguye wanapendwa sana na baba kuliko sisi, hali sisi ni kundi lenye nguvu. Hakika baba yetu yumo katika upotofu ulio wazi.(12:8)*

Wakapanga na njama za kumhujumu Yusufu(a.s) kwa kumuua ili mapenzi ya baba yao yawageukie wao kwa kuwa tu Yusufu(a.s) aliwazidi kwa tabia njema. Wakapanga na kuazimia kuwa;

ٱقْتُلُوا۟ يُوسُفَ أَوِ ٱطْرَحُوهُ أَرْضًا يَخْلُ لَكُمْ وَجْهُ أَبِيكُمْ
وَتَكُونُوا۟ مِنۢ بَعْدِهِۦ قَوْمًا صَـٰلِحِينَ ﴿٩﴾

*Muueni Yusufu au mtupeni nchi za mbali ili uso wa baba yenu ukuelekeeni na baada ya haya mtakuwa watu wema(12:9)*

Hatimaye wakakubaliana kumtumbukiza kisimani badala kumwua,wazo hili lilitolewa na mmoja wao ambaye angalau aliogopa kubeba dhima ya kufanya dhambi kubwa ya kuiua nafsi pasina haki. Akasema;

لَا تَقْتُلُوا۟ يُوسُفَ وَأَلْقُوهُ فِى غَيَـٰبَتِ ٱلْجُبِّ يَلْتَقِطْهُ بَعْضُ
ٱلسَّيَّارَةِ إِن كُنتُمْ فَـٰعِلِينَ ﴿١٠﴾

*Msimuue Yusufu lakini mtupeni Yusufu katika(jiwe la ndani) ya kisima kirefu, watamuokota baadhi ya wasafiri, kama ninyi mnataka kufanya kitu.(12:10)*

**Kutumbukizwa Yusufu(a.s) Kisimani**

Pamoja na kuwa na dhamira ile mbaya ya kutaka kufanya kosa la kuua mtu asiyekuwa na hatia , wakaongeza kosa lingine la kusema uwongo. Wakasema;

قَالُوا۟ يَـٰٓأَبَانَا مَا لَكَ لَا تَأْمَ۫نَّا عَلَىٰ يُوسُفَ وَإِنَّا لَهُۥ لَنَـٰصِحُونَ
﴿١١﴾ أَرْسِلْهُ مَعَنَا غَدًا يَرْتَعْ وَيَلْعَبْ وَإِنَّا لَهُۥ لَحَـٰفِظُونَ ﴿١٢﴾

*Ewe baba yetu, mbona hutuamini juu ya Yusufu, hakika sisi ni wenye kumtakia mema. Mruhusu kesho pamoja nasi atakula kwa furaha na kucheza; hakika sisi tutamlinda(12:11-12)*

Ingawa mzee Ya'aquub(a.s) alionesha wasiwasi, lakini hatimaye aliwaruhusu waandamane naye. Huko wakamtumbukiza kisimani wakiwa wameishika kanzu ya nabii Yusufu(a.s) ikiwa na damu ya uongo. Wakati nafsi zao zinawasuta kwamba hawasemi kweli, wakasema;

يَٰٓأَبَانَآ إِنَّا ذَهَبۡنَا نَسۡتَبِقُ وَتَرَكۡنَا يُوسُفَ عِندَ مَتَٰعِنَا فَأَكَلَهُ ٱلذِّئۡبُۖ وَمَآ أَنتَ بِمُؤۡمِنٖ لَّنَا وَلَوۡ كُنَّا صَٰدِقِينَ ١٧

*Ewe baba yetu! Hakika sisi tulikwenda kushindana mbio na tukamuacha Yusufu penye vyombo vyetu, basi mbwa mwitu akamla; lakini hutatuamini ingawa tunasema kweli(12:17)*

Ya'aquub (a.s.) alikuwa na mategemeo makubwa ya kupata mrithi bora atakayeendeleza kazi yake.Hata hivyo hatumwoni mzee Ya'aquub akikata tamaa kwa kufadhaika au kukufuru. Yeye akawajibu;

قَالَ بَلۡ سَوَّلَتۡ لَكُمۡ أَنفُسُكُمۡ أَمۡرٗاۖ فَصَبۡرٞ جَمِيلٞۖ وَٱللَّهُ ٱلۡمُسۡتَعَانُ عَلَىٰ مَا تَصِفُونَ ١٨

*“Nafsi zenu zimekushawishini jambo. Basi (langu mimi ni) subira njema; na Mwenyezi Mungu ndiye aombwaye msaada kwa haya mnayoyasema” (12:18).*

Hii ndio tabia ya Muislamu. Kurejea na kumtegemea zaidi Allah (s.w) afikwapo na msiba.

**Yusufu aokotwa na kuuzwa nchini Misri**

Huko nyuma wapita njia walikisogelea kisima kwa lengo la kuteka maji. Walipomuibua mtoto ndani ya kisima, akaruka mmoja wao kwa furaha.

يَٰبُشۡرَىٰ هَٰذَا غُلَٰمٞۚ

*Ee,furaha njema! Huyu hapa kijana mwanaume.(12:19)*

Walimchukua hadi Misri kwa Aziz au Waziri , na;

وَشَرَوۡهُ بِثَمَنِۭ بَخۡسٖ دَرَٰهِمَ مَعۡدُودَةٖ وَكَانُواْ فِيهِ مِنَ ٱلزَّٰهِدِينَ

*Wakamuuza kwa thamani chache ya pesa za kuhesabika, na hawakuwa na haja naye(12:20)*

**Yusufu(a.s) apewa elimu na kukumbana na mtihani**

Alipofikia umri wa utu uzima alipewa hukumu na elimu. Yaani akapewa jukumu la utume. Qur'an inasema:-

وَلَمَّا بَلَغَ أَشُدَّهُۥٓ ءَاتَيْنَٰهُ حُكْمًا وَعِلْمًا ۚ وَكَذَٰلِكَ نَجْزِى
ٱلْمُحْسِنِينَ ﴿٢٢﴾

*"Na (Yusuf) alipobaleghe, tulimpa hukumu na ilimu. Na namna hivi tunawalipa wanaotenda mema" (12:22).*

Katika kipindi hiki cha utu uzima mke wa Waziri alifanya vitimbi na hata kumshika Yusufu kwa nguvu ili azini naye. Lakini Yusufu alikataa kufanya zinaa, tendo ovu na chafu lenye kuzaa mabalaa na magonjwa. Alipoambiwa 'njoo', Yusufu akasema;

قَالَ مَعَاذَ ٱللَّهِ ۖ..........إِنَّهُۥ لَا يُفْلِحُ ٱلظَّٰلِمُونَ ﴿٢٣﴾

*Najikinga kwa Mwenyezi Mungu. Hakima madhalimu hawatengenekewi(12:23)*

Mke wa Waziri badala ya kuonea aibu tendo lake lile ovu, na pengine kuomba radhi. Aliwaita wanawake wenzie na kumpitisha Yusufu mbele yao. Lengo likiwa waushuhudie uzuri wa Yusufu, hivyo waone "hajafanya kosa kumtamani". Nao wanawake wale badala ya kumshutumu na kumrudi mwenzao wakadhihirisha nao uovu wao kwa kumtazama Yusufu kwa matamanio.

Ikumbukwe kuwa huyu alikuwa ni mke wa mtu mkubwa. Hivyo hata wanawake walioitwa walikuwa ni wale wa daraja la juu. Hali hii ya wanawake hawa kudhihirisha matamanio yao, bila ya aibu, ni kielelezo cha kuanguka kwa maadili katika jamii hiyo. Yaonesha ufuska ulikuwa umechanua sana kiasi kwamba aibu haikuwa ni kitu chenye nafasi tena katika maumbile yao.

Hali ilivyokuwa katika jamii hiyo haitofautiani na hali ya leo ambapo watu huzungumzia uhuru wa kufanya ufuska. Kwamba kufanya ufuska ni uhuru na haki ya mtu.

**Yusufu(a.s) atupwa gerezani.**

Mkewe Waziri hakumkatia tamaa Yusufu(a.s). Uovu wake ulimchochea kuzidi kumuandama Yusufu(a.s). Alimpa Yusufu chaguzi mbili: Ama akubali kuzini naye au amfanyie hila atiwe gerezani.

وَلَئِن لَّمْ يَفْعَلْ مَآ ءَامُرُهُۥ لَيُسْجَنَنَّ وَلَيَكُونًا مِّنَ ٱلصَّـٰغِرِينَ

*Na kama hatafanya ninalomuarisha, hakika atafungwa gerezani na atakuwa miongoni mwa madhalili(12:32)*

Kwa kumukhofu Allah(s.w) na kuchukia tendo chafu la zinaa, Yusufu akasema

رَبِّ ٱلسِّجْنُ أَحَبُّ إِلَىَّ مِمَّا يَدْعُونَنِىٓ إِلَيْهِ ۖ وَإِلَّا تَصْرِفْ عَنِّى كَيْدَهُنَّ أَصْبُ إِلَيْهِنَّ وَأَكُن مِّنَ ٱلْجَـٰهِلِينَ ﴿٣٣﴾

*Ee Mola wangu! Nastahabu zaidi gereza kuliko haya wanayoniitia..(12:33)*

**Maisha ya Yusufu (a.s.) gerezani.**

Yusufu anajikuta yupo gerezani, si kama mhalifu bali aliyeonewa kwa uadilifu na uaminifu wake. Lakini pia hasononeki kwa dhulma ile anayofanyiwa kwani kuwepo gerezani kumemtenga na watu waovu waliotaka kumtia kwenye uchafu.

Uadilifu na sifa zake njema zilikuwa zimezagaa kila mahali. Hata alivyoingia gerezani wafungwa wenzake walimpa heshima ya pekee. Walikiri kwamba Yusufu(a.s) ni miongoni mwa watu wazuri.

**Yusufu afikisha ujumbe wa Uislamu kwa wafungwa**

Ilitokea kule gerezani wafungwa wenzake wakaota ndoto na kumtaka Yusufu(a.s) awape tafsiri yake.

وَدَخَلَ مَعَهُ ٱلسِّجْنَ فَتَيَانِ ۖ قَالَ أَحَدُهُمَآ إِنِّىٓ أَرَىٰنِىٓ أَعْصِرُ خَمْرًا ۖ وَقَالَ ٱلْـَٔاخَرُ إِنِّىٓ أَرَىٰنِىٓ أَحْمِلُ فَوْقَ رَأْسِى خُبْزًا تَأْكُلُ ٱلطَّيْرُ مِنْهُ ۖ نَبِّئْنَا بِتَأْوِيلِهِۦٓ ۖ إِنَّا نَرَىٰكَ مِنَ ٱلْمُحْسِنِينَ ﴿٣٦﴾

*Na wakaingia pamoja naye gerezani vijana wawili. Mmoja wao akasema: Hakika nimeona(katika ndoto) nakamua ulevi"; na mwingine akasema: Hakika nimeona(katika) ndoto nabeba mikate juu ya kichwa changu ambayo ndege wanaila. Tuambie tafsiri yake; kwa yakini sisi tunakuona wewe ni miongoni watu wazuri(12:36)*

Yusufu(a.s) hakuwatekelezea ombi lao moja kwa moja, alitumia fursa hiyo kuwaelimisha Upweke wa Allah(s.w) aliyempa yeye elimu na hikma ya kufasiri ndoto. Akawaambia:

يَٰصَٰحِبَيِ ٱلسِّجۡنِ ءَأَرۡبَابٞ مُّتَفَرِّقُونَ خَيۡرٌ أَمِ ٱللَّهُ
ٱلۡوَٰحِدُ ٱلۡقَهَّارُ ﴿٣٩﴾

*"Enyi wafungwa wenzangu wawili! Je, waungu wengi wanaofarikiana ndio bora (kuabudiwa) au Mwenyezi Mungu Mwenye nguvu (juu ya kila kitu)" (12:39).*

مَا تَعۡبُدُونَ مِن دُونِهِۦٓ إِلَّآ أَسۡمَآءٗ سَمَّيۡتُمُوهَآ أَنتُمۡ
وَءَابَآؤُكُم مَّآ أَنزَلَ ٱللَّهُ بِهَا مِن سُلۡطَٰنٍۚ إِنِ ٱلۡحُكۡمُ إِلَّا
لِلَّهِۚ أَمَرَ أَلَّا تَعۡبُدُوٓاْ إِلَّآ إِيَّاهُۚ ذَٰلِكَ ٱلدِّينُ ٱلۡقَيِّمُ وَلَٰكِنَّ
أَكۡثَرَ ٱلنَّاسِ لَا يَعۡلَمُونَ ﴿٤٠﴾

*"Hamuabudu badala yake (Mwenyezi Mungu) ila majina (matupu) mliyopanga nyinyi wenyewe na baba zenu. Mwenyezi Mungu hakuteremsha dalili kwa hayo. Haikuwa hukumu ila hii ya Mwenyezi Mungu tu; ameamrisha msimuabudu yoyote isipokuwa Yeye tu. Hiyo ndiyo dini iliyonyooka lakini watu wengi hawajui." (12:40).*

Baada ya kuwafikishia ujumbe huu muhimu, nabii Yusufu(a.s) akaanza kuwaeleza taawili ya ndoto zao kuwa:

يَٰصَٰحِبَيِ ٱلسِّجۡنِ أَمَّآ أَحَدُكُمَا فَيَسۡقِي رَبَّهُۥ خَمۡرٗاۖ وَأَمَّا ٱلۡأٓخَرُ
وَأَمَّا ٱلۡأٓخَرُ فَيُصۡلَبُ فَتَأۡكُلُ ٱلطَّيۡرُ مِن رَّأۡسِهِۦۚ قُضِيَ ٱلۡأَمۡرُ
ٱلَّذِي فِيهِ تَسۡتَفۡتِيَانِ ﴿٤١﴾

*Enyi wafungwa wenzangu wawili! Mmoja katika ninyi atarejeshwa kazini kwake akamnyweshe bwana wake ulevi. na yule mwingine atauawa kwa kusulubiwa, na ndege watamla kichwa chake. Limekwishakatwa (huko kwa Firaun) hili jambo mlilokuwa mkiuliza(12:41)*

**Ndoto ya Mfalme: Kufunguliwa Yusufu(a.s) kutoka gerezani**

Yusufu(a.s) alisahauliwa gerezani kwa muda mrefu. Kilichopelekea akumbukwe ni ndoto aliyoota mfalme. Alipoamka aliwaambia makuhani wake:

إِنِّيٓ أَرَىٰ سَبۡعَ بَقَرَٰتٖ سِمَانٖ يَأۡكُلُهُنَّ سَبۡعٌ عِجَافٞ وَسَبۡعَ
سُنۢبُلَٰتٍ خُضۡرٖ وَأُخَرَ يَابِسَٰتٖۖ يَٰٓأَيُّهَا ٱلۡمَلَأُ أَفۡتُونِي فِي
رُءۡيَٰيَ إِن كُنتُمۡ لِلرُّءۡيَا تَعۡبُرُونَ ٤٣

*Hakika mimi nimeona ng’ombe saba wanene wanaliwa na ng’ombe saba ving’onda. Na nimeona mashuke saba mabichi na mengine yaliyokauka. Enyi wakubwa nitafsirieni ndoto yangu ikiwa ninyi mnaweza kutafsiri ndoto(12:43)*

قَالُوٓاْ أَضۡغَٰثُ أَحۡلَٰمٖۖ وَمَا نَحۡنُ بِتَأۡوِيلِ ٱلۡأَحۡلَٰمِ بِعَٰلِمِينَ ٤٤

*Wakasema: Ni ndoto iliyovurugika wala sisi hatujui tafsiri ya ndoto hizi(12:44)*

Yule mfungwa aliyefasiriwa ndoto na Yusufu(a.s) (kuwa atatolewa gerezani) akamkumbuka. Akawaambia:

أَنَا۠ أُنَبِّئُكُم بِتَأۡوِيلِهِۦ فَأَرۡسِلُونِ ٤٥

*Mimi nitakwambieni tafsiri yake. Basi nitumeni(12:45)*

Alipofika gerezani, yule aliyekuwa mfungwa akamwita:

يُوسُفُ أَيُّهَا ٱلصِّدِّيقُ أَفۡتِنَا فِي سَبۡعِ بَقَرَٰتٖ سِمَانٖ يَأۡكُلُهُنَّ
سَبۡعٌ عِجَافٞ وَسَبۡعِ سُنۢبُلَٰتٍ خُضۡرٖ وَأُخَرَ يَابِسَٰتٖ لَّعَلِّيٓ
أَرۡجِعُ إِلَى ٱلنَّاسِ لَعَلَّهُمۡ يَعۡلَمُونَ ٤٦

*Yusufu! Ewe mkweli! Tueleze hakika ya ng’ombe saba wanene kuliwa na ng’ombe saba dhaifu. Na mashuke saba mabichi na mashuke makavu, ili nirejee kwa watu wapate kujua.(12:46)*

قَالَ تَزْرَعُونَ سَبْعَ سِنِينَ دَأَبًا فَمَا حَصَدتُّمْ فَذَرُوهُ فِي سُنۢبُلِهِۦٓ إِلَّا قَلِيلًا مِّمَّا تَأْكُلُونَ ﴿٤٧﴾

*Akasema: Mtalima miaka saba mfululizo kwa juhudi. Na mtakavyovivuna viacheni katika mashuke yake isipokuwa kidogo mnavyokula.(12:47)*

ثُمَّ يَأْتِي مِنۢ بَعْدِ ذَٰلِكَ سَبْعٌ شِدَادٌ يَأْكُلْنَ مَا قَدَّمْتُمْ لَهُنَّ إِلَّا قَلِيلًا مِّمَّا تُحْصِنُونَ ﴿٤٨﴾

*Kisha itakuja baadaye miaka saba ya shida itakayokula vile mlivyoipa, isipokuwa kidogo mtakachohifadhi (12:48)*

Walipopata taawili ya ndoto hii, mfalme kwa furaha kubwa kabisa alisema

ٱئْتُونِي بِهِۦٓ أَسْتَخْلِصْهُ لِنَفْسِي ۖ فَلَمَّا كَلَّمَهُۥ قَالَ إِنَّكَ ٱلْيَوْمَ لَدَيْنَا مَكِينٌ أَمِينٌ ﴿٥٤﴾

*Mleteni kwangu nimchague awe mtu wangu mwenyewe. Basi alipozungumza naye(mfalme) alisema, Hakika wewe leo kwetu umekwishakuwa ni mwenye hishima na muaminiwa.(12:54)*

Hakika Yusufu(a.s) alikuwa ni kijana mwenye tabia nzuri na mwenendo bora kabisa. Alijiepusha kabisa na ufuska wa kufanya zinaa ambayo ni njia mbaya yenye uchafu unaoiangamiza jamii kwa magonjwa, vifo na mauaji. Na ndio maana akamtaka mfalme aeleze ni nani muovu kati yake na wanawake waliosababishwa afungwe. Mke wa mfalme pamoja na wanawake wale wangine, wakathibitisha kuwa Yusufu(a.s) hakuwa mzinifu. Wakasema:

حَٰشَ لِلَّهِ مَا عَلِمْنَا عَلَيْهِ مِن سُوٓءٍ ۚ قَالَتِ ٱمْرَأَتُ ٱلْعَزِيزِ ٱلْـَٰٔنَ حَصْحَصَ ٱلْحَقُّ أَنَا۠ رَٰوَدتُّهُۥ عَن نَّفْسِهِۦ وَإِنَّهُۥ لَمِنَ ٱلصَّٰدِقِينَ ﴿٥١﴾

*"... Hasha lillah! Sisi hatukujua ubaya wowote kwake (tumejitahidi afanye mabaya na sisi, hakukubali kufanya)" mkewe Waziri (naye) akasema: "Sasa haki imedhihirika, mimi ndiye niliyemtamani kinyume cha nafsi yake, na bila shaka yu miongoni mwa wakweli (kabisa)" (12:51).*

Baada ya hapo ndipo Yusufu(a.s) alipokubali heshima ile aliyopewa na kupendekeza awe msimamizi wa hazina ya nchi.

قَالَ ٱجْعَلْنِى عَلَىٰ خَزَآئِنِ ٱلْأَرْضِ ۖ إِنِّى حَفِيظٌ عَلِيمٌ ﴿٥٥﴾

*Akasema Nifanye niwe mtazamaji wa hazina ya nchi; hakika mimi ni mlinzi mzuri na mjuzi hodari(12:55)*

Tendo hili la Yusufu(a.s) kudai kesi yake na wanawake iangaliwe na mfalme na haki itolewe, lilinyanyua sana hadhi yake. Kwanza aliifasiri ndoto ngumu ya mfalme ambayo iliwashinda wachawi, wanganga na watabiri wote wa kutegemewa katika nchi. Pili alipotakiwa na mfalme atoke gerezani, alikataa mpaka kesi ifikishwe mahakamani, mkosaji abainishwe. Matokeo ya kesi wanawake wanakiri mbele ya hadhara ya mfalme kuwa Yusufu(a.s) hana hatia bali wao ndio waovu.

Ilidhihiri kwa kila mtu kuwa hakuna yeyote miongoni mwao, ila amezidiwa na Yusufu(a.s) kwa uadilifu na tabia njema kwa ujumla. Haiwi ni kitu cha ajabu basi tunapoona Yusufu anapewa dhamana ya kuangalia hazina yote ya nchi.Huu ni wadhifa unaohitajia mtu aliyepea kwa uadilifu na hakuwepo aliyemzidi Yusufu(a.s)

**Yusufu (a.s.) akutana na ndugu zake**

Njaa ilitokea na ikawa hapana sehemu nyingine yoyote yenye chakula ila Misri.Watu wakamiminika Misri kuhemea chakula. Miongoni mwao wakawa ni wale ndugu zake Yusufu(a.s).

وَجَآءَ إِخْوَةُ يُوسُفَ فَدَخَلُوا۟ عَلَيْهِ فَعَرَفَهُمْ وَهُمْ لَهُۥ مُنكِرُونَ

*Wakaja ndugu zake Yusufu, na wakaingia kwake akawajua(12:58)*

Wakapewa chakula na wakarejeshewa bidhaa zao walizoleta kubadilisha na chakula. Kisha Yusufu (a.s.) akawaagiza:

قَالَ ٱئْتُونِى بِأَخٍ لَّكُم مِّنْ أَبِيكُمْ ۚ أَلَا تَرَوْنَ أَنِّىٓ أُوفِى ٱلْكَيْلَ

وَأَنَا۠ خَيْرُ ٱلْمُنزِلِينَ ﴿٥٩﴾

*Nijieni na ndugu yenu wa kwa baba. Je hamuoni ya kwamba mimi ninatimiza kipimo, na ni mbora wa wakaribishao(12:59)*

وَلَمَّا جَهَّزَهُم بِجَهَازِهِمْ قَالَ ٱئْتُونِى بِأَخٍ لَّكُم مِّنْ أَبِيكُمْ ۚ
أَلَا تَرَوْنَ أَنِّىٓ أُوفِى ٱلْكَيْلَ وَأَنَا۠ خَيْرُ ٱلْمُنزِلِينَ ﴿٥٩﴾

*Basi waliporejea kwa baba yao, walisema: "Ewe baba yetu! Tutazuiliwa (chakula mara ya pili mpaka twende na ndugu yetu); basi mpeleke ndugu yetu pamoja nasi ili tupate kupimiwa; na yakini sisi tutamlinda." (12:63).*

Mzee Ya'aquub(a.s), akasema

لَنْ أُرْسِلَهُۥ مَعَكُمْ حَتَّىٰ تُؤْتُونِ مَوْثِقًا مِّنَ ٱللَّهِ لَتَأْتُنَّنِى
بِهِۦٓ إِلَّآ أَن يُحَاطَ بِكُمْ ۖ فَلَمَّآ ءَاتَوْهُ مَوْثِقَهُمْ قَالَ ٱللَّهُ عَلَىٰ مَا
نَقُولُ وَكِيلٌ ﴿٦٦﴾

*Sitampeleka pamoja nanyi mpaka munipe ahadi kwa jina la Allah kwamba lazima mtamrejesha kwangu, isipokuwa nyote mzungukwe (na hatari au kufa). Basi walipompa ahadi yao alisema: Mwenyezi Mungu ndiye mlinzi juu ya haya tuyasemayo(12:66)*

Kule Misri, Yusufu(a.s) alifanya mbinu akambakisha yule ndugu yake. Hali hii ilizidi kumhuzunisha mzee Ya'aquub (a.s.) lakini hakukata tamaa.

يَـٰبَنِىَّ ٱذْهَبُوا۟ فَتَحَسَّسُوا۟ مِن يُوسُفَ وَأَخِيهِ وَلَا تَا۟يْـَٔسُوا۟ مِن
رَّوْحِ ٱللَّهِ ۖ إِنَّهُۥ لَا يَا۟يْـَٔسُ مِن رَّوْحِ ٱللَّهِ إِلَّا ٱلْقَوْمُ ٱلْكَـٰفِرُونَ ﴿٨٧﴾

*Enyi wanangu! Nendeni mkamtafute Yusufu na nduguye, wala msikate tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu. Hawakati tamaa ya rehema na Mwenyezi Mungu isipokuwa watu makafiri(12:87)*

Walipofika Misri walimtaka Yusufu(a.s) awatendee wema wa kuwapa chakula wakimweleza kuwa Mwenyezi Mungu huwalipa watu wanaowatendea wema mwenzao. Hapo Yusufu(a.s) akawakumbusha:

قَالَ هَلْ عَلِمْتُم مَّا فَعَلْتُم بِيُوسُفَ وَأَخِيهِ إِذْ أَنتُمْ جَـٰهِلُونَ ﴿٨٩﴾

*Akasema: Je! Mnajua mliyomfanyia Yusufu na nduguye mlipokuwa ujingani?(12:89)*

قَالُوٓاْ أَءِنَّكَ لَأَنتَ يُوسُفُۖ قَالَ أَنَا۠ يُوسُفُ وَهَٰذَآ أَخِيۖ قَدۡ مَنَّ
ٱللَّهُ عَلَيۡنَآۖ إِنَّهُۥ مَن يَتَّقِ وَيَصۡبِرۡ فَإِنَّ ٱللَّهَ لَا يُضِيعُ أَجۡرَ
ٱلۡمُحۡسِنِينَ ﴿٩٠﴾

*Wakasema: Je! Wewe ndiye Yusufu? Akasema: Mimi ndiye Yusufu, na huyu ni ndugu yangu. Mwenyezi Mungu ametufanyia hisani. Hakika anayemcha Mungu na kusubiri , basi Mwenyezi Mungu hapotezi malipo ya wafanyao mema(12:90)*

Nduguze wakakiri makosa yao waliyomfanyia Yusufu(a.s) na kumuomba awasamehe.

قَالُواْ تَٱللَّهِ لَقَدۡ ءَاثَرَكَ ٱللَّهُ عَلَيۡنَا وَإِن كُنَّا لَخَٰطِـِٔينَ ﴿٩١﴾

*Wakasema: Wallahi! Mwenyezi Mungu amekuchagua juu yetu, na hakika sisi tulikuwa wenye makosa(12:91)*

**Ndoto ya nabii Yusufu(a.s) yatimia**

Yusufu (a.s.) aliwasamehe na kuwaagiza waende wakamlete baba yao mzee Yaaqub (a.s.).

قَالَ لَا تَثۡرِيبَ عَلَيۡكُمُ ٱلۡيَوۡمَۖ يَغۡفِرُ ٱللَّهُ لَكُمۡۖ وَهُوَ أَرۡحَمُ
ٱلرَّٰحِمِينَ ﴿٩٢﴾

*Akasema: “Hakuna lawama juu yenu leo; Mwenyezi Mungu atakusameheni, naye ni Mwenye rehema zaidi kuliko wanaorehemu(12:92)*

ٱذۡهَبُواْ بِقَمِيصِي هَٰذَا فَأَلۡقُوهُ عَلَىٰ وَجۡهِ أَبِي يَأۡتِ بَصِيرٗا
وَأۡتُونِي بِأَهۡلِكُمۡ أَجۡمَعِينَ ﴿٩٣﴾

*Nendeni na kanzu yangu hii na muiweke mbele ya uso wa baba yangu: naye atafunuka macho aone. Na nijieni pamoja na watu wenu wote(12:93)*

Waliporudi nyumbani wakachukuzana wote, familia nzima akiwemo baba yao mzee Ya'aquub(as) wakafika Misri.

فَلَمَّا دَخَلُوا۟ عَلَىٰ يُوسُفَ ءَاوَىٰٓ إِلَيْهِ أَبَوَيْهِ وَقَالَ ٱدْخُلُوا۟ مِصْرَ
إِن شَآءَ ٱللَّهُ ءَامِنِينَ ﴿٩٩﴾

*Na walipoingia kwa Yusufu aliwakumbatia wazazi wake na akasema; "Ingieni Misri, Inshaa-Allah mumo katika amani.(12:99)*

وَرَفَعَ أَبَوَيْهِ عَلَى ٱلْعَرْشِ وَخَرُّوا۟ لَهُۥ سُجَّدًا ۖ وَقَالَ يَٰٓأَبَتِ
هَٰذَا تَأْوِيلُ رُءْيَٰىَ مِن قَبْلُ قَدْ جَعَلَهَا رَبِّى حَقًّا ۖ وَقَدْ أَحْسَنَ
بِىٓ إِذْ أَخْرَجَنِى مِنَ ٱلسِّجْنِ وَجَآءَ بِكُم مِّنَ ٱلْبَدْوِ مِنۢ بَعْدِ
أَن نَّزَغَ ٱلشَّيْطَٰنُ بَيْنِى وَبَيْنَ إِخْوَتِىٓ ۚ إِنَّ رَبِّى لَطِيفٌ لِّمَا يَشَآءُ ۚ
إِنَّهُۥ هُوَ ٱلْعَلِيمُ ٱلْحَكِيمُ ﴿١٠٠﴾

*Aliwainua wazazi wake na kuwaweka katika kiti cha Ufalme. Na wote wakaporomoka kumsujudia. Na Yusufu akasema: "Ewe babangu! Hii ndiyo hakika ya ndoto yangu ya zamani. Hakika Mola wangu ameithibitisha. Na amenifanyia hisani akanitoa gerezani na akakuleteni ninyi kutoka jangwani; baada ya Shetani kuchochea baina yangu na ndugu zangu. Hakika Mola wangu ni mwenye kulifikia alitakalo. Bila shaka Yeye ni Mjuzi na Mwenye hekima.(12:100)*

**Shukurani za nabii Yusufu(a.s) kwa Allah(s.w)**

Nabii Yusufu(a.s) alimshukuru Allah(s.w) aliyemuokoa, kumlinda na kulea, na ambaye alimfunza elimu na hikima na akampa heshima na hadhi kubwa.Nabii Yusufu(a.s) alimshukuru Allah(s.w) akisema kwa unyenyekevu:

رَبِّ قَدْ ءَاتَيْتَنِى مِنَ ٱلْمُلْكِ وَعَلَّمْتَنِى مِن تَأْوِيلِ ٱلْأَحَادِيثِ ۚ
فَاطِرَ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ أَنتَ وَلِىِّۦ فِى ٱلدُّنْيَا وَٱلْءَاخِرَةِ ۖ
تَوَفَّنِى مُسْلِمًا وَأَلْحِقْنِى بِٱلصَّٰلِحِينَ ﴿١٠١﴾

*"Ee Mola wangu! Hakika umenipa ufalme na umenifundisha tafsiri ya mambo. Ewe Muumba wa mbingu na ardhi! Wewe ndiye Mlinzi wangu katika dunia na Akhera. Nifishe hali ya kuwa ni muislamu na unichanganyishe na watendao mema(12:101)*

**Mafunzo kwa muhtasari**

(i) Hila za watu wenye roho mbaya na husda dhidi ya watu wema, mwisho wake huwafedhehesha wenyewe.Allah(s.w) huwafedhehesha kwa kuwafanya wajulikane na kila mtu katika jamii kuwa wao si wa kweli bali ni waongo na wazushi wenye mioyo michafu na matendo maovu.Funzo hili linapatikana katika wasifu wa nduguze Yusufu(a.s) na mkewe waziri ambao walidhania kuwa mafanikio yanapatikana kwa kufanya fitina,majungu,dhulma,au kushawishi watu watende maovu.

(ii) Mwenyezi Mungu daima yu pamoja na watu wakweli, wanashikamana na subira na kutenda mema. Hivyo wema na ukweli ndivyo vitakavyo dumu daima, na huwanyanyua daraja watu watakaoshikamana navyo kama ilivyokuwa kwa nabii Yusufu(a.s)

(iii)Muungwana katika watu na waumini ni yule anayekiri kosa na kukubali kujirekebisha pale anapooneshwa na ndugu zake kuwa kakosea. Na kwa upande mwingine tunajifunza kuwa daima watu wema si wenye kukaa na dukuduku moyoni au dhamira ya kulipiza ovu kwa uovu waliotendewa. Bali wao hujitahidi kujibu kwa kutenda mema na kusamehe kwa kutajia radhi za Allah(s.w).Funzo hili linajitokeza kwenye mgogoro wa Yusufu(a.s) na ndugu zake.

(iv) Tabia njema  ni ngome iliyojaa ulinzi wa Mwenyezi Mungu unaomkinga mtu asidhurike na husda, majungu, fitna na matendo yatokanayo na dhamira mbaya yanayofanywa na watu waovu dhidi yake. Hili ndilo lililomfanya Yusufu(a.s) aibuke mshindi.

(v) Uislamu ni dini rahisi ya kimaumbile inayopaswa kutekelezwa katika mazingira yoyote yale, na mvuto wake humuathiri kila mtu isipokuwa wale wanaoamua kukataa ukweli baada ya kuwadhihirikia. Ni Uislamu uliomfanya Yusufu(a.s) apendwe sana na baba yake na nyumbani kwa mfalme na hata gerezani alionesha hilo kwa wafungwa.

(vi) Tunapohukumu kesi yenye tuhuma ya uzinzi au kubaka ni lazima na ni jambo la busara sana kusikiliza madai na ushahidi wa pande zote mbili. Itakuwa ni dhulma kubwa kumtia mtu katika kashfa ya uzinzi kwa kutegemea ushahidi wa(mezani) kutunga na hali ya kuwa mazingira, sheria na mantiki vyote havimtii mtu huyo hatiani.

(vii) Tunapokubalika na kuhitajika kuwaongoza watu hatuna budi kupendekeza tukabidhiwe kuongoza katika eneo tunaloweza kulimudu kielimu, uzoefu na maadili yetu.

(viii) Aidha, tunafundishwa kuchagua viongozi waadilifu na wenye tabia njema ili kuongoza nchi kama walivyofanya watu wa Misri kumchagua nabii Yusufu ijapokuwa hakuwa mzawa. Walichozingatia wao ni ile tabia yake ya kutokuwa mzinzi, ukweli na uaminifu wake.

(ix) Kiongozi safi ni yule anayekumbuka na kuzingatia kuwa wadhifa alionao ni amana aliyokabidhiwa na Mwenyezi Mungu kwa manufaa ya jamii, hivyo hujiepusha na kibri, majivuno, kujikweza au tabia yoyote inayoashiria dharau kwa wenzake. Funzo hili linapatikana kwenye dua ya nabii Yusufu(a.s)

## HISTORIA YA NABII MUSA(a.s)

Nabii Musa(a.s) ni Mtume aliyeandaliwa na Allah(s.w) na alitumwa kuwakomboa Waisraili waliofanywa kuwa watumwa nchini Misri. Waisraili ni kizazi cha nabii Ya'aquub ambapo nabii Yusufu(a.s) ndiye alianza kukaa Misri kisha wakafuatia wazazi na ndugu zake wote wakati alipokuwa kiongozi nchini humo.



Allah(s.w)alimtuma nabii Musa(a.s)kuwakomboa Waisraili kwasababu haki yao ya kuwa huru ambayo Allah(s.w) amempa kila mwanadamu, iliporwa! Maadamu Waisraili waliporwa haki hii kuu ya msingi; Allah(s.w) kwa uadilifu wake akamtuma nabii Musa kutekeleza jukumu zito la kuwakomboa na kuwarejeshea haki za binadamu walizonyang’anywa.

إِنَّ فِرْعَوْنَ عَلَا فِى ٱلْأَرْضِ وَجَعَلَ أَهْلَهَا شِيَعًا يَسْتَضْعِفُ طَآئِفَةً
مِّنْهُمْ يُذَبِّحُ أَبْنَآءَهُمْ وَيَسْتَحْىِۦ نِسَآءَهُمْ ۚ إِنَّهُۥ كَانَ مِنَ
ٱلْمُفْسِدِينَ ﴿٤﴾

*Hakika Firauni alitakabari katika ardhi, na akawafanya watu wa huko makundi mbalimbali. Akalidhoofisha kundi moja miongoni mwao, akiwachinjwa watoto wao wakiume na kuwawacha hai watoto wao wa kike. Hakika yeye alikuwa miongoni mwa waharibifu(28:4)*

Aya hizi zimeweka wazi ukiukwaji wa haki za binadamu walioufanya watawala wa Misri. Lengo la kuhalalisha ukatili na mauwaji hayo lilikuwa ni kuwadhoofisha wananchi wenye nasaba ya nabii Yusufu(a.s) wasipate nafasi ya kuongoza tena.

**Kuzaliwa kwa Musa(a.s) na maisha yake ya utoto**

Musa alizaliwa wakati bado msako unafanywa na askari wa Firauni kumwua kila mtoto wa kiume wa Kiisrail anayezaliwa. Kwa rehema zake Allah (s.w) mama Musa alijifungua bila kutambulika kwa askari wa Firauni. Na ili kumlinda zaidi Allah (s.w) alimteremshia Wahy mama yake Musa.

أَنِ ٱقْذِفِيهِ فِى ٱلتَّابُوتِ فَٱقْذِفِيهِ فِى ٱلْيَمِّ فَلْيُلْقِهِ ٱلْيَمُّ
بِٱلسَّاحِلِ يَأْخُذْهُ عَدُوٌّ لِّى وَعَدُوٌّ لَّهُۥ

*Ya kwamba mtie sandukuni, kisha litie mtoni, na mto utamtupa ufukoni ili amchukue adui yangu na adui yake(amlee)(20:39)*

Baada ya kumtupa mtoni, mama yake akamtuma dada yake Musa kufuatilia;

وَقَالَتْ لِأُخْتِهِۦ قُصِّيهِ ۖ فَبَصُرَتْ بِهِۦ عَن جُنُبٍ وَهُمْ
لَا يَشْعُرُونَ ﴿١١﴾

*Akamwambia dada yake: "Mfuate". Basi yeye akamwangalia kwa mbali bila wao kumjua(28:11)*

Watu wa Firauni wakamwokota yule mtoto na kumwonesha Firauni.

وَقَالَتِ ٱمْرَأَتُ فِرْعَوْنَ قُرَّتُ عَيْنٍ لِّى وَلَكَ ۖ لَا تَقْتُلُوهُ عَسَىٰٓ
أَن يَنفَعَنَآ أَوْ نَتَّخِذَهُۥ وَلَدًا وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٩﴾

*Na mkewe Firauni akasema(Kumwambia mumewe) "Usimuuwe, atakuwa kiburudisho cha macho kwangu na kwako; na msimuuwe;huwenda atatunufaisha, au tumpange kuwa mtoto wetu,walisema haya hali ya kuwa hawatambui(28:9)*

Watu wa Firauni walipomwokota Musa bila shaka walitambua kuwa ni mtoto wa Kiisrail na walimpeleka kwa Firauni ili auawe kama watoto

wengine Wakiisrail. Lakini mke wa Firauni anafurahishwa na uzuri wa mtoto Musa. Ambaye kwa kweli Allah (s.w) alimfanya awe ni mwenye kupendeza machoni kwa watu.

**Allah(s.w) ajaalia Musa(a.s) kunyonyeshwa na mama yake mzazi**

Kwa uwezo wake, Mwenyezi Mungu aliharamisha Musa asinyonyeshwe na yeyote yule isipokuwa mama yake. Hivyo, dada yake Musa alijitokeza nyumbani kwa Firauni na kupendekeza:

هَلْ أَدُلُّكُمْ عَلَىٰٓ أَهْلِ بَيْتٍ يَكْفُلُونَهُۥ لَكُمْ وَهُمْ لَهُۥ نَٰصِحُونَ ﴿١٢﴾

*Je nikuonesheni watu wa nyumba watakaomlea kwa ajili yenu, na pia watakuwa wema kwake?(28:12)*

Dada yake Musa(a.s) alimpendekeza mama yake ambaye Firauni hawakumjua kuwa ndiye mama mzazi wa nabii Musa. Ombi hilo lilikubaliwa na Musa(a.s)alirejeshwa kwa mama yake kama tunavyofahamishwa.

فَرَدَدْنَٰهُ إِلَىٰٓ أُمِّهِۦ كَىْ تَقَرَّ عَيْنُهَا وَلَا تَحْزَنَ وَلِتَعْلَمَ أَنَّ وَعْدَ
ٱللَّهِ حَقٌّ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا يَعْلَمُونَ ﴿١٣﴾

*Basi tukamrejesha kwa mama yake ili macho yake yaburudike, wala asihuzunike; na ajue ya kwamba ahadi ya Mwenyezi Mungu ni kweli, lakini watu wengi hawajui(28:13)*

**Allah(s.w) amruzuku Musa(a.s) Elimu**

Ili kuweza kutekeleza jukumu la kutetea haki za binadamu na kuwaongoza watu katika njia iliyonyooka, Mwenyezi Mungu akamjaalia Musa elimu ya kutosha na akili yenye upeo mkubwa wa kupembua mambo. Tunafahamishwa kuwa:

وَلَمَّا بَلَغَ أَشُدَّهُۥ وَٱسْتَوَىٰٓ ءَاتَيْنَٰهُ حُكْمًا وَعِلْمًا ۚ وَكَذَٰلِكَ
نَجْزِى ٱلْمُحْسِنِينَ ﴿١٤﴾

*Na Musa alipofikia baleghe yake na kustawi, tulimpa akili na elimu, na hivi ndivyo tunavyowalipa watu wema(28:14)*

**Musa(a.s) ahamia Madiani**

Mchana wa siku moja Musa alimuona mtu wa Firauni amemuelemea myahudi akimtwanga makonde mazito. Musa alichukizwa na kitendo kile, hivyo alipoombwa msaada alijikuta amemtwika mmisri huyo ngumi nzito na kumuuwa. Hapo Musa(a.s) akashituka kwa majuto akisema”

قَالَ رَبِّ إِنِّي ظَلَمْتُ نَفْسِي فَٱغْفِرْ لِي فَغَفَرَ لَهُۥٓ ۚ إِنَّهُۥ هُوَ ٱلْغَفُورُ ٱلرَّحِيمُ ﴿١٦﴾

*Mola wangu! Bila shaka nimedhulumu nafsi yangu, basi nisamehe; naye (Allah) akamsamehe. Kwa hakika yeye ni Mwingi wa kusamehe, Mwingi wa kurehemu. (28:16)*

قَالَ رَبِّ بِمَآ أَنْعَمْتَ عَلَىَّ فَلَنْ أَكُونَ ظَهِيرًا لِّلْمُجْرِمِينَ ﴿١٧﴾

*Akasema: Mola wangu! Kwa kuwa umenineemesha, basi sitakuwa kabisa msaidizi wa watu wabaya(28:17)*

Baadaye ilibidi ahamie Madiani, mji ambao ulikuwa umbali karibu maili 300 Mashariki ya Misri katika Peninsula ya Sinai. Leo wajulikana kama Al-Bid.

**Ndoa ya Musa huko Madiani**

Alipofika Madiani Musa aliwasadia wasichana wawili waliokuwa wamezuiwa kunywesha wanyama wao. Mabinti hao walimweleza baba yao aliyekuwa mzee sana juu ya kijana aliyewasaidia. Wote walipendezwa na kuvutiwa sana na kile kitendo cha Musa kuwasaidia pasina kuhitaji malipo yoyote kutoka kwao.

فَجَآءَتْهُ إِحْدَىٰهُمَا تَمْشِى عَلَى ٱسْتِحْيَآءٍ قَالَتْ إِنَّ أَبِى يَدْعُوكَ لِيَجْزِيَكَ أَجْرَ مَا سَقَيْتَ لَنَا ۚ

*Basi akamjia mmoja katika (wasichana) wale wawili, anakwenda na huku anaona haya, akasema: “Baba yangu anakuita ili akulipe ujira wa kutunyweshea(28:25)*

Musa alipofika kwa yule mzee alimsimulia hali halisi kuhusu dhulma, ukandamizaji na ukiukwaji wa haki za binadamu uliopo nchini Misri, pamoja na kisa kilichompelekea yeye kuhamia Madiani. Yule mzee akamtuliza Musa(a.s), akasema:

قَالَ لَا تَخَفْ ۖ نَجَوْتَ مِنَ ٱلْقَوْمِ ٱلظَّٰلِمِينَ ﴿٢٥﴾

*Usiogope umekwisha kūokoka na watu madhalimu(28:25)*

قَالَ إِنِّىٓ أُرِيدُ أَنْ أُنكِحَكَ إِحْدَى ٱبْنَتَىَّ هَٰتَيْنِ عَلَىٰٓ أَن تَأْجُرَنِى ثَمَٰنِىَ حِجَجٍ ۖ

*Akasema: Mimi nataka nikuoze mmojawapo katika binti zangu hawa wawili kwa kunitumikia miaka minane.(28:27)*

Musa(a.s) aliafiki suala hilo, na mmoja katika wale mabinti aliridhia kuolewa na Musa(a.s) kwa mahari ya kutoa nguvukazi kwa miaka minane.

**Musa achaguliwa kuwa Mtume wa Allah(s.w)**

Musa alipotimiza muda wa miaka minane, alifunga safari na ahali zake kurejea Misri. Njiani aliona moto upande wa mlimani akawaambia ahali zake:

ٱمْكُثُوٓا۟ إِنِّىٓ ءَانَسْتُ نَارًا لَّعَلِّىٓ ءَاتِيكُم مِّنْهَا بِخَبَرٍ أَوْ جَذْوَةٍ مِّنَ ٱلنَّارِ لَعَلَّكُمْ تَصْطَلُونَ ﴿٢٩﴾

*Ngojeni hakika nimeona moto; labda nitakujieni na habari za huko au kijinga cha moto ili muote(28:29)*

فَلَمَّآ أَتَىٰهَا نُودِىَ يَٰمُوسَىٰٓ ﴿١١﴾ إِنِّىٓ أَنَا۠ رَبُّكَ فَٱخْلَعْ نَعْلَيْكَ ۖ إِنَّكَ بِٱلْوَادِ ٱلْمُقَدَّسِ طُوًى ﴿١٢﴾

*Basi alipofika, aliitwa: "Ewe Musa! Hakika Mimi ndiye Mola wako. Basi vua viatu vyako. Hakika wewe uko katika bonde takatifu la Tuwa.(20:11-12)*

وَأَنَا ٱخْتَرْتُكَ فَٱسْتَمِعْ لِمَا يُوحَىٰٓ ﴿١٣﴾ إِنَّنِىٓ أَنَا ٱللَّهُ لَآ إِلَٰهَ إِلَّآ أَنَا۠ فَٱعْبُدْنِى وَأَقِمِ ٱلصَّلَوٰةَ لِذِكْرِىٓ ﴿١٤﴾

*Nami nimekuchagua, (uwe mtume). Basi yasikilize unayoelezwa kupitia wahy. Kwa yakini Mimi ndiye Mwenyezi Mungu, hakuna aabudiwaye kwa haki ila Mimi, Basi niabudu na usimamishe Swala kwa kunitaja(20:13-14)*

**Miujiza: Ushahidi wa Utume wa nabii Musa(as) kwa Firaun**

Allah(s.w) alimjaalia nabii Musa(as) miujiza ya kuthibitisha Utume wake. Miujiza si viinimacho kama ilivyo mazingaombwe.Muujiza ni jambo halisi lisilokawaida ambalo hakuna awezaye kulifanya ila Mtume. Musa alipoulizwa Allah (s.w) kuwa ameshika nini

قَالَ هِيَ عَصَايَ أَتَوَكَّؤُا۟ عَلَيْهَا وَأَهُشُّ بِهَا عَلَىٰ غَنَمِى وَلِىَ فِيهَا
مَـَٔارِبُ أُخْرَىٰ ﴿١٨﴾

*Akasema: "Hii ni fimbo yangu, ninaiegemea na ninaangushia majani kwa ajili ya wanyama wangu. Tena ninaitumia kwa mambo mengine.(20:18)*

Inadhihirika hapa kuwa nabii Musa alikuwa na fimbo ya kawaida kabisa, lakini Allah(as) anaigeuza kuwa muujiza.

قَالَ أَلْقِهَا يَـٰمُوسَىٰ ﴿١٩﴾ فَأَلْقَىٰهَا فَإِذَا هِىَ حَيَّةٌ تَسْعَىٰ ﴿٢٠﴾ قَالَ
خُذْهَا وَلَا تَخَفْ ۖ سَنُعِيدُهَا سِيرَتَهَا ٱلْأُولَىٰ ﴿٢١﴾

*Allah(s.w) akasema: Itupe, ewe Musa". Akaitupa. Mara ikawa nyoka anayekwenda mbio. Mungu akasema: "Ikamate wala usiogope, sasa hivi Tutairudisha hali yake ya kwanza.(20:19-21)*

وَٱضْمُمْ يَدَكَ إِلَىٰ جَنَاحِكَ تَخْرُجْ بَيْضَآءَ مِنْ غَيْرِ سُوٓءٍ ءَايَةً
أُخْرَىٰ ﴿٢٢﴾ لِنُرِيَكَ مِنْ ءَايَـٰتِنَا ٱلْكُبْرَى ﴿٢٣﴾

*"Na uambatanishe mkono wako katika kwapa yako; utatoka ukiwa mweupe sana pasipo na ubaya wowote. Huu ni muujiza mwingine. Ili Tukuoneshe miujiza mingine mikubwa(20:22-23)*

Inabainika wazi kuwa chanzo cha miujiza yote aliyokuwa nayo Musa na mitume wengine, ni Allah(s.w). Hakuna Mtume au nabii aliyefanya miujiza kwa uweza wake mwenyewe!

**Harun(a.s), achaguliwa na Allah(s.w) kushirikiana na Musa(as)**

Nabii Musa alimwomba Allah(s.w) amchague Harun ili wafanye pamoja kazi ya kupigania haki za binadamu.

قَالَ رَبِّ ٱشْرَحْ لِى صَدْرِى ﴿٢٥﴾ وَيَسِّرْ لِىٓ أَمْرِى ﴿٢٦﴾ وَٱحْلُلْ
عُقْدَةً مِّن لِّسَانِى ﴿٢٧﴾ يَفْقَهُوا۟ قَوْلِى ﴿٢٨﴾ وَٱجْعَل لِّى وَزِيرًا
مِّنْ أَهْلِى ﴿٢٩﴾ هَـٰرُونَ أَخِى ﴿٣٠﴾ ٱشْدُدْ بِهِۦٓ أَزْرِى ﴿٣١﴾
كَىْ نُسَبِّحَكَ كَثِيرًا ﴿٣٣﴾ وَنَذْكُرَكَ كَثِيرًا ﴿٣٤﴾ إِنَّكَ كُنتَ بِنَا
بَصِيرًا ﴿٣٥﴾

*Akasema: Ewe Mola wangu! Nipanulie kifua changu(nipe subira). Na unifanyie wepesi katika kazi yangu. Na ufungue fundo lililo katika ulimi wangu. Wapate kufahamu maneno yangu. Na unifanyie waziri katika jamaa zangu. Ndugu yangu Harun. Nitie nguvu kwa huyu. Na umshirikishe katika kazi yangu hii. Ili tukutukuze sana. Na tukutaje kwa wingi. Hakika Wewe unatuona(20:25-35)*

Allah(s.w) alilikubali ombi la nabii Musa(a.s), akamfanya Harun(a.s) kuwa nabii pamoja naye. Allah(s.w) akasema kumwambia Musa:

قَالَ قَدْ أُوتِيتَ سُؤْلَكَ يَـٰمُوسَىٰ ﴿٣٦﴾

*Hakika umekubaliwa maombi yako, Ewe Musa(20:36)*

**Musa na Harun(as) waingia Ikulu ya Firauni kumfikishia ujumbe**

Jukumu kubwa la kwanza walilokabidhiwa Musa(a.s) na Harun(a.s) lilikuwa kumwambia Firauni amwamini Allah(s.w) na awache kukiuka haki za binadamu kwa kuwapa Waisraili uhuru wao. Allah(s.w) akawaambia:

فَأْتِيَاهُ فَقُولَآ إِنَّا رَسُولَا رَبِّكَ فَأَرْسِلْ مَعَنَا بَنِىٓ إِسْرَٰٓءِيلَ وَلَا
تُعَذِّبْهُمْ ۖ قَدْ جِئْنَـٰكَ بِـَٔايَةٍ مِّن رَّبِّكَ ۖ وَٱلسَّلَـٰمُ عَلَىٰ مَنِ ٱتَّبَعَ ٱلْهُدَىٰٓ

*Basi mwendeeni na kamwambieni: Kwa hakika sisi ni Mitume wa Mola wako. Basi waachie wana wa Israili watoke pamoja nasi, wala usiwaadhibu. Hakika tumekuletea ishara zitokazo kwa Mola wako. Na amani itakuwa kwa wale wanaofuata uongofu(20:47)*

Firauni kwa jinsi alivyokuwa amezama katika siasa za kidhalimu na unyonyaji hakupenda kabisa kuona Waisraili wanarejeshewa haki zao za

kibinadamu za kuwa huru. Akasema Firauni kwa kibri na jeuri kubwa kuwa:

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلْـمَلَأُ مَا عَلِمْتُ لَكُم مِّنْ إِلَـٰهٍ غَيْرِى

*Enyi wakuu! Simjui kwa ajili yenu, mungu asiyekuwa mimi.(28:38)*

فَقَالَ أَنَا۠ رَبُّكُمُ ٱلْأَعْلَىٰ ﴿٢٤﴾

*Akasema: Mimi ndiye mola wenu mkuu(79:24)*

**Propaganda za Firauni dhidi ya Musa na Harun(as)**

Nabii Musa (a.s.) alijitahidi kumuelimisha Firauni na watu wake juu ya Mungu mmoja anayekataza dhulma, ukandamizaji na ukiukaji wa haki za binadamu. Lakini Firauni kwasababu ya kupenda sana dhulma, akazusha uongo akiwatangazia watu kwa kuwaambia:

إِنَّ رَسُولَكُمُ ٱلَّذِىٓ أُرْسِلَ إِلَيْكُمْ لَمَجْنُونٌ ﴿٢٧﴾

*Bila shaka mtume wenu aliyetumwa kwenu ni mwendawazimu(26:27)*

Pamoja na kujibiwa kwa dharau na kukashifiwa, Musa aliendelea kufafanua zaidi juu ya Mwenyezi Mungu anayemiliki ulimwengu mzima.

رَبُّ ٱلْمَشْرِقِ وَٱلْمَغْرِبِ وَمَا بَيْنَهُمَآ ۖ إِن كُنتُمْ تَعْقِلُونَ ﴿٢٨﴾

*(Allah ndiye) Mola wa Mashariki na Magharibi na vilivyomo baina yake ikiwa (mna akili) mfahamu(26:28)*

Aliposhindwa kujibu hoja hiyo, Firauni akapandwa hasira na kuanza kumtisha Musa(a.s) akidhania kwamba atamfunga mdomo kwa kumtisha kwa nguvu za dola alizonazo.

قَالَ لَئِنِ ٱتَّخَذْتَ إِلَـٰهًا غَيْرِى لَأَجْعَلَنَّكَ مِنَ ٱلْمَسْجُونِينَ ﴿٢٩﴾

*Firauni akasema: Kama ukishikilia (kuwa kuna) Mungu mwingine badala yangu, kwa hakika nitakufanya miongoni mwa wenye kufungwa gerezani(26:29)*

Lakini Musa(a.s)

hakutishika kabisa kwa hizo kauli za Firauni. Badala yake akataka kumdhihirishia kuwa Allah(s.w) ana nguvu na uweza wa kufanya mambo makubwa ya kutisha kuliko hivyo viaskari vya Firauni na magereza yao.

فَأَلْقَىٰ عَصَاهُ فَإِذَا هِيَ ثُعْبَانٌ مُّبِينٌ ﴿٣٢﴾ وَنَزَعَ يَدَهُۥ فَإِذَا هِيَ
بَيْضَآءُ لِلنَّٰظِرِينَ ﴿٣٣﴾

*Basi(Musa) akatupa fimbo yake, mara ikawa nyoka aliye dhahiri. Na akatoa mkono wake, na mara ukawa mweupe (kweli kweli) kwa watazamao(26:32-33)*

Hapo Firaun akatishika na alidhani kuwa ile miujiza aliyokuja nayo nabii Musa(a.s) kuwa ni sawa na mazingaombwe au viinimacho wanavyofanya wachawi.

قَالَ لِلْمَلَإِ حَوْلَهُۥٓ إِنَّ لَسَٰحِرٌ عَلِيمٌ ﴿٣٤﴾ يُرِيدُ أَن يُخْرِجَكُم
مِّنْ أَرْضِكُم بِسِحْرِهِۦ فَمَاذَا تَأْمُرُونَ ﴿٣٥﴾

*Akasema, kuwaambia wakuu waliomzunguka: Hakika huyu ni mchawi ajuae sana. Anataka kukutoeni katika nchi yenu kwa uchawi wake; basi mnasemaje?(26:34-35)*

**Wachawi wasalimu amri na kusilimu**

Mawaziri waliokuwa washauri wakuu wa Firauni wakataka wakusanywe magwiji waliobobea katika uchawi nchi nzima, kisha wapambanishwe na nabii Musa(as).

فَلَمَّا جَآءَ ٱلسَّحَرَةُ قَالُوا۟ لِفِرْعَوْنَ أَئِنَّ لَنَا لَأَجْرًا إِن كُنَّا نَحْنُ
ٱلْغَٰلِبِينَ ﴿٤١﴾ قَالَ نَعَمْ وَإِنَّكُمْ إِذًا لَّمِنَ ٱلْمُقَرَّبِينَ ﴿٤٢﴾

*Basi walipofika wachawi, wakamwambia Firauni: Je, tutapata ujira tukiwa sisi ndio tutakaoshinda. Akasema: Naam, na pia mtakuwa miongoni mwa wale wanaowekwa mbele katika(serikali)(26:41-42)*

فَأَلْقَوْا۟ حِبَالَهُمْ وَعِصِيَّهُمْ وَقَالُوا۟ بِعِزَّةِ فِرْعَوْنَ إِنَّا لَنَحْنُ
ٱلْغَٰلِبُونَ ﴿٤٤﴾

*Basi wakatupa kamba zao na fimbo zao, na wakasema: Kwa nguvu za Firauni sisi tutakuwa ndio wenye kushinda(26:44)*

فَأَلْقَىٰ مُوسَىٰ عَصَاهُ فَإِذَا هِيَ تَلْقَفُ مَا يَأْفِكُونَ ﴿٤٥﴾

*Kisha Musa akatupa fimbo yake, nayo mara ikavimeza(vyote) walivyozusha wachawi(26:45)*

فَأُلْقِيَ ٱلسَّحَرَةُ سَـٰجِدِينَ ﴿٤٦﴾ قَالُوٓاْ ءَامَنَّا بِرَبِّ ٱلْعَـٰلَمِينَ
رَبِّ مُوسَىٰ وَهَـٰرُونَ ﴿٤٧﴾ ﴿٤٨﴾

*Hapo wachawi walipinduka wakasujudu. Wakasema: Tumemuamini Mola wa walimwengu wote. Mola wa Musa na Harun(26:46-48)*

Inabainika hapa kuwa uchawi si sawa na muujiza, na ndio maana wachawi walishindwa. Hakika uliwadhihirikia ukweli kwamba Musa(a.s) ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Ndio maana Firauni alipotangaza kuwa atawasulubu kwa kuwakata miguu na mikono yao kwasababu wamesilimu pasina ridhaa yake; hawakuyumba katika imani yao.

قَالُواْ لَا ضَيْرَ ۖ إِنَّآ إِلَىٰ رَبِّنَا مُنقَلِبُونَ ﴿٥٠﴾ إِنَّا نَطْمَعُ أَن يَغْفِرَ
لَنَا رَبُّنَا خَطَـٰيَـٰنَآ أَن كُنَّآ أَوَّلَ ٱلْمُؤْمِنِينَ ﴿٥١﴾

*Wakasema: Haidhuru, hakika sisi sote tutarejea kwa Mola wetu. Kwa yakini sisi tunatumai ya kwamba Mola wetu atatusamehe makosa yetu, maana sisi tumekuwa wa kwanza wa wenye kusilimu hapa(26:50-51)*

**Kuangamizwa Firauni na majeshi yake**

Baada ya ushindi alioupata Musa(a.s) dhidi ya wachawi, umati wa watu waliokuwa wamekusanyika kushuhudia mapambano baina ya haki na batili, waliona ukweli kuwa Musa(a.s) ndiye kiongozi halali anayepaswa kutiiwa, na haifai kabisa kutiiwa Firauni dhalimu. Kuanzia hapo walipomuamini Musa wakapata adha na mateso zaidi kutoka kwa Firauni. Ndipo Allah(s.w) alipomuamuru Musa(a.s):

أَنْ أَسْرِ بِعِبَادِىٓ إِنَّكُم مُّتَّبَعُونَ ﴿٥٢﴾

*"Nenda na waja wangu wakati wa usiku(mtoke nchini Misri), bila shaka mtafuatwa(26:52)*

فَلَمَّا تَرَٰٓءَا ٱلْجَمْعَانِ قَالَ أَصْحَـٰبُ مُوسَىٰٓ إِنَّا لَمُدْرَكُونَ ﴿٦١﴾
قَالَ كَلَّآ ۖ إِنَّ مَعِىَ رَبِّى سَيَهْدِينِ ﴿٦٢﴾

*Na yalipokutana majeshi mawili. Watu wa Musa walisema. Hakika tutakamatwa. Musa akasema: La, kwa yakini Mola wangu Yu pamoja nami bila shaka ataniongoza.(26:61-62)*

Waisraili walikuwa wamekwama kuendelea na safari kutokana na kuzuiwa na bahari hali ya kuwa Firauni na majeshi yake yamekwisha wakaribia. Kwa huruma na rehema zake, Allah(s.w) akamuongoza Musa kwa kumwambia:

أَنِ ٱضْرِب بِّعَصَاكَ ٱلْبَحْرَ ۖ فَٱنفَلَقَ فَكَانَ كُلُّ فِرْقٍ كَٱلطَّوْدِ ٱلْعَظِيمِ ﴿٦٣﴾

*Piga bahari kwa fimbo yako; basi ikatengana, na kila sehemu ikawa kama mlima mkubwa(26:63)*

Bahari iligawanyika sehemu mbili na kuwacha njia ambayo nabii Musa alipita na watu wake kwa salama. Lakini majeshi ya Firaun yalizamishwa na kuangamizwa yote. Firaun akawa anatapatapa, akijitupa huku na kule huku akizidi kuwa na yakini kuwa hana uungu wowote wa kujinusuru. Hapo akasema:

ءَامَنتُ أَنَّهُۥ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا ٱلَّذِىٓ ءَامَنَتْ بِهِۦ بَنُوٓا۟ إِسْرَٰٓءِيلَ وَأَنَا۠ مِنَ ٱلْمُسْلِمِينَ ﴿٩٠﴾

*Naamini ya kwamba hakuna Mola aabudiwaye kwa haki ila Yule wanayemuamini wana wa Israeli, na mimi ni miongoni mwa wanaotii(10:90)*

ءَآلْـَٰٔنَ وَقَدْ عَصَيْتَ قَبْلُ وَكُنتَ مِنَ ٱلْمُفْسِدِينَ ﴿٩١﴾ فَٱلْيَوْمَ نُنَجِّيكَ بِبَدَنِكَ لِتَكُونَ لِمَنْ خَلْفَكَ ءَايَةً ۚ وَإِنَّ كَثِيرًا مِّنَ ٱلنَّاسِ عَنْ ءَايَٰتِنَا لَغَٰفِلُونَ ﴿٩٢﴾

*(Malaika wakamwambia)" Sasa(ndio unaamini)! Hali uliasi kabla ya hapo na ukawa miongoni mwa waharibifu. Basi leo tutakuokoa kwa kuuweka mwili wako ili uwe dalili kwa ajili ya wa nyuma yako. Na watu wengi wameghafilika na ishara zetu.(10:91-92)*

Nabii Musa na watu wake walivuka salama salimini, lakini Firauni akagharikishwa yeye na majeshi yake na ukawa ndio mwisho wa utawala wao wa kidhalimu na kinyonyaji.

**Kupewa Taurati.**

Taurati ni Kitabu cha Allah(s.w) alichokabidhiwa nabii Musa(a.s) ili kiwe mwongozo kwa Waisraili. Siku arubaini ziliteuliwa ili mtume Musa(a.s) aweze kujiandaa mwenyewe kwa kufunga na kuswali kwa ajili ya kazi ngumu inayomsubiri. Allah(s.w) anabainisha hili kwa kuwakumbusha Waisraili kuwa:

وَإِذْ وَٰعَدْنَا مُوسَىٰٓ أَرْبَعِينَ لَيْلَةً ثُمَّ ٱتَّخَذْتُمُ ٱلْعِجْلَ مِنۢ
بَعْدِهِۦ وَأَنتُمْ ظَٰلِمُونَ ﴿٥١﴾

*Na kumbukeni tulipomuahidi Musa siku arobaini(afanye ibada mfululizo). Mkamfanya ndama (kuwa mungu) baada yake, na mkawa madhalimu(2:51)*

Waisraili wakashawishika kuabudu ndama wakati Musa alipoitikia wito wa Allah(s.w) kwenda kupokea Taurati. Aliporejea na kuwakuta katika hali hiyo, alighadhibika sana kiasi cha kuangusha mbao zilizoandikwa mwongozo wa Allah(s.w)

وَلَمَّا سَكَتَ عَن مُّوسَى ٱلْغَضَبُ أَخَذَ ٱلْأَلْوَاحَ ۖ وَفِى نُسْخَتِهَا
هُدًى وَرَحْمَةٌ لِّلَّذِينَ هُمْ لِرَبِّهِمْ يَرْهَبُونَ ﴿١٥٤﴾

*Na zilipotulia ghadhabu za Musa, aliziokota zile mbao. Na katika maandiko yake(mbao hizi) ulikuwamo uongofu na rehema kwa wale wanaomwogopa Mola wao(7:154)*

**Mafunzo kwa muhtasari**

(i) Allah(s.w) hapendi dhulma, ukandamizaji na ukiukaji wowote wa haki za binadamu. Ndiyo maana Aliwatuma nabii Musa na Harun (a.s) kwenda kuwakomboa Waisraili waliotiwa utumwani na utawala dhalimu wa Firauni. Fundisho hapa ni kwamba; ni jukumu la kila muislamu kufanya kila jitihada kuhakikisha kila mtu anatendewa haki na uadilifu katika jamii.

(ii) Hakuna hila wala nguvu zinazoweza kuzuia jambo analotaka Allah(s.w) liwepo au lisiwepo katika jamii. Yeye anazo namna nyingi za kumlinda mja wake na vile vile anaweza kumwangamiza mbabe yeyote katika muda na namna isiyotarajiwa. Tumeona Allah(s.w) alivyomlinda nabii Musa(a.s) asichinjwe, kadhalika tumeona alivyomuangamiza Firaun na majeshi yake.

(iii) Elimu ndiyo nyenzo ya kwanza itakayomwezesha mtu kuwa kiongozi atakayeweza kusimamisha haki na uadilifu katika jamii. Tumeona kuwa nabii Musa alipewa elimu kwanza kabla ya kuchaguliwa kuwa mtume aliyepambana na kutokomeza siasa za ukandamizaji, na shirki iliyokuwa imestawi katika utawala wa Firauni.

(iv) Muumini wa kweli hana budi kuchukia vitendo vya dhulma. Anapaswa kuwasaidia watu wanaonyanyaswa na kuonewa katika jamii. Aidha, ni muhimu kuwa makini ili tusichupe mipaka ya Allah(s.w) pale tunapopata fursa ya kuwasaidia wanaoonewa au kukandamizwa. Nabii Musa(a.s) hakulenga kumuua yule mmisri wakati alipokuwa akimsaidia myahudi. Lakini alijikuta amemuua pasina kukusudia.

(v) Mtu hawezi kuwa kiongozi mkweli mwenye kusimamia haki na uadilifu katika jamii, endapo hasimamishi swala na kumkumbuka Allah(s.w) katika kila kipengele cha maisha yake ya kila siku. Hili linajitokeza pale Allah(s.w) alipomsisitizia Musa(a.s) kuwa: *"Kwa yakini Mimi ndiye Mwenyezi Mungu, hakuna aabudiwaye kwa haki ila mimi, basi niabudu na usimamishe swala kwa kunitaja"(20:14)*

(vi) Miujiza waliyokuja nayo mitume ni katika ushahidi wa utume wao, na ni dalili zinaoonesha kuwepo Mwenyezi Mungu.Nabii Musa alikuwa na fimbo ya kawaida kabisa, lakini Allah(as) anaigeuza kuwa muujiza uliozima hila za wachawi, na kuwafanya wasilimu papo hapo.

(vii) Jukumu la kulingania Uislamu linahitajia ushirikiano baina ya viongozi, na kiongozi wa Kiislamu ni yule anayependekeza watu wachamungu kuwa viongozi wa kushirikiana nao katika kulingania Uislamu. Nabii Musa(a.s) alimwomba Allah(as) amchague Harun(a.s) ili wafanye kazi ya kupigania haki za binadamu kwa pamoja.

(viii) Mtu anayemwamini Allah(s.w) na siku ya mwisho hawezi kushirikiana na watawala madhalimu katika kuendeleza dhulma. Tunafahamu kwamba nabii Musa alikuwa na fursa ya kuishi maisha ya raha na ya kifahari chini ya utawala wa Firauni. Lakini hakuridhia hilo kwasababu starehe zote za Firauni na mawaziri wake, zilikuwa ni matunda ya chumo haramu lililopatikana kwa kuwakandamiza wananchi waliofanywa kuwa watumwa.

(ix) Ni kawaida ya watawala madhalimu kutunga uongo wa kuwapakazia sifa mbaya watu wema, wanaosimama kidete kukemea maovu wanayowafanyia watu kwa siri. Tumeona jinsi Firauni alivyokazana kutangaza kuwa, nabii Musa ni kichaa,mchawi, na kwamba ni mtu anaye hatarisha amani na kuleta vurugu za kisiasa, kwasababu tu, alitaka Waisraili wawe huru, wasidhulumiwe na kuonewa.

(x) Thamani ya mtu kukubali haki na ukweli ni kubwa mno mbele ya Allah(s.w) kuliko uhai wa mwanadamu na starehe za maisha ya dunia. Tumeona kuwa pale haki na ukweli vilipowadhihirikia, wachawi hawakuona ubora wa wao kuendelea kuwa wapambe wa kutetea batili, uwongo na dhulma ili kuheshimika mbele ya Ikulu ya Firauni. Wao waliona bora wasulubiwe na kufa kuliko kushikamana na watu madhalimu.

(xi) Toba anayoikubali Allah(s.w) ni ile mtu anayofanya kabla ya kufikwa na mauti. Hivyo, mtu anatakiwa kukubali ukweli na kuyaacha maovu haraka iwezekanavyo, na kutenda mema ili asiwe kama Firaun ambaye toba yake haikukubaliwa. Maana Allah(s.w) anasema:

وَلَيْسَتِ ٱلتَّوْبَةُ لِلَّذِينَ يَعْمَلُونَ ٱلسَّيِّـَٔاتِ حَتَّىٰٓ إِذَا حَضَرَ
أَحَدَهُمُ ٱلْمَوْتُ قَالَ إِنِّى تُبْتُ ٱلْـَٔـٰنَ وَلَا ٱلَّذِينَ يَمُوتُونَ وَهُمْ
كُفَّارٌ ۚ أُو۟لَـٰٓئِكَ أَعْتَدْنَا لَهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿١٨﴾

*Hawana toba wale ambao hufanya maovu mpaka mauti yanapomfika mmoja wao, akasema: "Hakika mimi sasa natubu." Wala wale wanaokufa katika hali ya ukafiri. hao tumewaandalia adhabu iumizayo.(4:18)*

(xii)Hakuna marefu yasiyokuwa na ncha. Hakuna dhalimu atayeshi milele wala mbabe asiyekufa. Wanadamu wote wako chini ya mamlaka ya Allah(s.w), naye ndiye pekee awezaye kuzima pumzi za uhai wa kila mtu.

## HISTORIA YA NABII DAUD (A.S.)

Nabii Daudi (a.s.) aliishi Bait-Ul-Lahm karibu na mji wa Jerusalem. Nasaba yake inatokea kwa Mtume Ya'aquub (a.s.). Pamoja na kuwa Mtume wa Allah (S.W.) Daudi alikuwa pia mfalme wa Mayahudi (Bani Israil).

### Kupewa Daud(a.s) utume na ufalme

Daudi alipewa utume na ufalme baada ya kumuua Jaluti kwenye vita vilivyopiganwa na Waisraili chini ya uongozi wa Taluti, dhidi ya majeshi yaliyoongozwa na Jaluti. Kabla ya hapo, wakubwa wa Kibanii Israili waliomba wapatiwe Mfalme atakayewaongoza kupigana vita dhidi ya maadui waliowatoa kwenye majumba yao.

أَلَمْ تَرَ إِلَى ٱلْمَلَإِ مِنۢ بَنِىٓ إِسْرَٰٓءِيلَ مِنۢ بَعْدِ مُوسَىٰٓ إِذْ قَالُوا۟
لِنَبِىٍّ لَّهُمُ ٱبْعَثْ لَنَا مَلِكًا نُّقَٰتِلْ فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ ۖ

*Hukusikia habari ya wakubwa wa kibanii Israili baada ya Musa, walipomwambia nabii wao: Tuwekee mfalme ili tupigane katika njia ya Mwenyezi Mungu..(2:246)*

وَقَالَ لَهُمْ نَبِيُّهُمْ إِنَّ ٱللَّهَ قَدْ بَعَثَ لَكُمْ طَالُوتَ مَلِكًا ۚ قَالُوٓا۟
أَنَّىٰ يَكُونُ لَهُ ٱلْمُلْكُ عَلَيْنَا وَنَحْنُ أَحَقُّ بِٱلْمُلْكِ مِنْهُ وَلَمْ يُؤْتَ
سَعَةً مِّنَ ٱلْمَالِ ۚ قَالَ إِنَّ ٱللَّهَ ٱصْطَفَىٰهُ عَلَيْكُمْ وَزَادَهُۥ بَسْطَةً فِى
ٱلْعِلْمِ وَٱلْجِسْمِ ۖ وَٱللَّهُ يُؤْتِى مُلْكَهُۥ مَن يَشَآءُ ۚ وَٱللَّهُ وَٰسِعٌ عَلِيمٌ

*Na huyo mtume wao akawaambia: Mwenyezi Mungu amekuchagulieni Taluti kuwa mfalme. Wakasema: Vipi atakuwa mfalme juu yetu, naye hakupewa wasaa wa mali? Akasema: Mwenyezi Mungu amemchagua juu yenu na amemzidishia wasaa wa elimu na kiwiliwili. Na Mwenyezi Mungu humpa ufalme wake amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa, Mwenye kujua(2:247)*

Taluti alichaguliwa kuwa mfalme.

إِنَّ ٱللَّهَ مُبْتَلِيكُم بِنَهَرٍ فَمَن شَرِبَ مِنْهُ فَلَيْسَ مِنِّى وَمَن لَّمْ
فَإِنَّهُۥ مِنِّىٓ إِلَّا مَنِ ٱغْتَرَفَ غُرْفَةًۢ بِيَدِهِۦ ۚ فَشَرِبُوا۟ مِنْهُ إِلَّا قَلِيلًا مِّنْهُمْ ۚ

*Basi Taluti alipoondoka na majeshi, alisema: Mwenyezi Mungu atakufanyieni mtihani kwa mto. Basi atakayekunywa humo si pamoja nami, na asiyekunywa humo atakuwa pamoja nami; ila atakayeteka kwa kiasi kidogo cha kujaza kitanga cha mkono wake. Basi walikunywa humo ila wachache tu miongoni mwao...(2:249)*

Wale waliotii walivuka mto pamoja na Taluti kuelekea uwanja wa vita. Walipoyaona majeshi ya Jaluti waliogopa wakisema:

لَا طَاقَةَ لَنَا ٱلْيَوْمَ بِجَالُوتَ وَجُنُودِهِۦ ۚ قَالَ ٱلَّذِينَ يَظُنُّونَ أَنَّهُم مُّلَـٰقُوا۟ ٱللَّهِ كَم مِّن فِئَةٍ قَلِيلَةٍ غَلَبَتْ فِئَةً كَثِيرَةًۢ بِإِذْنِ ٱللَّهِ ۗ وَٱللَّهُ مَعَ ٱلصَّـٰبِرِينَ ﴿٢٤٩﴾

*Leo hatumuwezi Jaluti na majeshi yake. Wakasema wale wenye yakini ya kukutana na Mola wao: "Makundi mangapi madogo yameshinda makundi makubwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu Yu pamoja na wafanyao subira(2:249)*

Waumini wa kweli walijua fika kuwa ushindi wao uko katika mamlaka na ridhaa ya Mwenyezi Mungu. Walichotakiwa wao ni kupambana kadri ya uwezo wao huku wakifanya subira. Katika hali hiyo wakamuomba Allah(s.w) wakisema:

رَبَّنَآ أَفْرِغْ عَلَيْنَا صَبْرًا وَثَبِّتْ أَقْدَامَنَا وَٱنصُرْنَا عَلَى ٱلْقَوْمِ ٱلْكَـٰفِرِينَ ﴿٢٥٠﴾

*Mola wetu! Tumiminie subira na uithibitishe miguu yetu, na utusaidie juu ya watu hawa makafiri(2:250)*

فَهَزَمُوهُم بِإِذْنِ ٱللَّهِ وَقَتَلَ دَاوُۥدُ جَالُوتَ وَءَاتَىٰهُ ٱللَّهُ ٱلْمُلْكَ وَٱلْحِكْمَةَ وَعَلَّمَهُۥ مِمَّا يَشَآءُ ۗ وَلَوْلَا دَفْعُ ٱللَّهِ ٱلنَّاسَ بَعْضَهُم بِبَعْضٍ لَّفَسَدَتِ ٱلْأَرْضُ وَلَـٰكِنَّ ٱللَّهَ ذُو فَضْلٍ عَلَى ٱلْعَـٰلَمِينَ ﴿٢٥١﴾

*Basi wakawaendesha mbio (maadui) kwa idhini ya Mwenyezi Mungu; na Daudi akamuua Jaluti, na Mwenyezi Mungu akampa ufalme na hikma na akamfundisha aliyoyapenda. Na kama Mwenyezi Mungu asingelizuia watu, baadhi yao kwa wengine, kwa hakika dunia ingeliharibika. Lakini Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila kuu(2:251)*

**Allah(s.w) amfunza Daudi namna ya kutoa hukumu**

Baada ya kumpa ufalme, Allah(s.w) akamfunza nabii Daud(a.s) namna ya kuhukumu kesi mbalimbali.Allah(s.w) akawatuma Malaika katika umbile la mwanadamu.

إِذْ دَخَلُوا۟ عَلَىٰ دَاوُۥدَ فَفَزِعَ مِنْهُمْ ۖ قَالُوا۟ لَا تَخَفْ ۖ خَصْمَانِ بَغَىٰ
بَعْضُنَا عَلَىٰ بَعْضٍ فَٱحْكُم بَيْنَنَا بِٱلْحَقِّ وَلَا تُشْطِطْ وَٱهْدِنَآ
إِلَىٰ سَوَآءِ ٱلصِّرَٰطِ ﴿٢٢﴾

*Walipomuingilia Daudi, akawaogopa. Wakasema: "Usiogope hakika sisi ni wagombanao wawili, mmoja wetu amemdhulumu mwenziwe; basi hukumu kwa haki wala usipendelee, na utuongoze katika njia iliyo sawa.(38:22)*

إِنَّ هَٰذَآ أَخِى لَهُۥ تِسْعٌ وَتِسْعُونَ نَعْجَةً وَلِىَ نَعْجَةٌ وَٰحِدَةٌ
فَقَالَ أَكْفِلْنِيهَا وَعَزَّنِى فِى ٱلْخِطَابِ ﴿٢٣﴾

*Hakika huyu ni ndugu yangu; yeye ana kondoo majike tisini na tisa, na mimi nina kondoo mmoja tu jike, lakini amesema "nipe huyu wako nikufugie, na amenishinda katika maneno.(38:23)*

قَالَ لَقَدْ ظَلَمَكَ بِسُؤَالِ نَعْجَتِكَ إِلَىٰ نِعَاجِهِۦ ۖ وَإِنَّ كَثِيرًا
مِّنَ ٱلْخُلَطَآءِ لَيَبْغِى بَعْضُهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ إِلَّا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ وَعَمِلُوا۟
ٱلصَّٰلِحَٰتِ وَقَلِيلٌ مَّا هُمْ ۗ وَظَنَّ دَاوُۥدُ أَنَّمَا فَتَنَّٰهُ فَٱسْتَغْفَرَ
رَبَّهُۥ وَخَرَّ رَاكِعًا وَأَنَابَ ۩ ﴿٢٤﴾

*Akasema: "Kweli amekudhulumu kwa kukuomba kondoo wako kuongeza katika kondoo wake; na bila shaka washirika wengi hudhulumiana wao kwa wao, isipokuwa wale walioamini na kutenda mema, nao ni wachache". Na mara Daudi akaona ya kwamba tumemtia mtihanini. Akaomba msamaha kwa Mola wake, na akaanguka kunyenyekea.(38:24)*

فَغَفَرْنَا لَهُۥ ذَٰلِكَ ۖ وَإِنَّ لَهُۥ عِندَنَا لَزُلْفَىٰ وَحُسْنَ مَـَٔابٍ ﴿٢٥﴾

*Basi tukamsamehe hayo. Na kwa hakika ana yeye kwetu cheo kikubwa na mahala pazuri(38:25)*

يَٰدَاوُۥدُ إِنَّا جَعَلْنَٰكَ خَلِيفَةً فِى ٱلْأَرْضِ فَٱحْكُم بَيْنَ ٱلنَّاسِ
بِٱلْحَقِّ وَلَا تَتَّبِعِ ٱلْهَوَىٰ فَيُضِلَّكَ عَن سَبِيلِ ٱللَّهِ ۚ إِنَّ ٱلَّذِينَ يَضِلُّو
نَ عَن سَبِيلِ ٱللَّهِ لَهُمْ عَذَابٌ شَدِيدٌۢ بِمَا نَسُوا۟ يَوْمَ ٱلْحِسَابِ ﴿٢٦﴾

*"Ewe Daud! Hakika tumekujalia kuwa khalifa katika ardhi, basi wahukumu watu kwa haki wala usifuate matamanio ya nafsi yasije yakakupoteza na njia ya Mwenyezi Mungu. Kwa yakini wale waliopotea wakaacha njia ya Mwenyezi Mungu, wao watapata adhabu kali kwa sababu ya kusahau (kupuuza) kwao siku ya Hisabu." (38:26).*

## Kupewa Zaburi.

Katika Qur'an vinatajwa vitabu vikuu vinne vya ujumbe wa Allah (S.W.). Vitabu hivyo ni Zaburi, Taurati, Injili na Qur'an. Zaburi alipewa Mtume Daud (a.s.).

وَءَاتَيْنَا دَاوُۥدَ زَبُورًا ﴿١٦٣﴾

*"...Na Daudi tukampa Zaburi" (4:163).*

## Allah(s.w) amuwezesha Daud(as) kuwasiliana na viumbe wengine

ٱصْبِرْ عَلَىٰ مَا يَقُولُونَ وَٱذْكُرْ عَبْدَنَا دَاوُۥدَ ذَا ٱلْأَيْدِ ۖ إِنَّهُۥٓ أَوَّابٌ
﴿١٧﴾ إِنَّا سَخَّرْنَا ٱلْجِبَالَ مَعَهُۥ يُسَبِّحْنَ بِٱلْعَشِىِّ وَٱلْإِشْرَاقِ ﴿١٨﴾
وَٱلطَّيْرَ مَحْشُورَةً ۖ كُلٌّ لَّهُۥٓ أَوَّابٌ ﴿١٩﴾

*Subiri juu ya hayo wanayoyasema, na umkumbuke mja wetu Daudi mwenye nguvu; kwa hakika yeye alikuwa mwelekevu sana. Hakika sisi tulimtiishia milima pamoja naye, ikimtukuza(Allah) asubuhi na jioni. Na pia ndge waliokusanywa, wote walikuwa wanyenyekevu kwake.(38:17-19)*

**Nabii Daud(a.s) aruzukiwa mtoto mwema aitwaye Suleiman**

وَوَهَبْنَا لِدَاوُۥدَ سُلَيْمَـٰنَ ۚ نِعْمَ ٱلْعَبْدُ ۖ إِنَّهُۥٓ أَوَّابٌ ﴿٣٠﴾

*Na tukampa Daudi(mtoto anayeitwa) Suleimani, aliyekuwa mtu mwema; na alikuwa mnyenyekevu(38:30)*

**Ustadi katika Matumizi ya chuma**

Umuhimu wa matumizi ya chuma hasa katika kuihami dini ya Allah ni jambo kongwe katika historia ya mwanadamu. Moja ya neema aliyopewa nabii Daudi ni ujuzi wa kukifua chuma na kutengeneza zana mbali mbali.

**Uadilifu na Hekma**

Katika jumla ya matunda ya lazima kupatikana kwa watu kutokana na kufuata mwongozo wa Allah (s.w.) ni uadilifu katika jamii. Kwa kujua kuwa yupo Allah (s.w.) Mjuzi wa yote ambaye atawahukumu watu kesho Akhera, hayupo yeyote hata mwenye madaraka kiasi gani katika jamii atakayethubutu kuleta dhuluma ya aina yoyote. Aidha hayupo atakayehofia kuisema haki na kukosoa pale anapoona haki inakiukwa. Na yule anayekosolewa kwa kukiuka haki (kwa kukosea) hataona uzito kurejea kwenye hukumu iliyo sawa. Qur’an inatufahamisha kuwa nabii Daudi alipewa ilimu na akili ya kukata hukumu kwa uadilifu.

وَشَدَدْنَا مُلْكَهُۥ وَءَاتَيْنَـٰهُ ٱلْحِكْمَةَ وَفَصْلَ ٱلْخِطَابِ ﴿٢٠﴾

*Na tukautia nguvu mfalme wake na tukampa elimu na (audilifu) katika kukata hukumu(38:20)*

**Mafunzo kwa muhtasari**

(i) Katika Uislamu, kiongozi huchaguliwa kwa kuzingatia elimu, afya na nguvu, uchamungu (ukweli,auminifu na utii) wake katika kutekeleza maamrisho ya Allah(SW).

(ii) Utii kwa kiongozi mchamungu, na kumtegemea Allah(s.w) wakati wote ndiyo msingi wa mafanikio kwa Waislamu. Udogo au uchache wa askari katika jeshi la waislamu haiwezi kuwa sababu ya wao kushindwa, endapo wanapigania jambo la haki. Watu wachache wa Twaluti walihisi isingekuwa rahisi kulishinda jeshi kubwa la Jaluti. Katika kuipigania dini ya Allah(s.w) wingi sio hoja, bali imani thabiti, subra na kumtegemea Mwenyezi Mungu.

(iii) Tunapotakiwa kuhukumu juu ya jambo ni lazima tusikileze maelezo ya pande zote mbili na kuyapima hakika yake, tusiridhike na maelezo au ushahidi wa upande mmoja na kutumia kama kigezo cha kuhukumu kesi. Tumeona kuwa baada ya kutoa hukumu, nabii Daudi(s.w) aligundua kuwa hakufanya uadilifu kwasababu hukumu yake ilitokana na maelezo ya upande mmoja.

## HISTORIA YA NABII SULEIMAN (A.S.)

Suleiman(a.s) alikuwa mtoto wa nabii Daudi (a.s.) na pamoja na kuwa Mtume alirithi pia kiti cha ufalme wa baba yake.

وَوَرِثَ سُلَيْمَٰنُ دَاوُۥدَ ۖ وَقَالَ يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ عُلِّمْنَا مَنطِقَ ٱلطَّيْرِ
وَأُوتِينَا مِن كُلِّ شَىْءٍ ۖ إِنَّ هَٰذَا لَهُوَ ٱلْفَضْلُ ٱلْمُبِينُ ﴿١٦﴾

*"Na Suleimani alimrithi Daudi na akasema: "Enyi watu! Tumefundishwa (hata kutambua) usemi wa ndege na tumepewa kila kitu, hakika hii ni fadhila iliyo dhahiri" (27:16).*

Nabii Suleiman anatajwa katika historia kama mfalme ambaye haujapata kutokea ufalme mkubwa kama wake. Mwenyezi Mungu alimpa uwezo hata wa kumiliki majini. Wakimtumikia katika kazi zake mbali mbali. Ufalme huu unatajwa kuwa Nabii Suleiman(a.s) aliupata baada ya kumuomba Mola wake ampe ufalme ambao hataupata mwingine yeyote baada yake.

قَالَ رَبِّ ٱغْفِرْ لِى وَهَبْ لِى مُلْكًا لَّا يَنۢبَغِى لِأَحَدٍ مِّنۢ بَعْدِىٓ ۖ
إِنَّكَ أَنتَ ٱلْوَهَّابُ ﴿٣٥﴾

*"Akasema: "Mola wangu! Nisamehe na unipe ufalme, asiupate yoyote baada yangu. Bila shaka wewe ndiwe Mpaji" (38:35).*

Dua hii nabii Suleiman ameomba akiwa tayari ni mfalme. Lakini baada ya hapo ndio ufalme wake ukapanuka.

فَسَخَّرْنَا لَهُ ٱلرِّيحَ تَجْرِى بِأَمْرِهِۦ رُخَآءً حَيْثُ أَصَابَ ﴿٣٦﴾
وَٱلشَّيَٰطِينَ كُلَّ بَنَّآءٍ وَغَوَّاصٍ ﴿٣٧﴾ وَءَاخَرِينَ مُقَرَّنِينَ فِى
ٱلْأَصْفَادِ ﴿٣٨﴾

*"Basi tukamtiishia upepo unaokwenda pole pole kwa amri yake, anakotaka kufika. Pia na (Tukamtiishia) mashetani, kila ajengaye na azamiaye (lulu). Na wengine wafungwao minyororoni (wanapokhalifu amri zake)" (38:36-38).*

Pamoja na ufalme na mamlaka makubwa kiasi hiki aliyopewa Suleiman(a.s), lakini pia alipewa elimu ya kumtambua Allah (s.w).Na utume. Kwa hiyo alikuwa ni mja mwenye shukrani kwa neema hizo alizofadhilishwa:

وَلَقَدْ ءَاتَيْنَا دَاوُۥدَ وَسُلَيْمَٰنَ عِلْمًا ۖ وَقَالَا ٱلْحَمْدُ لِلَّهِ ٱلَّذِى
فَضَّلَنَا عَلَىٰ كَثِيرٍ مِّنْ عِبَادِهِ ٱلْمُؤْمِنِينَ ﴿١٥﴾

*"Na bila shaka tuliwapa Daudi na Suleiman ilimu (kubwa kabisa na wakamshukuru Mwenyezi Mungu) wakasema: "Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu, aliyetufadhilisha kuliko wengi katika waja wake waliomuamini:" (27:15).*

**Kusilimu Malkia wa Sabaa**

Sabaa ulikuwa mji katika nchi inayojulikana leo kama Yemen. Watu wa Sabaa walikuwa wakiabudu jua na walikuwa wakitawaliwa na mwanamke Malkia Bilqis.

Siku moja ndege Hud-hud alikuwa ametoweka kwenye Kasiri la nabii Suleiman(as). Nabii Suleiman(a.s)akashangaa, "imekuwaje mbona simuoni Hud-hud?"

فَمَكَثَ غَيْرَ بَعِيدٍ فَقَالَ أَحَطتُ بِمَا لَمْ تُحِطْ بِهِۦ وَجِئْتُكَ
مِن سَبَإٍۭ بِنَبَإٍ يَقِينٍ ﴿٢٢﴾

*"Basi hakukaa sana mara (Hud-hudi akafika) akasema (kumwambia nabii Suleiman)) Nimegundua usilogundua, na ninakujia hivi kutoka (nchi inayoitwa) Sabaa na (nakuletea) habari yenye yakini."(27:22)*

إِنِّي وَجَدتُّ ٱمۡرَأَةٗ تَمۡلِكُهُمۡ وَأُوتِيَتۡ مِن كُلِّ شَيۡءٖ وَلَهَا
عَرۡشٌ عَظِيمٞ ﴿٢٣﴾

*"Hakika nimekuta mwanamke anawatawalia; naye amepewa kila kitu na anacho kiti cha enzi kikubwa."(27:23)*

وَجَدتُّهَا وَقَوۡمَهَا يَسۡجُدُونَ لِلشَّمۡسِ مِن دُونِ ٱللَّهِ وَزَيَّنَ
لَهُمُ ٱلشَّيۡطَٰنُ أَعۡمَٰلَهُمۡ فَصَدَّهُمۡ عَنِ ٱلسَّبِيلِ فَهُمۡ لَا
يَهۡتَدُونَ ﴿٢٤﴾

*"Nimmemkuta yeye na watu wake wanalisujudia jua badala ya Mwenyezi Mungu; na shetani amewapambia vitendo vyao na akawazuilia njia (ya kheri), kwa hivyo hawakuongoka." (27:24).*

Baada ya taarifa hizo nabii Suleiman(a.s) alituma ujumbe kumnasihi malkia aingie katika Uislamu.

قَالَ سَنَنظُرُ أَصَدَقۡتَ أَمۡ كُنتَ مِنَ ٱلۡكَٰذِبِينَ ﴿٢٧﴾ ٱذۡهَب بِّكِتَٰبِي
هَٰذَا فَأَلۡقِهۡ إِلَيۡهِمۡ ثُمَّ تَوَلَّ عَنۡهُمۡ فَٱنظُرۡ مَاذَا يَرۡجِعُونَ ﴿٢٨﴾

*Akasema(Suleiman) "Tutatazama kama unasema kweli au umo katika waongo" Nenda na barua yangu hii na uwafikishie, kisha uwaache, na utazame watashauriana vipi(27:27-28)*

قَالَتۡ يَٰٓأَيُّهَا ٱلۡمَلَؤُاْ إِنِّيٓ أُلۡقِيَ إِلَيَّ كِتَٰبٞ كَرِيمٌ ﴿٢٩﴾ إِنَّهُۥ
مِن سُلَيۡمَٰنَ وَإِنَّهُۥ بِسۡمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحۡمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ ﴿٣٠﴾ أَلَّا تَعۡلُواْ
عَلَيَّ وَأۡتُونِي مُسۡلِمِينَ ﴿٣١﴾

*(Yule Malkia akawakusanya mawaziri wake) akasema: "Enyi wakuu wangu! hakika nimeletewa barua tukufu. Imetoka kwa Suleimani, nayo ni: Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu. Msinifanyie jeuri, na fikeni kwangu hali ya kuwa mmekwisha silimu(27:29-31)*

قَالَتْ يَٰٓأَيُّهَا ٱلْمَلَؤُا۟ أَفْتُونِى فِىٓ أَمْرِى مَا كُنتُ قَاطِعَةً أَمْرًا
حَتَّىٰ تَشْهَدُونِ ﴿٣٢﴾

*(Na malkia) akasema: Enyi wakuu wangu! Nipeni shauri katika jambo hili, maana sikati shauri lolote mpaka muwepo(27: 32)*

قَالُوا۟ نَحْنُ أُو۟لُوا۟ قُوَّةٍ وَأُو۟لُوا۟ بَأْسٍ شَدِيدٍ وَٱلْأَمْرُ إِلَيْكِ فَٱنظُرِى
مَاذَا تَأْمُرِينَ ﴿٣٣﴾

*Wakasema: "Sisi ni wenye nguvu na ni wenye vita vikali; na amri iko kwako, basi angalia ni nini unaamrisha (27:33)*

Malkia baada ya kushauriana na mawaziri wake aliona apoteze lengo la Sulaiman kwa kumpa zawadi.

وَإِنِّى مُرْسِلَةٌ إِلَيْهِم بِهَدِيَّةٍ فَنَاظِرَةٌۢ بِمَ يَرْجِعُ ٱلْمُرْسَلُونَ ﴿٣٥﴾

*Lakini mimi nitawapelekea zawadi, nami nitangoja watakayorudi nayo wajumbe(27:35)*

Lakini nabii Suleiman(a.s) hakuzugwa na hiyo zawadi ya rushwa toka kwa malkia. Kwa hiyo nabii Suleiman(a.s) alimrejeshea zawadi zake na akaendeleza harakati za kumvuta malkia katika haki mpaka akasilimu. Alipofika kwa Suleimani akaambiwa:

قِيلَ لَهَا ٱدْخُلِى ٱلصَّرْحَ ۖ فَلَمَّا رَأَتْهُ حَسِبَتْهُ لُجَّةً وَكَشَفَتْ عَن
سَاقَيْهَا ۚ قَالَ إِنَّهُۥ صَرْحٌ مُّمَرَّدٌ مِّن قَوَارِيرَ ۗ قَالَتْ رَبِّ إِنِّى ظَلَمْتُ
نَفْسِى وَأَسْلَمْتُ مَعَ سُلَيْمَٰنَ لِلَّهِ رَبِّ ٱلْعَٰلَمِينَ ﴿٤٤﴾

*Liingie behewa la nyumba yangu. Alipoliona alidhani kuwa ni eneo la maji, na akapandisha nguo mpaka katika miundi yake. (Suleimani) akasema: "Hakika hilo ni behewa lililosakafiwa kwa vioo. (malkia) akaomba: "Mola wangu, nalidhulumu nafsi yangu, najisalimisha pamoja na Suleimani kwa Mola wa walimwengu(27:44)*

### Kusingiziwa Nabii Suleiman(a.s) Uchawi

Pamoja na Ucha-Mungu aliokuwa nao nabii Suleiman(a.s) watu hawakuacha kumsingizia mambo machafu. Nabii Suleiman(a.s) alisingiziwa kuwa alikufuru akafundisha watu elimu ya uchawi. Qur'an inajibu shutuma hizo katika aya ifuatayo:

وَمَا كَفَرَ سُلَيْمَـٰنُ وَلَـٰكِنَّ ٱلشَّيَـٰطِينَ كَفَرُوا۟ يُعَلِّمُونَ ٱلنَّاسَ ٱلسِّحْرَ وَمَآ أُنزِلَ عَلَى ٱلْمَلَكَيْنِ بِبَابِلَ هَـٰرُوتَ وَمَـٰرُوتَ

*"...Na Suleiman hakukufuru, bali mashetani ndio waliokufuru, waliwafundisha watu uchawi (waliokuwa wakiujua wenyewe tangu zamani) na uchawi) ulioteremshwa kwa malaika wawili; Haruta na Maruta; katika (mji wa) Babil..." (2:102).*

### Kifo cha Nabii Suleiman(a.s)

Pamoja na utukufu na umadhubuti wa ufalme wake nabii Suleiman(a.s) muda wake wa kuishi ulipotimia alikufa kama mitume, wafalme na wanadamu wengine. Kifo chake kilikuwa ndio mwanzo pia wa kuanguka kwa himaya kubwa aliyokuwa ameijenga.

فَلَمَّا قَضَيْنَا عَلَيْهِ ٱلْمَوْتَ مَا دَلَّهُمْ عَلَىٰ مَوْتِهِۦٓ إِلَّا دَآبَّةُ ٱلْأَرْضِ تَأْكُلُ مِنسَأَتَهُۥ ۖ فَلَمَّا خَرَّ تَبَيَّنَتِ ٱلْجِنُّ أَن لَّوْ كَانُوا۟ يَعْلَمُونَ ٱلْغَيْبَ مَا لَبِثُوا۟ فِى ٱلْعَذَابِ ٱلْمُهِينِ ﴿١٤﴾

*"Na Tulipomkidhia mauti (alipokufa) hakuna aliyewajulisha mauti yake ila mnyama wa ardhi, (mchwa) aliyekula fimbo yake. Basi ilipoanguka, majini walitambua kama wangalijua siri wasingalikaa katika adhabu hiyo idhalilishayo." (34:14).*

Baada ya Nabii Suleiman(a.s) waliomfuatia waliendesha maisha ya ufuska na anasa na kidogo kidogo tabia hiyo ikawa inabomoa ufalme mpaka ukaporomoka. Kuporomoka kwa ufalme kuliyafanya majini yawe huru pia.

**Mafunzo kwa muhtasari**

(i) Ni muhimu sana kujua habari za wakazi wa sehemu mbalimbali katika vijiji, miji, nchi na dunia kwa ujumla. Nabii Suleimani(a.s) aliweza kuwaokoa watu wa Sabaa waliokuwa wamezama kwenye giza nene la shirki. Hivyo, hatuna budi kutafiti jamii mbalimbali kwa lengo la kuwalingania Uislamu. Twaweza kufanya hivyo kwa kutembelea maoneo mbalimbali, kusoma habari na makala za magazeti au kusikiliza taarifa za habari za redio na televisheni.

(ii) Tunapopata habari au uvumi wa jambo fulani juu ya watu, itabidi tutafute uthibitisho wa kuyakinisha kama jambo hilo lipo, limetendeka au la. Kisha tuangalie namna ya kulifanyia kazi ikiwa ni kweli ama kuachana nalo. Tukumbuke kuwa, nabii Suleimani (a.s)hakuzichukua habari alizoletewa na Hud-hudi kuwa ni za kweli mia kwa mia mpaka alipozithibitisha.

(iii) Kushauriana kabla ya kutoa maamuzi ya kufanya jambo, ni moja wapo ya mbinu muhimu za uongozi. Ni vyema basi kiongozi katika darasa, shule, taasisi, familia au nchi, ashauriane na wenzake katika kuyaendea mambo, pasina kufanya uimla(udikiteta). Mawaziri walimshauri malikia wa Sabaa, kupigana vita dhidi ya Suleimani(a.s). Lakini kwa upande wake, malkia aliona vita si njia nzuri sana, japo ingefaa.

(iv) Mara nyingi watawala hulewa tamaa ya kujilimbikizia madaraka na mali wakasahau wajibu wao mbele ya Muumba wao. Malkia wa Sabaa alidhani kwa kumuhonga mali angemtoa nabii Suleiman(a.s) katika lengo lake. lakini haikumyumbisha, nabii Suleimani alibakia katika msimamo wake ule ule!

(v) Kujifundisha na kuufanyia kazi uchawi ni kufru na atakayehiari kuufuata hatakuwa na sehemu yoyote katika Akhera.

(vi) Imekuwa ni tabia ya watu wabaya kuwasingizia mitume na watu wema uovu ili wapate kuwapoteza watu na njia ya Allah(s.w). Kama vile nabii Suleimani(a.s) alivyosingiziwa uchawi, ndivyo makafiri wanawapachika watu wema majina mabaya au kuwahusisha na maovu.

## HISTORIA YA NABII ZAKARIA (A.S)

Mtume Zakaria(a.s) alikuwa ndiye mlezi wa Bibi Maryam, mama wa Mtume Issa (a.s.). Alikuwa muangalizi mkuu wa nyumba ya Ibada.

### Nabii Zakaria amuomba Allah(s.w) amjaalie mtoto mwema

Mtume Zakaria (a.s.) hakujaaliwa kupata mtoto mpaka kufikia uzeeni. Hali hiyo ilimtia huzuni kwani alitamani awe na mrithi ambaye angefanya na kusimamia kazi ya kuendesha harakati za Kiislamu baada yake. Katika huzuni hiyo alinyanyua mikono kumuomba Mola wake:

ذِكْرُ رَحْمَتِ رَبِّكَ عَبْدَهُۥ زَكَرِيَّآ ﴿٢﴾ إِذْ نَادَىٰ رَبَّهُۥ نِدَآءً خَفِيًّا

*"(Huu ni) ukumbusho wa rehema ya Mola wako (kumrehemu) mja wake Zakaria. Alipomlingania (alipomwomba) Mola wake kwa mlingano wa siri.(19:2-3)*

قَالَ رَبِّ إِنِّى وَهَنَ ٱلْعَظْمُ مِنِّى وَٱشْتَعَلَ ٱلرَّأْسُ شَيْبًا وَلَمْ أَكُنۢ بِدُعَآئِكَ رَبِّ شَقِيًّا ﴿٤﴾

*Akasema: "Mola wangu! Bila shaka mifupa yangu imekuwa dhaifu na kichwa kinawaka (kinang'ara) kwa mvi, wala sikuwa mwenye bahati mbaya, (mwenye kukhasirika) Mola wangu, kwa kukuomba wewe."*

*"Na hakika mimi nawahofia jamaa zangu baada yangu (kuharibu dini). Na mke wangu ni tasa. Basi nipe mrithi (anijie) kutoka kwako."*

*"Atakayenirithi (ilimu yangu na uwongozi wangu), na kuwarithi (wazee wake wengine) kizazi cha Ya'aquub. Na umfanye, Mola wangu, mwenye kukuridhisha."*

*"(Akaambiwa): "Ewe Zakaria! Tunakupa habari njema ya (kuwa utazaa) mtoto, jina lake ni Yahya. Hatujafanya kabla yake aliye na jina namna hilo" (19:4-7).*

### Mafunzo kwa muhtasari

(i) Mtume Zakaria alikuwa mtu mwema aliyeutumia umri wake wote kuelimisha na kusimamisha dini ya Allah.

(ii) Katika hali ya kawaida watu hutegemewa kupata kizazi katika umri wa ujana kabla ya uzee hasa wanawake. Upo umri akishapindukia mwanamke, hatarajii kupata mtoto tena. Lakini hapa tunamuona Mtume Zakaria (a.s.) pamoja na uzee wake na ukongwe

wa mkewe hakukata tamaa na Rehma za Allah. Bali alimwomba Mola wake ampatie urithi. Aidha hatumuoni Mtume Zakaria akielekea kwenye mambo ya ushirikina na kama ilivyo kwa wengi wetu hii leo tufanyavyo tunapopatwa na mtihani wa kukosa mtoto. Tatu, Zakaria hakutaka mtoto tu kwa manufaa yake binafsi. Bali alitamani kupata mtoto mwema atakayefanya kazi ya kuwaongoza watu katika Njia ya Allah(a.s)

(iii) Uwezo wa Allah haumithiliki wala hauna mipaka. Mtume Zakaria(a.s) alikuwa kikongwe na mkewe kikongwe pia. Aidha mkewe zaidi ya ukongwe wake alishajihesabu kuwa tasa. Lakini pamoja na hayo yote; Allah (s.w) akawapa mtoto.

**NABII YAHYA(AS)**

Allah(s.w), alijibu dua la nabii Zakaria (a.s)kwa kujaalia nabii Yahya(a.s) kuwa mwanawe atakayerithi na kuendeleza harakati za Uislamu.

يَٰزَكَرِيَّآ إِنَّا نُبَشِّرُكَ بِغُلَٰمٍ ٱسْمُهُۥ يَحْيَىٰ لَمْ نَجْعَل لَّهُۥ مِن
قَبْلُ سَمِيًّا ﴿٧﴾

*"(Akaambiwa): "Ewe Zakaria! Tunakupa habari njema ya (kuwa utazaa) mtoto, jina lake ni Yahya. Hatujafanya kabla yake aliye na jina namna hilo" (19:7).*

**Kupewa mtume nabii Yahya**

Kuhusu kupewa utume nabii Yahya, Allah(s.w) anatufahamisha hili pale apomwambia;

يَٰيَحْيَىٰ خُذِ ٱلْكِتَٰبَ بِقُوَّةٍ ۖ وَءَاتَيْنَٰهُ ٱلْحُكْمَ صَبِيًّا ﴿١٢﴾

*"Ewe Yahya! Kishike Kitabu (hiki unachopewa) kwa hima kubwa." Na tulimpa hikima angali mtoto.(19:12)*

Nabii Yahya(a.s) alikuwa mwema sana kwa wazazi wake, kiasi ambacho Allah(s.w) anamtaja kwa sifa hii ili iwe kigezo kwa wanadamu. Tabia hii njema aliyokuwa nayo nabii Yahya inatajwa kwenye aya zifuatazo:

وَحَنَانًا مِّن لَّدُنَّا وَزَكَوٰةً ۖ وَكَانَ تَقِيًّا ﴿١٣﴾ وَبَرًّۢا بِوَٰلِدَيْهِ وَلَمْ
يَكُن جَبَّارًا عَصِيًّا ﴿١٤﴾ وَسَلَٰمٌ عَلَيْهِ يَوْمَ وُلِدَ وَيَوْمَ وَبَرًّۢا
وَلَمْ يَكُن جَبَّارًا عَصِيًّا ﴿١٤﴾

*Na (Tukamfanya ni) rehema kutoka Kwetu, na utakaso, na alikuwa mchamungu.Na mwema kwa wazazi wake wala hakuwa jeuri asi. Na amani ilikuwa juu yake siku aliyozaliwa na siku aliyokufa na siku atakayofufuliwa hai." (19:12-15).*

**Mafunzo kwa muhtasari**

(i) Mtoto anayependwa sana na Allah(s.w) ni yule anayewatendea wema wazazi wake wawili. Ni dhahiri kuwa Allah(s.w) anatutajia tabia njema ya Yahya(a.s) ili kutukumbusha na kututaka tuwatendee wema wazazi wetu na tusiwe wakaidi na wajeuri kwao pale wanatuamrisha kutenda mambo mema.

(ii) Mtu huzaliwa akiwa muislamu akiwa na amani na radhi za Allah(SW). Ataendelea kupata radhi na amani ya Allah(s.w) katika maisha ya dunia endapo atafuata mwongozo wa Allah(s.w). Hivyo, siku ya kufa atakuwa katika amani na radhi za Allah(s.w), kama ilivyojatwa kwa nabii Yahya(a.s)

## HISTORIA YA NABII ISA(a.s)

Nabii Isa(a.s) huitwa Yesu, na Jesus katika Biblia ya kiswahili na Kiingereza. Majina yote hayo matatu yanamkusudia mwana wa Maryamu aliyezaliwa bila baba, ambaye ni mtume wa mwisho kwa Waisraili.

**Nasaba ya nabii Isa(a.s)**

Nabii Isa(a.s) ni mtoto wa Maryamu aliyekuwa mwana wa Imraani. Kizazi cha Imraani kilichaguliwa na Allah(s.w) kupewa utume kama tunavyofahamishwa:

إِنَّ ٱللَّهَ ٱصْطَفَىٰٓ ءَادَمَ وَنُوحًا وَءَالَ إِبْرَٰهِيمَ وَءَالَ عِمْرَٰنَ عَلَى ٱلْعَٰلَمِينَ ﴿٣٣﴾

*Hakika Mwenyezi Mungu alimchagua Adamu na Nuhu na kizazi cha Ibrahiimu na kizazi cha Imraani juu ya walimwengu wote(3:33)*

**Kuzaliwa Maryamu, mamake nabii Isa(a.s)**

Mke wa Imraani aliweka nadhiri kwa Allah(s.w) kuwa mtoto atakayemzaa atamuweka wakfu. Alitarajia kuwa atazaa mtoto wa kiume.

إِذْ قَالَتِ ٱمْرَأَتُ عِمْرَٰنَ رَبِّ إِنِّى نَذَرْتُ لَكَ مَا فِى بَطْنِى مُحَرَّرًا فَتَقَبَّلْ مِنِّىٓ ۖ إِنَّكَ أَنتَ ٱلسَّمِيعُ ٱلْعَلِيمُ ﴿٣٥﴾

*Aliposema mke wa Imraani: “Mola wangu! Nimeweka nadhiri kwako aliye tumboni mwangu kuwa wakfu, basi nikubalie, bila shaka Wewe ndiye usikiaye na ujuaye.(3:35)*

فَلَمَّا وَضَعَتۡهَا قَالَتۡ رَبِّ إِنِّي وَضَعۡتُهَآ أُنثَىٰ وَٱللَّهُ أَعۡلَمُ بِمَا
وَضَعَتۡ وَلَيۡسَ ٱلذَّكَرُ كَٱلۡأُنثَىٰۖ وَإِنِّي سَمَّيۡتُهَا مَرۡيَمَ وَإِنِّيٓ
أُعِيذُهَا بِكَ وَذُرِّيَّتَهَا مِنَ ٱلشَّيۡطَٰنِ ٱلرَّجِيمِ ٣٦

*Basi alipomzaa alisema: “Mola wangu! Nimezaa mwanamke”- Na Mwenyezi Mungu anajua sana aliyemza-”Na mwanaume si sawa na mwanamke. Na nimempa jina Maryamu. nami namkinga kwako, yeye na kizazi chake, uwalinde na shetani aliyewekwa mbali na rehema zako(3:36)*

**Nabii Zakaria(a.s) akabidhiwa jukumu la kumlea Maryamu**

Baada ya kupigwa kura juu ya nani awe mlezi wa Maryam, nabii Zakaria akachaguliwa kuwa mlezi wa Maryam. Allah(s.w) akaikubali ile nadhiri na dua ya mama yake Maryamu.

فَتَقَبَّلَهَا رَبُّهَا بِقَبُولٍ حَسَنٖ وَأَنۢبَتَهَا نَبَاتًا حَسَنٗا وَكَفَّلَهَا
زَكَرِيَّاۖ كُلَّمَا دَخَلَ عَلَيۡهَا زَكَرِيَّا ٱلۡمِحۡرَابَ وَجَدَ عِندَهَا رِزۡ
قٗاۖ قَالَ يَٰمَرۡيَمُ أَنَّىٰ لَكِ هَٰذَاۖ قَالَتۡ هُوَ مِنۡ عِندِ ٱللَّهِۖ إِنَّ ٱللَّهَ
يَرۡزُقُ مَن يَشَآءُ بِغَيۡرِ حِسَابٍ ٣٧

*Basi Mola wake akampokea(mtoto) kwa mapokezi mema na akamkuza kwa makuzi mema, na akamfanya Zakaria awe mlezi wake. Kila mara Zakaria alipoingia chumbani(kwa Maryamu) alikuta vyakula pamoja naye. Akauliza: “Ewe Maryam! Unapatawapi hivi? Akajibu: “Hivi vinatoka kwa Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu humruzuku amtakaye bila kutarajia(3:37)*

Aya hizi zinatuonesha kuwa Maryamu alikuwa katika malezi mema na uangalizi wa karibu toka kwa nabii Zakaria(as) kiasi cha kuepusha mazingira ya ufuska yasimfikie.Allah(s.w) aliweka maandalizi haya mapema ili atakapoleta muujiza wake wa Maryamu kuzaa mtoto bila ya

kuwa na mume isionekane kuwa alikuwa mzinifu, bali iwe ni dalili ya kuwepo Allah(s.w) mwenye nguvu na uweza wa kila kitu.

Kutokana na mazingira hayo na hifadhi ya Allah (s.w) Maryamu akakua vyema na kupata hadhi ya kuwa mwanamke bora kuliko wanawake wote:

وَإِذْ قَالَتِ ٱلْمَلَـٰٓئِكَةُ يَـٰمَرْيَمُ إِنَّ ٱللَّهَ ٱصْطَفَىٰكِ وَطَهَّرَكِ
وَٱصْطَفَىٰكِ عَلَىٰ نِسَآءِ ٱلْعَـٰلَمِينَ ﴿٤٢﴾

*"Na (kumbuka) Malaika waliposema: "Ewe Maryamu! Kwa hakika Mwenyezi Mungu amekuchagua na kukutakasa na kukutukuza kuliko wanawake wa ulimwengu (wote).(3:42)*

**Maryamu apewa habari za kumzaa nabii Isa(as)**

Baada ya maandalizi hayo ya kimalezi pamoja na hifadhi ya Allah(s.w) aliyopewa Maryamu, Allah(s.w) akamtuma Malaika kumueleza Bi Maryamu habari za kumzaa masihi, Isa(a.s) bila ya baba ila kwa amri ya Allah(s.w) ya "Kuwa!" ikawa. Malaika akamwambia:

إِذْ قَالَتِ ٱلْمَلَـٰٓئِكَةُ يَـٰمَرْيَمُ إِنَّ ٱللَّهَ يُبَشِّرُكِ بِكَلِمَةٍ مِّنْهُ ٱسْمُهُ
ٱلْمَسِيحُ عِيسَى ٱبْنُ مَرْيَمَ وَجِيهًا فِى ٱلدُّنْيَا وَٱلْـَٔاخِرَةِ وَمِنَ
ٱلْمُقَرَّبِينَ ﴿٤٥﴾

*Ewe Maryamu! Mwenyezi Mungu anakupa habari njema (za kumzaa mtoto kwa) neno litokalo kwake. Jina lake Masihi Isa bin Maryamu, mwenye heshima katika dunia na akhera, na ni miongoni mwa waliotukuzwa.(3:45)*

وَيُكَلِّمُ ٱلنَّاسَ فِى ٱلْمَهْدِ وَكَهْلًا وَمِنَ ٱلصَّـٰلِحِينَ ﴿٤٦﴾

*Naye atazungumza na watu katika utoto na katika utu uzima wake, na ni katika watu wema(3:46)*

قَالَتْ أَنَّىٰ يَكُونُ لِى غُلَـٰمٌ وَلَمْ يَمْسَسْنِى بَشَرٌ وَلَمْ أَكُ بَغِيًّا ﴿٢٠﴾

*Akasema: "Nitawezaje kupata mtoto, hali hakunigusa mwanaume, wala mimi si mwenye kuzini(19:20)*

قَالَتْ رَبِّ أَنَّىٰ يَكُونُ لِي وَلَدٌ وَلَمْ يَمْسَسْنِي بَشَرٌ ۖ قَالَ كَذَٰلِكِ
اللَّهُ يَخْلُقُ مَا يَشَاءُ ۚ إِذَا قَضَىٰ أَمْرًا فَإِنَّمَا يَقُولُ لَهُ كُن فَيَكُونُ ﴿٤٧﴾

*Akasema:Mola wangu! Na hali mtu yoyote hakunigusa? Akajibu: Ndivyo, vivyo hivyo; Mwenyezi Mungu huumba anavyopenda: anapohukumu jambo, huliambia 'Kuwa', likawa(3:47)*

وَيُعَلِّمُهُ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَالتَّوْرَاةَ وَالْإِنجِيلَ ﴿٤٨﴾ وَرَسُولًا
إِلَىٰ بَنِي إِسْرَائِيلَ

*Na Mwenyezi Mungu atamfunza kuandika na kumuelimisha, na kujua Taurati na Injili. Na ni mtume kwa wana wa Israili(3:48-49)*

**Kuzaliwa nabii Isa(as)**

Allah(s.w) anatueleza kuwa nabii Isa(a.s) alizaliwa chini ya mtende, na wala hakuzaliwa kwenye zizi la ng'ombe lenye najisi.

فَحَمَلَتْهُ فَانتَبَذَتْ بِهِ مَكَانًا قَصِيًّا ﴿٢٢﴾ فَأَجَاءَهَا الْمَخَاضُ
إِلَىٰ جِذْعِ النَّخْلَةِ قَالَتْ يَا لَيْتَنِي مِتُّ قَبْلَ هَٰذَا وَكُنتُ
نَسْيًا مَّنسِيًّا ﴿٢٣﴾

*Basi akachukua mimba yake, na akaondoka nayo mahali pa mbali. Kisha uchungu ukampeleka katika shina la mtende, akasema: "Laiti ningekufa kabla ya haya, na ningekuwa niliyesahaulika kabisa.(19:22-23)*

فَنَادَاهَا مِن تَحْتِهَا أَلَّا تَحْزَنِي قَدْ جَعَلَ رَبُّكِ تَحْتَكِ سَرِيًّا ﴿٢٤﴾
وَهُزِّي إِلَيْكِ بِجِذْعِ النَّخْلَةِ تُسَاقِطْ عَلَيْكِ رُطَبًا جَنِيًّا ﴿٢٥﴾
فَكُلِي وَاشْرَبِي وَقَرِّي عَيْنًا ۖ

*Mara ikamfika sauti kutoka chini yake inamwambia: "Usihuzunike". Hakika Mola wako amejaalia kijito cha maji chini yako". Na litikise kwako shina la mtende, litakuangushia tende nzuri, zilizo mbivu. Basi ule na unywe litue jicho lako.(19:24-26)*

**Nabii Isa(Yesu) (a.s) azungumza akiwa kichanga**

Maryamu akamtwaa mwanawe, akaenda naye kwa jamaa zake

amembeba. Watu wakastaajabu na kuwaza, imewezekanaje Maryamu asiye mzinzi kumpata mtoto bila kuolewa. Na wengine wakauliza:

قَالُوا۟ يَٰمَرْيَمُ لَقَدْ جِئْتِ شَيْـًٔا فَرِيًّا ﴿٢٧﴾ يَٰٓأُخْتَ هَٰرُونَ
مَا كَانَ أَبُوكِ ٱمْرَأَ سَوْءٍ وَمَا كَانَتْ أُمُّكِ بَغِيًّا ﴿٢٨﴾

*Wakasema: "Ewe Maryamu! Hakika umeleta jambo la ajabu: Ewe dada yake Haruni! Baba yako hakuwa mtu mbaya wala mama yako hakuwa hasharati(19:27-28)*

Kwa maswali hayo, ikawepo haja ya kumtakasa Maryamu kuwa japo hakuolewa, hakumpata mtoto huyo kwa zinaa. Ndipo ikatimia kauli ya Allah(sw) kupitia Malaika kuwa nabii Isa(a.s) atazungumza akiwa kichanga.

فَأَشَارَتْ إِلَيْهِ ۖ قَالُوا۟ كَيْفَ نُكَلِّمُ مَن كَانَ فِى ٱلْمَهْدِ صَبِيًّا ﴿٢٩﴾

*Maryam akaashiria kwake(yule mtoto wamuulize yeye). Wakasema: "Tutazungumzaje na aliye bado mtoto kitandani?(19:29)*

قَالَ إِنِّى عَبْدُ ٱللَّهِ ءَاتَىٰنِىَ ٱلْكِتَٰبَ وَجَعَلَنِى نَبِيًّا ﴿٣٠﴾ وَجَعَلَنِى
مُبَارَكًا أَيْنَ مَا كُنتُ وَأَوْصَٰنِى بِٱلصَّلَوٰةِ وَٱلزَّكَوٰةِ مَا دُمْتُ
حَيًّا ﴿٣١﴾ وَبَرًّۢا بِوَٰلِدَتِى وَلَمْ يَجْعَلْنِى جَبَّارًا شَقِيًّا ﴿٣٢﴾

*(Yule mtoto) akasema: "Hakika mimi ni mja wa Mwenyezi Mungu, Amenipa kitabu na Amenifanya Nabii. Amenifanya mbarikiwa popote nilipo. Na Ameniusia sala na zaka maadamu ni hai. Na Ameniusia kumfanyia wema mama yangu. Wala hakunifanya niwe jeuri, muovu. Na amani iko juu yangu siku niloyozaliwa, siku nitakayokufa na siku nitakapofufuliwa kuwa hai(19:30-32)*

Lakini Biblia inasema kuwa Yesu alikuwa mtoto jeuri na mkaidi kwa mama yake. "Mtoto Yesu alibakia nyuma huko Yerusalem na wazazi wake wakawa hawana habari. Wakawa wakimtafuta katika jamaa zao na wenzao; na walipomkosa, wakarejea Yerusalemu, huku wakimtafuta.

Na walipomwona walishangaa, na mama yake akamwambia, mwanangu, mbona umetutenda hivi? tazama, tulikuwa tukikutafuta kwa huzuni. Akawaambia, Kwanini kunitafuta?(Luka 2:48-49)

**Je, nabii Isa(Yesu)(a.s) ni mtoto wa Mungu?**

Mwenyezi Mungu si kiumbe. Yeye ndiye Muumba wa kila kitu kilicho na kisicho na uhai. Kuzaa ni sifa za viumbe vya Mwenyezi Mungu, hivyo Mungu si baba mzazi wa Yesu wala si baba wa mwanadamu yeyote duniani. Qur,an tukufu inatuamrisha hivi:

قُلۡ هُوَ ٱللَّهُ أَحَدٌ ﴿١﴾ ٱللَّهُ ٱلصَّمَدُ ﴿٢﴾ لَمۡ يَلِدۡ وَلَمۡ يُولَدۡ ﴿٣﴾
وَلَمۡ يَكُن لَّهُۥ كُفُوًا أَحَدُۢ ﴿٤﴾

*Sema: Yeye Mwenyezi Mungu ni Mmoja. Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kuhitajiwa na viumbe. Hakuzaa wala Hakuzaliwa. Na wala hakufanana na yeyote(112:1-4)*

Ama katika Biblia, neno Baba limetumika kuonesha sifa ya ulezi wa Mwenyezi Mungu kwa viumbe wake, hivyo, Mwenyezi Mungu kuitwa Baba haimaanishi kuwa kamzaa Yesu au binadamu yeyote miongoni mwetu. Na ndiyo maana akasema:

*Wala msimwite mtu baba duniani, Maana Baba yenu ni mmoja aliye wa mbinguni, wala msiitwe viongozi;maana kiongozi wenu ni mmoja, naye ndiye Kristo(Mathayo 23:9-10)*

Na katika maandiko mengine ya Biblia, Yesu amenukuliwa akisema:

*Basi ninyi salini hivi; Baba yetu uliye mbinguni; Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, hapa duniani kama mbinguni(Mathayo 6:9-10)*

Kwa maana hii, Mwenyezi Mungu ni Baba wa watu wote, si baba wa (Yesu) nabii Isa(a.s) tu. Ni Baba yetu, ila si kwamba katuzaa, bali ulezi wake wa kutujaalia riziki za kila aina na kutupatia elimu na teknolojia ya kuweza kuzitumia neema na riziki hizo. Hivyo (Yesu) si mwana wa Mungu wa kuzaa, bali ni kiumbe wake aliyemuumba kwa neno la 'Kuwa', likawa kama alivyo muumba Adamu.

إِنَّ مَثَلَ عِيسَىٰ عِندَ ٱللَّهِ كَمَثَلِ ءَادَمَۖ خَلَقَهُۥ مِن تُرَابٖ ثُمَّ
قَالَ لَهُۥ كُن فَيَكُونُ ﴿٥٩﴾

*Bila shaka mfano wa (Yesu) Isa mbele ya Mwenyezi Mungu ni kama Adamu; alimuumba kwa udongo, kisha akamwambia "Kuwa", akawa.(3:59)*

**Nabii Isa(a.s) alitumwa kwa kina nani?**

Mtume Isa(Yesu) (a.s.) alipewa utume na kuamrishwa kufikisha ujumbe wa Allah kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israil. Akibainisha juu ya jambo hili, nabii Isa(a.s) alisema:

يَٰبَنِيٓ إِسۡرَٰٓءِيلَ إِنِّي رَسُولُ ٱللَّهِ إِلَيۡكُم مُّصَدِّقٗا لِّمَا بَيۡنَ يَدَيَّ
مِنَ ٱلتَّوۡرَىٰةِ وَمُبَشِّرَۢا بِرَسُولٖ يَأۡتِي مِنۢ بَعۡدِي ٱسۡمُهُۥٓ أَحۡمَدُۖ
فَلَمَّا جَآءَهُم بِٱلۡبَيِّنَٰتِ قَالُواْ هَٰذَا سِحۡرٞ مُّبِينٞ ﴿٦﴾

*"Enyi wana wa Israili; Mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu, nisadikishaye yaliyokuwa kabla yangu katika Taurati na kutoa habari njema ya Mtume atakayejia nyuma yangu ambaye jina lake litakuwa Ahmad . (61:6).*

Na katika Biblia tunafahamishwa kuwa nabii Isa (Yesu) (a.s)alisema kauli hiyo kwamba yeye ni mtume kwa wana wa Israili tu. Ukweli huu unajitokeza pale Yesu alipojibu, akisema:

*Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israili(Mathayo 15:21-24)*

**Ujumbe wa nabii(Yesu) Isa kwa Waisraili**

**(i) Mungu ni Mmoja, wapekee, si watatu, na yeye (Yesu) si Mungu**

Kwanza kabisa, nabii Isa(a.s) aliwataka watu wamjue na kumuamini Mwenyezi Mungu mmoja aliye wa pekee, na kuwataka wakubali kuwa yeye ni mtume wa Mwenyezi Mungu. Akawaambia:

إِنَّ ٱللَّهَ رَبِّي وَرَبُّكُمۡ فَٱعۡبُدُوهُۚ هَٰذَا صِرَٰطٞ مُّسۡتَقِيمٞ ﴿٥١﴾

*Hakika Mwenyezi Mungu ni Mola wangu na ni Mola wenu. Basi mwabuduni. Hii ndiyo njia iliyonyooka(3:51)*

Ujumbe huu wa nabii Isa, unapatikana pia katika Biblia. Hata humo nabii Isa amenukuliwa akifundisha Waisraili kuwa yeye si Mungu, ila ni mtume, na kwamba Mwenyezi Mungu ni mmoja, wapekee na ndiye Mungu wa kweli.

*Na uzima wa milele ndiyo huu, wakujue wewe Mungu wa pekee wa kweli na Yesu Kristo uliyemtuma.(Yohana 17:3)*

Maneno haya ya nabii Isa yanatuonesha ukweli kuwa yeye si mungu, na wale wanaong'ang'ania kumwita, Yesu ni mungu, hawayafuati mafundisho yake, bali wanafuata uzushi wa mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu. Hili analithibitisha nabii Isa(Yesu)(a.s) mwenyewe pale aliposema:

*Enyi wanafiki, ni vyema alivyotabiri Isaya kwa habari zenu, akisema,Watu hawa wananiheshimu kwa midomo; ila mioyo yao iko mbali nami. Nao wananiabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu.(Mathayo 15:7-9)*

**(ii) Hakuna dhambi ya asili**

Yesu amefundisha kuwa kila mwanadamu huzaliwa akiwa huru pasina tone lolote la dhambi, na kwamba watoto ndio wakuu katika ufalme wa mbinguni na ufalme wa mbinguni ni wao.Na hakuna yeyote atakayeingia katika ufalme wa mbinguni(peponi) ila atakayejitahidi kutotenda maovu, na kujitahidi kufanya mema akawa safi kama mtoto.

*Saa ile wanafunzi wake wakamwendea Yesu wakisema, Ni nani basi aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni? Akaita mtoto mmoja, akamweka katikati yao, akasema, Amini, nawaambia, Msipoongoka na kuwa kama vitoto, hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni. Basi yeyote ajinyenyekeshaye mwenyewe kama mtoto huyu, huyo ndiye aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni(Mathayo 18:1-4)*

Na katika maandiko mengine ya Biblia, tunasoma hivi kuwa:

*Yesu akasema: Waacheni watoto wadogo waje kwangu; wala msiwazuie; kwa maana walio mfano wa hao, ufalme wa mbinguni ni wao(Mathayo19:14)*

Kutokana na mafundisho haya ya Yesu, hakuna mtu yeyote muovu atakayeingia katika ufalme wa mbinguni(Peponi), kwa kuamini kwamba Yesu kafa msalabani kwa ajili ya dhambi zake.

**(iii)Waumini wanatakiwa kufuata sheria za Mwenyezi Mungu kwa kuweka ufalme wake hapa duniani**

Nabii Isa aliwafundisha watu wamuabudu Mwenyezi Mungu peke yake katika kila kipengele cha maisha yao. Na kwamba njia ya maisha yenye kuleta amani ya kweli na maisha ya furaha ni kufuata sheria za Mwenyezi Mungu na kuacha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu. Katika Qur,an tunafahamishwa kuwa aliwaambia Waisraili.

إِنَّ ٱللَّهَ رَبِّى وَرَبُّكُمْ فَٱعْبُدُوهُ هَٰذَا صِرَٰطٌ مُّسْتَقِيمٌ ﴿٥١﴾

*Hakika Mwenyezi Mungu ni Mola wangu na ni Mola wenu. Basi mwabuduni. Hii ndiyo njia iliyonyooka(3:51)*

Na katika Biblia, amenukuliwa akiwataka watu wamuombe Mwenyezi Mungu awezeshe ufalme wake ustawi duniani kama mbinguni ili dunia isitawaliwe na kuongozwa kwa sheria zistawishazo ufuska na ufisadi katika jamii.

*Basi ninyi salini hivi; Baba yetu uliye mbinguni; Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje, hapa duniani kama mbinguni(Mathayo 6:9-10)*

**Je (Yesu) nabii Isa alifanya miujiza kwa uwezo wake mwenyewe?**

Ni Mwenyezi Mungu pekee ndiye aliyewawezesha Mitume na manabii kufanya miujiza. Allah(s.w) aliwapa mitume miujiza ili kuwa dalili ya kuwathibitishia watu kuwa yeye ndiye aliyewatuma. Hakuna mtume au nabii aliyedai kufanya miujiza kwa uwezo wake mwenyewe. Na hivi ndivyo nabii Isa alivyowaambia wana wa Israili.

أَنِّي قَدْ جِئْتُكُم بِآيَةٍ مِّن رَّبِّكُمْ ۖ أَنِّي أَخْلُقُ لَكُم مِّنَ الطِّينِ
كَهَيْئَةِ الطَّيْرِ فَأَنفُخُ فِيهِ فَيَكُونُ طَيْرًا بِإِذْنِ اللَّهِ ۖ وَأُبْرِئُ الْأَكْمَهَ
وَالْأَبْرَصَ وَأُحْيِي الْمَوْتَىٰ بِإِذْنِ اللَّهِ ۖ.... إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَةً لَّكُمْ
إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ ﴿٤٩﴾

*Nimekujieni na hoja kutoka kwa Mola wenu, ya kwamba nakuumbieni katika udongo, kama sura ya ndege, kisha nampuliza, mara anakuwa ndege kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na ninawaponesha vipofu na wenye ukoma, na ninawafufua waliokufa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu..... Bila shaka katika haya imo hoja (ya kuonesha kuwepo Mwenyezi Mungu) kwenu ikiwa ni watu wa kuamini(3:49)*

Ni dhahiri kuwa miujiza yote aliyoifanya nabii Isa(a.s), aliifanya kwa lengo la kuwathibitishia watu kuwa yeye ametumwa na Mwenyezi Mungu. Katika Biblia, Yesu alibainisha hili wazi kabla hajafanya muujiza wa kumfufua Lazaro:

*Yesu akainua macho yake juu, akasema: Baba nakushukuru kwa kuwa umenisikia. Nami nalijua ya kuwa wewe wanisikia siku zote; lakini ni kwa ajili ya mkutano huu wanaohudhuria nalisema haya, ili wapate kusadiki kuwa ndiwe uliyenituma. Naye akiisha kusema hayo, akalia kwa sauti kuu, Lazaro, njoo huku nje. Akatoka nje yule aliyekufa, amefungwa sanda miguuni na mikononi, na uso wake umefungwa leso. Naye Yesu akawaambia, Mfungueni, mkamwache aende zake(Yohana 11:41-44)*

Kwa kuzingatia maandiko haya, utabaini kuwa hawasemi kweli wale wanaodai kuwa Yesu ni Mungu eti kwasababu alifanya miujiza ya kufufua wafu.

**Wito wa nabii Isa(a.s) kwa wanafunzi wake**

Nabii Isa(a.s) alipoona ukaidi wao umeshitadi, akatoa wito maalum kwa wanafunzi wake ili wajitokeze wale watakaokuwa tayari kuwa naye bega kwa bega kupambana na madhalimu na kuufikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu kwa wengine. Hivyo, akawauliza:

فَلَمَّآ أَحَسَّ عِيسَىٰ مِنْهُمُ ٱلْكُفْرَ قَالَ مَنْ أَنصَارِىٓ إِلَى
ٱللَّهِ ۖ قَالَ ٱلْحَوَارِيُّونَ نَحْنُ أَنصَارُ ٱللَّهِ ءَامَنَّا بِٱللَّهِ وَٱشْهَدْ بِأَنَّا
مُسْلِمُونَ ﴿٥٢﴾ رَبَّنَآ ءَامَنَّا بِمَآ أَنزَلْتَ وَٱتَّبَعْنَا ٱلرَّسُولَ
فَٱكْتُبْنَا مَعَ ٱلشَّٰهِدِينَ ﴿٥٣﴾

*Lakini Isa alipoona ukaidi wao, alisema: Nani watakuwa wasaidizi wangu katika kumtangaza Mwenyezi Mungu(mmoja)? Wanafunzi wakasema: "Sisi ni wasaidizi wa Mwenyezi Mungu. Tumemwamini Mwenyezi Mungu na ushuhudie kwamba sisi tumejisalimisha. Mola wetu! Tumeyaamini uliyoyateremsha na tumemfuata mtume, basi tuandike pamoja na washuhudiao(3:52-53)*

Baada ya hapo, wanafunzi wa nabii Isa(a.s) wakamtaka awaombee chakula maalumu kutoka kwa Allah(s.w), wakasema:

يَٰعِيسَى ٱبْنَ مَرْيَمَ هَلْ يَسْتَطِيعُ رَبُّكَ أَن يُنَزِّلَ عَلَيْنَا مَآئِدَةً
مِّنَ ٱلسَّمَآءِ ۖ قَالَ ٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ ﴿١١٢﴾

*Ewe Isa Mwana wa Maryam! Je Mola wako anaweza kututeremshia chakula kutoka mbinguni? Akasema(nabii Isa), "Mcheni Mwenyezi Mungu kama kweli ninyi ni wenye kuamini kweli(5:112)*

قَالُوا۟ نُرِيدُ أَن نَّأْكُلَ مِنْهَا وَتَطْمَئِنَّ قُلُوبُنَا وَنَعْلَمَ أَن قَدْ
صَدَقْتَنَا وَنَكُونَ عَلَيْهَا مِنَ ٱلشَّٰهِدِينَ ﴿١١٣﴾

*Wakasema: "Tunataka kula katika hicho, na ili nyoyo zetu zitulie na tuwe miongoni mwa wanaoshuhudia(muujiza huo)(5:113)*

قَالَ عِيسَى ٱبْنُ مَرْيَمَ ٱللَّهُمَّ رَبَّنَآ أَنزِلْ عَلَيْنَا مَآئِدَةً مِّنَ ٱلسَّمَآءِ
تَكُونُ لَنَا عِيدًا لِّأَوَّلِنَا وَءَاخِرِنَا وَءَايَةً مِّنكَ ۖ وَٱرْزُقْنَا وَأَنتَ خَيْرُ
ٱلرَّٰزِقِينَ ﴿١١٤﴾

*Akasema Isa bin Maryamu: "Ewe Mwenyezi Mungu, Mola wetu! Tuteremshie chakula kutoka mbinguni ili kiwe Sikukuu kwa ajili ya wa mwanzo wetu, na wa mwisho wetu, na kiwe Ishara itokayo kwako, basi turuzuku, kwani wewe ndiye mmbora wa wanaoruzuku(5:114)*

قَالَ ٱللَّهُ إِنِّى مُنَزِّلُهَا عَلَيْكُمْ ۖ فَمَن يَكْفُرْ بَعْدُ مِنكُمْ فَإِنِّىٓ أُعَذِّبُهُۥ
عَذَابًا لَّآ أُعَذِّبُهُۥٓ أَحَدًا مِّنَ ٱلْعَٰلَمِينَ ﴿١١٥﴾

*Mwenyezi Mungu akasema: "Bila shaka Mimi nitakiteremsha juu yenu, lakini miongoni mwenu atakayekataa baada ya haya, basi Mimi nitamuadhibu adhabu ambayo sijamwadhibu yoyote katika walimwengu(5:115)*

**Njama za Mayahudi kutaka kumuua nabii Isa(Yesu)(a.s)**

Njama za kutaka kumuua nabii Isa(a.s) zilianza kwa kumuuliza maswali ya kumtega na kumfitinisha kwa Serikali ili imuone kuwa anachochea watu wasilipe kodi na kuhatarisha maslahi ya wakubwa Serikalini. Fitina hizi zilifanywa na Mafarisayo na Makuhani, wakamwendea Yesu wakisema;

*Mwalimu, twajua ya kuwa wewe u mtu wa kweli, na njia ya Mungu waifundisha katika kweli, wala hujali cheo cha mtu awaye yote, kwa maana hutazami sura za watu. basi utuambie waonaje? Ni halali kumpa kaisari kodi, ama sivyo?(Mathayo 22:16-17)*

Lakini Yesu akaufahamu uovu wao, akasema:

*Mbona mnanijaribu enyi wanafiki? Nionyesheni fedha ya kodi. Nao wakamletea dinari. Akawaambia, Ni ya nani sanamu hii, na anwani hii? Wakamwambia, Ni ya Kaisari. Akawaambia, Basi mlipeni Kaisari yaliyo ya Kaisari, na Mungu yaliyo ya Mungu(Mathayo 22:18-21)*

Baada ya hila hizi kushindwa, zikapangwa njama za kutaka kumuua.

*Basi wakuu wa makuhani na Mafarisayo wakakusanya baraza, wakasema, Tunafanya nini? Maana mtu huyu anafanya ishara*

*nyingi.Tunamwachia hivi, watu wamwamini. Yafaa mtu mmoja afe kwa ajili ya watu, wala lisiangamie taifa zima(Mathayo11:47-48,50)*

**Ahadi ya Allah(s.w) kumuokoa nabii Isa(Yesu)(a.s)**

Nabii Isa(Yesu)(as.) alimuomba Allah(s.w) amlinde na shari za watu wabaya waliopanga njama dhidi yake. Yesu alikwenda bustani ya Gethsemane kuomba. Alipofika, akawaambia wanafunzi wake:

*Roho yangu ina huzuni kiasi cha kufa; kaeni hapa, mkeshe pamoja nami. Akaendelea mbele kidogo, akaanguka kifulifuli akaomba, akisema, Baba yangu, ikiwezekana kikombe hiki kiniepuke; walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe.(Mathayo 26:38 39)*

Kwa kuwa Yesu hana kosa lolote mbele yake na wala wale madhalimu waliokusudia kumuua hawakuwa na haki ya kufanya hivyo, Mwenyezi Mungu hakuungana na madhalimu hao, bali alikubali dua ya nabii Isa(a.s) kwa kumuhakikishia kuwa atamlinda dhidi ya njama za watu madhalimu.

إِذْ قَالَ ٱللَّهُ يَٰعِيسَىٰٓ إِنِّى مُتَوَفِّيكَ وَرَافِعُكَ إِلَىَّ وَمُطَهِّرُكَ مِنَ ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ وَجَاعِلُ ٱلَّذِينَ ٱتَّبَعُوكَ فَوْقَ ٱلَّذِينَ كَفَرُوٓا۟ إِلَىٰ يَوْمِ ٱلْقِيَٰمَةِ ۖ ثُمَّ إِلَىَّ مَرْجِعُكُمْ فَأَحْكُمُ بَيْنَكُمْ فِيمَا كُنتُمْ فِيهِ تَخْتَلِفُونَ ﴿٥٥﴾

*Mwenyezi Mungu aliposema: "Ewe Isa! Mimi nitakukamilishia muda wako wa kuishi na nitakuleta kwangu, na nitakutakasa na wale waliokufuru, na nitawaweka wale waliokufuata, juu ya wale waliokufuru mpaka siku ya kiama. Kisha marejeo yenu yatakuwa kwangu,Nitakuhukumuni katika yale mliyokuwa mkihitilafiana(3:55)*

Katika mahubiri yake huko nyuma, nabii Isa(a.s) aliwasisitiza sana watu kumtegemea Mwenyezi Mungu kwa kumuomba msaada. Aliwaambia:

*Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa; kwa maana kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona, naye abishaye hufunguliwa. Au kuna mtu yupi kwenu, ambaye, mwanawe akimwomba mkate, atampa jiwe? Au akiomba samaki, atampa nyoka? Basi ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, Je! si zaidi Baba yenu aliye mbinguni atawapa mema wao wamwombao?(Mathayo 7:7-11)*

Kwa mujibu wa Yesu mwenyewe,Mwenyezi Mungu humsikiliza maombi yake na kumkubalia daima. Hebu na tuyarejee maneno yake aliyoyasema pale alipoomba jambo kubwa la kumfufua Lazaro:

> *Yesu akainua macho yake juu, akasema: Baba nakushukuru kwa kuwa umenisikia. Nami nalijua ya kuwa wewe wanisikia siku zote; lakini ni kwa ajili ya mkutano huu wanaohudhuria nalisema haya, ili wapate kusadiki kuwa ndiwe uliyenituma. Naye akiisha kusema hayo, akalia kwa sauti kuu, Lazaro, njoo huku nje. Akatoka nje yule aliyekufa, amefungwa sanda miguuni na mikononi, na uso wake umefungwa leso. Naye Yesu akawaambia, Mfungueni, mkamwache aende zake(Yohana 11:41-44)*

Ndiyo kusema kuwa Yesu ametangaza kuwa,"Ombeni, nanyi mtapewa", Na kwakuwa Mungu, huwapa "mema wao wamwombao", na Yesu mwenyewe anakiri kuwa Mungu anamsikia siku zote, haiwezekani kabisa asulubiwe hali ya kuwa Mungu yupo na alishamuomba!

**Ilikuwaje kama nabii Isa (Yesu) (a.s) hakusulubiwa?**

Katika Qur,an tukufu, Mwenyezi Mungu aliye muweza na mjuzi wa mambo anathibitisha kuwa aliyesulubiwa si nabii Isa(Yesu). Anasema:

وَقَوْلِهِمْ إِنَّا قَتَلْنَا ٱلْمَسِيحَ عِيسَى ٱبْنَ مَرْيَمَ رَسُولَ ٱللَّهِ وَمَا
قَتَلُوهُ وَمَا صَلَبُوهُ وَلَـٰكِن شُبِّهَ لَهُمْ ۚ وَإِنَّ ٱلَّذِينَ ٱخْتَلَفُوا۟ فِيهِ لَفِى
شَكٍّ مِّنْهُ ۚ مَا لَهُم بِهِۦ مِنْ عِلْمٍ إِلَّا ٱتِّبَاعَ ٱلظَّنِّ ۚ وَمَا قَتَلُوهُ يَقِينًۢا
﴿١٥٧﴾ بَل رَّفَعَهُ ٱللَّهُ إِلَيْهِ ۚ وَكَانَ ٱللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا ﴿١٥٨﴾

> *Na kwa kusema kwao: "Sisi tumemuua Masihi Isa, mwana wa Maryamu Mtume wa Mungu", hawakumuua wala hawakumsulubu ila walibabaishiwa tu. Na hakika wale waliokhitilafiana katika hiyo wamo katika shaka nalo. Wao hawana yakini juu ya hili, isipokuwa wanafuata dhana tu. Na kwa yakini hawakumuua. Bali Mwenyezi Mungu alimnyanyua kwake, Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwenye hikima (4:157-158)*

**Aliyesulubiwa ni Simoni Mkirene, si Yesu**

Biblia inaonesha kuwa aliyesulubiwa si nabii Isa (Yesu)(a.s) bali Simoni Mkirene aliyeshurutishwa na maaskari kubeba msalaba wa Yesu na kisha kusulubishwa.

*Pilato akipenda kuwaridhisha makutano, akawafungulia Baraba; akamtoa Yesu, baada ya kumpiga mijeledi, ili asulubiwe. Nao askari wakamchukua ndani ya behewa, ndiyo Praitorio(yaani nyumba ya uliwali), wakakusanya pamoja kikosi kizima. Wakamvika wazi la rangi ya dhambarau, wakasokota taji ya miiba, wakamtia kichwani; wakaanza kumsalimu, Salamu, Mfalme wa Wayahudi! Wakampiga mwanzi wa kichwa, wakamtemea mate, wakapiga magoti, wakamsujudia. Hata wakiisha kumdhihaki, wakamvua lile vazi la dhambarau, wakamvika mavazi yake mwenyewe; wakamchukua nje ili wamsulubishe.* ***Wakamshurutisha mtu aliyekuwa akipita, akitoka mashamba, Simoni Mkirene, baba yao Iskanda na Rufo, ili auchukue msalaba wake. Wakamleta mahali paitwapo Golgotha, yaani fuvu la kichwa. Wakampa mvinyo iliyotiwa manemane, asiipokee. Wakamsulubisha.(Marko 15:15-24)***

### Nabii Isa(as) (Yesu) siku ya Kiyama

Siku ya kiyama itakuwa nzito sana kwa wale waliokuwa wakiamini na kutangaza kuwa nabii Isa(Yesu) ni Mungu, na kumuabudia kinyume cha alivyofundisha. Allah(s.w) atamuuliza nabii Isa(a.s)

يَٰعِيسَى ٱبْنَ مَرْيَمَ ءَأَنتَ قُلْتَ لِلنَّاسِ ٱتَّخِذُونِى وَأُمِّىَ
إِلَٰهَيْنِ مِن دُونِ ٱللَّهِ ۖ قَالَ سُبْحَٰنَكَ مَا يَكُونُ لِىٓ أَنْ أَقُولَ
مَا لَيْسَ لِى بِحَقٍّ ۚ إِن كُنتُ قُلْتُهُۥ فَقَدْ عَلِمْتَهُۥ ۚ تَعْلَمُ مَا فِى
نَفْسِى وَلَآ أَعْلَمُ مَا فِى نَفْسِكَ ۚ إِنَّكَ أَنتَ عَلَّٰمُ ٱلْغُيُوبِ ﴿١١٦﴾

*"Ewe Isa bin Maryam! Je wewe uliwaambia watu 'Nifanyeni mimi na mama yangu miungu badala ya Mwenyezi Mungu?'. Aseme: "Wewe umetakasika na kuwa na mshirika. Hainistahiki mimi kusema ambayo si haki yangu. Kama ningelisema bila shaka ungelijua; unayajua yaliyomo nafsini mwangu, lakini mimi siyajui yaliyo nafsini mwako; hakika wewe ndiwe ujuaye mambo ya ghaibu. (5:116)*

مَا قُلْتُ لَهُمْ إِلَّا مَآ أَمَرْتَنِى بِهِۦٓ أَنِ ٱعْبُدُوا۟ ٱللَّهَ رَبِّى وَرَبَّكُمْ ۚ
وَكُنتُ عَلَيْهِمْ شَهِيدًا مَّا دُمْتُ فِيهِمْ ۖ فَلَمَّا تَوَفَّيْتَنِى كُنتَ
أَنتَ ٱلرَّقِيبَ عَلَيْهِمْ ۚ وَأَنتَ عَلَىٰ كُلِّ شَىْءٍ شَهِيدٌ ﴿١١٧﴾

*Sikuwaambia lolote ila yale uliyoniamrisha; ya kwamba 'Mwabuduni Mwenyezi Mungu, Mola wangu na Mola wenu'. Na nilikuwa shahidi juu yao nilipokuwa nao; na uliponikamilishia muda wangu, Wewe ukawa mchungaji juu yao, na Wewe shahidi juu ya kila kitu.(5:117)*

إِن تُعَذِّبْهُمْ فَإِنَّهُمْ عِبَادُكَ ۖ وَإِن تَغْفِرْ لَهُمْ فَإِنَّكَ أَنتَ ٱلْعَزِيزُ
ٱلْحَكِيمُ ﴿١١٨﴾

*Ikiwa utawaadhibu, basi bila shaka hao ni waja wako; na ukiwasamehe basi kwa hakika wewe ndiwe Mwenye nguvu na Mwenye hikima.(5:118)*

قَالَ ٱللَّهُ هَٰذَا يَوْمُ يَنفَعُ ٱلصَّٰدِقِينَ صِدْقُهُمْ ۚ لَهُمْ جَنَّٰتٌ
مِن تَحْتِهَا ٱلْأَنْهَٰرُ خَٰلِدِينَ فِيهَآ أَبَدًا ۚ رَّضِيَ ٱللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا۟
عَنْهُ ۚ ذَٰلِكَ ٱلْفَوْزُ ٱلْعَظِيمُ ﴿١١٩﴾

*Mwenyezi Mungu atasema: "Hii ndiyo siku ambayo wakweli utawafaa ukweli wao". Wao watapata Bustani zipitazo mito mbele yake. humo watakaa milele. Mwenyezi Mungu amewawia radhi; nao wawe radhi naye. Huko ndiko kufaulu kukubwa(5:119)*

## ZOEZI – 5

1.Kwa mtazamo wa makafiri historia ni _______ ya ______ ya mwanaadamu katika mapambano yake dhidi ya maumbile asili, hii ni kwa sababu wamedai kuwa binaadamu ametokana na _____________

2.(a) ____ ndiye muasisi wa nadharia potofu juu ya chanzo cha binaadamu.

(b)Toa hoja mbili kukosoa nadharia potofu juu ya chanzo cha binaadamu.

(i)__________________

(ii)_________________

3.Kwa mtazamo wa Uislamu, historia ni ____ za matendo ya watu na matokeo ya matendo hayo katika maisha ya dunia na akhera.

4.Kwa mtazamo wa Kiislamu kazi ya historia ni:

(a)_____________________

(b)_____________________

(c)_____________________

(d)_____________________

(e)_____________________

5.(a) Adamu (a.s) ni mu na mtume wa Allah (s.w) wa kwanza hapa duniani. Adamu (a.s) aliumbwa na vitu viwili vifuatavyo:

(i)_____________________

(ii)_____________________

(b)Binaadamu hapa duniani anatarajiwa awe__________ wa Allah (s.w).

(c)____________ ndio nyenzo ya kwanza ya msingi inayomuwezesha binaadamu kuwa Khalifa wa Allah (s.w) hapa ardhini.

(d)Adui wa kwanza wa binaadamu ambaye ni dhidi ya lengo la kuumbwa kwake ni ______________, ambaye amelaaniwa na Allah (s.w).

(e)Tabia ya kujivunia ubora utokanao na ukabila, utaifa, rangi, nasaba, n.k. ni tabia ya ___________________________.

(f)Adhabu iliyowapata Adamu na Hawa baada ya kula tunda walilokatazwa ni _______________________________

(g)Hakuna dhambi ya Asili kwa sababu Adamu na Hawa walileta toba na ___________________ na Mola wao.

6.Nabii Idris (a.s) ametajwa katika Qur-an kwa sifa ya _____________, hivyo tunatakiwa tumuige.

7.(a) Katika jitihada za kufikisha ujumbe wa Allah kwa watu wake, Nabii Nuhu alitumia mbinu mbali mbali zifuatazo:

(i)________ (ii)_________(iii)________(iv)______(v)______

(b)Miungu wa kisanamu waliokuwa wakishirikishwa na Allah (s.w) wakati wa Nabii Muhu ni:

(i)________ (ii)_________(iii)________(iv)______(v)______

(c)Baada ya watu wa Nabii Nuhu kukataa ujumbe wake na kung'ang'ania katika uasi, Allah (s.w) aliwaadhibu kwa _____________________.

(d)Kwa mtoto wa Nabii Nuhu kuangamia pamoja na walioangamia, licha dua ya baba yake aliyomuombea, tunajifunza kuwa ________________

(e)Waliookoka na adhabu ya Allah (s.w) ni wale waliopanda katika safina ambao walikuwa ni ________________________.

8.(a) Nabii Hud (a.s) aliletwa kuliongoza taifa la_________________.

(b) Watu wa Hud (a.s) walimuasi Mtume wao na kumtukana kwa kumuita __________________ na ___________________

(c) Watu wa Nabii Hud (a.s) waliobobea katika uasi waliangamizwa kwa __________________________

9.(a) Nabii Salih (a.s) ni Mtume wa Allah aliyeletwa kuwaongoza watu wa _______walioishi kaskazini mwa Bara Arab katika sehemu iitwayo_______ambao walikuwa wakijenga numba zao kwa ____________________.

(b) Muujiza aliopewa Nabii Salih (a.s) kama alama ya Utume wake ni _________________________

(c) Watu wa Nabii Salih (a.s) waliozidi kubobea katika uasi hata baada ya kuonywa waliangamizwa kwa _______________

10.(a) Kutokana na Nabii Ibrahim (a.s) kuanza kumlingania Uislamu baba yake tunajifunza kuwa ____________

(b)Njia aliyoitumia Nabii Ibrahim (a.s) katika kukanusha hadharani uongo wa nyota, mwezi na jua, inatufundisha kuwa katika kulingania Uislamu tunatakiwa kutumia __________

(c)Nabii Ibrahimu (a.s) alivunja masanamu yote ndani ya hekaru na kulibakisha kubwa lao ili ____________________.

(d)Muujiza iliyotokea katika maisha ya Nabii Ibrahimu (a.s) ni hii ifuatayo:

(i)___________________________________.
(ii)___________________________________.
(iii)___________________________________.

(e)Nabii Ibrahimu alipewa mitihani mingi na Mola wake, na mtihani mkubwa kuliko yote ni ule wa _________________________.

11. (a)Miji ya Sodom na gomora ilikuwa chini ya Nabii ______________

(b)Watu wa miji ya Sodom na gomora walikuwa wakifanya uovu uliopindukia wa __________________________________.

(c)Watu wa Lut (a.s) baada ya kupindukia mipaka ya Allah (s.w) na kukataa kuonyeka, waliangamizwa kwa _____________________.

12.(a) Nabii Ibrahim alimuomba Allah ampe watoto wema. Dua yake ilijibiwa kwa kupatikana kwa _____________na ______________ ambao wote walikuwa manabii.

(b)Nabii Issa (a.s) anatokana na Nabii Ibrahim (a.s) kupitia kwa __________________ambapo Nabii Muhammad (s.a.w) anatokana na Nabii Ibrahim (a.s) kupitia kwa _________________________.

(c)Mtoto wa Nabii Ibrahim (a.s) aliyesaidiana na baba yake katika kujenga Ka’abah ni ______________________________.

(d)Chimbuko la kizazi cha Mayahudi (Waisrail) ni Nabii ____________.

13.(a) Nabii Yusufu (a.s) ni katika watoto _______________ wa mzee Yaquub (a.s)

(b)Mtihani mkubwa aliopewa Nabii Yusufu katika maisha yake ni ule ______________________.

(c)Yusuf (a.s) alipokuwa mdogo alihusudiwa na kama zake ambao waliamua kumtokomeza kwa ____________________

(d)Nabii Yusuf (a.s) alipokuwa mtoto aliota kuwa _________________ na ndoto hiyo ilikuwa inaashiria kuwa __________________ jambo ambalo lilitokea baada ya wazazi wake na ndugu zake kuhamia Misr.

(e)Mfalme wa Misr aliota kuwa _____________________________

(f)NabiiYusuf (a.s) aliitafsiri ndoto ya mfalme kuwa______________

14.(a) Nabii Mussa (a.s) alilelewa na adui yake na adui wa Uislamu ambaye ni ___________.

(b) Nabii Mussa (a.s) alihamia Madina baada ya kupata habari za hakika kuwa ________________.

(c)Nabii Mussa (a.s) alipewa Utume katika bonde la ______________

(d)Dalili mbili alizopewa nabii Mussa (a.s) kuthibitisha Utume wake ni:

(e)Nabii __________ alifanywa kuwa msaidizi wa Nab ii Mussa (a.s).

(f)Firaun na majeshi yake waliangamizwa kwa _________________

15.(a) Nabii Daud (a.s) aliteuliwa kuwa Mtume wa Allah baada ya kuua _______________ aliyekuwa mfalme wa kitwaghuti.

(b) Nabii Daud (a.s) amesifiwa katika Qur-an kwa mkazo mkubwa kuwa alikuwa muadilifu katika _____________. Alikuwa akihukumu kwa mujibu wa kitabu cha Allah cha ___________________.

16. Licha ya Nabii Sulaiman (a.s) kupewa neema kubwa tatu za _______, na _________________- hakuwa mwenye kutakabari.

(b) Teknologia wakati wa Nabii Sulaiman (a.s) ilikuwa juu zaidi kuliko hivi sasa kwa hoja kuu mbili zifuatazo:

(i)_____________________________________.

(ii)_____________________________________.

(c) Nabii Sulaiman (a.s) alipata ufalme ambao haujapatikana kwa yeyote katika historia ya duinia kwa hoja zifuatazo:

(i)Alikuwa akimiliki majeshi ya ______, _____ na _________.

(ii)Alikuwa akiwatumia _______, kumfanyia kila kazi aliyoitaka.

(iii)Alikuwa akitumia ________________ kusafiria.

17. (a) Nabii Yahya (a.s) ni mtoto wa Nabii_____________. Alizaliwa kwa muujiza kwa sababu __________________.

(b)Maryamu bint Imraani alikuwa bint mwema aliyelelewa na Nabii _______baada ya baba yake kufariki.

(c)Nabii Issa (a.s) amezaliwa kwa muujiza kwa sababu _________

(d) Nabii Issa (a.s) alijaaliwa kuzungumza akiwa mchanga ili kumtakasa mama yake na uchafu wa ________________

(e) Miongoni mwa miujiza mine aliyoionyesha Nabii Issa (a.s) ni:

(i)_________________.

(ii)_________________.

(iii)_________________.

(iv)_________________.

(f) Mayahudi walidhamiria kumuua Nabii Issa (a.s) lakini Allah (s.w) alimuokoa kwa___________________________.

(g) Nabii Issa (a.s) aliwafundisha Mayahudi Uislamu kwa kutumia Taurat na _______________.

*Wabillah Tawfiiq.*